

Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake. Kwa bahati mbaya, itikadi na mila za kiasili bado hazitupi nafasi ya kuwashangilia wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja naya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi, wapinga mila na watovu wa utii.

Maswali

- (a) Eleza chanzo cha dhuluma kwa wanawake. (alama. 2)
- (b) Huku ukitoa mafano, fafania hali ya dhuluma kwa wanawake kama inavyodhihirika katika makala. (alama. 4)
- (c) Eleza hatua ambazo mwanamke amechukua kujikomboa (alama. 4)
- (d) Je, jamii imechangia vipi katika kumdunisha mwanamke (alama. 2)
- (e) Fafania maana ya misemo ifuatayo; (alama. 3)
- i) Wamekiuka misingi
- ii) Kupitishwa kwa maazimio
- iii) Wanaojitolea mhanga

1. UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata

Ama kwa kweli maisha ya vijana wa kisasa yanatofautiana na kuhitilafiana na yale ya wazee wao. Sio katika mavazi, mienendo, mitazamo, mawazo na mielekeo tu bali pia katika kipengele kingine chochote utakachofikiria. Yote haya ni vielelezo vya jinsi kizazi cha leo kinavyoishi katika ulimwengu ambao ni kivuli tu cha ule wa vizazi vilivyotangulia. Baadhi ya watu wameieleza hali hii kuwa maisha sio jiwe.

Kwao basi, si ajabu katu kuwaona vijana wakizungumza lugha yao ya kipekee au wakivaa nguo zinazobana ajabu na kudhihirisha bayana maungo yao badala ya kuyasitiri.

Hata hivyo watu wengi wameonelea kwamba hali ya maisha ya vijana wa leo ni maasia yanayotokana na utundu na hata ukatili wao. Upane huu umetoa rai kwamba kizazi hiki kisingepotoka kama tu kingezingatia na kustahi utamaduni wa wahenga wao ambamo wazazi wao ndimo walimokulia. Wanazidi kufafania kuwa nyendo hizi za ukarimu, unyenyevu, hadhari katika kila jambo, utiifu na pia kujitegemea. Yote haya yamesahauliwa ama tuseme yamepuuzwa katika —Utamaduni wa kisasa.” Swali linalozuka sasa ni je, tunapaswa kuwahukumu vijana wa leo kwa kutumia vigezo au masharti gani? Tuwapige darubini kwa kutegemea hali ilivyo hivi leo duniani ama tuwapime kwa mujibu wa jinsi maisha ya baba na babu zao yalivyokuwa. Jibu la swali hili ni gumu na sharti lifafanuliwe kwa makini, lisije likaegemea upande wowote. Mathalan, ni jambo lisilopingika kuwa maisha ni utaratibu unaoathirika na hivyo kubadilika daima.

Angalia kwa mfano jinsi maendeleo ya elimu, sayansi, mawasiliano na hata ufundi yalivyo yageza maisha siku hizi. Yamkini vijana wa barani Afrika wakaona na hata kuzungumza kwa wenzao kutoka Uropa, Asia na Marekani bila hata kunyanyuka hapa kwao nyumbani. Athari ya filamu, video, vitabu, magazeti, majarida na kadhalika haikadiriki. Haya, kwa kiasi yamefanya vijana hata kupevuka kabla ya wakati wao. Isitoshe, mambo hayo yameweza kuwazuzua na kuwaaminisha ya kuwa yale wanayojifunza ni kweli.

Matokeo yamekuwa ni wao kudunisha utamaduni wao wa asili na kuupapua ule wa wageni waliowaathiri. Tulisahau kuwa ujana ni tembo la mnazi na rahisi kwao kubadili mawazo.

Lakini hatuwezi kuwasamehe vijana wanaokosa akili kwa kupotoshwa na kucharika na yote wanayoyapokea kutoka ugenini na hivyo kuanza kudhalilisha utamaduni wa Waafrika. Hata hivyo, badala ya kuwakashifu wanapopotea njia ama kuwapongeza wanapotenda yale tunayoyategemea tu, ni wajibu mkubwa wa wazazi kuwaongoza na kuwasaidia vijana kuwa na uwezo mkubwa wa kufanya uteuzi mwafaka katika maisha yao.

- (a) Bila kupoteza maana asilia fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 40 (Alama 6, 1 ya utiririko)
- (b) Fufisha aya mbili za mwisho (maneno 50) (Alama 9, 1 ya utiririko)
3. **MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**
- (a) Taja irabu mbili za nyuma kisha ueleze kwa nini huitwa hivyo. (Alama 2)
- (b) Toa mfano mmoja kwa kila mojawapo. (Alama. 2)
- i) Kipasuo
- ii) Kitambaza
- (c) Eleza maana ya, (Alama. 2)
- i) Silabi
- ii) Mofimu
- (d) Bainisha viwalikishi katika sentensi ifuatayo (Alama. 2)
- Alimpiga mwanafunzi mtundu
- (e) Eleze maana mbili za sentensi hii (Alama. 2)
- Jane alifagia chakula chote
- (f) Ainisha matumizi ya na katika sentensi (Alama. 2)
- i) Marafiki hawa hutembelele sana

- ii) Amina ni tofauti na kakake
- (g) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali. (Alama. 3)
Msichana mtukutu alifukuzwa shule leo asubuhi
- (h) Tunga sentensi kwa kutumia nomino katika ngeli ya pa- ku- mu. (Alama. 3)
- (i) Tambua na ueleze aina za vielezi katika sentensi hizi. (Alama. 2)
- i) Mama alimwamrisha mtoto wake kijeshi
- ii) Askari hutembea makundi makundi
- (j) Andika katika hali ya udogo
Mbwa mwenye ukali alimfukuza mtoto (Alama. 2)
- (k) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumiza ya ritifaa (Alama. 2)
- (l) Tambua aina ya vitenzi kwa kutaja majina yake
Babu angali anasoma gazeti (Alama. 2)
- (m) Kwa kutungia sentensi, tofautisha vitate hivi. (Alama. 2)
- i) Ghali
- ii) Gari
- (n) Tumia 'O' rejeshi. (Alama. 2)
- i) Msichana ambaye huja ni mwanasheria
- ii) Maovu ambayo aliyatenda hayasahauliki
- (o) Andika katika msemu wa taarifa;
"Fusipofanya kazi yetu kwa bidii na kujitegemea, tutabaki kuwa watumwa katika nchi yetu" Rais alisema. (Alama. 2)
- (p) Kanusha sentensi hii
Ugonjwa huu ungalidhibitiwa mapema kifo kingaliepukwa (Alama. 2)
- (q) Tambua shamirisho kipozi, kitondo na shamirisho ala katika sentensi ifuatayo.
Baba amemnunulia mtoto fulana nzuri iliyoshonwa kwa uzi mwekundu. (Alama. 3)
- (r) Badilisha katika kauli ya kutendua.
Tundika picha hiyo ukutani na uyabandike maandishi kitabuni. (Alama. 2)
- (s) Tambua kishazi huru na kishazi tegemezi
Tumeanzisha shirika ili tunyanyue hali yetu (Alama. 1)
- 4. ISIMU JAMII (Alama 10)**
- (a) Eleza juhudi zozote **tano** zinazotumiwa kukiendeleza Kiswahili sanifu nchini Kenya. (Alama 5)
- (b) Eleza jinsi uwililugha unaweza kuleta athari katika lugha na mawasiliano miongoni mwa wanajamii. (Alama. 5)

MAKUENI COUNTY CLUSTER PREPARATORY EXAMINATIONS 2016**102/3****KISWAHILI****KARATASI YA 3****FASIHI****JULAI/ AGOSTI 2016****MUDA: 2 ½****SEHEMU A: USHAIRI****1. LAZIMA****Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Zitavuma,
Zitakoma,
Nitakwima,
Mti-mle.

Na muda nikisimama,
Nitatongoa nudhuma,
Kwa tenzi zilizo njema,
Nilisifu mti – mle.

Tazipanga tathlitha, tungo zilizo na hekima,
Za huba na thiatha, za kuburudi mitima,
Mashairi mabuthutha, musome mnaosoma.

Mti nishainukia, namea kuwa mzima,
Mizizi yadidimia, ardhini imeuma,
Nanena kitarbia, tungo zilizo adhama
Japo ni tungo za zama, mti-mle hutumia.

Zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,
Dharuba kinitikisa, mti-mle huinama,
Huyumba nikaziasa, matawi yakakingama,
Gharika ikishapisa, hurudi nikawa wima,
Na tungo za takhimisa, mti-mle huzipima.

Maswali

- (a) Shairi hili ni la kimapokea. Toa sababu mbili kuunga kauli hii. (Alama.2)
- (b) Taja bahari kuu ya ushairi ambayo imetumiwa na mshairi. Fafanua. (Alama.2)
- (c) Fafanua dhamira ya mshairi. (Alama.2)
- (d) Kwa kutoa mifano bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (Alama.2)
- (e) Eleza jinsi mshairi ametumia idhini ya ushairi katika utungo huu. (Alama.2)
- (f) Andika ubeti wa nne kwa lugha natharia. (Alama.4)
- (g) Mshairi anamaanisha nini anaposema zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma, (Alama.2)
- (h) Eleza toni ya shairi hili. (Alama.2)
- (i) Eleza maana ya msamiati ufuatao. (Alama.2)
- i) Nitatongoa
- ii) Zitapusa.

SEHEMU YA B**TAMTHILIA****T. Arege; Mstahiki Meya*****Jibu Swali la 2 au 3***

2. Huyu Meya wetu ana washauri ambao huwasikiliza zaidi hata kama wanampotosha. (Alama.20)
- Fafanua.
3. Mwafulani I: Nilikusahau lini ndiyo sasa nije kukusahau?.....”
- Mwafulani II:tusikie
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama.4)
- (b) Bainisha mbinu ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili. (Alama.2)
- (c) Fafanua mambo yoyote **manne** yanayo zungumziwa na mwafulani wa pili kulingana na muktadha wa dondoo. (Alama.4)
- (d) Fafanua maudhui yoyote **matano** yanayojitokeza kulingana na muktadha wa dondoo hili. (Alama.10)

SEHEMU C**Kidagaa Kimemwozea; Ken Walibora
Jibu Swali la 4 au 5**

4. Eleza jinsi mbinu ya kwelikinzani imetumika kwa kurejelea riwaya ya kidagaa kimemwozea. (Alama.20)
5. **Kidagaa Kimemwozea; Ken Walibora**
Ningemweka hai afikishwe mahakamani kweli idhihiri na uongo ujitenge”.
- (a) Eleza muktadha wa dondoo. (Alama.4)
- (b) Fafanua kwa kutolea mifano ukweli wa kauli ~~kweli~~ idhihiri”. (Alama.6)
- (c) Eleza hulka ya mmenaji. (Alama.4)
- (d) Vitaje vitushi vyovyote **vitatu** vilivyomshangaza msemaji kulingana na muktadha wa dondoo. (Alama.6)

SEHEMU YA D.**Hadithi fupi, Ken Walibora**

6. **Kanda la Usufi** - (R. Nyaga)
- (a) Kanda la usufi ni anwani mwafaka.
Fafanua kwa kutolea mifano. (Alama.10)
- (b) Lini angepata nafasi ya kupenya kwenye chungio...”
Fafanua jinsi msemewa angepata nafasi na changamoto zake. (Alama.10)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**Jibu Swali la 7 au 8.**

7. **i) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**
Mtu mmoja alimpa mke wake nambari yake ya simu. Kila mara bibi akipigia mumewe simu, ilipokelewa na sauti nyororo —~~teja~~ wa nambari uliopiga hapatikani kwa sasa.” Alifunga safari kumtembelea mume wake mjini na kukabiliana na huyu kisura.

MASWALI

- a) Bainisha kipera cha utungo huu. (Alama.2)
- b) Onyesha sifa **tano** za kipera hiki. (Alama.5)
- c) Eleza manufaa **tano** ya kipera hiki. (Alama.5)

ii) Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali

Ewe mpwa wangu,
Kwetu hakuna mwoga, usiwe kama msichana.
Uoga ukikufika, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja ili uwe mwanamume
Iwapo utatingiza kichwa
Uhamie kwa wasiokatwa
Waume wa mbari yetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo.

Simama jicho liwe juu
Ngariba alilala jikoni
Visu ametia makali
Kabiliana na kisu kikali
Wengi wasema ni kikali
Mbuji utampata
Na hata shamba la mahindi
Usiende kwa wasiotahiri.

MASWALI

- (a) Huu ni wimbo gani? Fafanua (Alama.2)
- (b) Eleza shughuli **mbili** za kiuchumi zinazodokezwa na wimbo huu. (Alama.2)
- (c) Onyesha taasubi ya kiume inavyojitokeza katika wimbo huu. (Alama.4)
8. a) Eleza mambo manne yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (Alama.8)
- b) Eleza maana ya ngoma katika fasihi simulizi kisha utoe dhima zake nne. (Alama.5)
- c) Eleza maana ya maapizo. (Alama.2)
- d) matambiko ni nini? Eleza dhima zake mbili. (Alama.5)

MTIHANI WA PAMOJA WA KUWED - 2016.**102/1****KISWAHILI****INSHA****KARATASI YA I****JULAI/AGOSTI- 2016****Maswali****1. LAZIMA**

Wewe ni raia katika nchi ya Mzalendo. Mwandikie barua mhariri wa gazeti la Kumekucha Leo ukitoa maoni yako jinsi serikali yako inavyoweza kupunguza umaskini nchini.

2. Utandawazi una athari mbaya katika maisha ya vijana. Jadili.
3. Andika insha inayodhihirisha maana ya 'Mchelea mwana kulia hulia yeye'
4. Kamilisha insha yako kwa maneno :.....sitaisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka kama nilivyoaibika siku hiyo.

MTIHANI WA PAMOJA WA KUWED - 2016.*(Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)***102/2****KISWAHILI****KARATASI YA 2****LUGHA****JULAI/AGOSTI- 2016****MUDA: SAA 2 1/2****1. UFAHAMU (Alama 15)****Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

KUKITHIRI kwa visa vya utoaji wa hongo kwa wapiga kura walioshiriki chaguzi ndogo zilizofanyika Jumatatu katika eneobunge la Malindi na Kaunti ya Kericho ni ithibati tosha kuwa ufasidi ume-kita mizizi nchini.

Kadhalika, visa hivyo vilidhihirisha kuwa demokrasia imedidimia na taasisi za kupambana na visa vya ufasidi zimeffia.

Mwezi uliopita, Wakenya kupitia mitandao ya kijamii walishitumu Rais wa Uganda Yoweri Museveni kutokana na kile walichotaja kuwa matumizi ya 'mabavu' kuhifadhi kiti chake baada ya kuwatishia wapinzani wake.

Watumiaji wa mitandao ya kijamii pia walimkosoa Rais Uhuru Kenyatta kwa kumpongeza mwenzake wa Uganda huku wakisema aliunga mkono ukandamizaji wa demokrasia.

Lakini, visa vya uhongaji wa wapiga kura vilivyoshuhudiwa katika maeneo ya Malindi na Kericho vikitekelezwa na viongozi wa kisiasa hata wengine wakiwa wa muungano tawala wa Jubilee, ni dhahirisho tosha kuwa Wakenya hawakuwa na sababu ya kushitumu Rais Museveni.

Utumiaji wa mabavu au kununua wapiga kura ili kushinda uchaguzi ni hujuma kwa demokrasia. Baadhi ya wanasiasa pia wameripotiwa kuwa wanatumia fedha za kusafirisha watu kutoka eneo moja hadi jingine ili wajiandikishe kuwa wapiga kura na wawachague katika uchaguzi ujao. Huu pia ni ukiukaji wa misingi ya demokrasia.

Ununuaji wa wapiga kura unamaanisha mabwanyenye ambao wamehusishwa na sakata mbalimbali za ufasidi ndio wataendelea kushikilia nyadhifa mbalimbali za uongozi kwa kuwa wao ndio wana mabunda ya fedha za kuhonga wapiga kura.

Viongozi wanaochaguliwa baada ya kuwahonga wapiga kura hawatafanya maendeleo yoyote na badala yake, watakuwa wakihusika na wizi wa rasilimali za umma ili kupata fedha za kuwahonga watu katika uchaguzi unaofuatia. Mabwanyenye hawa wanafanya kila wawezalo kuhakikisha wapiga kura wanaendelea kuzama katika lindi la umaskini ili waweze kununuliwa kwa urahisi. Sawa na Esau tuliyelezwa katika Biblia kwamba aliua urithi wake wa kuzaliwa kwa Yakobo kwa kubadilishana na chakula, maskini pia wako tayari kuuza haki yao ya kuchagua kiongozi bora kwa shilingi mia moja.

Viongozi wanaotoa hongo kwa wapiga kura kwa lengo la kushinda uchaguzi ni ishara kwamba hawana maono wala sera za mandeleo. Badala yake wanang'ang'ania mamlaka ili kujilimbikizia utajiri wala si kusaidia mpiga kura kujiinua kimaisha.

*(Taifa leo. Machi 10, 2016)***Maswali**

- a) Kwa kurejelea kifungu, visa vya kutoa rushwa kwa wapiga kura vinadhihirisha nini? (Alama 3)
- b) Bainisha jinsi mne ambazo viongozi wa kisiasa wanatumia kuendelea ukiukaji wa misingi ya demokrasia (Alama 4)
- c) Fafanua athari za uozo unaorejelewa katika taarifa kwa
 - (i) Viongozi (Alama 2)
 - (ii) Raia (Alama 2)
- d) Thibitisha kuwa nyani haoni ngokoye katika muktadha wa makala haya (Alama 2)
- e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa (Alama 2)
 - (i) Mitandao ya kijamii
 - (ii) Mabwanyenye

2. Ufupisho (alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Tangu miaka ya uhuru, serikali za Afrika zimekuwa zikikariri kwa dhiti na hata kula viapo vya kulinda na kutetea haki za raia wao kama zilivyoainishwa kwenye katiba. Kadiri miaka inavyozidi na ulevi wa mamlaka kuchukua nafasi katika nafsi za viongozi hao, kiapo chao huishia kuapuliwa katika muda wa kupepesa macho. Ikasalia hali ya maskini pita chini miye mwenye nazo nipite juu. Katika hali kama hii, wanaoishia kuumia aghalabu ni watoto.

Kwa miaka mingi, mtoto wa Afrika amekuwa akiteseka na kusalitika katika dunia hii ya mwenye nguvu mpishe, hasa akiwa anatoka katika familia maskini na jamii isiyothamini utu. Si ajabu kupata mtoto wa Afrika akiishi katika mabanda *yaliyo* kando ya machimbo katika migodi akitumikishwa katika machimbo hayo. Katika hali kama hizi, siku nenda rudi, utawapata watoto *wamevalia* matambara, miguu imeparara na midomo kuwakauka huku vichwani wakiwa wamebeba karai za madini kutoka machimboni. Na mchakato wote wa kutafuta madini hayo unawashirikisha watoto, isipokuwa kupokea pesa, ambao hufanywa na mabwanyenye wanaoishia kuwapa (au hata kuwanyima) watoto wale malipo duni au badala yake wakawalipa wazazi wa watoto hao.

Hali huwa sawa na hiyo katika maeneo ambayo shughuli za uvuvi hutekelezwa. Watoto wengihuingizwa katika *biashara* ya samaki kwa kisingizio cha kuwapa namna ya kujitegemea katika siku za usoni. Ajabu ni kwamba, mwisho wao huwa papo hapo uvuvini.

Kinachosikitisha sana ni udhalimu ambao umekuwa ukitekelezwa na kundi la watu ambao wanafaa- kwa msingi wa kazi zao- kuwalinda watoto hao na kuwaelekeza katika masuala ya maisha. Je, ni kwa nini mtu mwenye akili zake timamu, ambaye tayari alikwishamaliza masomo na hata kupata kazi, amtunge mimba mwanafunzi na kumzimia ndoto yake maishani? Kwa nini mtoto kama huyo abebeshwe mzigo wa uzazi badala ya kumsaidia na kumtua (au kuwatua wazazi wake) mzigo wa elimu kwa kumpa vifaa vya elimu au kumlipia karo? Pigo kuu huwa pale mtoto kama huyo ni yatima na ndiye anayetegemewa na mhisani wake kuja kuwaauni ndugu zake, kama anao. Jamani, ubinadamu umeenda wapi?

Sikitiko jingine ni pale watoto wanatekwa nyara na kutumikishwa vitani kupigana na mibabe wa kivita. Hii, bila shaka, ni dhuluma ya hali ya juu kwa watoto na ukiukaji mkubwa wa haki zao. Hebu niambie, mtoto mwenye uzani wa chini ya kilo arubaini kuvalishwa sare nzito za kijeshi na kubebeshwa bunduki au hata makombora ambayo yamewazidi uzani. Unyama ulioje huu?

Pamoja na hayo, licha ya serikali za Afrika kuahidi mara kwa mara kwa vinywa vipana kuwa watalinda haki za kimsingi za kila mtoto katika himaya zao ambayo ni kuhakikisha wanapata lishe bora, wanaishi katika mazingira safi, wanapata elimu bora ya msingi na kupata tiba mwafaka - mamilioni ya watoto barani Afrika bado hawaendi shule kwa sababu ya changamoto mbalimbali. Aidha, wengine lukuki huaga kila mwaka kutokana na utapiamlo na ukosefu wa chakula. Dhana kuwa maradhi sugu yameangamizwa ni ya kupotosha kwani kila mwaka, maelfu ya watoto huaga kutokana na maradhi ya kuambukiza au yale yanayoweza kuzuiliwa au kutibiwa, kama malaria. Mamilioni ya wengine wangali wanaishi katika mitaa ya mabanda na hata kukosa huduma za kimsingi kama maji safi ya matumizi.

Kwa kuwa changamoto hukabiliwa na changamoto, hakuna siku ambapo viongozi wataweza kumaliza utepetevu huu kimiujiza. Muhimu ni kwa kila kiongozi kuitazama jamii yake kwa jicho la ndani na kuweka mikakati ya namna bora ya kuikomboa kutoka katika rima la umaskini, magonjwa na ujinga.

Hili litawezekana tu kwa kuwaona watu wote kuwa na umuhimu katika kuibadilisha jamii wala si kubagua kundi au jamii fulani na kuipendelea nyingine.

- a) Fafanua changamoto zinazomkabili mtoto wa Afrika kwa maneno 80. (Alama 7, 1 ya utiririko)
b) Bainisha mielekeo ambayo viongozi wa Afrika hukazania kuzingatia (maneno 65) (Alama 8, 1 ya utiririko)

3. Matumizi ya lugha: (Alama 40)

- a) (i) Taja na utofautishe sauti mwambatano za menoni.
(ii) Andika neno lenye mfumo ufuatao wa vitamkwa. Nazali ya ufizi + kipasuo cha kaakaa gumu + irabu ya juu nyuma + kizuiwa ghuna cha kaakaa laini + irabu ya chini wastani. (Alama 1)
- b) i) Eleza maana ya kiambishi (Alama 1)
ii) Tumia *ki* katika sentensi kuonyesha hali ya kuendelea kwa kitendo kwa muda (Alama 1)
- c) Onyesha muundo wa silabi katika neno wachanjwao (Alama 1)
- d) Ainisha maneno katika sentensi ifuatayo:-
Shehena ya dawa ilikuwa bandarini (Alama 1)
- e) Tumia mzizi- enye katika sentensi kama kihusishi (Alama 1)
- f) Sahihisha sentensi hii.
Wasichana mabinti mapacha waliozeshwa mume mmoja (Alama 1)
- g) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo.
Amenijibu kwa hasira (Alama 2)
- h) Unda nomino moja kutokana na nomino zozote mbili za Kiswahili sanifu (Alama 2)
- i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali:
Ule mkongojo ulioletewa babu utauzwa na fundi maarufu. (Alama 3)
- j) Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kielezi cha namna kiigizi. (Alama 1)
Sauti ya waimbaji haikusikika ilikuwa imedidimia _____ wageni walipofika jukwaani.
- k) Andika visawe viwili vya nahau:
Fanya inda (Alama 2)
- l) Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha kuwa neno *bunda* ni kitawe. (Alama 2)

- m) (i) Akifisha sentensi ifuatayo kuonyesha usemi halisi: (Alama 1)
Mosi atakuja kesho
- (ii) Onyesha jinsi moja ya matumizi ya alama za dukuduku (Alama 1)
- n) Changanua vipashio vya kisarufi katika kiarifa cha sentensi ifuatayo.
Hawa ndio waliopigana (Alama 2)
- o) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (Alama 1)
(i)Siwa (ii)Kipunye
- p) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia neno badala ya ki ya masharti. (Alama 1)
Ukifika mapema utampata.
- q) Bainisha viwakilishi nafsi katika sentensi ifuatayo: (Alama 2)
Mimi ninataka kumwona mwanariadha aliyepata nishani ya dhahabu.
- r) Eleza maana mbili za sentensi: (Alama 2)
Mali atawaalika wengine.
- s) Geuza sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendata: (Alama 1)
Miyaa maridadi ilisukwa na msusi stadi.
- t) Kanusha sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (Alama 1)
Amekuja hapa
(ii) Andika kwa msembo halisi: (Alama 2)
Tajiri alishangaa kuwa niliweza kuubeba mzigo huo peke yangu.
- v) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kugeuza moja kuwa kishazi tegemezi
i) Majisifu aliingia ukumbini
ii) Sote tulisimama (Alama 1)
- w) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo. (Alama 1)
Mama anapika kutwa kwa sababu ya wageni (Tilia mkazo kwa kinyume)
- x) Tunga sentensi na ubainishe namna mbili za uamilifu wa kundi nomino (Alama 2)
- y) Andika methali inayoafiki maelezo: (Alama 4)
Hakuna chema kisichokuwa na madhara.
4. **Isimujamii (Alama 10)**
- a) Eleza sababu **nne** zinazowafanya vijana kupenda kutumia sheng' katika mawasiliano yao. (Alama 4)
- b) Fafanua jinsi mambo hafuatayo huweza kusababisha kutoweka kwa lugha: (Alama 2)
i) Vita (Alama 2)
ii) Ndoa za mseto (Alama 2)
- c) Huku ukitoa mifano, bainisha mbinu mbili zinazotumiwa kuunda istilahi mpya katika jamii ya leo (Alama 2)

MTIHANI WA PAMOJA WA KUWED - 2016.*(Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)***102/3****KISWAHILI****FASIHI****KARATASI YA 3****JULAI/AGOSTI- 2016****MUDA: SAA 2 ¹/₂****SEHEMU YA A: USHAIRI****Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali ,**

Angawa mdogo, dagaa, amekomaa
 Kaanga kidogo, dagaa, atakufaa
 Kalia kinaya, dagaa h'ondoa njaa

Wa kwako udogo, kijana, sio balaa
 Na sio mzigo, kijana bado wafaa
 Toka kwa mtego, kijana sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana, ukubwa jaa
 Jikaze kimbogo, kijana, acha kukaa
 Chimbua mhogo, kijana, usibung'aa

Na wake udogo, dagaa, ndani hukaa,
 Kuliko vigogo, dagaa, hajaambaa
 Hapati kipigo, dagaa hana fazaa

Maisha si mwigo, kijana, ushike taa
 Sihofu magego, kijana, nawe wafaa
 Kazana kidogo, kijana, kugaagaa

Maswali

- | | |
|---|-----------|
| a) Lipe shairi hili anwani mwafaka | (Alama 2) |
| b) Eleza arudhi zilizofuatwa katika kutunga shairi hili | (Alama 4) |
| c) Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake | (Alama 3) |
| d) Tambua bahari katika shairi hili | (Alama 3) |
| e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari | (Alama 4) |
| f) Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi | (Alama 2) |
| g) Eleza toni la shairi hili | (Alama 2) |

SEHEMU YA B: TAMTHILIA**MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE.****Jibu swali la 2 au 3**

- | | |
|---|------------|
| 2. –Hadi sasa sijaelewa kwa nini hakujitokeza kueleza hali ilivyo.....Huenda hii ni dalili za.....” | |
| a) Eleza muktadha wa dondoo hili. | (Alama 4) |
| b) Fafanua masuala matano yanayofaa kuelezewa kuhusu hali inayorejelewa. | (Alama 10) |
| c) Eleza umuhimu wa anayerejelewa | (Alama 4) |
| d) Bainisha matumizi ya tamathali moja katika dondoo | (Alama 2) |
| 3. Kwa kurejelea tamthilia ya <u>Mstahiki Meya</u> , fafanua vichocho vya migogoro katika jamii ya Cheneo | (Alama 20) |

SEHEMU YA C: RIWAYA**KIDAGAA KIMEMWOZEA - KEN WALIBORA****Jibu swali la 4 au 5**

- | | |
|---|------------|
| 4. —.....wanaume wangewastahi wanawake kidogo,.....dunia ingekuwa pahala pema zaidi pa kuishi. | |
| a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. | (Alama 4) |
| b) Kwa kurejelea wahusika wanne, onyesha jinsi Mtemi Nasaba Bora anavyochangia kumkandamiza mwanamke | (Alama 16) |
| 5. Riwaya ya kidagaa kimemwozea inaonyesha jitihada za vijana kujenga jamii mpya. Thibitisha kwa kutoa mifano | (Alama 20) |

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI
DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

Jibu swali la 6 au 7.

6. –Sisi kama wazazi.....hukabili ana na mengi.....mara nyingi tabia zao hutupiga chenga.....”
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (Alama 4)
 b) Dhihirisha mbinu NNE za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili (Alama 4)
 c) Jadili yaliyomsibu mrejelewa. (Alama 12)
7. a) Jadili matatizo KUMI ya kijamii ukirejelea hadithi –Mwana wa Darubini (Alama 10)
 b) Thibitisha jinsi anwani –Damu Nyeusi” inafiki yaliyomo katika hadithi (Alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

- 8 a) Ni nini maana ya Ulumbi (Alama 2)
 b) Eleza sifa za mtendaji katika ulumbi (Alama 8)
 c) Ngomezi zina majukumu yapi katika jamii yako? (Alama 8)
 d) Toa mifano miwili ya ngomezi katika jamii yako (Alama 2)

JARIBIO LA TATHMINI LA PAMOJA GATUZI NDOGO LA KIRINYAGA MAGHARIBI 2016
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI

102/1

Kiswahili

Karatasi 1

(Insha)

JULAI /AGOSTI 2016

Muda: Saa 1³/₄

1. Umeibuka kuwa mwanafunzi bora kabisa katika kaunti yenu katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne. Andika mahojiano yako na mwana habari.
2. Unyanyasaji wa kijinisia umekithiri katika jamii yetu ya kisasa. Jadili
3. Methali - Akipenda chongo huita kengeza.
4. Andika insha inayomalizia kwa;
... nikapiga darubini nyuma na kuhaha, nikajuta si kidogo. Laiti ningalijua laiti ningalijua.

JARIBIO LA TATHMINI LA PAMOJA GATUZI NDOGO LA KIRINYAGA MAGHARIBI 2016
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI

102/2

KISWAHILI

KARATASI 2

(Ufahamu, Ufupisho, Sarufi na Isimu Jamii)

JULAI /AGOSTI 2016

MUDA: 2 ½

1. UFAHAMU.(alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

Imefika wakati ambapo kila mmoja lazima ajiulize swali kuhusu tuelekeapo kama jamii, mustakabali wa kizazi cha sasa ni upi?

Nauliza swali kuhusiana na misururu ya visa ambayo kwa kweli imebua hofu na wasiwasi kuhusu msingi wa kimaadili miongoni mwa vijana wetu. Kuna hatari ijapo; mbaya sana. Ni hali ambayo huenda ikatusahaulisha msingi wa tulikotoka na tuelekeapo.

Kwanza, ni kisa cha Alhamisi usiku ambapo zaidi ya vijana 300 walinaswa katika nyumba moja katika mtaa wa Phenom, Nairobi katika kile kiliaminika kuwa —hfla ya ukosefu wa maadili”. Kisa hicho kilikujia siku chache baada ya serikali kupiga marufuku hafla moja ya burudani na ukosefu wa maadili maarufu —Project X” ambapo vijana walikuwa wakitarajiwa kuhudhuria.

Kulingana na taarifa za kanuni za tamasha hiyo, vijana walitakiwa kuvaa mavazi mafupi ambayo yanaonyesha sehemu zao za mwili kwa wazi. Taarifa zilisema kuwa washiriki pia wangeruhusiwa kucheza densi wakiwa uchi kama mojawapo ya kanuni za burudani. Isitoshe, kisa hicho kinakujia baada ya vingine vingi, ambapo vijana wamenaswa na maafisa wa polisi wakijiburudisha kwa vileo katika klabu nyakati za usiku. Vile vile wanafunzi wengi wamenaswa wakishiriki katika vitendo vya ukosefu wa maadili. Baadhi ya wanafunzi hao huwa chini ya miaka 18! Jijini Nairobi visa hivyo vimekuwa kama —hli za kawaida”.

Yasikitisha kuwa nyakati za wikendi hutakosa kuona kila aina ya vioja na viroja, hasa katika maeneo ya mijini. Ni nyakati hizi ambapo mabinti huenda katika vituo vya burudani wakiwa wamevaa kila aina ya mavazi. La kushangaza ni kuwa, mabinti hao hushindana kuhusu mbinu za —konyesha” uchi wao kwa njia mbalimbali. Kwa haya yote, kile kinadhihirika ni kuwa jamii yetu inaelekea kubaya tu katika safari ya kifo. Safari hii huenda ikatufikisha Jehanamu ambayo kuna uwezekano wa kutojikomboa. Kilicho wazi ni kwamba msingi wetu wa kimaadili umetererereka kiasi cha kutorekebika kabisa. Nchi imegeuka jaa la mwigo wa tamaduni zote za kimagharibi. Kwa mfano, tamasha ya Project X ni mwigo wa filamu maarufu ya wanafunzi wa shule za upili iliyorekodiwa nchini Amerika kwenye filamu hivyo, wanafunzi hao wanajihusisha katika kila aina ya uovu wa kimaadili, ufasiri wake mkuu ukiwa ni burudani kwa msingi wa tamaduni za kimagharibi.

Kikweli, huu si msimamo wa tamaduni za Kiafrika. Huu si msingi wetu wa kimadili hata kidogo! Huu ni mwigo wa kishetani ambao lengo lake ni kuizamisha jamii yetu katika lindi la mgogoro wa kitamaduni na kimaadili.

Mawali.

1. Maadili ya vijana yamezorota. Kwa mujibu wa taarifa hii thibitisha kauli hii. (alama 4)
2. Ni nini asili ya projct X? (alama 2)
3. Nyakati za wikendi hutakosa kuona kila aina ya vioja na viroja. Fafanua. (alama 2)

4. Mwandishi ana maana gani anaposema visa hivyo vimekuwa kama hali za kawaida. (alama 1)
5. Mwandishi ana msimamo upi kuhusu tamaduni za kimagharibi. (alama 2)
6. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika kwenye kifungu. (alama 4)
- (i) Kupiga marufuku
(ii) Mustakabali
(iii) Umetetereka
(iv) Filamu
2. **MUHTASARI** (alama 15)

Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata.

Je, mtazamo hasi ni nini? Huwa na athari gani kwa binadamu? Mtazamo hasi ni kukata tamaa, kutamauka kuhusu hali, mtu au jambo fulani. Ni hisia ya kutotaka kushiriki wala kuhusishwa na jambo au hali fulani. Mtazamo huu ndio huwafanya wanafunzi wengi kuchukua au hata kudunisha baadhi ya masomo na walimu wanaoyafundisha. Licha ya wengi kuwa na mtazamo huu, kwa kweli huwa hawatambui. Asilimia kubwa ya wanaotambua hutatizika kujikwamua kutoka katika hali hii.

Inakadiriwa kwamba mtu wa wastani huwa na takribani mawazo elfu sitini ya kibinafsi kwa kila saa 24. Asilimia 95 ya fikra hizi huwa sawa na siku iliyotangulia, na asilimia 80 ya fikra hizi zilizorudiwa huwa hasi. Isitoshe, fikra hizi nyingi hutokea bila mtu mwenyewe kutambua na huwa ni mazoea. Hii ina maana kwamba watu wengi hawana ufahamu wa athari za fikra hizi maishani mwao.

Mitazamo hasi ina vyanzo na pia suluhu. Mwanzo kabisa ni imani potovu. Hiki ndicho chanzo cha mitazamo hasi. Kushikilia imani potovu kuhusu maisha pamoja na matukio fulani maishani hujenga mtazamo hasi. Unayaona maisha kwa macho ya imani zako na iwapo imani hizo ni potovu, basi hutayathamini maisha yako ili kukabiliana na hali hii, sharti kwanza ubadili imani yako. Uamini kwamba mabadiliko yanaweza kutokea na uchukue hatua ya kuanzisha mabadiliko hayo maishani mwako. Unahitaji kuepuka fikra hasi zinazoambatana na maisha yako ya awali na kulithamini kila tukio maishani kama tukio huru; Lisilo na uhusiano na yaliyowahi kukutamausha.

Kujikwamua kutoka katika imani duni unahitaji kuibuka na idadi kubwa ya imani chanya kuliko zilizo hasi kuhusu hali mahsusi. Baada ya hilo, zikabili imani zako potovu moja baada ya nyingine huku ukijiuliza endapo imani hizo ni kweli na endapo zina mashiko. Tumia dakika tano hivi kila siku kushadidiafikra chanya inayokinzana na ile inayokudidimiza. Ukifanya hivi kwa takriban siku thelathini imani yako itaanza kuchukua mkondo unaofaa. Familia yako na rafiki unaoandamana nao huathiri pakubwa hisia zako. Wakiwa na mtazamo hasi huweza kukushawishi ukaanza kuhisi wanavyohisi na kuyaona mambo kwa mtazamo wao. Kukabiliana na hali wapaswa kudhibiti hisia zako.

Tawala namna unavyohisi na kukabiliana na hali mbalimbali bila kuathiriwa na wandani hawa. Epuka wandani wa aina hii kadri inavyowezekana, ikiwezekana, jitenge nao ili ujifunze kuwa na uhuru wa kufanya maamuzi yako binafsi bila kuathiriwa nao. Unapaswa kupunguza ushirika hata na jamaa zako wanaokuingiza katika hali ya kutamauka. Punguza muda wa kukaa nao hasa wanapogeukia mkondo huu wa kukutatiza tamaa.

Mazingira hasi ni kizingiti kingine. Pengine huoni ukuruba baina ya maisha yako na mazingira unamokulia au unamokaa. Ukweli ni kwamba, huenda umedumu katika mazingira hayo na kuyazoea hata ukafikiri huwezi kuyabadilisha. Kadri unavyohisi huna uwezo wa kuyabadilisha ndivyo unajizamisha zaidi mtazamo hasi. Ili kukabiliana na hali hii, unahitaji kuelewa kwamba fikra zako au za watangulizi wako ndizo silikuingiza katika mazingira haya. Kwa hivyo, unapaswa kubadili mkondo wa fikra zako na kuanza kujaribu mazoezi ambayo umekuwa ukiyaona kama usiyoyaweza. Hatua kwa hatua utagundua panapo jitihada na uelekezi unaofaa kwamba mazoezi hayo yamekuwa mepesi na hivyo kukubakikishia kuyabadilisha mazingira yako.

unapojikuta ukilalamika jinsi ulivyokerwa na hali fulani, hii ndiyo sababu hasa ya kuwa na mtazamo hasi kuhusu hali hizo. Inaweza kukuwia vigumu kulikubali hili lakini kadiri utakavyolikubali mapema ndivyo utayaboresha maisha yako mapema. Kulalamika tu kutakudumisha katika hali zisizokuridhisha. Kwa hivyo, ili uyabadilishe maisha yako sharti ukome kulalamika tu kutakudumisha katika hali zisizokuridhisha. Kwa hivyo, ili uyabadilishe maisha yako sharti ukome kulalamika na kuanza kujikwamua toka kwenye hali hizo. Katika kufanikisha jambo lolote jema sharti viwepo vizingiti njiani. Mtendaji wa jambo lolote jema liwalo ana jukumu la kuibuka na mikakati mwafaka ya kuvikabili vizingiti hivi ili afanikishe ndoto yake. Hii ndiyo sababu unapaswa kuchukua hatua kutokea sasa ili kupanga na kutekeleza mikakati itakayoupindua mtazamo wako hasi uwe chanya. Kwa jinsi hii utayabadilisha maisha yako yawe ya kuridhisha zaidi na kuwa kielelezo kwa wengi waliotamaushwa na mitazamo hasi.

Maswali.

- (a) Fupisha aya ya kwanza. (maneno 45-50) (alama 6, 1 utiririko)
- (b) Eleza namna ya kukabiliana na mitazamo hasi. (maneno 70 - 80) (alama 9, utiririko 1)
3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)
- (a) Andika sifa mbilimbili bainifu za sauti. (alama 2)
- /gh/
/a/
- (b) Bainisha silabi katika neno lifuatalo. (alama 1)

- nyweshwa
- (c) Tofautisha kwa kueleza maneno ya istilahi zifuatazo. (alama 2)
 (i) Silabi funge
 (ii) Silabi mwambatano
- (d) Tunga sentensi moja ukitumia maneno yafuatayo ili kutofautisha maana. (alama 2)
 Buda
 Bunda
- (e) Kwa kutolea mfano eleza maana ya mofimu Huru. (alama 2)
- (f) Ainisha uamilifu wa viambishi katika neno lifuatalo. (alama 3)
 Alimlilia
- (g) Bainisha aina za nomino zilizotumika katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
 Wema alimpa mtoto yule maji ya baraka.
- (h) Andika katika umoja. (alama 2)
 Ile ya kujengea haijaletwa
- (i) Andika kulingana na maagizo. (alama 1)
 Sherehe ilikuwa na walakini kwa kukosa mpambe.
 (Tumia neno lingine badala ya walakini)
- (j) Tunga sentensi ukitumia kihisishi cha mwitikio. (alama 1)
- (k) Andika kitenzi kifuatacho katika hali ya kuamrisha kwa wingi. (alama 1)
 (-la).
- (l) Kanusha katika wakati ujao hali timilifu. (alama 2)
 Bwana arusi alivaa suti ya kupendeza.
- (m) Unda kitenzi kutokana na nomino; (alama 1)
 abiria
- (n) Eleza maana ya kishazi. (alama 1)
- (o) Bainisha aina za vishazi vilivyotumika katika sentensi hii; (alama 2)
 Kule alikoenda alilakiwa vizuri.
- (p) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizobanwa. (alama 2)
 Fundika (kitendua)
 nata (kutendesha)
- (q) Tunga sentensi yenye Fungu tenzi lenye muundo; (alama 2)
 Ts + T + E
- (r) Andika methali inayotumiwa kutuhimiza kuthamini vitu viliyo karibu kwani ndivyo vitufaavyo wakati wa janga. (alama 1)
- (s) Chagua kwa muundo wa jedwali. (alama 4)
 Waliamua kusafiri usiku ingawa walitahadharishwa.
- (t) Kwa kutoa mifano eleza matumizi mawili ya alama ya kinyota. (alama 2)
- (u) Andika katika ukubwa wingi. (alama 2)
 Njia hii inafaa zaidi kuliko ile.
- (v) Tunga sentensi ukitumia 'na' kama; (alama 2)
 (i) Kuunganisha
 (ii) Kihusishi
4. **ISIMU JAMII.** (alama 10)
- (a) Nini maana ya dhana ya usanifishaji wa lugha. (alama 2)
- (b) Nchi za Afrika Mashariki ziliunda kamati ya lugha ili kusanifisha na kukuza Kiswahili. Eleza malengo **manne** makuu na mafanikio yake katika juhudi za usanifishaji. (alama 8)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA GATUZI NDOGO LA KIRINYAGA MAGHARIBI 2016
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI

102/3

KISWAHILI

KARATASI 3

FASIHI

JULAI / AGOSTI 2016

MUDA: 2¹/₂**SEHEMU A: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE.**1. **Swali la kwanza (Lazima)**

–Kero hizi na dhara zinamfanya kuthamini zaidi utu wake”

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Wafrika hupitia changamoto nyingi sana wakiwa masomoni ughaibuni. Thibitisha. (alama 4)
 (c) Onyesha jinsi ukatili unavyojitokeza kwa kurejelea hadithi zifuatazo. (alama 12)
 (i) Kanda la usufi
 (ii) Shaka ya mambo
 (iii) Mwana wa darubini
 (iv) Ndoa ya Samani.

SEHEMU B: RIWAYA**KEN WALIBORA - KIDAGAA KIMEMWOZEA.****Jibu swali la 2 au la 3.**

2. –Kwa nini mnaifunga mnyororo ile doggy mgonjwa? Mbona msiiwache free”.
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Onyesha jinsi wahusika riwayani wamefungwa minyororo. (alama 6)
 (c) Minyororo inayorejelewa katika (b) hapo juu ilifunguliwaje? (alama 10)
3. Kufariki kwa kitoto Uhuru ni jazanda inayoashiria hali halisi ya mambo riwayani. Jadili. (alama 20)

SEHEMU C: TAMTHILIA**TIMOTHY AREGE MSTAHIKI MEYA.****Jibu swali la 4 au la 5.**

4. –Huu ni ukoloni mamboleo”
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Eleza umuhimu wa msemewa katika tamthilia hii. (alama 8)
 (c) Jadili namna ukoloni mamboleo unavyojitokeza katika tamthilia. (alama 8)
5. Jumuiya ya ‘Mstahiki Meya’ inaafiki kwa kiasi kikubwa jamii ya kisasa. Thibitisha. (alama 20)

SEHEMU D: USHAIRI.**Jibu swali la 6 au la 7.**

6. **Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali.**
1. Ajaye kisimani mbele hunywa maji maenge,
 Asinywe yalo na vunju,
 Yakampa kigegezi,
 Yakamkibua roho akaona na kinyaa,
 Awali ndio awali, awali mbovu hamna.
2. Kiwa utalimatia.
 Utayaramba makombo,
 Utadata vitu cheche,
 Kisomo chenye dhamana kikakupa kisogo,
 Inajuzu ujihimu
 Mwanafuu darasani,
 Urauka po mapema,
 Katu hutayaramba makombo,
 Hutakosa kisebeho.
3. Dereva hata utingo,
 Natija ni asubuhi,
 Wateja utawawahi,

Wasaa kuzingatia,
Uwafikishe kazini,
Kwa wasaa ufao,
Wasije wakateteshwa,
Na bosu wao kazini,
Nao wakakuapiza.

4. Na ewe mwanazaraa,
Mpini uukamate,
Kabla jua kuwaka sana,
Majasho kutiririsha mwilini,
Yang'oe yote magugu,
Kutoka kwa lako konde.

5. Mhadimu mwenye ajizi,
Yakujuza ujihimu,
Ununue na maziwa,
Majogoo uyawahi mapema,
Usije ukayadata,
Chai mkandaa ukaandaa,
Wateja wakuambae mithili ya ibilisi.

Maswali

- (a) Eleza nasaha yoyote inayotolewa kwa wafanyakazi wowote watatu kwenye shairi. (alama 3)
(b) Taja sifa zozote za kimuundo zilizotumiwa na mtunzi. (alama 3)
(c) Eleza toni ya mshairi. (alama 3)
(d) Nafsi nenewa anahimizwa kufanya nini. (alama 2)
(e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (alama 4)
(f) Toa mifano miwili ya uhuru wa mshairi. (alama 3)
(g) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumiwa kwenye shairi. (alama 3)
(i) Maji maenge
(ii) Natija
(iii) Majogoo

7. Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali.

1. Wasiwasi n'ondokeya, ondoka enenda zako,
Ondoka andama ndiya, nondosheya uso wako,
Ondoka wanisikiya, ziwate jeuri zako,
Jishughulishe na yako, yangu wayatakiyani?
2. Wasiwasi siitaki, suhuba yako si nzuri,
Haistahamilikii, uovu umekithiri,
Inganyoshwa hainyoki, ikukutene kikiri,
Sikati yako shari, enda zako wasiwasi.
3. Huna kazi ufanyayo, ela kuwafitinisha,
Viumbe na zao nyoyo, vitina kuwagotanisha,
Hiino ndio kaziyo, yenye kukufurahisha,
Ni kazi isiyokuchosha, mno umeizoeya.
4. Mara waja na habari, mambo yalivyo nyumbani,
Ati mambo si mazuri, mambo yote tatashani,
Wanitaka nifikiri, usemayo ni yakini,
Nisononeke moyoni, upate kufurahika.
5. Au mara hunijiya, na kingine kisahani,
Kuhusu zao afiya, hao waliyo nyumbani,
Huwa husishi nambiya, hali zao taabani,
Zingawa wakati gani? Ni zako au ni zao?
6. Na mara kuja mambiya, nitakapotoka humu,
Na kwamba yaningojea, nde maisha magumu,
Uliloni kusudiya, ni kunitiya wazimu,
Kama ndiyo yako hamu, basi unshatahayari.

7. Huo urafiki wako, wa kuja niungulisha,
Kunipa masikitiko, na mateso yasokwisha,
Kutoka leo ni mwiko, sitautaka maisha,
Kamwe hutanikondesha, tokomeya mwana kwenda.

Maswali

- (a) Eleza ujumbe uliojitokeza katika shairi hili. (alama 1)
 (b) Fafanua muundo wa ubeti wa tatu. (alama 3)
 (c) Eleza aina ya shairi hili. (alama 1)
 (d) Fafanua arudhi za utunzi alizozingatia mshairi. (alama 3)
 (e) Eleza toni ya mshairi. (alama 2)
 (f) Andika ubeti wa tano katika lugha ya kinathari. (alama 4)
 (g) Eleza mifano mitatu ya uhuru wa mshairi. (alama 3)
 (h) Eleza maana ya misamiati ifuatayokama ilivyotumika katika shairi. (alama 3)
 (i) ndiya
 (ii) kisahani
 (iii) nde

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Eleza maana ya maghani. (alama 2)
 (b) Taja sifa nne za maghani. (alama 4)
 (c) Fafanua mbinu **nne** ambazo hutumika kuzua misimu. (alama 8)
 (d) Eleza vikwazo mbali mbali vinavyotatiza ukuaji wa Fasihi Simulizi. (alama 6)

GATUZI NDOGO LA KIRINYAGA MAGHARIBI 2016
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KISWAHILI
102/2

1. Ufahamu.
- (a) (i) Vijana walitarajiwa kuhudhuria hafla moja ya burudani na ukosefu wa maadili maarufu Project X iliyopigwa marufuku na serikali.
(ii) Vijana walitakiwa kuvaa mavazi mafupi yaliyoonyesha sehemu zao za mwili kwa wazi.
(iii) Washiriki wangeruhusiwa kucheza densi wakiwa uchi kama mojawapo ya kanuni za burudani.
(iv) Visa vya vijana kunaswa na maafisa wa polisi wakijiburudisha kwa vileo katika klabu nyakati za usiku. (hoja 4 x 1 = al 4)
- (b) Filamu maarufu ya wanafunzi wa shule za upili✓ iliyorekodiwa nchini Amerika, ambapo wanajihusisha katika kila aina ya uovu✓ wa kimaadili (hoja 2 x 1 = al 2)
- (c) Ni nyakati hizi ambapo mabinti huenda katika vituo vya burudani wakiwa wamevaa kila aina ya mavazi. Mabinti hushindana kuonyesha uchi wao kwa njia mbalimbali.✓✓ (hoja 2 x 1 = al 2)
- (d) mazoea, desturi (hoja 1 x 1 = al 1)
- (e) tamaduni za kimagharibi zinazua mgogoro wa kimaadili.✓ Ni kinyume na msimamo wa tamaduni za Kiafrika.✓ (hoja 2 x 1 = al 2)
- (f) Kukatazwa kuzuiliwa
Maisha ya baadaye
Umeharibika
Sinema, picha (al 4)
2. Muhtasari.
- (a) (a) Mtazamo hasi ni kutamauka kuhusu hali, mtu au jambo fulani.✓
(b) Ni hisia ya kutotaka kushiriki wala kuhusishwa na jambo au hali fulani.✓
(c) Mtazamo huu huwafanya wanafunzi kuchukiana.✓
(d) Kudunisha baadhi ya masomo na wanaoayafundisha.✓
(e) Walio na mtazamo huu hawatambui.✓
(f) Wanaotambua hutatizika kujikwamua kutoka hali hii.✓
- (b) (a) Kuibuka na idadi kubwa ya imani changa kuliko hasi.✓
(b) Kukabili imani potovu moja baada ya nyingine.✓
(c) Tumia dakika tano kila siku kushadidia fikra chanya.✓
(d) Inayokinzana na inayokudidimiza.✓
(e) Kudhibiti hisia zako unapokabiliana na familia yenye mtazamo hasi.✓
(f) Tawala namna unavyohisi na kukabiliana na hali mbalimbali bila kuathiriwa na wandani.✓
(g) Kupunguza ushiriki na jamaa wanaokuingizakatika hali ya kutamauka.✓
(h) Kubadili mkondo wa fikra zako na kuanza kujaribu.✓
(i) Mazoezi ambayo umekuwa ukiyaona kama usiyoyaweza.✓
(j) Kukoma kulalamika na kuanza kujikwamua toka kwenye hali zisizokuridhisha.✓
3. Mwongozo wa matumizi ya lugha.
- (a) gh/ - Kikwamizo
- hutamkiwa kwenye kaaka laini✓
- sauti ghuna✓
/a/ - irabu ya kati chini✓
mdomo hutandazika✓
- (b) nywe-shwa(al 1)
- (c) Silabi funge - Silabi inayoishia kwa konsonanti.✓
Silabi mwambatano - Silabi ambazo zinapatikana kwa kuweka pamoja zaidi ya konsonanti moja.✓ (2 x 1 = 2)
- (d) buda - mwanaume aliyezeeka sana ndovu mzee asiyekuwa na pembe mtu asiye na meno
bunda - feli ama shindwa mtihani
- fungu la kitu
Mwanafunzi atunge sentensi moja akidhihirisha maana iliyo hapo juu. (hoja 1 x 2 = al 2)
- (e) Mofimu iliyoundwa kwa neno kamili. Neno hilo hujitosheleza kwa kuwa haliwezi kugawika katika vijishemu vidogo zaidi bila kupoteza maana. Mwalimu kuhakiki maelezo (al 2)
- (f) A - kiambishi kiwakilishi ch anafsi III - yeye✓
li - kiambishi kiwakilishi cha wakati (uliopita)✓
m - kitendewa✓
li - mzizi
Li - kauli✓
a - kiishio✓
- (g) Wema - Nomino ya pekee✓
mtoto - Nomino ya kawaida / Jumla✓
maji - Nomino ya wingi✓
baraka - Nomino dhahania✓

- (h) ule wa kujengea haujaletwa. (hoja $1 \times 2 = 2$)
- (i) Sherehe ilikuwa na dosari / ila kwa kukosa mpambe (al 1)
- (j) Atumie vihishishi kama
Bee! Labeka!, Naam! ($1 \times 1 = al 1$)
- (k) kuleni ($1 \times 1 = al 1$)
- (l) Bwana arusi hatakuwa amevaa suti ya kupendeza ($1 \times 2 = al 2$)
- (m) abiri ($1 \times 1 = al 1$)
- (n) Kishazi ni neno au kifungu cha maneno chenye kiima na kiarifa au kiarifa pekee ambalo huwa ni sehemu ya sentensi kuu. ($1 \times 1 = al 1$)
- (o) Kule alikoenda - kishazi tegemezi alilakiwa vizuri - kishazi huru ($2 \times 1 = al 2$)
- (p) Fundua
Nasa ($2 \times 1 = al 2$)
- (q) Mtahini kukadiria jibu km: atakuwa amelala kitandani ($1 \times 2 = al 2$)
- (r) Fimbo ya mbali haiui nyoka.
Kamba ya mbali haifungi kuni
Hamadi kibindoni silaha mkononi. (yoyote $1 \times 1 = 1$)
- (s)
- | | | | | | |
|------|----|---|----|----|--|
| | | S | | | |
| S1 | | U | S2 | | |
| KN | KT | | KN | KT | |
| Ts T | E | | T | | |
- O Waliamua kusafiri usiku ingawa O walitahadharishwa ($1 \times 1 = al 1$)
- (t) (i) Kuonyesha kuwa maendeleo ya neno fulani yana makosa. ✓
(ii) Kuashiria kuwa mpangilio wa maneno katika sentensi una makosa. ✓
(iii) Kuashiria msomaji kuhusu jambo fulani ambalo maelezo yake yanapatikana sehemu ya chini ya ukurasa huo. ✓
(iv) Kuonyesha kuwa sentensi au fungu la maneno lina makosa ya kisarufi. ✓
- (u) Majia haya yanafaa zaidi kuliko yale. ($1 \times 2 = al 2$)
- (v) Kiunganishi : Mama na baba wanalima
(kiunganishi cha kuongeza)
Kihusishi : Walipigwa na wezi (kihusishi cha mtenda) ($2 \times 1 = 2$)

4. Isimu jamii

- (a) Usanifishaji ni uamuzi wa kuchagua lugha moja au mojawapo ya lahaja za lugha kufanyia marekebisho ya kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi ili iweze kutumika katika shughuli rasmi.
- (b) Malengo ya kamati.
- (i) Kusanifisha maandishi na kuhakikisha mtindo mmoja unazingatiwa. ✓
(ii) Kuchapisha vitabu. ✓
(iii) Kuwahimiza na kuwasaidia maandishi wa Kiswahili. ✓
(iv) Kuidhinisha vitabu vya kianda na vya ziada vinavyohitajika kufundisha shuleni. ✓
(v) Kuwapasha maandishi, habari zozote zile kuhusu njia tofauti au mitindo ya kusomeshea katika kila nchi. ✓
(zozote $4 \times 1 = 4$)

Mafanakio ya kamati.

- (i) Vitabu vingi vya sarufi, kilimo na hadithi vilichapishwa kwa mfano: Modern Kiswahili Grammar.
(ii) Tafsiri ilifanywa na vitabu kuchapishwa kwa Kiswahili kwa mfano: Kisima chenye Hazina.
(iii) Kamusi tatu zilichapishwa: Kiswahili - Kiswahili, Kiswahili - Kiingereza h.k
(iv) Vitabu vingi vya kufundishia Kiswahili viliidhinishwa. ($4 \times 1 = 4$)

Adhibu - Isimu Jamii Makosa 6 ya hijai $\times \frac{1}{2} = 3$

Makosa 6 ya sarufi $\times \frac{1}{2} = 3$

MTIHANI WA TATHMINII YA PAMOJA WILAYA YA MAARA**102/1****KISWAHILI****INSHA****Karatai ya 1**

1. Ulevi umekithiri nchini. Wewe kama mkurugenzi wa shirika la kupambana na vileo, andika hotuba utakayoisoma katika mkutano wa hadhara kuhusu madhara ya ulevi.
2. Kupunguza mishahara ya watumishi wa umma ni hatua mwafaka kama maendeleo ya nchi yatafanikiwajadili.
3. Akufukuzaye hakwambii toka.
4. Andika insha itakayoishia kwa maneno haya.
5.unyama umewatoka wanyama na kuwaingia watu!

MTIHANI WA TATHMINII YA PAMOJA WILAYA YA MAARA**102/2****KISWAHILI****Karatai ya 2****1. UFAHAMU (alama 15)**Soma taarifa inavofuata kisha uyajibu maswali

Ukosefu wa ajira hususan miongoni mwa vijana ni tatizo ambalo usugu wake umefikia kima kisichostahimilika tena. Ingawa limejitokeza kama tatizo la ulimwengu mzima lakini katika mataifa ya ulimwengu wa tatu, hasa barani Afrika, limekolea zaidi. Ni kweli kwamba tatizo hili si geni ulimwenguni kwani lilikuwepo miaka michache baada ya uhuru wa nchi nyingi za Kiafrika lakini wakati huo mhusika mkuu aliyelaumiwa kwa ukosefu wa ajira ulikuwa ukosefu wa elimu.

Katika ulimwengu wa sasa mambo yamebaidika kabisa kama mbingu na ardhi kwani ukosefu wa elimu sio sababu ya ukosefu wa ajira. Ukweli ni kwamba kuwa na elimu ndiyo sababu ya kukosa ajira.

Serikali za mataifa mengi zimechukua hatua mbali mbali ili kukabiliana na tatizo hili, si hoja kama baadhi ni za kutapatapa mithili ya mfa maji ambaye hushika maji. Miongoni mwa hatua hizi ni pamoja na kuboreshamazingira ya uwekezaji ili vitega uchumi viongezeke na hivyo kubuni nafasi za ajira. Kupanua fursa za INMMR. ngazi zote na kuhimiza mafunzo ya ujasiriamali na ufundi ni hatua nyingine. Vile vile serikali zingine zimebuni mipango inayolenga kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe.

Waama, serikali zingine zimechukua hatua za kijasiri kwa kulegeza masharti ya uwekezaji kwa wawekezaji wa kigeni ili kuwavutia waanzishe miradi katika nchi zao kwa tamaa kwamba watabuni nafasi za ajira katika nchi husika. Changamoto moja ambayo imetokea ni kwamba baadhi ya wawekezaji hawa wanatengea wananchi wa nchi walizotoka kazi za kitaalamu na zenye malipo bora huku wenyeji wakiachiwa zile zinazoitwa 'kazi za mikono' tu. Wanawapuza wataalamu na wasomi walio katika mataifa hayo. Tuisahau pia kuwa baadhi ya wawekezaji hupelekwa katika mataifa wanayowekeza tabia na mienendo inayokinzana na maadili ya nchi pokezi.

Tabia kama ubasha au usenge na ndoa za jinsia moja zimenasibishwa na tamaduni ngeni miongoni mwa Waafrika. Katika mkumbo huu ni tatizo la matumizi ya mihadarati ambalo sasa limefuzu kujiunga na majanga mengine ya kimataifa kama ukimwi. Ukweli mchungu ni kwamba maovu haya yametokana na ukarimu wa mataifa yenye tamaa ya kutaka wawekezaji wa kigeni ambao pamoja na kuwekeza, wao huja na 'yao'. Na kwa sababu mkata hana lake, mataifa pokezi yamehiari kuwapokea wawekezaji wa kigeni wakibeza athari mbaya zinazoletwa na watakuja **kutahamaki** baadaye kwamba mgeni kumpokea kumbe ni kujitongea.

Suluhisho lingine, ambalo huenda ni bora zaidi, ni kuwawezesha vijana kujiajiri. Jambo hili linawezekana, mathalani endapo serikali itatenga hazina maalum katika bajeti yake ili kuwapa vijana mikopo yenye masharti nafuu ili waanzishie miradi yao. **Itajuzu** misaada hii itolewe kwa makundi ya vijana yaliyoandikishwa kama tahadhari moja ya kukabiliana na ufujaji wa pesa unaoweza kutokea misaada ikitolewa kwa watu binafsi. Vile vile kutolewa kwa mafunzo kuhusu usimamizi kwa vijana kabla ya kukabidhiwa pesa hizi itakuwa hatua nyingine ya kuepukana na ubadhirifu.

Isitoshe, ustawishaji wa kilimo unaweza kutoa suluhisho lingine kwa tatizo la ukosefu wa ajira. Sharti vijana wahamasishwe ili washiriki katika kilimo ambapo watazalisha maii na kubuni nafasi za ajira katika nchi zao. Hii itarahisishwa kwa kufundisha somo la **zaraa** katika shule kama somo la lazima.

Hakuna shaka kwamba juhudi hizi, na zingine ambazo hazijashughulikiwa katika makala haya, zikizingatiwa, usugu wa ukosefu wa ajira utageuzwa na kuwa tatizo tu!

Maswali

- a) Kwa nini mwandishi amerejea ukosefu wa ajira kama tatizo sugu. (alama2)
- b) Taja hatua nne ambazo zimechukuliwa na mataifa mbalimbali ili kulitatua tatizo la ukosefu wa ajira. (alama 4)

- c) Majilio ya wawekezaji wa kigeni yanaweza kuchukuliwa kama hali ya 'kula sumu ili kupata kuishi'. Thibitisha jinsi 'sumu' inavyoahihirika kwa kurejelea mifano miwili katika makala haya (alama 4)
- d) Eleza maana ya msamiati ufuatao katika muktadha wa makala haya. (alama3)
- a) Kutahamaki
- b) Itajuzu
- c) Zaraa

UFUPISHO (alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Wataalamu wa maswala ya kielimu wanadai kuwa huenda nchi ikalaumiwa kwa kuendeleza mfumo wa elimu unaozingatia maslahi ya wakwasi na kuwapuuza wachochole. Mfumo huu wa elimu umezua mfumo mwingine wa kijamii ambapo watoto wa wenye hadhi wanapata elimu bora kuliko watoto wa maskini. Pengo baina ya haya matabaka linazidi kupanuka kama ardhi na mbingu.

Watoto kutoka jamii hohehahe wanasomea katika shule za umma zisizo na lolote wala chochote na watoto wa kifahari wanasomea katika shule za kibinafsi zilizo na vifaa mufti na mazingira faafu. Mfumo wa jinsi hii ni wa kuitia jamii kitanzi kwa sababu ya kuzulca kwa matabaka yanayohasimiana.

Katika nchi ambapo asilimia sitini ya watu inaishi katika hali ambayo ni chini ya dola moja kila siku, watoto wengi huenda shuleni bila kula chochote na hushinda hivyo kutwa nzima na wasing'amue chochote darasani. Walimu wao nao hawana ilhamu au kariha ya kufanya kazi kwa sababu mazingira ya kikazi ni mabovu na huenda shuleni shingo upande kama wakulima bila pembejeo. Madarasa yao ni mabanda na wengine husomea chini ya miti ambayo inaweza kukatwa wakati wowote na wachoma makaa waliokosana na mazingira. Unapowatazama watoto hawa, kile kinachoitwa sare ya shule kinakirihisha na kuyaudhi macho. Ni matambara yaliyosheheni viraka vya kila aina ama katika mseto wa

Tatizo hili limekuwa nyeti hasa kutokana na utandawazi na mfumo wa soko huru ambao unaruhusu shule za kibinafsi kuendeshwa kama mashirika ya kibiashara. Karo inayolipwa katika shule hizi ni ya kibiashara, majengo na vifaa ni vya kibiashara, walimu ni wa kibiashara, ilimradi kila jambo lalenga maslahi ya kibiashara ya walalahoi. Hapo ndipo chimbuko la makabila mawili maarufu nchini yaani, matajiri walamba vidole na maskini wanaostakimu madongo-kuinama.

Uchunguzi umethibitisha kwamba zaidi ya asilimia sitini ya wanafunzi wanaojiunga na shule za kitaifa hutoka katika shule za kibinafsi zinazomilikiwa na matajiri. Mbinu ya wizara ya elimu ya kugawa nafasi kwa njia ya haki katika shule za kitaifa haijafua dafu kwa sababu matajiri wajanja huwasajili watoto wao kufanyia mtihani katika shule zisizokuwa na ushindani mkubwa zilizomo mashambani. Kwa kufanya hivyo watoto wa maskini huwa wamefungiwa njia kote kote na kuporwa haki yao. Ama kweli, mwenye nguvu mpishe kwani dau la mnyonge haliendi joshi.

Wanafunzi katika shule za kibinafsi hufunzwa katika makundi madogo madogo ambayo humwezesha mwalimu kushughulikia mahitaji ya kibinafsi ya kila mtoto. Wazazi wao pia huwaajiri walimu wakati wa mapumziko ili kugongomeza au kushadidia mada ambazo hawakuzielewa vizuri shuleni. Upeo wa lugha wa watoto hawa hauwezi kulinganishwa na wa wenzao kwa sababu shule zao zina maktaba za kisasa, vifaa vya kisasa na vitumeme na hufunzwa teknolojia za kileo kuhusu mawasiliano. Watoto hawa huandaliwa ziara za kielimu ili kutanua uelewa wao wa mambo na vile vile hualikiwa watu wanaosifika katika jamii ili kuwahutubia shuleni mwao kuhusu mada mbali mbali. Wawasilishaji hawa huwa na kielelezo tosha kwa watoto hawa. Mzazi aliyesoma hujua umuhimu wa elimu na hivyo basi huandaa mikakati mahususi ili kumfaulisha mwanawe kinyume na wazazi wakata.

Ni bayana kuwa iwapo hivi ndivyo mambo yalivyo basi hata vyuo vikuu vitakuwa himaya ya watoto wa matajiri huku watoto wa kimaskini wakisubiri kuajiriwa nao kama walinzi na matopasi. Sera za elimu nchini haziwezi kufanikiwa pale ambapo raslimali muhimu zinatengewa watu wachache katika jamii. Watoto wa waunda sera hizi husomea shule ambazo hufuata mifumo ya kimataifa ambayo haina mkuruba na yetu hafifu. Katika majukwaa ya kisiasa utawasikia wakisifu mfumo ambao watoto wao wanaukwepa kama ukoma. Imekuja kudhihirika kuwa, wale wanaosemekana kuwa viongozi wa kesho ni wale ambao sasa hivi wanasomea katika akademika na kufuata mifumo ya kigeni au akademika zinazofuata mfumo wetu katika mazingira teule. Swali ni hili, kesho ya mtoto wa kimaskini ni ipi?

Inahitajika mikakati ya kimakusudi ili kulitanzua swala hili kabla ya milipuko ya kijamii kama vile ujambazi, uuaji, ubakaji, uraibu wa mihadarati na kadhalika. Ipo lazima ya kujenga shule vielelezo katika kila wilaya ambazo zitafadhiliwa na serikali kwa kupewa mahitaji yote muhimu na lazima ya kuanzisha mpango wa lishe bora katika shule ili kukidhi matilaba ya watoto wote. Udahili wa wanafunzi katika shule za kitaifa na katika vyuo vikuu ni sharti uvalishwe vazi la utu na uzalendo bila ubaguzi. Shule za umma ziwe na walimu wa madarasa ya kutosha ili kutatua matatizo yaliyoibuka kutokana na kuanzishwa kwa mpango wa elimu ya bure katika shule za msingi. Sera kuhusu shule za chekechea lazima izinduliwe kitaifa ili kusawazisha msingi wa kila mtoto kielimu. Walimu wa shule hizi za malezi lazima wawe na maandalizi sawa yatakayowawezesha kusawazisha viwango kitaaluma. Mitaala yetu ilenge kuzalisha kwa binadamu ambaye atajinufaisha yeye binafsi na taifa kwa jumla.

Maswali

- a) Ni mambo yapi muhimu yanayojitokeza katika aya ya tatu hadi ya saba. (alama7)
- b) Ni mapendekezo yapi yanayotolewa katika aya ya mwisho (alama6)
- MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**
- a) Taja sauti mbili zilizotamkiwa kwenye kaaka laini (alama2)
- b) Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama1)
- c) Toa maana mbili za neno : kiberenge. (alama2)
- d) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Mwanafunzi yule mtoro hupenda kutembea katikati ya barabra kila wakati
- e) Tumia kiambishi 'ji' kutunga sentensi. (alama2)
- f) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano. (alama2)
lia (kutendeshwa)
Ja (kutendea)
- g) Unda nomino moja moja kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama2)
i) Jaribu
ii) Chuma
- h) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 3)
–Nitawatuza watahiniwa wote watakaopita mtihani mwaka huu.' Mbunge aliwaahidi wanafunzi.”
- i) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemesi katika sentensi ifuatayo. (alama2)
Tulibeba maji ya kutosha tulipoenda safari Turkana
- j) Ainisha viamishi katika sentensi hii. (alama 2)
Sitakupiga
- k) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale. (alama 3)
Yule mgeni aliyefika jana ameondoka leo.
- l) Yakinisha kwa umoja. (alama 2)
Mizigo hii haiwi mizito ikibebwa na watu wengi.
- m) Andika sentensi hii kwa hali ya udogo wingi. (alama 2)
Mtoto amefunga mlango wa nyumba yao.
- n) Tofautisha maana katika sentensi hizi. (alama 2)
Chakula chote kitaliwa Chakula chochote kitaliwa
- o) Andika kinyume: (alama2)
Wanaskauti wengi walivunja kambi jana asubuhi.
- p) Tunga sentensi ukitumia kitenzi kishirikishi kipungufu. (alama2)
- q) Bainisha yambwa katika sentensi ifuatayo. (alama2)
Rais aliandikiwa barua na wanasiasa.
- r) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama2)
Jua nilisemalo ni muhimu kwetu.
- s) Tambua hisia zinazojitokeza katika sentensi hizi (alama2)
i) Ng'oo! mtu kama wewe huwezi faulu.
ii) Maskini! alikuwa mtoto mzuri.
- 4. ISIMUJAMII (alama 10)**
- a) Eleza umuhimu wa usanifishaji wa Kiswahili. (alama5)
fafanua dhima za lugha katika jamii. (alama 5)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA MAARA**102/3****KISWAHILI****Karatai ya 3****1. LAZIMA : SEHEMU YA 'A'****USHAIRI**

Kiia nikaapo hushika tama
Na kuwazia hali inayonizunguka.
Huyawazia madhila
Huziwazia shida
Huiwazia dhiki

Dhiki ya ulezi
Shida ya kudhalilishwa kazini.
Madhila ya kufanyiwa dharau
Kwa sababu ya jinsia ya kike.

Hukaa na kujidadisi
Hujidadisi kujua kwa nini
Jamii haikisikii kilio changu
Wenzangu hawanishiki mikono
Bali wananidharau kwa kuukosoa utamaduni

Hukaa na kujiuliza
I wapi raha yangu uimwengu huu?
I wapi jamaa nzima ya wanawake?

MASWALI

- (a) Shairi hili ni la aina. gani? Eleza (alama2)
(b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)
(c) Kwa kutolea mifano eleza maana ya mistari mishata. (alama 2)
(d) Taja na ueleze tamathali mbili zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
(e) Tambulisha nafsi-neni katika shairi hili. (alama 2)
(f) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)
(g) Fafanua maudhui mawili ya shairi hili. (alama 2)
(h) Onyesha namna nafasi neni anavyosalitiwa. (alama 2)
(i) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
(ii) Madhila
(ii) Kudhalilishwa.

SEHEMU YA B**TAMTHILIA:****Mstahiki Meya : Timothy M. Arege****Jibu swali la 2 au la 3**

2. Mwandishi wa tamthilia ya Mstahiki Meya ametumia wahusika kukuza kazi yake, Thibitisha kauii hili kwa kuwarejelea wahusika wafuatao. (alama 20)
(i) Diwani wa tatu
(ii) Bili
(iii) Mhubiri
(iv) Diwani I na II
3. –Duniani kuna watu na viatu.”
(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea tamthilia nzima ya Mstahiki Meya. (alama 16)

SEHEMU YA C**RIWAYA:****Kidagaa kimemwozea : Ken Walibom****Jibu swali la 4 au la 5**

4. Kuvunjwa kwa haki na sheria lilikuwa jambo la kawaida chini ya uongozi wa Mtemi Nasaba bora. Thibitisha ukweli wa Kauli hii ukirejelea riwaya ya *Kidagaa kimemwozea*. (alama 20)
5. —**A**kuwa na kiu lakini si ya maji, kadhalika alikuwa na njaa lakini si ya chakula Habebeki mwanamume habebeki.....”
(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake . (alama 4)

- (b) Eleza tamathali mbili zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
 (c) Eleza aina za kiu na njaa zilizomkumba mrejelewa wa kwanza. (alama 4)
 (d) Mrejelewa wa pili alishindwa mtihani wa maisha. Jadili. (alama 8)

SEHEMU YA D:
FASIHI SIMULIZI
Jibu swali la 6

6. a) Maigizo ni nini. (alama 2)
 b) Fafanua maiukumu manne ya maigizo. (alama 4)
 c) Taia na ueleze vipera vinne wa utanzu wa maigizo. (alama 8)
 d) Eleza sifa sita za maigizo. (alama 6)

SEHEMU YA E:
HADITHI FUPI
Damu Nyeusi na Hadithi nyingine : Ken Walibora na Said A. Mohamed
Jibu swali la 7 au la 8

7. Elimu imeshindwa kutimiza lengo la kuwapa vijana uwezo wa kukabiliana na maisha ya kisasa. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo. (alama 20)
 (a) Mke wangu
 (b) Samaki wanchi zajoto
 (c) Damu nyeusi.
8. —.....Alimaliza kwa kuandika, —ajayo yapokee”
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)
 (b) Thibitisha ufaafu wa anwani ya hadithi hii. (alama16)

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA 2016**102/1****KISWAHILI****Karatasiya 1****INSHA****Muda: Saa 1¼****1. LAZIMA**

Wewe ni mhariri wa gazeti la **ChanukaUendeleo**. Andika tahariri kuhusu kuenea kwa tatizo la ubadhirifu wa mali ya umma katika magatuzi mbali mbali na kupendekeza njia mbali mbali za kukabiliana nalo.

2. Mradi wa serikali wa vipakatalishi kwa shule za msingi nchini utakuwa na manufaa sihaba. Jadili.

3. Tungakisakitakachodhihirishamaanayamethaliifuatayo:

Fimboyambalihaiuinyoka.

4. Tungakisakitakachomalizikawamanenoyafuatayo:

.....nilishushapumzikwahisiazashukrani, safari hiihaikuwarahisinawengihawakutarajiakuwaningefaululichayawingu la simanzinamisukosukolililoniandamatarikinzi.

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA 2016**KISWAHILI****KARATASI YA 2****LUGHA****MACHI 2016****MUDA: SAA 2½****UFAHAMU (alama 15)**

Idara ya polisi nchini imelaumiwa kwa muda mrefu kutokana na visa vya mauaji ya kiholela, **utepetevu** na ufisadi miongoni mwao. Ni kutokana na kilio cha mwananchi pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ambapo serikali **imejitolea sabili** kubadili hali katika idara hiyo huku tume mbali mbali zilizobuniwa zikitoa mapendekezo muhimu ya kurekebisha idara hiyo. Matokeo ya hivi punde kutoka kwa shirika la Transparency International liliorodhesha idara ya polisi kama idara fisadi zaidi nchini, maoni ambayo yalisitiziwa na shirika la kutetea haki za kibinadamu. **Ufisadi bado umekita mizizi katika idara ya polisi tangu mabadiliko yaanze upande wa trafiki na hata ndani ya polisi.**

Serikali imejitolea kupambana na ufisadi unaonekana kuwa kidonda ndugu katika idara ya polisi. Wananchi wanasema kuwa polisi ni mafisadi na kusahau kuwa ufisadi unashirikisha watu wawili na wote wanapaswa kufunguliwa mashtaka, lazima raia na polisi wazingatie hili. **Na ili kuleta mabadiliko muhimu katika idara ya polisi, mapendekezo yote pamoja na ya tume zingine za hapo awali lazima yatekelezwa na kwa mujibu wa katiba mpya.** Lazima mabadiliko yaanze kuanzia juu kwani maafisa wadogo hulazimiswa kuchukua hongo ili wapelekee wakubwa wao, ni lazima shughuli ya kuwachagua maafisa waliobora ifanyike kisheria ili mabadiliko yaanze kutoka kwa wakuu wa maafisa wa polisi.

Polisi kidogo wameweza kubadili ile lugha yao ya matusi na ukali kwa rai. Raia nao hawajabadilika, bado wana uwoga dhidi ya polisi na itachukua muda kwani wanadhania kuwa kikosi ni kile kile cha kitambo. Kwa upande wa polisi, hakuna mageuzi yamefanyika. Unaposafiri kuja mjini polisi wangali wana chukua hongo kutoka kwa wenye matatu na kuwaruhusu kubeba kupita kiasi, pia usalama umedorora sana kwani kumekuwa na visa vingi vya mauaji hapa mjini. Ukiangalia maafisa wa polisi hakuna mageuzi makubwa yameshuhudiwa haswa kwa upande wa maafisa wa trafiki bado ni wale wale na ufisadi ungali upo.

Mabadiliko ambayo tunataka ni ile polisi wasikae mahali kwa muda hadi wanajuana na mafisadi na majambazi. Maafisa wa polisi wanafaa kuhudumu katika kituo kimoja kwa muda usiozidi miaka mitatu. Kwa kufuata njia hiyo mabadiliko yatapatikana. **Juhudi nyingi zikielekezwa katika kubadili kikosi cha polisi wananchi wanapaswa kuhamasishwa ili nao wawezakubadilika haswa kuhusuiana na mtazamo wao kwa maafisa wa polisi.** Na huku tukijaribu kubadili maafisa wa polisi wananchi pia wanapaswa kuelimishwa ili waweze kubadili mtazamo wao kuhusu maafisa hao. **Ni bayana kuwa ili kuweza kuleta mabadiliko ya kutamanika katika kikosi cha polisi** na haswa katika kupambana na ufisadi uliokita mizizi wananchi sawia na maafisa wa polisi wanajukumu la pamoja kuleta mabadiliko hayo yatakayopelekea kuwepo kwa mlahaka mzuri kati ya maafisa wa polisi na raia. Hatimaye kuwepo kwa huduma bora itakayochangia pakubwa kuboresha uchumi wa taifa na kuafikiwa kwa ruwaza ya mwaka 2030.

Maswali

- a) Kipe kifungu hiki kichwa mwafaka. (alama 1)
- b) Thibitisha kwamba ufisadi ni kidonda ndugu ukirejelea makala haya.. (alama 2)
- c) Ni vipi ufisadi katika idara ya polisi unaweza kuzikwa katika kaburi la sahau? (alama 2)
- d) _Wananchi ndio wanapaswa kulaumiwa kwa ufisadi._ Thibitisha. (alama 3)
- (e) —Serikali imepiga hatua katika kuleta mabadiliko katika idara ya polisi—. Onyesha kinayacha usemi huu. (alama 2)
- (f) Taja manufaa yoyote mawili yanayotokana na mabadiliko katika idara ya polisi (alama 2)

- (g) Eleza maana ya:
 (i) Mlahaka
 (ii) Utepetevu
 (iii) Kujitolea sabili

(alama 3)

UFUPISHO (Alama 15)**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanavofuata**

Kwa miaka na dahari, nchi nyingi za Asia, Amerika Kusini na Afrika, zimekuwa na mamilioni ya watoto wanaoteseka. Matatizo huwakumba kwenye hali nyingi. Si kielemu, si kiafya, si kiutamaduni na kimakuzi tu, bali hata kiuchumi. Nguvu zao na uwezo wao hufujwa kwa njia zinazokirihisha nyoyo. Wale wanaopenda maendeleo na kutilia nguvu haki za kibinadamu huudhiwa kupindukia.

Wazazi wengi wa sehemu hizo wamekuwa wakiamini mambo kipuuzi. Wamekuwa wakidhani kuwa wingi ni hoja, lakini wazazi hawa huwapata watoto wengi wasioweza kuwatunza. Isitoshe, huwachukulia watoto kama sehemu ya mali yao badala ya kuwachukulia kuwa ni binadamu wenzao. Akili haziwapigi na kutambua kuwa, hata nao yinyang 'arika', wakitunzwa vizuri na kupewa nafasi mwafaka za kuwainua kimaendeleo, wataweza kuwa watu wa kutajika katika jamii. Wazazi kama hao wanadhania ya leo ni leo tu, msema kesho ni mwongo. Dhana hizo finyu na potovu zimewapelekea kuthamini uzaaji wa watoto wengi ili watoto hawa wawe punda wa dobi. Wazazi hawa wanajihisi matajiri wa kupindukia wanaopata vijana wengi wa kuwasaidia katika kazi zao bure bilashi.

Baadhi ya watoto hunyimwa nafasi ya kwenda shule. Wale wanaonjeshwa masomo kidogo, huachishwa kisomo hicho mapema. Sababu za kuhinishwa huko kwa kisomo zinafahamika vizuri na wahusika hao. Mara nyingi, huachishwa shule ili wawe mayaya wa watoto wenzao au wakafunge mifugo, kulima shambani, kusaidia biasharani na katika sekta za juakali. Watoto hawana nguvu za kukataa kwani ni kinyume cha utamaduni kuwapinga wazazi. Isitoshe, watoto hawa wanawategemea wazazi hao kwa kila kitu. Utiifu huu, ingawa una uzuri wake unazorotesha maendeleo kupindukia.

Unyonge wa aina hii umefanya mashirika ya viwanda, ya mashamba kama ya chai, kahawa, ya pamba na ya juakali kuwatumia watoto vibaya bila ya kujali maslahi ya watoto hao. Baadhi ya watu wameanzisha mashirika ya uasherati na utumwa. Watoto wanateswa na kuingizwa kwenye majanga yanayotokana na ukimwi na mengine ya uzinifu. Kutokana na dhuluma hizi, watoto hukandamizwa na kupewa posho duni ya kuwapa uhai tu. Matajiri wamezidi kufutuka kiuchumi kutokana na jasho la watoto hao. Watoto hawapewi kinga zozote za kemikali wala kuonyeshwa jinsi ya kuzitumia kemikali hizo. Wakuu wao hutumia saikolojia duni za watoto kuwawezesha kujikuza kiuchumi. Huwapa viperemende hafifu na viungo ovyo ili watoto waimbe na kucheza ngoma za watu hao. Watoto, kwa kutojua, huwasifu wakuu wao badala ya kuwalaani kwa kuwanyonya hadi mifupani na kupewa vijipesa tu. Kwa kuwa ni watoto hawatambui kuwa wanahiniwa.

Matajiri nao husahau kuwa watoto hao wakisoma vizuri hadi mwisho, wanaweza kutoa huduma bora nchini. Inadhihirika kuwa lengo potovu la watu hao ni kukwepa kulipa mishahara mikubwa kwa watu wazima. Lakini nasema si sawa kuwanyonya watoto. Matajiri hawa wangehisi vipi kama watoto wao nao wangepanywa hivyo? Ama ni yule ya mkuki kwa nguruwe, kwa mwanadamu uchungu? Serikali zina mikono mirefu. Inafaa ziwachukulia hatua kali wazazi na maafisa wanaotumia watoto kama matambara mabovu. Watoto nao wanafaa kuzinduka na kutaka kusoma kinyuki. Inafaa wajue kuwa vipesa vya ujakazi ni sumu.

Mashirika ya aina hiyo, inafaa yakipatikana na hatia, yapewe adhabu kali. Yalazimishwe kuwasomesha na kuwakimu watoto hao vilivyo, bila kuwanyanyasa ndipo wasome, kadri ya uwezo wao.

Maswali

- (a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa fupisha aya mbili za mwanzo kwa maneno (45-50) (al. 6, 1 utiririko)
 (b) Kwa kuzingatia taarifa hii eleza namna maonevu dhidi ya watoto yameendelezwa. tumia maneno (50-55) al. 9, 1 utiririko)

MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

- a) Kutokana na kigezo cha jinsi hewa inavyozuliwa, taja aina mbili za konsonanti na utolee mifano kila moja. (alama 2)
 b) Bainisha muundo wa silabi katika neno Gongwa (alama 2)
 c) Eleza maana ya mofimu funge na kutoa mfano mwafaka (alama 1)
 d) (i) Eleza maana ya kiarifu. (alama 1)
 (ii) Onyesha kiarifu katika sentensi ifuatayo (alama 1)
 Mtoto aliyezungunza na nyanyake ameingia darasa lililochafuliwa na watundu.
 e) Bainisha shamirisho katika tungo lifuatalo. (alama 2)
 Mwanafunzi alipewa dawati na mwalimu jana jioni
 f) Bainisha matumizi ya kiambishi .ku katika sentensi hii (alama 2)
 Naomi atakupikia chai halafu aende kule uwanjani

- g) Tambua aina ya kivumishi na kihusishi katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Kijana mgeni amekaribishwa na mgeni
- h) Tunga sentensi ukitumia kitenzi **-nywa** katika kauli ya kutendeka. (alama 1)
- i) Tunga sentensi iliyo na kitenzi kishirikishi kilicho na kiambishi nafsi na wakati (alama 1)
- j) i) Eleza dhana ya kishazi. (alama 1)
ii) Onyesha aina za vishazi kwa kutumia sentensi moja. (alama 1)
- k) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vishale (alama 4)
Alimwona mamba majini alipopiga mbizi.
- l) Yakinisha (alama 2)
Mgonjwa huyo hakupona wala kurejea nyumbani
- m) Sahihisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Mgeni ambaye aliyekuja atarudi jana.
- n) Akifisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Juma Maria ulimwona Farida Maria la hakuwepo jana
- o) Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 1)
Ua unaozunguka nyumba una ua lililopandwa.
- p) Weka nomino hizi katika ngeli zake (alama 1)
(i) Mbalungi
(ii) Mturuki
- r) Andika katika hali ya udogo (alama 2)
Alishikwa na jipu ambalo lilivimbisha kidole chake cha mguu mithili ya pera.
- s) Andika katika usemi wa taarifa (alama 2)
—B! Kumbe wazuri hawajazaliwa,” Omari alisema baada ya kumwona kisura huyo.
- t) Andika misemo inayoafiki hali zifuatazo (alama 2)
(i) Kubahatika
(ii) Ubahaili
- u) Eleza maana tatu za sentensi ifuatayo (alama 3)
Mama alimwambia mwanawe.
- v) Tunga sentensi moja kutofautisha maana mbili ya neno **ziwa** (alama 2)
ISIMU JAMII (ALAMA 10)
- (a) Eleza maana ya istilahi hizi; (alama 2)
(i) Usanifishaji
(ii) Lahaja
- (b) Taja sifa zozote nne za lugha yoyote ile. (alama 4)
- (c) Eleza mambo yanayochangia makosa ya kisarufi na ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili (alama 4)

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA**Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari – Kenya****102/3****KISWAHILI****Karatasi ya 3****FASIHI****Machi/Aprili 2016****Muda: Saa 2½****A. HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE****1. Swali la lazima*****Kanda la Usufi***

–Hakujua maisha yake yangechukua mkondo upi. Mzo wa majuto ulimwandama. Ulimwengu wake ulivurugika, akawa kama tiara inayopeperushwa na upepo ikaenda arijojo”

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Taja na kueleza tamathali ya usemi kwenye dondoo hili. (alama 4)
 (c) Kwa kutolea mifano, onyesha jinsi anwani Kanda la Usufi inavyoafiki hadithi husika. (alama 12)

B. SEHEMU YA RIWAYA**Kidagaa Kimemwozea: *Ken Walibora******Jibu swali kila 2 au la 3***

2. –Nyamaza boza wewe. Wadhani sisi kazi tunaanza leo? Tumekutana na wauaji wangapi?
 a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 b) Dondoo hili linadokeza maudhui gani? Kwa kutoa mifano saba kwenye riwaya, bainisha jinsi maudhui hayo yanavyojitokeza. (alama 16)
 3. Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* imesheheni hali zinazotukia bil kutarajiwa. Fafanua. (alama 20)

C. SEHEMU YA TAMTHILIA**MSTAHIKI MEYA: *Timothy Arege***

4. Hayawezi kulinganishwa na tendo hili ndogo. Walifanya vizuri kuja.
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Fafanua nafasi ya wanaorejelewa kuwa –walifanya vizuri kuja” katika tamthilia hii. (alama 4)
 (c) Migogoro katika tamthilia hii hazikusuluhishwa vyema. Jadili. (alama 12)
 5. Jadili matumizi ya mbinu ya ishara katika tamthilia hii. (alama 20)

D. SEHEMU YA USHAIRI

6.

Nitafukuzwa mbinguni
 Kwa ushairi wangu mbaya
 Lakini hata motoni nitaimba:
 Wanasema
 Wanasiasa ni kama jizi
 Lililosukuma mtoto pembeni
 Na kunyonya ziwa la mama
 Wakati amelala usingizi usiku.

Wanasema
 Mwanasiasa afapo
 Tumejikomboa na domo
 Moja pana lizibwalo na mchanga
 Na kilima cha simenti ngumu
 Lisikike tena hadharani.

Wanasema pia
 Kusema haki
 Kwa kawaida
 Wanasiasa hatuwapendi.
 Kupiga kura ni hasira za mkizi
 Ni basi tu. Ni Ah!
 Ah!
 Wanamalizia
 Nchi mmefiilisi waacheni walimu
 Wakajenga taifa jipya.

Kama hamwezi kuona mbali
Bure kuweka mkono usoni,
Bure hakuna kichwa
Kama hamwezi kufikiri.

Ng'ombe amekamuliwa na wazungu
Waarabu, wahindi na wao
Sasa anatoa damu
Vilivyobaki ni chai ya rangi
Na madomo mapana zaidi
Yaliyo bado hai.
Kuimba nimeimba

Maswali

- (a) Mshairi ana dhamira gani? (alama 2)
(b) Shairi hili ni la kukatisha tama, tetea rai hii. (alama 2)
(c) Onyesha matumizi mawili ya mishata. (alama 2)
(d) Eleza mbinu zozote nne za lugha zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
(e) Andika ubeti wa mwisho katika lugha tutumbi. (alama 4)
(f) Fafanua umbo la shairi hili. (alama 3)
(g) Eleza maana ya mafungu ya maneno ya maneno yafuatayo: (alama 3)
(i) kupiga kura ni hasira ya mkizi
(ii) kuweka mkono usoni
(iii) ng'ombe amekamuliwa.

7. SABUNI YA ROHO

Ewe tunu ya mtima, kwa nini wanikimbia?
Ndiwe suluhu za zama, waja wakukimbilia,
Waja wanakutazama, madeni wakalipia,
Ndiwa sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mafuta ya roho, walisema wa zamani,
Utanunua majoho, majumba na nyumbani,
Umezitakasa roho, umekuwa mhisani,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvinja mlima.

Matajiri wanakujua, wema wako wameonja,
Nguo zao umefua, wakupata kwa ujanja,
Sura zao _mefufua, wanazuru kila njanja,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima, onana na maskini,
Watazame mayatima, kwao kumekua duni,
Webebe waliokuwa, wainue walio chini,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima, wapi kapata uwezo,
Umezua uhasama, waja kupata mizozo,
Ndiwe chanzo cha zahama, umewatia vikwazo,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Umevunja ushuba, familia zazozana,
Waliokuwa mahabuba, kila mara wagombana,
Roho zao umekaba, majumbani wachinjana,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Nakutafuta kwa hamu, sabuni unirehemu,
Sinilipue ja bomu, sije kawa marehemu,
Niondoe jahanamu, ya ufukara wa simu,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Naondoka wangu moyo, nikuitapo itika,
Fulusi wacha uchoyo, tatua yalonifika,
Nichekeshe kibogoyo, nami nipate kuwika,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Maswali

- (i) Taja nafsi nenewa. Thibitisha. (alama 2)
- (ii) Eleza toni ya nafsi neni. (alama 1)
- (iii) Eleza arudhi zozote nne zilizozingatiwa katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)
- (iv) Mshairi anawasilisha ujumbe gani katika mleo wa ubeti wa sita? (alama 1)
- (v) Ukitoa mfano eleza mbinu zozote tatu za lugha alizotumia mshairi. (alam 3)
- (vi) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alam 4)
- (vii) Jadili jinsi mshairi anatumia ruhusa ya mshairi. (alama 2)
- (viii) Kwa kurejelea mpangilio wa vina eleza bahari ambamo shairi hili linaweza kuainishwa. (alam 1)
- (ix) Fafanua maana ya :

(alama 2)

- (i) ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima
- (ii) jehanamu

C. FASIHI SIMULIZI

8. (a) Eleza maana ya mivigha. (alama 2)
- (b) Fafanua sifa zozote nne za mivigha. (alama 8)
- (c) Taja hasara zozote nne zinazohusishwa na mivigha. (alama 4)
- (d) Eleza njia zozote tatu unazoweza kutumia kukusanya data kuhusu mivigha. (alama 6)

MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU - JET
KISWAHILI
INSHA
102/1
KARATASI LA KWANZA

1. **Insha ya lazima**

- Shirika la Utangazaji la Jicho Pevu limetangaza nafasi ya kazi ya mhariri mkuu wa kitengo cha habari za Kiswahili. Umealikwa kushiriki mahojiano. Andika tawasifu utakayowasilisha kwa jopo tathmini.
2. Fafanua changamoto zinazokumba muumano na mshikamano wa kitaifa.
3. Kuinamako ndiko kuinukako.
4. Andika insha itakayokamilikia maneno haya: Alipofika hapo alielewa fika kwamba ingebidi aukate mkono uliokuwa ukimlisha tangu hapo, mradi hakukubaliana naye katika njama hiyo.

MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU - JET
KISWAHILI
102/2
LUGHA
KARATASI LA PILI

UFAHAMU (Alama15)

Soma makala yafuatao kisha ujibu maswali yanayofuata.

Miaka 15 iliyopita, Umoja wa Mataifa ulitangaza August 12 kila mwaka, kuwa ‘Siku ya Vijana Duniani’ ambapo kauli mbiu ya mwaka huu inasema ‘Vijana na Afya ya Akili’.

Kwa mujibu wa andiko kutoka Umoja wa Mataifa, asilimia 20 ya vijana duniani kote hupata tatizo linalohusiana na afya ya akili kila mwaka. Hatari zaidi hutokea katika kipindi cha kuhama kutoka utoto kuingia utu uzima.

Kutengwa pamoja na aibu mara nyingi huongeza zaidi tatizo kwa kuwa vijana wengine hushindwa kutafuta msaada wanaohitaji. Hivyo mwaka huu, Umoja wa Mataifa umeazimia kuitumia siku hii kukuza uelewa kuhusu afya ya akili kwa vijana.

–Wakati tunaadhimisha Siku ya Vijana Duniani 2014, tuwawezeshe vijana wenye matatizo ya afya ya akili kubaini umuhimu wao, na tuoneshe kuwa afya ya akili inatuhusu sote,” amesema Katibu Mkuu wa Umoja wa Maitafa, Ban Ki Moon kwenye maelezo yake.

Miongoni mwa sababu kubwa zinazochangia tatizo la afya ya akili ni umaskini unaochangiwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa ajira. Asimilia kubwa ya vijana walio chini ya miaka 25 au wale wanaohitimu masomo yao nchini hawana ajira. Wanachuo wengi wameendelea kuzunguka huku na kule kuomba kazi bila mafanikio. Wengi wamekaa zaidi ya miaka mitatu nyumbani tangu wamalize masomo yao bila kuwa na ajira inayowaingizia kipato.

Na pia wachache wanaopata kazi, wamekuwa wakilipwa ujira mdogo na hivyo kuendelea kuishi maisha magumu. Ukosefu wa ajira na kukosa fedha za kujikimu, umewafanya vijana wengi kuwa na msongo wa mawazo, tatizo kubwa linalohusiana na afya ya akili.

Tatizo ni kubwa zaidi pale ambapo takwimu zinaonesha kuwa kwa wastani soko la ajira nchini lina uwezo wa kuzalisha ajira zipatazo 300,000 kwa mwaka katika sekta rasmi ukilinganisha na wastani wa wahitimu 600,000 hadi 800,000 wanaoingia katika soko la ajira nchini.

Kwa kijana ambaye hana mahali pa kuishi, hajui atakula nini kesho, hana fedha za kununua nguo, kukata tamaa na kuamua kufanya lolote si kitu anachoweza kukifikiria mara mbili.

Kwa vijana wa kiume wapo wanaoamua kuwa wezi au matapeli huku wengine wakijikuta wakiwa walevi wa kutupwa au kuvuta unga kama njia ya kupunguza msongo wa mawazo unaotokana na maisha magumu. Utumiaji wa vilevi hivyo, umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza tatizo la afya ya akili kwa vijana wengine.

Kwa wasichana, ukosefu wa ajira, huwaingiza wengi katika wimbi la kutumia miili yao kujipatia kipato kutoka kwa wanaume. Wengine hujikuta wakiolewa mapema na hivyo kupoteza ndoto za kujiendeleza kielimu ili kujitegemea.

Mbaya zaidi katika maeneo ya vijijini kwakuwa wasichana wadogo huzalishwa katika umri mdogo na wengine kukumbana na unyanyasaji wa nyumbani kutoka kwa waume zao. Katika maeneo ya vijijini ambako shughuli kubwa ya kiuchumi ni kilimo, ufugaji au uvuvi, baadhi ya wasichana waliolewa, hujikuta wakiachiwa familia zao kwa muda mrefu na waume zao wanaoenda kutafuta maisha. Baadhi ya wanaume hao huondoka kimoja na kuwaachia wake mzigo wa ulezi wa familia.

Hivyo, tatizo kubwa la ajira kwa vijana lipo kwa wale ambao hawana elimu ya kutosha kustahili kuajiriwa katika ajira rasmi. Kwa mujibu wa survey iliyofanywa na Restless Development, Tanzania ina takriban watu milioni 25 walio chini ya miaka 25 nchini. Hiyo ina maana kuwa karibu nusu ya watu wote nchini ni vijana.

Dunia nzima, vijana wamekuwa wakitambulika kwa kuwa na mchango mkubwa kuanzia katika upatikanaji wa uhuru enzi za ukoloni hadi katika kuvumbua teknolojia mpya na kugundua njia mpya za sanaa na muziki. Vijana ndio wanaolisukuma zaidi gurudumu la maendeleo kwa uchapakazi wao kutokana na miili na akili zao kuwa na uchangamfu zaidi. Hata hivyo Tanzania ni nchi iliyo na matabaka yanayotokana na umri na jinsia huku vijana wakioneanza kutopewa fursa katika mchakato wa maamuzi katika hatua za kijamii na hata katika serikali.

Ili kuwapa nafasi zaidi vijana katika nafasi za juu za maamuzi, vijana wanapaswa kutambua kuwa huu ndio wakati wao na sio kesho. Vijana wanatakiwa kwanza kujiamini wao wenyewe kuwa hakuna nafasi ya baadaye kwakuwa huu ndio wakati unaowaruhusu kuwa wabunifu zaidi kushawishi maendeleo.

Mawazo yao mapya na njia zao tofauti za kukabiliana na mambo, yataleta utofauti mkubwa wa sera, maamuzi na muelekeo wa serikali au taasisi mbalimbali.

–Uongozi wa kizazi kipya upo tayari kushika hatamu za uongozi na kuijenga Tanzania mpya, kwa fikra mpya na maarifa mapya. Mabadiliko, kokote yalikota, yalidaiwa na kuongozwa na vijana. Vijana wa Tanzania washike usukani wa kuleta mabadiliko wanayoyataka. Ukiona kijana anamwambia kijana mwenzake hana uzoefu, basi kazi ya kuleta mabadiliko ni kubwa zaidi. Kutokuwa na uzoefu ni sifa ya kijana. Tusi kubwa kwa Obama mwaka 2008 lilikuwa ni kukosa uzoefu, kukosa rekodi. Tusi hilo lilikuwa muziki kwa wapiga kura wa Marekani. Tanzania mpya inahitaji viongozi wapya, mazoea mapya, fikra mpya na maarifa mapya. Inahitaji kuthubutu mambo makubwa sio kulinda uzoefu wa nyuma. Tunaweza,” aliandika January Makamba kwenye mtandao wa Facebook. Ni kweli muda wa vijana ni sasa na sio kesho tena.

Maswali

- | | |
|--|-----------|
| (a) Ipe makala hii anwani mwafaka. | (alama 1) |
| (b) Ni wakati gani ambapo vijana huwa hatarini sana kukumbwa na tatizo la afya ya akilini. | (alama 1) |
| (c) Ni nini lengo la Umoja wa Mataifa mwaka huu kuhusu vijana? | (alama 1) |
| (d) Taja changamoto zinazowakumba vijana wenye matatizo ya afya ya akili. | (alama 2) |
| (e) Eleza mambo ambayo huchangia matatizo ya afya ya akili miongoni mwa vijana. | (alama 4) |
| (f) Taja mambo ambayo huchangia kutamauka kwa vijana. | (alama 3) |
| (g) Ukosefu wa ajira umechangia uozo upi miongoni mwa vijana? | (alama 3) |

2. UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kulingana na maagizo.

Utoaji wa Huduma ya Kwanza.

Inaaminika kuwa majeruhi wengi katika mikasa ya ajali huaga au huathirika vibaya zaidi kutokana na hali mbaya ya uokoaji. Watu wengi ambao hujitolea kuokoa majeruhi baada ya ajali kama za barabarani, maporomoko ya ardhi au nyumba huwa hawang'amui hata chembe jinsi ya kukabiliana na uokoaji. Hatima ya juhudi zao ambazo hulenga kutenda mema ni kuathirika zaidi kwa majeruhi.

Hali ya uokoaji inaweza kurekebisha kwa kutoa elimu ya huduma ya kwanza kwa umma. Elimu hii yahitajika na kila Mkenya kwani mikasa ya ajali za barabarani na nyinginezo inaendelea kutokea kila siku. Ajali zinapotokea, si ajabu kuona makundi ya waokoaji yakibeba majeruhi hobelahobela bila kuzingatia madhara yanayoweza kuwaongezea kutokana na uebaji wao. Kutojua namna ya kumbeba majeruhi kunaweza kumhatarisha na hata kusababisha kifo.

Kuna mambo mbalimbali ambayo makundi ya waokoaji yanatakiwa kuzingatia wakati yanatoa huduma ya kuokoa. Kwanza, ni muhimu kuchunguza kama kuna hatari yoyote inayoweza ikatokea na kuwatia majeruhi na waokoaji hatarini zaidi. Makundi ya waokoaji yameweza kuhatarisha majeruhi kwa kuliingilia eneo la ajali mbumbumbu kama mzungu wa reli.

Hatua ya pili ni kutafuta idadi ya majeruhi. Pana uwezekano wa majeruhi kutupwa mbali na eneo la ajali. Vivyo hivyo, kuna majeruhi ambao huweweseka baada ya ajali na kuanza kutembea wasijue wanakoelekea. Wengi wao huanguka karibu na eneo la ajali au wakaenda mbali.

Hatua ya tatu ni kuchunguza kama majeruhi amezimia, moyo unapiga na jinsi anavyopumua. Ili kuhakikisha kuwa majeruhi anapumua, mwokoaji atazame kama kifua kinapanda na kushuka. Halikadhalika, mwokoaji anaweza kusikiliza au kuguza kifua na kuona kama kuna ishara za kupumua. Iwapo majeruhi anapumua, mwokoaji amweke katika hali ambayo itaimarisha kupumua kwake. Anaweza akamlaza chali au kumgeuza kwa pamoja na kichwa chake ili kufungua mkondo wa hewa. Pia, mwokoaji ahakikishe hamna chochote kinywani kinachoweza kumsakama. Ikiwa hapumui, mwokoaji anaweza kujaribu kumfanya apumue kwa kupuliza hewa mdomoni mwake. Fauka ya hayo, upulizaji wa hewa utahakikisha kuwa damu inazunguka mwilini vizuri.

Hatua nyingine ni kuchunguza vile amejeruhiwa. Chunguza kama majeraha ni vidonda tu au kuna kuvunjika kwa mifupa na kubainisha ni mfupa upi. Haya yatamwezesha mwokoaji kujua jinsi ya kumbeba majeruhi. Pakiwa na kuvunjika kwa mfupa, ni muhimu kutotumia kiungo kilichovunjika anapobebwa.

Pia, kuchunguza vile majeruhi amejeruhiwa, humwezesha mwokoaji kujua huduma ya dharura atakayotumia. Majeruhi akiwa anavuja damu sana, ni muhimu kuzuia uvujaji huu. Iwapo ni kidonda kidogo, kinahitaji kufungwa ili kuzuia uambukizaji. Mwokoaji anaweza kutumia kifaa chochote kilicho karibu kutolea huduma hizi. Kwa mfano, anaweza kupasua nguo ya majeruhi ili apate kitambaa cha kusaidia kuzuia kuvuja kwa damu au kumfunga kidonda.

Hatua inayofuata ni kumhamisha majeruhi kutoka eneo la ajali hadi hospitalini. Mwokoaji anaweza kuwatumia watu wengine kutafuta msaada. Wanaweza kupiga simu wakitumia nambari za simu za dharura kama zile za polisi, wazimamoto au makundi ya wataalamu wa shughuli za uokoaji. Nambari hii ya simu huwa 999 popote na huwa haina malipo. Wanaopiga simu ni vyema kutoa maelezo ya mahali ambapo ajali imetokea, aina ya ajali na huduma za dharura zinazohitajika pamoja na idadi ya majeruhi. Iwapo makundi haya ya uokoaji yameahidi kufika, ni bora kuyasubiri.

Ikiwa makundi ya wataalamu wa uokoaji hayakupatikana, ni jukumu la mwokoaji kuhakikisha majeruhi wamehamishwa na kupelekwa hospitalini. Majeruhi wakiwa wengi, ni bora kuanza na wale waliozimia au wenye matatizo ya kupumua kisha kuwaendea wanaovuja damu sana. Baadaye, mwokoaji awasaidie waliovinjika mifupa huku akimalizia na wenye majeraha yasiyohatarisha maisha. Ni muhimu kuwabeba majeruhi kwa kutumia machela. Hii hupunguza kuathirika zaidi kwa majeruhi. Iwapo hamna machela karibu, mwokoaji anaweza kuunda moja kwa kutumia vipande viwili vya mbao, blanketi, shuka au makoti. Ujuzi wa huduma ya kwanza ni mojawapo ya mambo muhimu ambavo kila mtu anapaswa kuwa nayo.

Maswali :

- (a) Fupisha aya mbili za kwanza kwa maneno **55 – 65**. (alama 6, 1 utiririko)
- (b) Eleza kwa kutumia maneno 90-100, hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa uokoaji. (alama 8, utiririko 1)
- (a) Eleza maana ya neno changamano huku ukitolea mfano. (alama 2)
- (b) Andika sentensi ifuatayo katika kauli iliyo mabanoni. (alama 2)
Paka analamba mchuzi (kutendwa)
- (c) Akifika sentensi ifuatayo kwa kutumia alama ya kibainishi kisha eleza matumizi yake. (alama 2)
Ntakwenda Unguja mwezi wa Disemba
- (d) Bainisha aina ya neno lililopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Kuimba kwa Yusufu kunaudhi
- (e) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 2)
Manukato haya yananukia vizuri
- (f) Eleza matumizi ya ku katika jozi zifuatazo za sentensi. (alama 3)
(i) Kuchora kwao kulikuwa kwa uangalifu mkubwa
(ii) Nilikuwa lakini hukuitika
- (g) Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani. (alama 2)
Kero.....
Nywele
- (h) Tambua viambishi awali na tamati katika neno ajaye (alama 3)
- (i) Ikarabati sentensi hii: (alama 2)
Mpira yangu amepotea
- (j) Tambua aina ya chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Walimu wataenda Mombasa Ijumaa ijayo.
- (k) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Viatu vyangu vimepotea
(ii) Viatu vyenyewe vinapendeza
- (l) Badilisha sentensi iwe katika hali ya kuamuru. (alama 1)
Rutto fagia chumba.
- (m) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. (alama 1)
Mwanasiasa huyu alishinda kura. (Tumia kiashiria kisistizi)
- (n) Onyesha hali katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Huenda mvua isinyeshe msimu huu.
(ii) Waislamu huenda msikitini kuomba kila Ijumaa.
- (o) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 4)
Aliyetujengea nyumba ni Omari
- (p) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama 2)
–Nitakuja kwenu kesho,” Mwalimu alisema.
- (q) Tambua na ueleze virai katika sentensi hii. (alama 2)
Kisichana kile kimejirembesha kwa manukato mazuri ajabu
- (r) Eleza tofauti baina ya sentensi hizi; (alama 2)
(i) Ningekuwa na pesa ningesafiri kwenda Pwani.

(ii) Ningalikuwa na pesa ningalisafiri kwenda Pwani.

(s) Tunga sentensi moja iliyo na shamirisho kitondo, kipozi na ala.

(alama 3)

ISIMU JAMII

- a) ...ya leo ni kuwapa pole wanaofuata na kuenzi makala ya Burudani, toleo la kila Ijumaa. Mwanamziki huyu aliteka nyoyo za wapenzi wa mtindo huu wa mziki. Kwa kweli ya Muumba hufumbwa tu! Mnapoyasoma wakumbukeni jamaa na wapenzi wa nyimbo zake.
- (i) Tambua sajili hii na utoe Ushahidi. (alama 2)
- (ii) Fafanua sifa zozote za sajili hii. (alama 4)
- b) Taja mambo yoyote manne yanayofanywa na Serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili. (alama 4)

MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU - JET

2016

KISWAHILI

102/3

KARATASI YA TATU

FASIHI

1. USHAIRI

Soma mashairi yafuatayo kasha ujibu maswali.

SIKUJUA!

1. Kama ningefuga ng'ombe, mafahali na vindama,
Zisingenidhuru pembe, ngeu kuniandama,
Samli ni lembelembe, na minofu ya minyama.
2. Kama ningefuga mbuzi, na kondoo kundi zima,
Ningewajengea zizi, na maziwa nikakama,
Ningewachuna na ngozi, kutengenezea ngoma.
3. Kama ningefuga bata, nao kuku kwa ujima,
Chakula siyo matata, ni machicha na mtama,
Mayai ningeyapata, na kitoweo kizima.
4. Kumbe nimefuga punda, mashuzi ndio heshima,
Ni ukaidi na inda, mateke kurusha nyuma,
Nyama limekuwa nunda, mfugaji humuuma.

Kitikio

Sikujua wa kufuga, mnyama mwenye faida

SHAIRI B

Afrika na Watu Wake

Mimi ninaona mgonjwa
Bado amelala kitandani.
Kama hatutamtoa miiba iliyobaki
Mgonjwa hataweka miguu yake chini
Ili kutembea bila ya kujiegemeza.

Miiba iliyomo ndani mwetu lazima
Pia iondolewe upesi kabla haijaingia
Kati ya mfupa na kufa pamoja nasi.
Baada ya kuitoa tuvae viatu vya chuma
Halafu tucheze nao mchezo wa siasa na uchumi.

Lakini kuitoa miiba hii
Tunahitaji macho makali
Mikono isiyotetemeka
Moyo usio na huruma
Na kuona miiba ilipoingilia.

MASWALI

- (a) Onyesha jinsi ujumbe unaopatikana katika ubeti wa nne wa Shairi A na Shairi la B unavyokatisha tamaa. (Alama 4)
- (b) Eleza maana ya mshororo huu kama unavyojitokeza kwenye ubeti wa pili wa shairi B. (Alama 2)
Baada ya kuitoa tuvae viatu vya chuma.
- (c) Linganua sifa za kimuundo ukizingatia ubeti wa pili wa Shairi A na Shairi B. (alama 4)
- (d) Ukizingatia Mshororo wa kwanza kwenye ubeti wa pili wa Shairi A, onyesha jinsi Mshairi alivyotumia kibali chake. (alama 2)
- (e) Onyesha sifa moja ambayo inadhihirika kwenye shairi la B na ambayo hutawala tungo za aina hii. (alama 2)
- (f) Nafsi neni amedhihirisha toni gani kwenye shairi A? (alama 1)
- (g) Taja nafsi mbili nenwa kwenye shairi la B. (alama 2)
- (h) Andika ubeti wa mwisho wa shairi B kwa lugha ya nadhari. (alama 3)

2. KIDAGAA KIMEMWOZEA

1. Wanyonge ndio wanyongwao ni kauli inayodhihirika vyema kupitia wahusika tofauti katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. Jadili. (alama 20).
2. —Apofikishwa kwenye zahanati hakushughulikiwa ipasavyo. Ubwete ni ugonjwa mmoja mbaya walioambukizwa madaktari na wauguzi wengi Tomoko”
- a) Eleza Muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Dhihirisha jinsi mtunzi alivyotumia tamathali yoyote moja inayobainika kifunguni. (alama 4)
- c) Riwaya Ya Kidagaa Kimemwozea ni muhtasari wa maradhi yanayolihujumu Bara Afrika. Tetea rai hii kwa mifano faafu riwayani. (alama 12)

3. FASIHI SIMULIZI

- (a) Eleza dhima ya lakabu kwa kurejelea hoja tano. (alama 5)
- (b) Jadili sifa tano za michezo ya watoto. (alama 5)
- (c) Fafanua mambo matano yanayomfanya mtu awe mlumbi bora. (alama 10)

4. MSTAHIKI MEYA

1. Jadili mbinu zifuatazo kama zilivyotumika katika Mstahiki Meya. (alama 20)
- (a) Jazanda
- (b) Uzungumzi nafsia
- (c) Majazi
- (d) Methali
2. Nonsense! Hivi huyu ana nia gani?
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Taja na ueleze mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
- (c) Jadili umuhimu wa msemaji katika tamthilia hii. (alama 6)
- (d) Jadili njia za kuondoa uozo katika jamii ukijikita katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 6)

5. DAMU NYEUSI

- Kamchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri jangwani”.
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- (b) Fafanua sifa zozote nne za mrejelewa (alama 8)
- (c) Eleza fani uliotumiwa na mwandishi katika dondoo hili (alama 2)
- (d) Kwa kurejea hadithi zozote tatu, eleza namna wahusika wowote watatu walivyoathiriwa na kiu. (alama 6)

TATHMINI YA PAMOJA YA KAMDARA - 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**

1. Baada ya kuhitimu masomo ya sekondari, uliweza kujiunga na kundi la vijana wa kaunti yenu wanaojaribu kuboresha maisha yao. Mwandikie gavana wa kaunti hiyo barua pepe ukimweleza changamoto mnazopitia na jinsi anavyoweza kusuluhisha.
2. Teknolojia ya kisasa ni kama sarafu yenye sura mbili. Jadili.
3. Umdhaniye ndiye siye. Onyesha ukweli wa methali hii.
4. Andika insha itakayomalizika kwa
..... tulijifunga vibwebwe kuwavua wahasiriwa waliokuwa wamefunikwa na vifusi. Lakini jitihada zetu ziliambulia patupu.

TATHMINI YA PAMOJA YA KAMDARA – 2016**2016****KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU (ALAMA 15)****Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Alipokuwa akiukemea utamaduni na dhana za kikabila katika nyimbo zake, marehemu Bob Marley aliufananisha ubepari na —wanyama wala watu.” Katika wimbo —Babylon System” (yaani mfumo wa kibepari), Marley alisema kuwa utamaduni huo ndio mzawa wa matatizo yote ya kiutawala ambayo yalikuwa yakiyakumba mataifa ya Weusi katika karne ya 20, wakati nchi zao zilikuwa zikitawaliwa na nchi za mataifa ya Ulaya.

Kwa mantiki hiyo, pengine Marley alikuwa na maono kuwa Afrika haingejikomboa kutoka kwa utumwa wa Kizungu, ikiwa ingeendelea kuziabadu na kuzishadidia tamaduni za Kimagharibi.

Utabiri huo nauoanisha na yanayoendelea nchini, ambapo serikali ya Jubilee imeonekana kushindwa kabisa kuikabili saratani ya ufnisadi, ambayo inahatarisha kuliangamiza taifa hili lenye uchumi dhalili.

Donda hili linazidi kuyatandaza mabawa yake kutoka, tisho kuu likiwa ni uvamizi wa taasisi —takatifu” ambazo tunazitegemea kulikabili donda hilo.

Ni nani tutategemea kukabiliana na rushwa ikiwa taasisi kama Bunge, Tume ya Maadili na Kukabiliana na Ufnisadi (EACC) kati ya zingine muhimu zimepakwa tope na saratani hiyo?

Kimsingi yote tunayopitia ni matunda ya uasi wa tamaduni za Kiafrika na uegemezi wa mifumo ya Kizungu kama mihimili ya jamii na nchi zetu.

Ndoto za watetezi wa Uafrika na nafasi ya Weusi kama marehemu Malcom X na Martin Luther King, zilikuwa ni kuona kuwa wameungana kabisa kukabiliana na matatizo yaliyowakabili bila kuzingatia mazingara waliyokuwemo.

Pindi tu baada ya mataifa mengi ya Kiafrika kujinyakulia uhuru wao katika miaka ya hamsini na sitini, viongozi wakuu walioziona nchi hizo kama Kwame Nkrumah, Jomo Kenyatta, Mwalimu Julius Kibarage Nyerere kati ya wengine walianza harakati za kuliunganisha bara hili na kubuni Muungano wa Nchi za Kiafrika (OAU) japo ndoto hiyo haikufikia. Kwa msingi huo, mhimili mkuu wa kiutawala ungekuwa ni mfumo wa kisosholista, ambao ungekuwa nguzo kuu ya kuyaunganisha mataifa hayo.

Hata hivyo, migawanyiko mikubwa ilianza kushuhudiwa, huku baadhi ya mataifa yakianza kukabiliwa na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa kutaasisika kwa maovu yote tunayoshuhudia sasa: ufnisadi na tamaa ya kuogofya kutoka kwa viongozi wetu.

Maswali

- a. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)
- b. Onyesha mambo mawili makuu ambayo msanii aliyapinga .(alama 2)
- c. Kwa nini ubepari umelinganishwa na—wanyama wala watu”? (alama 2)

- d. Kwa mujibu wa taarifa eleza sifa za Bob Marley. (alama 2)
- e. Swala linalozungumziwa limerejelewa kama-*Ɖonda*”.
- i) Eleza mbinu ya lugha iliyotumika.. (alama 2)
- ii) Ni kweli kuwa *donda* hili laelekea kuwa gumu? Thibitisha. (alama 2)
- f. Tatizo hili la -*Ɖonda*” ni kama kujipalia makaa. Fafanua. (alama 2)
- g. Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa taarifa. (alama 2)
- i) Mhimili
- ii). Taasisi

2. MUHTASARI

Soma taarifa ifatayo kwa makini kisha ujibu maswali yanayofuata.

Nchi nyingi duniani zimetia saina mkataba wa umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto.

Haki ni mambo mema ambayo watoto wanastahili kutendewa. Kwa kutia saina, nchi hizimetangaza kujitolea kwao kuzilinda na kuhahakikisha kuwa hakuna ukiukaji wake nakuwa watoto wote katika himaya zao wananufaika kutokana na haki hizi.

Miongoni mwa haki hizi ni kuwa kila mtoto ana haki ya kuishi na kupata chakula cha kutosha na chenye viinilishe bora. Pili, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu hii inafaa kutolewa bila ada na iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Kisha kila mtoto ana haki ya kutopigwa na kutodunishwa kwa namna yoyote, iwe kitabaka, kirangi, kijinsia na vinginevyo. Mtoto ana haki pia kutolazimishwa kufanya kazi za kiutumwa, nzito na zakushurutishwa. Hali kadhalika, ana haki ya kuishi katika nyumba au makazi bora nasalama, kutunzwa na kulindwa dhidiya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Anatakiwa ashirikishwe katika kufanya maamuzi. Fauka ya haya, ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum, michezo, upendo na habari. Isitoshe, anastahili kuheshimiwa kimawazo na kihisia. Haki hizi zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, hivyo serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba za nchi zao na sheria zao.

Walakini haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. La kusikitisha na kukera ni kuwa wanaotarajiwa kuwa vigogo vya kuzilinda haki hizi, ndio wanaoongoza kuzikiuka. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kunyimwa chakula, kufanyishwa kazi kipunda, kuteswa, kuishi katika mazingira hatari, na hata kuuawa. Kuna watoto wengi wanaolala nje, wengine hawapati chakula licha ya kuwa wanatakiwa kupata chenye lishe bora. Kwao kutarajiwa mlo awamu tatu kwa siku ni njozi kwani hata awamu moja ni adimu kupata.

Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Viongozi katika mataifa haya hawafanyi kitu ila kutazama tu wakati watoto wanaotakiwa kuwalinda wanageuzwa kuwa mibaba ya kuu na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia, huvalishwa mabuti ya kijeshi ambayo ni mizigo mizito ya kubeba mbali na bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani wakati wanatakiwa kuwa wamelindwa majumbani, na shuleni na wazazi wao na serikali.

Jukwaa la vijiji vya mataifa ya ulimwengu wa tatu limesheheni watoto wasioenda shule kwa sababu ya lindi la ufukara uliokithiri. Elimu ya bure inayogusiwa katika haki za watoto haipo. Wanaong'ang'ana iwepo ni kana kwamba ni waota ndotomchana. Jiulize watoto wangapi sasa hivi wamo majumbani bila kwenda shuleni kutokana na ukosefu wa karo? Wangapi wamo mitaani wakivuta na kunusa gundi huku wakiombaomba vishilingi?

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima na kuungana mikono kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu haki za watoto. Twapasa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wamo shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada mbungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati bali si kwa chati.

Maswali

- a) Fupisha aya mbili za kwanza. (maneno 65-70) (alama 8, utiririko 2)
- b) Eleza ni vipi ukiukaji wa haki za watoto unaweza kuepukwa. (maneno 30-35) (alama 4, utiririko 1)

3. **MATUMIZI YA LUGHA / SARUFI**

- a) Eleza sifa bainifu za sauti /j/. (alama 2)
- b) Fafanua maana ya shadda. (alama 2)
- c) Bainisha mofimu - **LI**- katika tungo hii. (alama 3)
- Alivyolikimbilia
- d) Bainisha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi hii. (alama 2)
- Nyanya ametengezewa kitanda kizuri na mjukuu wake.
- e) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (Alama 4)
- Bakari, Roda na Hirsi wamefurahi kupita mtihani.
- f) Kanusha sentensi ifuatayo :- (alama 2)
- Kuliko na vita kwahitaji amani.

- g) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi.
Msomi hakutuzwa siku hiyo. (alama 2)
- h) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya paradesi. (alama 2)
- i) Toa maana mbili ya sentensi ifuatayo:
Leteni! (alama 2)
- j. Eleza matumizi matatu ya kiambishi **-ku** (alama 3)
- K. Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika hali ya kufanyiza.(alama 3)
i) - La
ii) - Nywa
iii) -Fa
- L. Andika upya sentensi kwa kutumia O‘ rejeshi tamati. (alama 2)
Gari lililoanguka si lile unalolizungumzia.
- M. Unda nomino kutokana na kivumishi kifuatacho: (alama 1)
Tepetevu
- N. Ainisha vihusishi vilivyopigiwa mstari.
Atieno ndiye mtoto wa mwisho wa Ojwang lakini ni mwerevukuliko wengine. (alama 2)
- O. Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo .
Nimewaleta askari kituoni ili wawalinde wananchi wote wanaosumbuliwa na majambazi. (alama 3)
Anza:
Wananchi.....
- P. Andika sentensi hii katika hali ya ukubwa wingi. (alama 2)
Ng‘ombe mnono atachinjiwa wachezaji.
- Q. Taja uamilifu wa maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
i) Hapa ni pangu.
ii) Haraka yako itakuponza.
- R) Andika neno lenye muundo huu. (alama 1)
KKKKI
- 4. Isimu Jamii**
- i. Eleza maana ya lugha (alama 2)
- ii. Eleza mambo manne yanayopeleka kufifia / kufa kwa lugha. (alama 8)

TATHMINI YA PAMOJA YA KAMDARA – 2016
KISWAHILI
102/3
KARATASI YA TATU
FASIHI

SEHEMU YA A: USHAIRI

1. Swali la lazima

Soma shairihilikishaujibumaswaliyanayofuata:

ULIYATAKA MWENYEWE: D.P.B Massamba

Alikwambawako mama, kajifanyahupuliki,
 Kakuasakilajema, ukawang'oo!hutaki,
 Sasayamekusakama, popotehapashikiki,
 Uliyatakamwenyewe!

Babayolipokuonya, ukamwonaanachuki,
 Mambo ukaboronganya, kujifanyahushindiki,
 Sasayamekunganya, kwayeyotehupendeki,
 Uliyatakamwenyewe!

Mazuriuliodhania, yamekuletheadhiki,
 Mishikelimiamia, kwakoonahaitoki,
 Mwanzoungkumbukia, ngekuwahuaziriki,
 Uliyatakamwenyewe!

Dunianayohadaa, kwafukaranamaliki,
 Ulimwengunishujaa, hilokamahukumbuki,
 Yaninikuyashangaa?Elewahayafutiki,
 Uliyatakamwenyewe!

Mwenyeweumelichimba, la kukuzikahandaki,
 Ulijidhania simba, hutishikinafataki,
 Machunguyamekukumba, hatanenohutamki,
 Uliyatakamwenyewe!

Kwamnoulivuna, kwa mambo ukadiriki,
 Na tenaukajiona, kwambawemstahiki,
 Nduguumepatikana, mikanganyohuepuki,
 Uliyatakamwenyewe!

Majutonimjuku, hujakinyumerafiki,
 Ungejuamwishohuu, ungetendayalohaki,
 Ukorojuujuu, popotehapakuweki,
 Uliyatakamwenyewe!

Maswali

- Elezadhamirayashairihili. (alama 2)
- Tambuanjiambilianazotumiamtunziwashairihilikuusisitizaujumbe wake. (alama 2)
- Tajanautoemifanoyaainazozotembilizatamathalizaausemizilizotumikakatikashairi. (alama 4)
- Andikaubetiwatatukatikalughanathari/ tutumbi. (alama 4)
- Kwakutoamfanommojammojaonyeshaainambilizaidhinyakishairikatikashairihili. (alama 4)
- Bainishatoniashairihili. (alama 2)
- Elezamaanayamanenohayakamayalivyotumiwakatikashairi. (alama 2)
 - Mstahiki
 - Hupuliki

SEHEMU B: RIWAYA: KIDAGAA KIMEMWOZEA-KEN WALIBORA

JibuSwali la 2 au 3

- Umenenandiponduguyangu. HiyondiyotanziayaAfrikahuru.”
 - Elezamuktadhawadondoohili. (alama 4)
 - Ni ninisifazamvutozinazowaletapamojamzungumzajinamzungumziwa. (alama 4)

- c) Tambuanaufafanuembuinayotumikakatikadondoo. (alama 2)
 d) Kwamifanomwafakafafanuatanziahiyoinayorejelewakatikadondoo. (alama 10)
3. Kuvunjwakwahakina sharia lilikuwajambo la kawaidachiniyauongoziwaMtemiNasabaBora.Thibitishaukweliwakaulihiiukirejeleariwaya. (alama 20)

SEHEMU C: TAMTHILIA:MSTAHIKI MEYA- TIMOTHY AREGE

Jibuswali la 4 au 5

4. ~~Wapoumefanya, yapomengiambayohayakunyoka.~~
 a) Elezamuktadhawadondoohili. (alama 4)
 b) Tambuambinumojaileyotimikakatikamuktadhawadondoo. (alama 2)
 c) Fafanuakaulikwamba'yapomengiambayohayakunyoka'. (alama 8)
 d) Elezajinsibaadhiyawahusikawalivyojaribukuyanyoosha. (alama 6)
5. Kwakutoamifanokumi, elezavizingitiwalivyokumbananavyoWanacheneowakatiwakupiganiamageuzi. (alama 20)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE – K. WALIBORA NA S.A. MOHAMMED

6. —Eo nisiku, sikuyanyanikufaambapomitiyotehuteleza”
 a) Elezamuktadhawadondoohili. (alama 4)
 b) Bainishatamathalimbilizausemizinazojitokezakatikadondoohili. (alama 4)
 c) Hukuukitoamifano, thibitishamaudhuisitaambayoyamejitokezakatikahadithiyaDamuNyeusinawanayoyaendeleza. (alama 12)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

JibuSwali la 7 au 8

7. (a) **Maigizoninini?** (alama 2)
 (b) Tajasifannezamaigizo. (alama 4)
 (c) Eleza mambo **manne**anayopaswakufanyamwigizajiilikufanikishauigizaji wake. (alama 8)
 (d) Ni niniumuhimu wamaigizo. (alama 6)
8. Kushirikinimbinumojayakukusanya data katikautafitiwakazizafasihisimulizi.
 a) Elezahojatanokuhusuumuhimu wambinuyakushiriki. (alama 10)
 b) Elezahojatanozaudhai fuwambinuyakushiriki. (alama 10)

TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI YA NANDI KASKAZINI NA NANDI YA KATI 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**

1. Swali la lazima.
Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Mulika kuhusu **vyanzo vya ujauzito kwa wanafunzi wa kike nchini.**
2. Eleza jinsi udanganyifu katika mitihani utaathiri maisha ya kizazi kijacho.
3. Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti.
4. Andika insha ambayo utamaliza kwa:
.....Aha! Kumbe muungwana akivuliwa nguo huchutama! Sitahisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka maishani kama nilivyoaibika.

TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI YA NANDI KASKAZINI NA NANDI YA KATI 2016**KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU (ALAMA 15)****Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Lugha inaweza kuelezwa kwa jumla kuwa ni mfumo wa mawasiliano. Haiyamkiniki kwa mtu yeyote kueleza chanzo au kiini cha lugha na sote tunakubalina kuwa matumizi yake yameanza tangu kuumbwa kwa binadamu kwani ni vigumu kukisia kuwepo kwa jamii ya watu bila lugha ya mawasiliano yoyote ile.

Katika taifa lolote, huwapo na lugha moja au hata zaidi ya moja ambayo huwa ndicho chombo zatika cha mawasiliano ya taifa katika nyanja za: elimu maandishi, siasa na biashara. Kwa mfano mataifa ya Kanada hutumia lugha mbili kwa usawa kama lugha za taifa na za kikazi. Maana ya lugha ya taifa ni lugha moja ambayo huteuliwa kutumika katika shughuli zote za taifa hasa katika nchi yenye lugha nyingi za kikabila. Lugha ya taifa ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya taifa lolote lile. Lugha hii huwa ndiyo kiungo cha kueneza umoja na uelewano miongoni mwa jamii nyingi tofauti na huwa kama kitambulisho kwao kwa kuwa wao ni ndugu wa jamii moja kubwa, yaani taifa lao.

Kenya ni mfano mzuri wa taifa lenye lugha nyingi zinazozidi 40 za vikundi vidogo vidogo vya kikabila. Hapo kabla ya miaka mia moja hivi iliyopita kila kimojawapo cha vikundi hivi kilijitambulisha kama kabila huru. Baada ya kuja kwa serikali ya kikoloni na hasa baada ya Kenya kujinyakulia uhuru, haja ya kuunganisha raia wote chini ya taifa moja lenye uongozi na shabaha moja ilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana. Kwa hivyo utamaduni wa taifa Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila, desturi, imani na itikadi tofauti. Utamaduni humaanisha jumla ya amali na tabia za watu wa jamii fulani. Amali hizi zinafungamanisha fikira, ustaarabu, mila, taasisi na sanaa za aina zote za jamii inayohusika.

Ili kujieneza na kujiimarisha, taifa huhitaji chombo hicho kuwasiliana na kuunganisha watu wake wenye asili mbalimbali. Chombo hicho huwa ni lugha ambayo siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii bali pia ni njia muhimu sana ya kutawanyia na kustawishia ule utamaduni.

Katika taifa lenye lugha nyingi kama Kenya kwa mfano, lugha ya taifa inayozungumzwa na kueleweka na baadhi kubwa ya raia ambayo imekiuka mipaka na tofauti za kikabila ni njia muhimu sana ya kueneza maongozi ya taifa na kuleta ufahamikiano bora kote nchini. Kama

zilivyo taasisi kama wimbo wa taifa, bendera ya taifa au bunge la taifa, lugha ya taifa ndicho kielelezo cha taifa lolote lile. Lugha kama hiyo huvunja na hukomesha hisia za kibinafsi na kikabila na badala yake kuunda moyo wa uaminifu wa kitaifa.

Zaidi ya kuwa chombo cha mawasiliano, lugha ni kielelezo cha fikira na hisia za binadamu. Lugha ya watu fulani haituelezi tu ujuzi au maarifa yao bali pia mtazamo wao kimaisha, falsafa na mawazo yao. Kwa ufupi lugha hutufahamisha namna akili za watu waizungumzayo ile lugha zinavyofikiri na kufanya maazimio. Lugha ni sehemu ya utamaduni wa taifa tulimozaliwa na lazima lugha hiyo ifunzwe katika muktadha wa maisha ya jamii ihusikayo. Utamaduni wa jamii havitenganiki na lugha yake.

Maswali

- | | |
|---|-----------|
| (a) Huku ukirejelea kifungu, eleza fasiri na chanzo cha lugha. | (alama 2) |
| (b) Tofautisha baina ya lugha ya taifa na lugha ya kikazi. | (alama 4) |
| (c) Kwa nini lugha ya taifa huhitajika sana katika nchi kama Kenya. | (alama 4) |

- (d) Eleza kazi **nne** kuu zinazotekelezwa na lugha ya taifa. (alama 2)
- (e) Eleza maana ya mafungu yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa: (alama 3)
- (i) Amali na tabia za watu:.....
- (ii) Mukadha wa maisha ya jamii:.....
- (iii) Haiyamkiniki:.....

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Je, mtazamo hasi ni nini? Huwa na athari gani kwa binadamu hadi iwe sababu ya kuangaziwa katika safu hii? Mtazamo hasi ni kukata tama, kutamauka kuhusu hali, mtu au jambo fulani. Ni hisia ya kutotaka kushiriki wala kuhusishwa na jambo au hali fulani. Mtazamo huu ndio huwafanya wanafunzi wengi kuchukua au kudunisha baadhi ya masomo na walimu wanaowafundisha. Licha ya wengi kuwa na mtazamo huu, kwa kweli huwa hawatambui. Asilimia kubwa ya wanaotambua hutatizika kujikwambua kutoka katika hali hii.

Inakadiriwa kwamba mtu wa wastani huwa na takriban mawazo elfu sitini ya kibinafsi kwa kila saa 24. asilimia 95 ya fikra hizi huwa sawa na za siku iliyotangulia, na asilimia 80 ya fikra hizi zilizorudiwa huwa hasi.

Isitoshe, fikra hizi nyingi hutokea bila mtu mwenyewe kutambua na huwa mazoea. Hii ina maana kwamba watu wengi hawana ufahamu wa athari za fikra hizi maishani mwao. Katika makala haya tunaangazia vyanzo vya mitazamo hasi na suluhu.

Mwanzo kabisa ni imani potovu. Hiki ndicho chanzo kikuu cha mtazamo hasi. Kushikilia imani potovu kuhusu maisha pamoja na matukio fulani maishani hujenga mtazamo hasi. Unayaona maisha kwa macho ya imani zako na iwapo imani hizo ni potovu, basi hutayathamini maisha yako. Ili kukabiliana na hali hii, sharti kwanza ubadili imani yako. Uamini kwamba mabadiliko yanaweza kutokea na uchukue hatua ya kuanzisha mabadiliko hayo maishani mwako. Unahitaji kuepuka fikra hasi zinazoambatana na maisha yako ya awali na kulitathmini kila tukio maishani kama tukio huru; lisilo na uhusiano na yaliyowahi kukutamausha.

Kujikwambua kutoka katika imani duni unahitaji kuibuka na idadi kubwa ya imani chanya kuliko zilizo hasi kuhusu hali mahsusi. Baada ya hilo, zikabili imani zako potovu moja baada ya nyingine huku ukijiuliza endapo imani hizo ni kweli na endapo zina mashiko, tumia dakika tano hivi kila siku kushadidia fikira chanya inayokinzana na ile inayokudidimiza. Ukifanya hivi kwa takriban siku thelathini imani yako itaanza kuchuku mkondo unaofaa.

Familia au rafiki anaweza kuwa kikwazo. Pasipo kufahamu familia yako na rafiki unaoandamana nao huathiri pakubwa hisia zako. Wakiwa na mtazamo hasi huweza kukushawishi ukaanza kuhisi wanavyohisi na kuyaona mambo kwa mtazamo wao. Kukabiliana na hali wapaswa kudhibiti hisa zako.

Tawala namna navyohisi na kukabiliana na hali mbalimbali bila kuathiriwa na wandani hawa. Epuka wandani wa aina hii kadri inavyowezekana, ikiwezekana, jitenge nao ili ujifunze kuwa na uhuru wa kufanya maamuzi yako binafsi bila kuathiriwa nao.

Unapaswa kupunguza ushirika hata na jamaa zako wanaokuingiza katika hali ya kutamauka. Punguza muda wa kukaa nao hasa wanapogeuka mkondo huu wa kukukatiza tamaa.

Mazingira hasi ni kizingiti kingine. Pengine huoni ukuruba baina ya maisha yako na wazingira unamokulia au unamokaa. Ukweli ni kwamba, huenda umedumu katika mazingira hayo na kuyazoea hata ukafikiri huwezi ukayabadilisha. Kadri navyohisi huna uwezo wa kuyabadilisha ndivyo unajizamisha zaidi katika mtazamo hasi. Ili kukabiliana na hali hii, unahitaji kuelewa kwamba fikra zako au za watangulizi wako ndizo zilikuvingiza katika mazingira haya. Kwa hivyo unapaswa kubadili mkondo wa fikra zako na uanza kujaribu mazoezi ambayo umekuwa ukuyaona kama usiyoyaweza. Hatua kwa hatua, utagundua panapo jitihada na uelekezi unaofaa kwamba mazoezi hayo yamekuwa mepesi na hivyo kukuhakikishia kuyabadilisha mazingira yako.

Hali zisizoridhisha ni wakati unapojikuta ukilalamika jinsi ulivyokerwa na hali Fulani, hii ndiyo sababu hasa ya kuwa na mtazamo hasi kuhusu hali hizo. Inaweza kukuwa vigumu kulikubali hili lakini kadri utakavyokubali mapema ndivyo utakavyoboresha maisha yako mapema. Kulalamika tu ndiko kutakudumisha katika hali zisizokuridhisha. Ili uyabadilisha maisha yako sharti ukome kulalamika na kuanza kujikwambua toka kwenye hali hizo.

Katika kufanikisha jambo lolote jema sharti viwepo vizingiti njiani. Mtendaji wa jambo lolote jema liwalo ana jukumu la kuibuka na mikakati mwafaka ya kuvikabili vizingiti hivi ili afanikishe ndoto yake. Hii ndiyo sababu unapaswa kuchukua hatua kutokea sasa ili kupanga na kutekeleza mikakati itakayoipindua mtazamo wako hasi uwe chanya. Kwa jinsi hii utayabadilisha maisha yako yawe ya kuridhisha zaidi na kuwa kielelezo kwa wengi waliotamaushwa na mitazamo hasi.

Maswali

- (a) Fupisha ujumbe wa aya **nne** za mwanzo kwa maneno 80. (alama 7, 1 ya mtiririko)
- (b) Kwa kurejelea aya mbili za mwisho, fupisha ujumbe kwa maneno 70. (alama 6, 1 ya mtiririko)

3. **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

- a) (i) Taja sauti zozote **mbili** zinazotamkiwa kwenye kaakaa gumu. (alama 1)
(ii) Eleza maana ya kirai. (alama 1)
(iii) Onyesha aina ya virai katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mwanafunzi mzuri husoma ndani ya darasa.
- b) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia “O” rejeshi. (alama 2)
Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.
- c) Tumia kiwakilishi cha nafsi huru (nafsi ya pili wingi) katika sentensi. (alama 2)
- d) Eleza matumizi ya —**m**” katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Simba aliuawa na wawindaji haramu nasi tukawaripoti.
- e) Weka vitenzi hivi katika hali ya kuamrisha wingi. (alama 2)
(i) -nywa
(ii) Tubu
- f) Andika ngeli za nomino zifuatazo. (alama 2)
(i) Uwele
(ii) Vita
- g) Kanusha (alama 2)
Mwanafunzi ambaye amefika ametuzwa.
- h) Changanua kwa kutumia mchoro wa matawi. (alama 2)
Mvuvi hodari alifurahi alipofanikiwa kuvua jodari.
- i) Eleza matumizi moja moja ya viwakifishi vifuatavyo. (alama 3)
(i) Mshazari:.....
(ii) Paradesi.....
(iii) Ritifaa.....
- j) Andika katika ukubwa. (alama 2)
Mke wa mzee huyu hupenda watoto sana.
- k) Tunga sentensi **moja** kutofautisha ‘_thibiti’ na ‘_dhibiti.’ (alama 2)
- l) Geuza sentensi hii hadi usemi wa taarifa: (alama 3)
—sitakuja shuleni kesho,” mwalimu mkuu akasema, —itaenda kuhudhuria mkutano Mombasa.:
- m) Huku ukitumia mifano, tofautisha sentensi ambatano na sentensi changamano. (alama 4)
- n) Ainisha mofimu katika neno: (alama 2)
Walichimba
- o) Kwa kutumia mifano, tofautisha kati ya kishazi huru na kishazi tegemezi. (alama 2)
- p) Eleza maana **mbili** zinazojitokeza kwenye sentensi hii. (alama 2)
Wale wamekuja kutuliza.
4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**
- a) Eleza juhudi zozote **tano** za serikali ya Kenya katika kukuza Kiswahili. (alama 5)
- b) Taja na ueleze pingamizi zozote **tano** zinazokwamiza juhudi za kukuza Kiswahili. (alama 4)

TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI YA NANDI KASKAZINI NA NANDI YA KATI 2016**KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIH****SEHEMU YA A: USHAIRI (SWALI LA LAZIMA)**

(alama 20)

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

- 1) Hadhira e pulikeni, kisa changu mpaeni,
Mpateni mweleweni, mchekeni, mlieni,
Funzo lake mpateni, uamuzi mfanyeni,
Kisa hiki asilani, sisahau maishani.
- 2) Cha nne niliingiya, mtoto kafurahiya,
Malkia ungedhaniya, duniani meingiya,
Mapambo lijipambiya, kung'ara kikang'ariya,
Kisa change chatokeya, mwanzowe nafunguliya.
- 3) Darasani lizembea, bidii sikutilia,
Starehe nakwambia, nilipenda najutia,
Kimadaha litembea, tausi nilitulia,
Kisa kilinigonjea, mtume! Ningalijua.
- 4) Muhula kutamatika, dafu sikufua, kaka,
Enda, Ewe, Embe, fika, alama duni, viraka,
Nilipokea waraka, mzazi kahitajika,
Kisa kijatambulika, nakuomba makinika.
- 5) Muhula wa pili sasa, nikarudia makosa,
Sikupigeni msasa, makali nikayakosa,
Kisu sikunoa hasa, sikukata cha darasa,
Kisa ndicho hicho sasa, ninakupa pasi pesa.
- 6) Sasa muhula wa tatu, umetimia wanetu,
Mtihani kama chatu, nimeuogopa, mtu,
Sijausomea katu, ningalilindaje utu?
Kisa mkasa wa chatu, kilinipata wa kwetu.
- 7) Mbwa katu hafi maji, kiona ufuko, maji,
Tajaribu sife maji, hata akiyanywa maji,
Ilibidi twende jiji, kuwasaka wajuaji,
Kisa change mfumbaji, sasa dawa lihitaji.
- 8) Mpango ulitolewa, mchango ulipangiwa,
Pesa tele litolewa, na simu kununuliwa,
Mtandao liwekewa, kunani kupakuliwa,
Kisa cha simu kujuwa, linifanya kupagawa.
- 9) Tulikata dari ona, simu yetu kufichana,
Usiku tulikutana, maswali kurushiana,
Majibu tulipeana, panga kabadilishana,
Kisa kinajulikana, vile nilivyokazana.
- 10) Niliyangoja majibu, nikiwa na hamu, babu,
Nilikimya kama bubu, nisije toa aibu,
Nilivichoma vitabu, bila kuwa na sababu.
Kisa kawa masaibu, kashindwa kuyaharibu.
- 11) Kutangazwa matokeo, nakumbuka hadi leo,
Lilishangaza toleo, sikuamini redio,
Lipokea matokea, yalinitia kimbio,
Kisa change mchocheo, haya yangu mapokeo.

- 12) Nilifeli mtihani, sababu simu juweni,
Najuta nisameheni, nijilaumu moyoni,
Ningalijua mbeleni, ningalisoma jamani,
Kisa nimemalizeli, wenzangu mzindukeni.
- 13) Watahiniwa mlipo, msiwe mithili popo,
Skuli kwenu kuwepo, nia mpate malipo,
Bidii hapo mlipo, toa uzembe pasipo,
Kisa change kingalipo, simu daima siwepo!

MASWALI

- a) Taja anwani mwafaka ya shairi hili. (alama 1)
- b) Fafanua mbinu **mbili** za lugha zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)
- c) Bainisha nafsi lengwa katika shairi hili. (alama 1)
- d) Changanua arudhi zilizotumiwa na mtunzi wa shairi hili. (alama 4)
- e) Andika ubeti wa kumi katika lugha nathari. (alama 4)
- f) Eleza maana ya maneno na vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa shairi. (alama 3)
- g) Eleza maana ya maneno na vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa shairi. (alama 3)
- (i) Sikukata cha darasa
- (ii) Yalinitia kimbio
- (iii) Kupagawa

SEHEMU YA B: TAMTHILIA**Jibu swali la 2 au 3**

2. –Nashukuru sasa umeanza kuona mambo yanavyostahili kwenda.”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Eleza sifa zozote **nne** za msemaji. (alama 4)
- c) Fafanua maudhui ya ufisadi kama yalivyoangaziwa na mwandishi wa tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 12)
3. Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo katika tamthilia – Mstahiki Meya. (alama 20)
- a) Majazi
- b) Taharuki

SEHEMU C: RIWAYA**KIDAGAA KIMEMWOZEA – K. WALIBORA****Jibu swali la 4 au 5**

4. –Kutowajibika kwa viongozi baada ya mkoloni kuondoka ni dhahiri.” Jadili kauli hii kwa mujibu wa Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)
5. –Hizi kurani zako ndizo zifanyazo nisije huku ...”
- a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
- b) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika dondoo hili kwenye riwaya. (alama 6)
- c) Eleza maisha ya msemaji yalivyokuwa kwa mujibu wa Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 10)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI.**Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine - K. Walibora na S.A. Mohammed -****Jibu swali la 6 au la 7****–Damu Nyeusi” (K. Walibora)**

6. –Nimemwita bwana huyu aje huku juu kusudi mumwone.”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Eleza sifa **tatu** za mzungumzaji. (alama 6)
- c) Jadili maudhui ya ubaguzi namna yanavyojitokeza katika hadithi husika. (alama 10)
- au**
7. Kwa kurejelea hadithi zozote **tano** katika Diwani Damu Nyeusi, jadili namna ambavyo wahusika wa kike wamesawiriwa. (alama 20)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

- 8.
- a) (i) Eleza maana ya ushairi simulizi. (alama 2)
- (ii) Eleza sifa **tano** za ushairi simulizi. (alama 5)
- b) (i) Eleza maana ya ushairi simulizi. (alama 3)
- (ii) Eleza sifa **nne** za matambiko. (alama 2)
- Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi.

MTIHANI WA TATHMINI YA ENEO GATUZI LA NANDI MASHARIKI, TINDERET NA NANDI KUSINI 2016
KISWAHILI
INSHA
102/1
KARATASI LA KWANZA

1. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la –Mwangaza” ukiangazia sababu na madhara ya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa nchini.
2. Vita vinavyoendelezwa na Serikali ya Kenya dhidi ya magaidi nchini Somalia vimeleta faidi nchini. Jadili.
3. Tunga kisha kinachothibitisha ukweli wa methali hii:
Mchuma janga hula na wa kwao.
4. Andika insha itakayoishia kwa:
..... alipohitimisha hotuba yake wanafunzi wote walikuwa wamepata mwanga kuhusu madhara ya mihadarati.

MTIHANI WA TATHMINI YA ENEO GATUZI LA NANDI MASHARIKI, TINDERET NA NANDI KUSINI 2016
KISWAHILI
102/2
LUGHA
KARATASI LA PILI

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Waziri wa uchukuzi Bwana Msafiri ametoa mwto kwa kila mwananchi kusingatia sheria za barabarani ili kumaliza visa vya ajali vilivyokithiri. Alisema kuwa ongezeko la ajali za barabarani linachangiwa pakubwa na watu binafsi.

Akiongea katika hafla ya kuzindua mbinu za kuhakikisha usalama barabarani, Bwana Msafiri alisema yasikitisha kuona kuwa ajali za barabarani zimeongezeka katika siku za hivi majuzi. Alielezea kuwa wizara yake imekerwa na utekelezaji wa majukumu na mapuza miongoni mwa wanaohusika na sekta ya uchukuzi.

Alisema wengi wa wenye magari wamepuza masharti mengi ambayo yaliwekwa na wizara, yaliyokusudiwa kugunguza ajali. Alisema magari mengi yamekuwa kachara na kwamba mengi yameng’olewa vidhibiti mwendo. Basi magari yanaendeshwa kwa kasi ya umeme. Hili limeongeza ajali kwa kiasi kikubwa. Mengi hayana mishihi ya usalama na wasafiri hukabiliwa na hatari wanaposafiri. Aliongeza kuwa sura ya magari hayo ni dhihirisho kuwa wenye magari wamepotoka kabisa, —magari mengi yamerembesha hata kwa picha chafu, jambo linalodhihirisha utovo wa mbeko na kutofuata sheria. Mengine yanacheza muziki kwa sauti ya juu hivi kwamba hata dereva na utingo hawawezi kusikia grudumu liking’oka. Baadhi yao yanaonyesha picha chafu chafu za video na kuufanya usafiri kuwa vyumba vya sinema chafu!” Alisema kutovaa sare kwa madereva na makondakta na kuwapakia abiria kupita kiasi ni kilele cha upuu wa sheria zilizowekwa.

Wasafiri pia wanapuza masharti yaliyowekwa kwa lengo la kuwafaa, —alisema waziri. Alisikitika kuwa wasafiri wengi hawafungi mishihi ya usalama hata inapopatikana, aidha wanakubali kuingia magari yaliyojaa tayari, hali inayoongezea uwezekano wa gari kupata ajali kwa kulemewa na uzito. Aliwakumbusha kuwa gali likipata ajali wakiwa wamepakiwa hivi, hawezi kugharamiwa na bima ya gari kwa vile bima yenyewe hukatiwa idadi mahususi ya wasafiri. Aliwalaumu watembeaji barabarani kwa kutozingatia sheria za kawaida. Alisema kwa mfano katika gurufu kuna mahali ambako kuna vivuko ili hawavitumii na wengine huishia kugongwa na magari.

Mwisho aliwalaumu maafisa wa trafiki wanaotekeleza majukumu yao. Akitisha kuwachukulia hatua kali, alisema kuwa yaskitisha kusikia kuwa wanachukua kadhongo na kuyaachilia magari yaliyo na kasoro badala ya kuyashtaki kulingana na sheria. Aliwaongezea lawama wasafiri kwa kunyamaza wanapoyaona haya yakitendeka machoni. Alisababisha kicheko aliposema kuwa baadhi ya wasafiri huwahimiza makondakta watoe chai haraka ili waendeleo na usafiri ya bila kujali hatari wanazojiingiza kwazo.

Akionya kuwa angechukua hatua ya kuregesha utulivu, alihitimisha kwa kusema kuwa wizara yake limetoa ilani kwa watumiaji wote wa barabarani. Alitoa makataa ya siku kumi na nne ambapo yoyote asiyefuata kaida zote za barabarani atachukuliwa hatua kisheria.

Maswali

- a) Fafanua sababu za mwito wa waziri wa uchukuzi Bwana Msafiri? (alama 2)
- b) Eleza jinsi wenye magaari wamechangia katika kukithiri kwa visa vya ajali barabarani? (alama 4)
- c) Fafanua mchango wa wasafiri katika kudorora kwa hali ya usalama barabarani. (alama 3)
- d) Eleza majukumu ya maafisa wa trafiki katika kudumisha usafiri kulingana na ufahamu. (alama 3)
- e) Toa visawe vya maneno yafuatayo. (alama 3)
 - (i) Kondakta:.....
 - (ii) Toa ilani:.....
 - (iii) Toa makataa:.....

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu imetoa mwongozo wa karo ambao unastahili kuzingatiwa katika shule za upili kufuatia haua ya shule mbalimbali kuongeza karo kwa viwango mbalimbali. Hatua hiyo inadhamiriwa kumking mzazi dhidi ya kunyanyaswa kifedha walimu hasa ikizingatiwa kuwa gharama ya maisha imepanda mara dufu.

Hata hivyo, ingekuwa bora ikiwa serikali ingefanya maamzi kwa ushirikiano na walimu wakuu maana kwa hakika suala la karo linahusu matumizi ya fedha ambayo pia huja na gharama zake. Gharama hii inaokana na ununuzi wa vitabu vya Kada na vya mazoezi, karatasi za uchapishaji mitihani, kwa kuwa wanafunzi sharti wasome na waandike.

Vilevile, gharama hii inatokana na ununuzi wa kemikali za kutumiwa katika maabara. Aidha kuna gharama ya kuendesha michezo na tamasha za muziki na drama. Wanafunzi wa shule za malazi hula na kulala na kwa sababu hiyo maamuzi ya kifedha lazima yafanywe.

Jambo ambalo linastahili kuangaliwa kwa makini ni viwango vya kupanda kwa gharama ya maisha. Lazima tujiulize gharama hiyo imepanda kwa kiasi gani na wapi? Kwa kweli haiwezekani kununua kilo moja ya mahindi kwa bei hiyo hiyo Kitale, Mombasa na Turkana. Vile vile ni muhimu kujiuliza ikiwa shule husika ni ya mashambani au ya mjini? Kwa hivyo sharti la kifedha ni muhimu katika kuamua karo ya shule na maeneo mbalimbali nchini.

Pili, hebu tuangalie ikiwa shule inavyohusika ni ya kiwango cha kaunti ndogo, kaunti au cha kitaifa. Hili ni muhimu kwa kuwa hali ya masomo katika shule hizo hutofautiana. Tofauti kuu hutokana na miundomisingi na programu za masomo zinazoendeshwa.

Kwa mfano, programu za kitahmini, kompyuta na zinazohusu ziara huhitaji fedha nyingi. Shule ambayo ina masomo kama vile muziki, sanaa na sayansikimu sharti zitoze karo ya juu kwa kuwa masomo hayo huandamana na gharama ya kununua vyombo na vyakula?

Sasa mbona fedha za ziada? Wanaotetea kupunguzwa kwa karo wana punguza mchango wa motisha katika ufanifu wa masomo. Ndio, baadhi ya shule hutoza karo ya juu ili kuwamotoha walimu kwa vyakula na kwa zawadi ili kuwastahi wanapopata matokea mema. Hali hiyo huwafanya kujikakamua kazini na kutoa huduma ya hali ya juu.

Fedha za ziada vile vile, hutumiwa kuwajiri walimu wa ziada ikizingatiwa kuwa serikali haijawaajiri walimu wa kutosha. Pia katika baadhi ya shule, wanafunzi huandaliwa vyakula spesheli tofauti na mseto wa maharagwe na mahindi almarufu maram uliozoeleka katika shule nyingi ikumbukwe kuwe lishe bora ni mojawapo ya haki za kimsingi kwa watoto ambayo sharti iheshimiwe.

Kwa marefu na mafupi yake, serikali haipaswi kuweka viwango sawa vya karo kwa kila shule kwa maana hilo huenda likazua mgogoro wa kiutawala katika shule nyingi. Shinikizo za kupunguzwa kwa karo inayotowza hasa katika shule za upili zinafaa kutetewa kimantiki wala si kihisia.

Mambo huenda yangukuwa tofauti ikiwa serikali ingewajibika kwa upande wake kwa kuwajiri walimu wa kutosha kuwaongeza walimu mshahara na kuwatambua kwa zawadi wanapofanya kazi nzuri na kuwapandisha vyeo. Hata hivyo, mgala muue na haki umpe; hatua kali zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya walimu wanaowatoza wazazi karo ya juu kupindukia ili kuendeleza maslahi yao ya kibinafsi.

Naamini kuwa hatua ya Waziri wa Elimu kukutana na washikadau katika sekta ya elimu kuhusu karo na uteuzi wa wanafunzi wa kujiunga na shule za upili ni ya busara na inafaa kuta mwelekeo mzuri kuhusu masuala tata yaliyopo kwa sasa.

(Makala kutoka gazeti la Taifa Leo, January 8, 2016)

- (a) Fafanua mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa katika kutathmini viwango vya karo katika shule nchini Kenya. (Maneno 65 – 70) (alama 8, 1 ya mtiririko)
- (b) Fupisha aya tatu za mwisho. (maneno 40 – 45) (alama 7, 1 ya mtiririko)

MATUMIZI YA LUGHA

- (a) Ukizingatia sehemu ya kutamkia, mwinuko wa ulimi na hali yam domo, tofautisha sauti zifuatazo. (alama 3)
/ e /, / l / na / u /
- (b) Ukitolea mfano eleza aina **mbili** za miundo ya silabi katika Kiswahili. (alama 2)
- (c) Eleza maana ya mghuno katika lugha ya Kiswahili. (alama 1)
- (d) Kwa kutolea mfano mwafaka, fafanua tofauti iliyopo kati ya kishazi na kirai. (alama 2)
- (e) Ukitolea mfano mwafaka, fafanua majukumu yoyote **manne** ya viambishi awali. (alama 2)
- (f) Nomino zifuatazo zinapatikana katika ngeli zipi? (alama 1½)

- i) Chumvi:.....
 ii) Nywele:.....
 iii) Mafuta:.....
- (g) Eleza matumizi ya kiambishi ku
Kulia kwake kulisababisha msongamano wa watu alikuwa. (alama 1½)
- (h) Tunga sentensi yenye muundo wa:
 N + V + T + H + N + E + U + T. (alama 4)
- (i) Yakinisha katika umoja:
 Msingalivumilia nyakati ile msingalipata zawadi kubwa. (alama 2)
- (j) Andika katika udogo.
 Jijipu lilipasuka lenyewe. (alama 1)
- (k) Ukitolea mfano fafana njia zozote tatu zinazotumiwa katika uunjdaji wa maneno. (alama 3)
- (l) Ukitungia sentensi, onyesha matumizi ya vivumishi vya nomino. (alama 2)
- (m) Tunga sentensi kubainisha matumizi ya vivumishi vya nomino katika ngeli ya U – I; katika umoja na wingi. (alama 2)
- (n) Ukitolea mfano mwafaka, eleza tofauti iliopo katika kauli zifuatazo.
 Kutendana na kutendana. (alama 2)
- (o) Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo.
 Mwamburi alitumia ufunguo kumfungulia Rashid mlango. (alama 2)
- (p) Andika katika usemi wa taarifa:
 –Nataka ufikirie sana juu ya maisha yako ya ndoa. Sitaki uishi maisha yasiyo na mweleko.” Babu alinishauri.(alama 3)
- (q) Kwa kutoa mfano, eleza matumizi mawili kila mojawapo wa alama zifuatazo:
 i) Ritifaa
 ii) Kama kituo
- (r) Eleza maana ya msemo ufuatao :
 Kula kitana. (alama 2)
3. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**
- a) Eleza maana ya lugha rasmi. (alama 2)
- b) Fafanua sifa zozote za lugha rasmi. (alama 8)

MTIHANI WA TATHMINI YA ENEO GATUZI LA NANDI MASHARIKI, TINDERET NA NANDI KUSINI 2016**KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIH****1. SEHEMU YA A: USHAIRI.**

(alama 20)

SIWE?

1. Siwe ulosema jana, ya kuwa u mashuhuri?
Ya kuwa wajuwa sana, aidha huna kiburi?
Nchini wajulikana, mwanasiasa mahiri,
Bungeni tukuajiri?
2. Siwe ulotushawishi, kwa chumvi na kwa sukari,
Na matamu matamshi, ukaziteka suduri,
Ukanena penya moshi, moto ndiyo yakwe siri,
Nawe ndiye hiyo nari?
3. Siwe uloji'ta moto, uwakao biribiri,
Kamba tatia fukuto, Litakalo leta kheri',
Utatufunua mato, Maisha yawe mazuri,
Tukupe kura waziri?
4. Siwe ulosema hayo, na mengi ukabashiri,
Ukamba wafata nyayo, nyayo ziso utiriri,
Tusiwe na wayowayo, wa kufikirifikiri,
Tukuachie ujari?
5. Siwe tulokuinua, Mabegani kama mwari,
Tungawa twalemelewa, waume tukajasiri,
Kamba tukikuchaguwa, mema kwetu yatajiri,
Tukakeyi kusubiri?
6. Siwe ulotugeuka, kwamba leo u waziri,
Wajiona melimuka, tena ukawa ayari,
Walaghai ukicheka, ukuu umekughuri,
Leo mekuwa hodari?
7. Siwe ulojawa raha, za hino yetu sayari,
Ukawa ja vile shaha, hatukupati shauri,
kutuona ni karaha, wakatiwo twahasiri,
Ushakiya msitari?
8. Siwe uliyetughura, ukafunga na safari,
Ukaelekea bara, Kwa wenzio matajiri,
Ukatuacha majura, na tama kukithiri,
Kanama Ushaghairi?
9. Siwe uliyetuasi, ukenda pasi kwaheri,
Mbona hutwambii nasi, tukajua yetu shari,
Leo una masidisi, husemi na aso gari,
Ndio mezidi jeuri?
10. Siwe lotwaa mgwisho, ukawa wajifakhiri?
Chenye mwanzo kina mwisho, hilo wajuwa dhahiri,
Vyaja kutoka vitisho, kwani hayo sidahari,
Mambo mengimdawari?
11. Siwe utakayeiza, mwishowo ukidhihiri,
Siku itayoteleza, kuja kwetu ansari,
Kuja kutubembeleza, kwa nyunga nalo khamri,
Tauya nazo nadhiri.

MASWALI

- a) Mtunzi wa shairi hili ana dhamira gani? (alama 2)
- b) Taja na ueleze bahari tatu za shairi hili? (alama 3)
- c) Onyesha jinsi mtunzi alivyotumia idhini ya kishairi. (alama 3)
- d) Taja na ufafanue tamahali ya usemi iliyotawala katika shairi hili. (alama 2)
- e) Anayerejelewa alibailika vipi? Eleza. (alama 4)
- f) Andika ubeti wa tisa kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- g) Mshairi ana maana gani kwa kusema:

- (i) Wakatiwo twahasiri. (alama 1)
(ii) Ukaziteka suduri. (alama 1)

SEHEMU YA B: RIWAYA : KIDAGAA KIMEMWOZEA

Jibu swali la 2 au 3

2. —.....usiniweke pembeni kama tanbihi, mimi na wanawake wenzangu kama wanaume wengine wafanyavyo waandikapo.....”
a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Bainisha tamathali ya usemi iliyotumika hapa. (alama 2)
c) Hakiki usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya hii. (alama 14)

AU

3. Mtemi Nasaba Bora ni kielelezo cha viongozi wa kiafrika wanaondeleza uongozi mbaya. Jadili kauli hii. (alama 20)

SEHEMU C: TAMTHILIA

T. AREGE: MSTAHIKI MEYA

Jibu swali la 4 au 5

4. –Mtu huvuna alichopanda, ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi.”
i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
ii) Anayeambiwa alisema nini baada ya kuambiwa haya? (alama 2)
iii) Thibitisha kuwa wanacheneo walipanda pojo. (alama 14)

AU

5. Eleza jinsi wanacheneo walivyotatua shida zinazowakumba. (alama 2)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

Jibu swali la 6 au la 7

K. Walibora na S.A. Mohamed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyinginezo.

“Damu Nyeusi” (Ken Walibora)

6. –Nashangaa vile kwetu tunavyoabudu watu hao wasiotujali.”
a) (i) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(ii) Jadili ukweli wa kauli hii. (alama 10)
b) Bainisha matumizi ya mbinu ya ishara kwa kurejelea hadithi ya gilasi ya mwisho makaburini. (alama 6)

AU

“Shaka ya Mambo” (Farouk Topan)

7. Eleza hali ya shaka ya mambo inavyojitokeza katika hadithi ya shaka ya mambo. (alama 20)

8. **SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

- a) Miagizo ni nini? (alama 2)
b) Taja sifa **nne** za maigizo. (alama 4)
c) Eleza mambo **manne** anayopaswa kufanya mwigizaji ili kufanikisha uigizaji wake. (alama 8)
d) Ni nini umuhimu wa maigizo? (alama 6)

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KANGEMA– 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**

1. Andika taarifa itakayosomwa katika idhaa ya Redio ya Wakwetu kuhusu vyanzo vya kuporomoka kwa maadili miongoni mwa vijana.
2. Hatua zinazochukuliwa na serikali kukabilia'na na vileo nchini zinafaa. Jadili.
3. Andika insha kudhihirisha ukweli wa methali :
Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.
4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo.
. . . . Tangu siku hiyo uhusiano wangu na rafiki yangu ni kama wa mafuta na maji.

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KANGEMA– 2016**KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU (alama 15)****Soma taarifa inayofuata kisha uyajibu maswali**

Nyumba ya Ndolo ya vyumba viwili ilikumbwa na hali mbili tofauti usiku huo. Chumbani alimolala Ndolo mwenyewe, kimya cha kaburi kilikatizwa na misono yake. Mara mojamoya alijigeuza kitandani na kuzifanya mbavu za kitanda zilalamikia : uzito wake. Katika chumba kingine, misono ya Ndolo na milio ya chenene ilimkirihhi Msela. Kuzidisha, mawazo kuhusu hali ya mamake na unyama aliotendewa babake yalimtoroshea usingizi. Akasalia kujilaza kwenye mkeka wake.

Kila alipotafakari maneno ya mzee Ndolo ndivyo Msela alivyoziidi kuamini kwamba matatizo ya familia yao yalisababishwa na Mzee Bonga. Lakini yote hayo akayapuuza. Kubwa kwake lilikuwa ni kumwona mama yake na kujua ni hatua gani atakayochukua licha ya uzito alioona mbele yake kwa kutokuwa na kipato. Msela alijikuta kwenye mtihamu mgumu ulioifanya mishipa ya kichwa kusimama na kichwa kumuuma.

Kwa sababii ya maiimivu hayo, Msela alijisogeza na kujiegemeza kwenye ukuta. Akawa anatazama iinsi Mungu alikuwa akiufanya muujiza wake ambao alikuwa ameukosa kwa muda. Alifurahi kuliona jua likipenyeza miale yake kisha kujitokeza na kuangaza dunia. Ingawa macho yake yalifurahia mapambazuko hayo, moyo wake ulikuwa na machungu. Akili yake ilikuwa na zigo zito la kutafuta ufumbuzi ambao kwa upande wake ilikuwa ni ndoto.

Msela alijiuliza mengi katika nafsi yake. Aliisaili nafsi yake kuhusu hisi za ndugu zake, kuhusu hali ya mama yao aliyesemekana kuwa mwendawazimu, na ikiwa walifahamu hilo. Alitaka kujua alikokula na alikolala mamake katika hali yake hiyo. Kila fikira iliyompitikia akilini ilitaka kupasua mishipa ya kichwa chake. 'Ina maana hawaoni au nao wamekuwa na roho ya korosho kama Mzee Bonga?' alijisaili Msela. Katika maswali yote hayo, alikosa majibu isipokuwa kuzidisha maumivu ya kichwa. Isingekuwa kwa machozi yaliyompunguzia baadhi ya machungu, labda angegeuka hayawani.

Macho ya Msela yalikuwa yamevimba, tena mekundu kutokana na ukosefu wa usingizi. Mwili wake nao ulionekana kunyong'onyea kwa sababu ya mazonge ya mawazo. Alichukua kikopo kilichochocha cha maji na kunawa uso kisha akaenda kukaa juu ya jiwe. Kibaridi kilichotokana na mvua iliyokuwa ikinyesha kilimpiga lakini hakujali. Angejali vipi yeye katika mtafaruku wa hali ya mamake?

Ingawa Mzee Ndolo alimwita ndani ili aipishe mvua, Msela alidinda. Badala yake, aliendelea kuuachilia mwili wake kuloweshwa na michonyoto ya mvua. Kila alivyofikiria maisha ya wendawazimu ndivyo moyo ulivyoziidi kumuuma. Akawa yuajiuliza mama yake aliukosea nini ulimwengu hata apate adhabu ile. Halafu fumo lake la mwisho moyoni ni madhara ya mvua na baridi ile kwa mamake. Hana makao, hana mavazi mazito, hana chochote! Alipowazia makazi ya jalalani na majumba mabovu ambayo siku zote amekuwa akiwaona wendawazimu wakifaliwa kwayo, aliachama.

Maswali

- | | |
|--|-----------|
| (a) Eleza ukinzani ulio katika nyumba ya Ndolo. | (alama 2) |
| (b) Ni yapi yaliyomkoshesha usingizi msela? | (alama 3) |
| (c) Kwa nini Msela hakuweza kuibadili hali yake. | (alama 4) |
| (d) Taja chanzo cha madhira ya Msela. | (alama 1) |
| (e) Muujiza wa Mungu unatoa taashira gani kwa hali ya msimulizi? | (alama 2) |
| (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao ukirejelea taarifa. | (alama 3) |

- i) robo ya korosho
- ii) alichama
- iii) kunyong'onyea

2. UFUPISHO (alama 15)

Soma kifungu kisha ujibu maswali

Upo msemu usemao kuwa kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa upishi. Msemu huu unaafiki kabisa ari ya watu wazima wengi ambao licha ya umri wao, wamo mbioni kutafuta elimu ili mbali na kupata nuru, wajiunge na wasomi wengine katika kuikuza na kuiendeleza jamii. Ni kwa sababu hii ndipo serikali, kwa ushirikiano na mashirika mengi yasiyokuwa ya kiserikali, imekuwa mstari wa mbele kutoa tunu hii kwa wazee ili kukata kiu yao ya elimu.

Watu wengi wa umri wa makamo ambao labda walikosa kumaliza masomo ya kiwango fulani au walikosa kabisa kwenda shuleni kwa sababu mbalimbali, hasa za kifedha, wamekuwa wakiweka elimu kama mojawapo ya majukumu yao ya utuuzima. Hii imekuwa dhahiri hasa baada ya serikali ya Kenya kuanzisha mpango wa elimu bila malipo katika shule za msingi, kwani idadi ya watu wazima ambao wamejitokeza kunufaika na mpango huo haisemeki. Pamoja na mpango huo, wapo wale ambao walikosa kusoma au kumaliza masomo kwa sababu ya karo, na kwa sababu sasa wana mapato, wameazimia kujiendeleza ili wapate vyeti. Hii ndiyo maana si ajabu kuona hata wafungwa kwenye magereza wakifanya mitihani ya kitaifa.

Elimu ya watu wazima hutekelezwa kwa njia mbalimbali. Kunayo elimu ambayo inalenga kuwapa watu hawa ujuzi wa kujiendeleza kiuchumi. Kutokana na ufundi wanaofundishwa, ambao huwa ni kazi kama useremala, umekanika, ushoni, usonara na kadhalika, huwawezesha kujitegemea kimapato, kwa hivyo wakaweza kuwapa wanao fursa ya kufaidi kile ambacho wao walikikosa.

Kunayo pia aina ya elimu ya watu wazima ambayo inaegemea maslahi ya watu hawa, hasa mafunzo kuhusu afya na usafi, masuala ya kifamilia na mahusiano na pia suala la ulezi. Kwa kufanya hivi, watu hawa hupata motisha ya kutangamana na watu wengine na kubadilishana nao mawazo kuhusu masuala yanayoathiri maisha yao Ndiyo sababu utapata watu wa aina hii wana ujuzi mkubwa wa kila kitu kinachoendelea katika kila kona ya nchi.

Aina nyingine ya elimu kwa watu wazima ni ile ya umma, inayohusu hasa masuala ya kisiasa. Mara nyingi, utawaona wakongwe wakipishwa kwenye foleni ili kwenda kupiga kura. Hii ni kwa sababu, mbali na kuwa huenda wakawa wamestaafu kikazi, bado wana jukumu muhimu sana katika kufanya maamuzi ya kisiasa kwa ajili ya vizazi vyao. Hivyo basi, serikali hufanya kila juhudi kuhakikisha kuwa hamasisho imetolewa kwa kila mwananchi, pamoja na kutoa mafunzo ya namna ya kupiga kura ili kura zisiharibike, hasa baada ya mtu kupitia utaratibu mrefu na wenye kuchosha wa kupiga kura. Kwa hili la kisiasa, watu wazima wengi hushangaza kwa jinsi wasivyoweza kushawishika kufanya maamuzi yanayokwenda kinyume na maazimio yao.

Maswali

- (a) Eleza masuala muhimu katika aya mbili za kwanza kwa maneno 60. (alama 7)
 - (b) Fafanua jinsi elimu ya watu wazima hutekelezwa ukitumia maneno 60 (alama 6)
3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)
- a) Taja sifa nne za sauti /a/ (alama 2)
 - b) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo: (alama 3)
Milangoni
 - c) Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Wao watakuja kuwa waandishi maarufu.
 - d) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)
Huyu amekuja kutuliza.
 - e) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo . (alama 2)
Mahindi ya mama yamekua kwa kupata mvua ya kutosha.
 - f) Nyambua kitenzi 'chwa' katika kauli ya kutendea kisha ukitungie sentensi. (alama 2)
 - g) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya neno 'vibaya' kama: (alama 3)
 - (i) Kivumishi
 - (ii) Kielezi
 - (iii) Kiwakilishi
 - h) Changanua kwa kutumiajedwali. (alama 2)
Yeye alifaulu ingawa hana adabu
 - i) Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 2)
Je ni nani alingoa mti wa kiprono
 - j) Taja msemu mwingine wenye maana sawa na : (alama 1)
piga maji
 - k) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha pekee cha kusisitiza katika ngeli ya U/U (alama 2)
 - l) Bainisha matumizi ya 'po' katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Alipowasili alionyesha walipo

- m) Bainisha matumizi ya 'ni'
Kimbieni! Huyu ni mnyama aliyeniuma mguuni. (alama 2)
- n) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana ya vitate rika na lika. (alama 2)
- o) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo .
Jane alitengenezewa kiti na fundi kwa nyundo (alama 3)
- p) Unda nomino dhahania kutokana na kitenzi - abudu. (alama 1)
- q) Tunga sentensi kwa kutumia kivumishi cha sifa kisichoambishika. (alama 2)
- r) Andika kwa wingi.
Seremala huyo alikula ndizi kwa uma. (alama 2)
- s) Kanusha sentensi ifuatayo bila kutumia kiunganishi. (alama 2)
Iwapo mvua itanyesha wakulima watapanda mapema.
- t) Eleza maana ya kiimbo. (alama 1)
- 4. ISIMU JAMII (alama 10)**
- a. Taja nadharia tatu zinazoelezea chimbuko la lugha ya Kiswahili. (alama 3)
- b. 'Mkinichagua, mimi tutaimarisha masomo, huduma za afya, barabara na pia maji mtapata hivi karibuni. (makofi na vigeregere)
- (i) Tambua sajili hii (alama 1)
- (ii) Eleza sifa sita za sajili hii. (alama 6)

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KANGEMA– 2016**KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIHI****1. LAZIMA : SEHEMU YA 'A'****USHAIRI**

Ole wangu! Ole wangu, nisikize Mola wangu,
Lipokee ombi langu, wanisikize wenzangu,
Washike ujumbe wangu, uloleta Mola kwangu,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Amri kumi za Mola, mumekwisha zikiuka
Ndipo hamuwezi lala, mumekwisha vurugika,
Mumemsahau Mola, ndipo nanyi mwasumbuka,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Mwaabudu mashetani, ushirikina ni mwingi,
Munaiba hadharani, waongo nao ni wengi,
Mwajawa na taraghani, na wazimu mwingi,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora,

Mwauana ovyoovyo, mwasemana ndivyo sivyo,
Fitina nazo zilivyo, mwarogana vivyo hivyo,
Matusi ni vile sivyo, munaisha ka isivyo,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Kuna dawa za kulevya, na hata pembe haramu,
Na ukimwi nakujavya, unaua wanadamu,
Na mimba nazo kuavya, watoto ni marehemu,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Wengine nao hudai, waoe jinisi moja,
Ati mwingine hafai, heri sawia ya mja,
Haya maoni ni hoi, tupinge kila mmoja,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.
Ploti mwazinyakua, na viwanja vya mipira,
Makaburi mwala pia, mabibi mwateka nyara,
Ibada zikifikia, mwafurika kwa majira
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Wengi tuwachaguo, si viongozi ni waizi,
Tamaa walio nao, yaongoza maamuzi,
Mishahara ile yao, huongezwa kila mwezi,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Usalama hatunao, wasiwasi umezidi,
Waja kiwa makazio, huogopa magaidi,
Mabomu walipuao, huruma wamekaidi,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Beti kumi namaliza, dua yangu imetimu,
Mungu amekwisha anza, kuhukumu mwanadamu,
Wote walojipotoza, waiepuke hukumu,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

MASWALI

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)
- (b) Shairi hili linaweza kuwekwa katika bahari kadhaa. Taja na ueleze bahari zozote tatu. (alama 3)
- (c) Taja na ueleze mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika ubeti **wa kwanza**. (alama 3)
- (d) Eleza sababu ya mshairi kutumia alama ya ritifaa katika ubeti wa nne (alama 2)
- (e) Tambua uhuru wa kishairi uliotumika katika ubeti wa tisa mshororo wa tatu na ueleze umuhimu wake. (alama 2)

- (f) Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi. (alama 4)
 (g) Taja mifano mitatu ya uozo anaolalamikia mwandishi. (alama 3)
 (h) Eleza toni ya mwandishi. (alama 2)

SEHEMU YA B**TAMTHILIA:****Mstahiki Meya : Timothy M. Arege****Jibu swali la 2 au la 3**

2. Mbona isiwe kweli? Wewe panga uwaleta tule matunda ya jasho letu nao watoto.
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Eleza mbinu mbili za uandishi katika dondoo hili. (alama 2)
 (c) Eleza yaliyopangwa baada ya usemi huu. (alama 14)
 3. Fafanua jinsi maudhui ya unafiki yamejidhihirisha katika tamthilia ya Mstahiki Meya, ukirejelea wahusika wowote watano. (alama 20)

SEHEMU YA C**RIWAYA:****Kidagaa kimemwozea : Ken Walibora****Jibu swali la 4 au la 5**

4. Mtoto ni mtoto hata likiwa bonge la nyama. Mtu hupata ajaliwalo sio alitakalo.
 (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Eleza tamathali ya lugha iliyotumika katika usemi huu. (alama 2)
 (c) Ukirejelea riwaya thibitisha kuwa mtu hupata ajaliwalo silo alitakalo. (alama 14)
 5. "Ndoto za uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi, jinamizi inayowafanya wazalendo kulia Kidagaa kimetuozea". Ukirejelea riwaya eleza sababu za wazalendo kulia Kidagaa kimetuozea. (alama 20)

SEHEMU YA D:**HADITHI FUPI****Damn Nyeusi na Hadithi nyingine : Ken Walibora na Said A. Mohamed****Jibu swali la 6 au la 7**

6. "Ingawa walifahamu sababu ya kuitwa pale mpango uliokuwepo ulikuwa usiku wa giza."
 (a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
 (b) Eleza tamathali iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
 (c) Onyesha vile wahusika mbalimbali hadithini waiivyoathiriwa na sababu ya kuitwa pale. (alama 14)
 7. Uozo katika jamii ni maudhui yaliyoshughulikiwa pakubwa katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*. Kwa kurejelea hadithi zozote tano fafanua kauli hii. (alama 20)

SEHEMU YA E:**FASIHI SIMULIZI**

8. a) i) Eleza maana ya vitendawili. (alama 2)
 ii) Chambua muundo wa vitendawili ukizingatia hatua muhimu katika utendaji. (alama 7)
 b) i) Ulumbi ni nini? (alama 2)
 ii) Eleza sifa zozote tano za ulumbi. (alama 5)
 iii) Ulumbi hutekeleza majukumu gani katika jamii. (alama 4)

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KERICHO– 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA****1. LAZIMA**

Kumekuwa na visa vingi vya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa humu nchini. Waziri wa Elimu ameitisha mkutano wa kamati aliyobuni kujadili chanzo na suluhisho la swala hili nyeti. Ukiwa katibu wake, andika kumbukumbu za mkutano huo.

2. Michezo na shughuli nyinginezo nje ya darasa zinawapotezea wanafunzi wakati wa masomo na zinafaa kupigwa marufuku. Jadili.

3. Andika kisa kischothibitisha ukweli wa methali hii: Kutangulia si kufika.

4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa :

. . . . Milipofungua bahasha na kusoma kijikaratasi cha matokeo, ukweli ulinibainikia kuwa hali yangu haikuwa rahisi.

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KERICHO– 2016**KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU (alama 15)**Soma taarifa inayofuata kisha uvaiibu maswali

Matumizi ya sheng' yameshamiri sana nchini Kenya hata miongoni mwa vijana. Ni kilugha ambacho kinakisiwa kuzuka katika miaka ya 60 na 70 katika makazi ya mashariki mwa jiji la Nairobi kama vile Kaloleni, Mbotela/ Bahati na kadhalika.

Kwa sasa ni kilugha kilichoenea kwingi nchini Kenya na kuwa kitambulisho cha takriban vijana wengi. Wataalam mbalimbali wanabainisha nadharia mbalimbali kuhusu chanzo cha lugha hii. Kuna nadharia mbili kuu kuhusu asili ya lugha ya Sheng: kwamba kilugha hiki kiliibuka kutokana na wahuni na wakora jijini Nairobi ambao lengo lao lilikuwa kuwasiliana kwa siri. Nadharia nyingine ni kuwa kilichipuka kutokana na vijana ambao walizua lugha ya kuwasiliana baada ya uhuru (kwa sababu walikichukia Kiswahili ambacho walikiona kama lugha ya uboi)

Dhana hizi kwa muda mrefu, zimeathiri mitazamo kuhusiana na kilugha hiki. Kwa sasa ni kilugha ambacho yjiasambaa katika sehemu mbalimbali za Kenya na watu wa matabaka mbalimbali wanakitumia. Kilugha hiki kimeanza kuashiria uhalisia mkubwa wa maisha ya kisasa, zaidi katika jamii ya Wakenya. Aidha, sheng imejitanzua kutoka hali ya kuwa kilugha cha maongezi pekee na sasa kinatumwa katika baadhi ya vitabu, hata waandishi wa vitabu wameanza kukitumia. Kwa mfano, katika miaka ya 80, David Mailu katika kitabu chake 'Without Kiinua Mgongo' alitumia Sheng. Katika siku za hivi karibuni, riwaya ya 'Kidagaa Kimemwozea' iliyoandikwa na Ken Walibora kilugha cha sheng kimepewa nafasi kama kitambulisho cha vijana kupitia kwa mhusika DJ Bob.

Vilevile kumezuka vyombo vya habari kama redio, mfano idhaa ya Ghetto, redio ambayo inaendeleza mawasiliano kwa matumizi ya Sheng. Kuna vipindi vya matangazo ya kibiashara katika runinga ambayo yanaendelezwa kwa Sheng. Kwa mfano, katika 'gazeti la Taifa Leo, kuna ukumbi wa 'Mchongoano' ambao umekuwa ukiendelezwa kwa Sheng.

Nchini Kenya ambapo asilimia 60% ya idadi ni vijana, Sheng imetokea kuwatambulisha vijana. Katika enzi hii ya **Teknohama**, wanaomiliki vyombo vya habari na sekta nyingine za biashara wamegundua kuwa matumizi ya Sheng ndiyo njia mwafaka zaidi ya kulifikia soko kubwa la vijana kwa ajili ya kueneza matangazo ya bidhaa na huduma za kibiashara. Kwa hivyo, Sheng imekuwa daraja la kuwafikia na kuwavutia vijana.

Hata hivyo, kwa upande mwingine matumizi ya Sheng yamelaumiwa na walimu wengi katika shule za msingi na zile za upili kuwa ni sababu mojawapo kuu ya kushuka kwa matokeo ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza miongoni mwa wanafunzi. Sheng imelaumiwa kwamba inasababisha wanafunzi kutozingatia mafunzo ya kanuni za sarufi na tahajia au maendeleo. Wataalam wanadai kuwa ni **msimbo** ambao hauzingatii sheria za sarufi na tahajia kwa sababu zisizofahamika, kwani ingawa muundo wake wa kisarufi hushahabiana na ule wa Kiswahili, Sheng hupuuza sarufi ya Kiswahili katika matumizi yake.

Ingawa sheng imekuwa ikipigwa vita, kuna wataalam ambao wana mtazamo kwamba juhudi hizo haziwezi kufanikiwa kwani Sheng ni chombo cha mawasiliano miongoni mwa vijana na kwa hivyo ina umuhimu wake ambao hauwezi kufumbiwa macho. Wanasema kuwa ni chombo ambacho kinafumbata hisia na mshikamano wa kizazi kipya kama ilivyojitokeza katika kauli mbiu ya mgombeaji urais mwaka wa 2012, 'Tunawesmake.

Katika hali ambapo kiwango cha ubora wa matokeo ya Kiswahili **validorora** katika mihani wa kidato cha nne (KCSE) mwaka wa 2012 na kuwa asilimia 35.81 pekee yakilinganishwa na asilimia 48.82 ya mwaka 2011, Sheng imekuwa ikilaumiwa kuwa ndicho chanzo cha kudorora kwa viwango vya ubora wa matokeo. Baadhi ya hao wataalamu wanasema kwamba Sheng haipaswi **kuhujumiwa**. kinachohitajika kufanywa ni kuwaelimisha vijana kuhusu mipaka ya matumizi yake.

Maswali

- a) Taja mada ya kifungu hiki. (alama 1)
- b) Fafanua nadharia mbili zilizoeleza asili ya lugha ya sheng. (alama 2)
- c) Eleza matumizi bainifu ya kilugha cha Sheng katika jamii ya sasa. (alama 4)
- d) Taja matokeo hasi ya matumizi ya Sheng katika jamii. (alama 2)
- e) Ni kwa nini mwandishi Walibora ameshirikisha matumizi ya Sheng katika kazi yake ya *Kidagaa Kimemwozea* (alama 2)
- f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu hiki. (alama 4)
- i) Teknohama
- ii) kudorora
- iii) msimbo
- iv) Kuhujumiwa

2. UFUPISHIO (alama 15)**Soma kifungu kisha uiibu maswali**

Ubinafishaji wa mashirika ya umma ni nguzo kuu katika ulimwengu wa leo. Kimsingi, ubinafsishaji ni hatua na harakati zinazochukuliwa kupunguza kushiriki kwa serikali katika uendeshaji wa mashirika na kuhimiza kupanuka kwa sekla ya kibinafsi.

Serikali huweza kuhimiza, kutokana na uuzaji, uhawilishaji wa mali kutoka umiliki wa umma hadi kwenye umilikaji wa sekta ya kibinafsi. Aidha, serikali inaweza kuuza hisa zake kwenye mashirika ya umma. Njia nyingine ni kuchochea ugavi wa zabuni kupitia kwa mikataba ambayo inashindaniwa na mashirika au kampuni tofauti. Lengo kuu la ubinafsishaji ni kuigatuanafasi ya serikali katika utendakazi na uendeshaji wa mashirika.

Uuzaji wamashirika ya kiserikali au hisa huwa chanzo cha mapato yanayoweza kutumiwa kuendesha miradi mingine, Hii ni njia ya kupunguza harija ya serikali inayotokana na uendeshaji wa mashirika yasiyoleta faida. Ubinafishaji huzuia uwezekano wa kuingiliwa kwa mashirika na wanasiasa, huimarisha utamaduni mpya wa muundo wa mashirika na huvunja uhodhi wa kiserikali. Ubinafishaji huweza kuatika mbegu za ujasiriamali wa raia kutamani kuanzisha amali tofauti.

Ubinafishaji huweza kuyaruhusu mashirika ya kimataifa kutwaa mashirika muhimu nchini, kufutwa kazi kwa wafanyikazi na kuongezeka kwa umaskini. Ubinafishaji wa sekta zinazohusiana na elimu na afya huweza kuathiri vibaya wenye mapato ya chini.

Ubinafishaji haumaanishi ufanisi wa utendakazi wa makampuni na mashirika. Aidha, ikiwa haupo utaratibu mzuri wa kutathmini au kupima thamani za hisa pana uwezekano wa hisa zinazouzwa kupewa thamani ya juu au ya chini.

Maswali

- a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa kifungu, andika muhtasari wa aya ya kwanza na ya pili. (Maneno 35 - 40) (alama 6, 1 ya utiririko)
- b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya ya tatu na ya nne. (Maneno 45 - 50 - alama 9, 1 ya utiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA.

- a) i) Eleza maana ya sauti. (alama 1)
- ii) Taja sifa mbili bainifu za vokali /i/ (alama 1)
- b) Tunga sentensi moja yenye viungo vya sarufi vifuatavyo; (alama 40)
- i) Kikanushi
- ii) Kiima katika nafsi ya pili wingi.
- iii) Kiwakilishi cha wakati uliopita.
- iv) Mtendewa katika nafsi ya tatu wingi.
- v) Mzizi wa kitenzi cha silabi moja.
- vi) Mnyambuliko wa kitenzi kauli ya kutendea. (alama 3)
- c) Huku ukitoa mifano, toafutisha kishazi huru na kishazi tegemezi. (alama 3)
- d) Ainisha vielezi katika sentensi hii. (alama 2)
- Mwalimu wetu anayefundisha kistadi hutembea kwa maringo
- e) Huki ukitoa mifano, fafanua miundo mitatu ya majina katika ngeli ya U-ZI (alama 3)
- f) Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha maana ya neno 'ilimradi' (alama 2)
- g) Andika kifungu kifuatacho katika msemo wa taarifa; (alama 3)
- Amani alilia, "Marafiki zangu, majambazi wamenipiga na kunipora pesa zangu zote. Mali yangu sasa nimbaya."
- h) Kanusha (alama 2)
- Ukiona vyaelea vimeundwa.
- i) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari, (Alama 4)
- Wakazi waligawiwa vyandarua vya mbu lakini wanavitumai kujengea nyua.
- j) Andika upywa sentensi ifuatayo ukianzia yambwa tendwa. Wakulima waliwakatia ngamia wote majani ya mti huo. (alama 2)

- k) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya mstari. (alama 2)
- l) Tambua matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Jino la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbaji yule.
- m) Sahihisha kwa kutumia kirejeshi cha mazoea. (alama 2)
Kambarau ambao iliyoundwa vyema haitatizi.
- n) Andika visawe vya maneno haya; (alama 2)
i) Wajihi
ii) Laazizi
- o) Tunga sentensi kudhihirisha maana ya msembo ufuatao. enda benibeni. (alama 2)
- p) Bainisha aina za viwakilishi katika sentensi ifuatayo; (alama 2)
Ule wangu niliopalilia unakua vizuri
- q) Andika kinyitme (alama 2)
Sufuria iliyoinjikwa mekoni ni chafu.
- 4. ISIMUJAMII (alama 10)**
- a) Eleza maana ya usanifishaji wa lugha, (alama 2)
- b) Fafanua umuhimu wa usanifishaji wa (alama 8)

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KERICHO– 2016

KISWAHILI

102/3

KARATASI YA TATU

FASIHI

1. LAZIMA : SEHEMU YA 'A'

USHAIRI

SIPENDI KUCHEKA

Pana jambo ninatukiya, kwangu hilo ni muhali,
Kitenda naona haya, kujishusha yangu hali
Sipendi unipe hidaya, sipendi kutenda hili
Sipendi mimi kucheka

Sipendi mimi kucheka, kuchekea mawi
Sipendi na ya dhihaka, kwangu nyemi hiwi
Sipendi kwa hakika, mwovu kistawika
Halafuye nikacheka!

Masikini akiteswa
Yatima akinyanyaswa
Mnyonge naye akinyonywa
Sipendi hata ikiwa
Unazo nguvu najuwa
Ni hili sitatekezwa

Mbona lakini nicheke, kwayo furaha?
Na wewe ukajiweke, uli na siha?
Na yatima ali pweke, wa anahaha?
Amenyimwa haki yake, hanayo raha!
Na moyo wangu ucheke, kwa ha ha, ha!
Kucheka kwa kucheka Mimi katu sitacheka.

MASWALI

- a) Shairi hili ni la aina gani? Thibitisha. (alama 3)
- b) Taj a sababu zinazomfanya mshairi asitake kucheka. (alama 3)
- c) Chambua umbo la shairi hili kwa kuzingatia ubeti wa mwisho. (alama 4)
- d) Tambua nafsini na nafsini enwa katika shairi hili. (alama 2)
- e) Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)
- f) Fafanua uhuru wa mshairi katika shairi hili. (alama 2)
- g) Andika ubeti wa pili kwa lugha tutumbi. (alama 3)
- h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi (alama 2)
i) Mawi

ii) Nyemi

SEHEMU YA B RIWAYA:**Kidagaa kmemwozea ; Ken Walibora****Jibu swali la 2 au la 3**

2. .. alisimama jadidi na kuwatazama hawa watu wawili waliosimama wima na kutetemeka kama waliopigwa na dhoruba ya theluji."
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Bainisha hulka ya mrejelewa. (alama 6)
- c) Huku ukitoa mifano mwafaka jadili mchango wa wanawake katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*. (alama 10)
3. Huku ukirejelea riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* thibitisha kwamba vijana wana suluhu to.sha kwa matatizo yanayoikumba jamii wanamoishi. (alama 20)

SEHEMU YA C TAMTHILIA:**Mstahiki Meva : Timothy M. Arege****Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Nilikusahau lini. . , ? Mtu haukati mkono unaomlisha.
- i) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- ii) Taja na ueleze mbinu ya kifasihi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
- iii) Eleza sifa nne za msemewa. (alama 4)
- iv) Kwa kutoa mifano mitano thibithisha jinsi viongozi wa cheneo walivyokata mkono uliokuwa ukiwalisha. (alama 10)
5. Matatizo yanayowakumba wanacheneo ni kielelzo cha matatizo yanayowakumba wananchi wa mataifa mengi ya ulimwengu wa tatu. Thibitisha. (alama 20)

SEHEMU YA D;**HADITHI FUP1****Damu Nyeusi na Hadithi nyingine : Ken Walibora na Said A. Mohamed**

6. "Asanteni sana kwa kuja, sisi. . . hukabiliana na mengi."
- i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- ii) Fafanua matukio yaliyosababisha mkutano huu. (alama 4)
- iii) Jadili changamoto sita zinazokumba jinsia ya kike katika hadithi hii. (alama12)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

7. a) i) Eleza maana ya misimu.
ii) Jadili dhima nne za misimu.
- b) Fafanua changamolo zinazomkabili mtafiti wa fasihi simulizi nyanjani. (alama 10)

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA LONDIANI- 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**

1. Wewe ni mwenyekiti wa baraza la wanafunzi shuleni mwenu. Mwandikie mwalimu mkuu barua ukimweleza hatua zinazopaswa kuchukuliwa kuimarisha matokeo ya mtihani shuleni mwenu.
2. Ufisadi umechangia pakubwa kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Jadili.
3. Afadhali kujikwaa kidole kuliko ulimi.
4. Andika insha itayomalizikia hivi:-
..... Jioni hiyo chajio kilinishinda, nikawazia hotuba ya Waziri wa Usalama kuhusu visa vya kudorora kwa usalama na mauaji yaliyokithiri.

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA LONDIANI- 2016**KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU****Soma nakala yafuatayo kishaujibu maswali**

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za Kulitadarukia tatizo la umaskini ambalo una kwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaokabili mataifa yanayoendelea. Unayatosha kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yaloyaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umaskini huu ni anuwai ; mathalan, ufisadi, uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalo husika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu na adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya xxxxxxxx mpaswa kuelewa kuwa umaskini unaoathiri nchi fulani unaathari pana sana. Uvunigu unaotokana na umaskini unaweza kuwa msingi ambako matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburai madeni mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwamuhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umaskini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora yakupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umasikini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima ya zingatia uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

- a) Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea? (alama4)
- b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama2)
- c) Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuji wa tatizo la umaskini? (alama4)
- d) Mfumo wa soko huru una mathara gani kwa mataifa machanga? (alama2)
- e) Ukirejea kifungu, eleza maana ya: (alama3)
 - i) Kulitadarukia
 - ii) Kuatika
 - iii) Kuyaburai madeni

2. MUHTASARI (ALAMA 15)**Soma taarifa ifuatayo kisha uiibu maswali**

Kiswahili ni lugha ambayo inakua na kuenea kila uchao. Imeenea kwa kasi hivi kwamba waliokuwa wameitweza wamelazimika kujifunza, kuizungumza na hata kuitumia katika maandishi

Lugha hii imetambuliwa kama mojawapo ya lugha za mawasiliano katika muungano wa Afrika. Magwiji wa Kiswahili wamechaguliwa kuunda msamiati mwafaka kutegemea mabadiliko ulimwenguni na kuingiza katika matumizi kupitia tarakilishi.

Mpango huu utakapo faulu, mtu ataweza kutumia tarakilishi akiwasiliana kwa Kiswahili. Juhudi hizi heri zizidi kupongezwa na nyingine kuimarishwa

Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili barani ni mojawapo wa hatua za kufanikisha juhudi hizi. Taasisi kama hiyo itatafiti historia ya lugha, mabadiliko yake na maenezi, msamiati wake na kuleta usawa wa mazungumzo kwa Kiswahili miongoni mwa mambo mengine.

Kuweka lugha hii katika maandishi ni jambo litakalochangia kuimarisha lugha ya Kiswahili. Vitabu ,magazeti, na majarida yatakayolenga kiwango cha wasomaji yaandikwe na bei yake isiwe ghali mno ili wengi waweze kugharamia. Tanzu zote za lugha zizingatiwe.

Lugha hii ifunzwe na kutahiniwa katika daraja zote za elimu. Lifanyapo hili, bila shaka lugha ya Kiswahili itaimarika.Uajiri wa wafanyikazi ukitambua ujuzi katika lugha hii hadhi yake itaimarika.

Tafsiri ya kazi zilizoandikwa katika lugha mbalimbali zikifanywa katika Kiswahili, lugha hii itakua na kukitamizizi kwingi ulimwenguni.Watu wengi watapata hamu ya kusoma kazi asilia na ile ya tafsiri yake.

Redio na magazeti ni vyombo muhimu katika kuwasiliana na kundi kubwa la watu kote duniani. Vyombo hivi vya mawasiliano kwa umma vikihimiza matumizi ya Kiswahili, bila shaka mchango mkubwa utaonekana katika kustawisha lugha hii. Vipindi maalumu matangazo na burudani vizingatie matumizi ya Kiswahili.

Mashindano kati ya shule na shule,nchi na nchi ya kianzishwa na kuzingatiwa yanaweza kuimarisha Kiswahili pakubwa. Mashairi, mijadala, matokeo ya utafiti fulani, nyimbo, ngano na hadithi za kufunza umma ni njia za kuwezesha kufanyiwa mashindano kama hayo.

Mikakati hii na mingine ikizingatiwa itakuwa mbolea nzuri ya kukuza lugha ya Kiswahili.

Maswali

- Bila kubadilisha maana iliyokusudiwa ,fupisha aya mbili za mwanzo. (maneno 35 - 40) (alama6 ; alama 1 ya utiriko)
- Andika kwa muhtasari juhudi zinazofaa katika uimarishaji wa lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa Makala haya. (maneno 70 -80) (alama 9; alama 2 ya utiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- Andika maneno mawili yaliyo na muundo KKI (alama 2)
 - Kiimbo ni nini? (alama 1)
 - Taja matumizi mawili ya Kiimbo (alama 2)
- Tunga sentensi moja ukitumia kinyume cha neno _chopeka' (alama 2)
- Yakinisha sentensi hii katika nafsi ya pili umoja. (alama1)
- Ngeli ni nini? (alama 1)
 - Maneno haya yamo katika ngeli gani? (alama 2)
 - Fagio
 - Nyigu
- Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili za neno _malaika' (alama 3)
- Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano (alama 3)
 - twa (kutendeka)
 - Kosa (Kutendesha)
 - Cha (Kutendwa)
- Kanusha sentensi hii
Nikimwona mwalimu wangu nitamjulisha habari hizo.
- Tunga sentensi yenye kiingizi na kihusishi cha mahali (alama 2)
- Andika kwa wastani umoja (alama 1)
Malima marefu yapendeza mno.
- Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatayo: (alama 2)
 - Hiji
 - Sifu
- Eleza matumizi mawili ya mshazari (alama 2)
- Tunga sentensi iliyo na shamirisho kipozi, kitondo na kitumizi (alama 3)
- Tenganishaviambishi katika neno _Walioteua' (alama 1)
- Pambanua kimistari sentensi hii. (alama 2)
Letu lilopaliliwa limetuletea mazao mengi sana.
- Eleza maana ya semi zifuatazo (alama 2)
Uma kidole

Tegea Kazi

- p. Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi_ji' (alama 2)
- q. Andika katika usemi taarifa. (alama 2)
—Sitakwenda shuleni leo ila nitakwenda kesho”, Nikamwambia.
- r. Tumia kivumishi kionyeshi kisisitizi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya U-I kutunga sentensi (alama2)
- s. Sahihisha sentensi hii. (alama 1)
Ningekuwa na pesa ningalinunua simu nzuri.
- t. Geuza sentensi ifutayo kwa kutumia _O' rejeshi tamati. (alama 1)
kitabu ambacho kiliraruka si kile ambacho unakitaka
- 4. ISIMUJAMII**
- a. Eleza maana ya Isimujamii (alama 1)
- b. Fafanua maana ya dhana zifuatazo (alama 3)
- i) Lugha
- ii) lafudhi
- iii) lahaja
- c. Fafanua sababu yoyote inayosababisha kosa katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. (alama 2)
- d. Eleza mambo mawili yaliyochangia kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini. (alama 4)

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA LONDIANI- 2016**KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIHI****SEHEMU YA A: TAMTHILIA****Timothy Arege, Mstahiki Meya**

1. ---Sote ni wafanyikazi wa baraza. Kile linachochuma Baraza tunagawana sote.”

- (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
 (ii) Fafanua sifa **tano** za msemaji (al. 10)
 (iii) Tunagawana sote ni kinyume ejia hali halisi. Thibitisha. (al.6)

SEHEMU YA B: RIWAYA**Ken Walibora- Kadagaa Kimemwozea.****Jibu swali la 2 au la 3**

2. -Tembo itakuu ndugu yangu. Punguza ulevi bwana.Siku hizi naona aibu kukuita ndugu yangu.”

- (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (al.4)
 (b) Wahusika hawa wawili ni kama shilingi kwa ya pili.Thibitisha. (al.16)
 3. Eleza namna mwandishi wa kidagaa Kimemwozea alivyofaulu kuzitumia fani zifuatazo kwa kutolea mifano mitano..
 (i) Barua (al 10)
 (ii) Majazi (al 10)

SEHEMU YA C: USHAIRI**4. SHAIRI A**

Wewe,

Utazame mlolongo wa

Waja unaoshika njia likiwapo;

Unaofuata pembe za barabara zisokuwapo,

Kwenda kuisaka auni,

Kuitafuta kazi inayowachenga.

Itazame migongo ya wachapa kazi,

Watokwao na jasho kapakapana,

Wanaotafunwa uhai na jua liso huruma:

Wakiinua vyuma na magunia,

Wakiinua makontena,

Wakichubuka mashambani,

Wakiumia viwandani,

Wakiteseka makazini,

Halafu

Uangalie ule ujira wa kijungu meko,

Mshahara uso kifu haja,

Nguo zisizositiri miili dhaifu,

Kilio chao kisichokuwa na machozi,

Na

Ujiangalie

Mwili wako unaomereta ujana wa ufanisi,

Gari lako la kifahari lililozibwa vioo,

Jumba lako la kujishasha kama uwanja mdogo,

Malaki yapesa unayomiliki,

Ujiitapo mwajiri kwa raha, hunusi usaha wa hali yao?

SHAIRI B

Dunia kitendawili, hakuna ateguaye;

Dunia kama tapeli, hadaa nyingi ujuye;

Dunia mwenye akili, inampiku na yeye;

Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Dunia na yake hali, hupumbaza hatimaye;

Dunia ina akili, binadamu sichezeze;

Dunia uwe na mali, huiwezi dhorubaye;
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Dunia wenye muali, ambao waichezeze;
Dunia kipigo kali, huwakumba hatimaye;
Dunia wakaja kuli, —~~en~~ipata nini miye?"
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu

Maswali

- (a) Je, mashairi haya mawili ni ya aina gani? Toa sababu. (alama2)
- (b) Taja dhamira kuu katika kila shairi. (alama 2)
- (c) Kwa kutoa hoja zozote **tatu** linganua mashairi haya kiumbo. (alama 3)
- (d) Taja na uelezee **nafsi-pokezi** katika mashairi haya mawili. (alama 2)
- (e) Kwa kutolea mfano **mmoja mmoja** eleza matumizi ya mbinu hizi (alama 2)
- (i) Kweli –kinzani
- (ii) Mishata
- (f) Tambua **idhini** ya kishairi iliyo tumika katika neno —~~Wa~~ichezeze"
Na uelezee dhima yake katika utoshelezi wa kian Idhi. (alama 1)
- (g) Dondoa mfano **mmoja mmoja** wa mbinu ya tashihisi kutoka kwenye Mashairi yote mawili. (alama 2)
- (h) Andika ubeti wa **tatu** katika **shairi la A** kwa lugha nathari. (alama 4)
- (i) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotu? nika katika vifungu hivi. (alama 2)
- (i) Inampiku.
- (ii) Makontena.

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

Damu Nyeusi Na Hadithi Nyingine-Ken Wal'ibora Na S.Ahmed

Jibu swali 5 au 6

5. —Hivi vitu lazima viwepo, au kama havipo ni lazima view ni vipengee mahususi vya uhalisia wa maisha yetu:
- (a) Liweke dondoo katika muktadha wake faafu. (alama4)
- (b) Fafanua sifa zozote nne za msemaji wa maneno haya. (alama4)
- (c) Eleza kwa tafsili matatizo yoyote mawili yanayoikumba jamii ya hadithi mlimotolewa nukuu hii (alama4)
- (d) —~~M~~ungu akikupa kilema, hukupa na mwendowe"
Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi Mzizi na Matawi. (alama8)
6. Vijana wana kumbwa na changamoto kadhaa katika jamii. Jadili baadhi ya changamoto Hizi kwa kurejelea hadithi zozote tano kutoka diwani ya **Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.** (Alama20)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 7 au 8

7. a) Fafanua maana ya —~~N~~gomezi" (Alama 2.)
b) Eleza majukumu yoyote matano ya ngomezi. (Alama 10)
c) Jadili sifa nne za vivugo. (Alama8)
8. a) Fafanua njia sita jinsi jamii ya leo inavyoendeleza fasihi simulizi. (al.6)
b) Eleza umuhimu wa kufundisha mbinu za ukusanyaji na uhifadhi wa fasihi simulizi katika shule za upili. (al.4)
c) Eleza sifa tano za tendi. (al.5)
d) Bainisha dhima tano za majigambo (al.5)

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA NTIMA– 2016**KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU : (ALAMA 15)****Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Zaraa ndio uti wa mgongo wa taifa la Kenya. Viwanda vingi nchini hutegemea kilimo kama malighafi yake na kuwalisha wafanyakazi. Licha ya umuhimu wa sekta hii, mkulima ambaye ndiye nguzo za zaraa anaendelea kukabiliwa na matatizo mbalimbali yanavokwamiza juhudi zake.

Mojawapo ya matatizo yanayomkabili mkulima ni ukosefu wa ushauri wa zaraa. Wataalamu wanaotarajiwa kumshauri mkulima kuhusu njia bora za kuzalisha na kuongeza pato lake ni haba ikilinganishwa na idadi ya wakulima wanaohitaji ushauri. Wachache walioko nao wanakwamizwa na mambo tofauti. Matalani, utawapata hawaendi nyanjani ili kukutana na wakulima kwa kuwa hawana usafiri. Iwapo usafiri upo, huenda petroli ikawa ni kizungumkuti. Halikadhalika, usisahau kuwa baadhi ya wataalamu hawa ni walazadamu au mafisadi. Kuna wale wanaofika ofisini na kushinda siku nzima wakisoma gazeti huku wakijaza miraba, wakicheza bao au karata. Kuna wale nao ambao hufika ofisini wakaangika koti au sweta kitini ili waonekane kuwa bado wapo na kisha kutokomea kwenda kushughulikia mambo yao ya kibinafsi yasiyohusu ndewe wala sikio kazi waliyoajiriwa kuifanya.

Ukosefu wa sera mwafaka kuhusu ardhi nalo ni tatizo jingine linalotatiza kilimo nchini. Serikali haijaweka sera mahususi kuhusu matumizi ya ardhi. Wananchi wengi huongozwa na taratibu za utamaduni wa nasaba zao. Taratibu hizi hupendekeza ugawaji wa ardhi kwa minajili ya urithi kulingana na warithi waliopo. Si ajabu kuwa kote nchini, ardhi inayofaa kwa kilimo imekatwakatwa vipande vidogo vidogo ambavyo haviwezi kuwa na faida kwa zaraa.

Kushindwa kwa mkulima kuongeza virutubishi ardhini ni changamoto nyingine inayokabili kilimo nchini. Ulimaji wa kile kipande cha ardhi mwaka nenda mwaka rudi, bila kukipa nafasi ya kukipumzisha, huufanya mchanga kupoteza virutubishi muhimu vinavyohitajiwa na mimea. Hili nalo huchangia kupunguza uzalishaji wa mazao. Ili kutatua tatizo hili, wakulima wengi hukimbilia mbolea za kisasa ambazo badala ya kumsaidia, humwongezea madhila. Mbolea hizi zinatambulikana kuchangia uchafuzi wa mchanga na ardhi.

Mabadiliko ya hali ya anga nayo huongeza msururu wa madhila ya mkulima. Mabadiliko haya yamemfanya mkulima kushindwa kupanga wakati anaotakiwa kutayarisha shamba, kupanda, kupalilia, kunyunyizia dawa na kadhalika. Mvua imekuwa adimu. Badala yake panakuwa na vipindi virefu vya kiangazi ambavyo huathiri bidii za mkulima. Maji nayo yanaendelea kupungua na wakulima wengi hawawezi kukimu mahitaji ya unyunyuzaji maji mashambani.

- (a) Andika anwani inayofaa kifungu hiki. (alama 1)
- (b) Huku ukirejelea kifungu, fafania umuhimu wa kilimo hapa nchini. (alama 2)
- (c) Eleza changamoto tatu zinazowakabili wataalamu wa kilimo (alama 3)
- (d) Mbali na matatizo yanayowakumba wataalamu onyesha matatizo mengine matatu yanayokumba sekta ya zaraa. (alama 6)
- (e) Eleza maana za msamiati ufuatao kulingana na taarifa. (alama 3)
- (i) yanayokwamiza
- (ii) sera
- (iii) adimu

2. UFUPISHO (ALAMA 15)**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali za barabarani bado inaendelea kuwafedhehesha wahusika katika sekta ya uchukuzi na mawasiliano licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama.

Ajali za barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka wakiwemo viongozi na watu mashuhuri. Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani pamoja na uendeshaji kasi kupita inavyotakikana, yaani kukiuka masharti yaliyowekwa na wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano. Madereva wengi hung'oa vidhibiti mwendo vilivyowekwa, hawarekebishi mikanda ya usalama, wala hawayapeleki magari yao kukaguliwa mara kwa mara kama inavyopaswa. Yale yanayopelekwa kwa ukaguzi, mengi hushindwa kutekeleza kanuni zilizoweka kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani. Fauka ya hayo, madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari hayo wakiwa walevi. Dawa za kulevya kama miraa na bangi hutumiwa sana na hawa na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Hata hivyo, lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee. Ukiangazia barabara nchini Kenya utapata kuwa barabara haziko katika hali nzuri. Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidimbwi mithili ya michimbo ya madini yaliyojaa maji baada ya kuachwa wazi. Na zile barabara zisizokuwa na lami zimeharibika kiasi kwamba

ni vigumu kuzitofautisha na njia za ng'ombe kwenye maeneo kame. Kinachohitajika ni kuzirudisha katika kiwango ambacho zinaweza kufaa tena.

Wananchi pia inafaa waelimishwe ili wasikubali kupanda magari ambayo tayari yamejaa. Hili litawasaidia wananchi wenyewe kudumisha usalama wao barabarani. Pia inawafaa watambue ya kwamba wana jukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva anaendesha kwa kasi kuliko ile ya kilomita themanini kwa saa iliyokubaliwa. Inafahamika kuwa maafua wa usalama ndio wafisadi zaidi, hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita vya ufasadi na ajali za barabarani ni mwanachi mwenyewe ambaye atawezesha kukomesha hali hii. Kwa mfano, afisa wa usalama akipatikana akichukua hongo, yeye pamoja na yule aliyetoa hongo wakamatwe na kupelekwa kwenye vituo vya kukabiliana na ufasadi na kuchukuliwa hatua kali, matatizo haya yataisha. Lakini kabla kufikia hapo, ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala hili la ufasadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza kukabiliana na ufasadi, hatimaye izilainishe sekta zote wala si ya uchukuzi na mawasiliano pekee.

- (a) Kwa kurejelea aya ya pili na ya tatu, eleza mambo yanayochangia ajali za barabarani. (Maneno 45-50) (alama 6, 1 ya mtiririko)
- (b) Fupisha ujumbe wa aya ya mwisho. (maneno 50-55) (Alama 6, 2 za mtiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- a) i) Andika sauti yenye sifa zifuatazo; (alama 1)
- Kikwamizo
 - Kaakaa gumu
 - Sighuna
- ii) Andika sifa mbili za irabu / u / (alama 1)
- b) i) Eleza maana ya sentensi ya masharti. (alama 1)
- ii) Tunga sentensi ya masharti. (alama 2)
- c) Ainisha viambishi katika kitenzi kifuatacho. (alama 3)
- Walimtembelea
- d) Tunga sentesi moja kutofautisha maana ya: (alama 2)
- ngoma
goma
- e) Tumia neno 'Nairobi' katika sentensi kama : (alama 2)
- i) Nomino
- ii) Kielezi
- f) Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani ? (alama 2)
- i) Kiziwi
- ii) Uzi
- g) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa. (alama 2)
- Yaya alimpikia mtoto chakula kitamu.
Anza : chakula.....
- h) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya kuendelea. (alama 2)
- Juma anafundisha katika shule hii.
- i) Andika vitenzi vifuatavyo katika mnyambuliko uliropewa. (alama 2)
- i) kunja (tendaraa)
- ii) la (tendesheana)
- j) Onyesha kishazi hum na kishazi tegemezi katika sentensi hii (alama 2)
- Ijapokuwa kulikuwa na joto kali niliondoka kwenda sokoni.
- k) Onyesha matumizi ya kiambishi 'ni' katika sentensi ifuatayo: (alama 2)
- Maria ni mpole ndio ninapenda kwenda kwao.
- l) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)
- Kazi yako itamalizika kesho." Tajiri alimwambia mwajiriwa.
- m) Onyesha kiama na kiarifa katika sentensi ifuatayo: (alama 2)
- Kitabu chake kilianguka majini.
- n) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya wastani. (alama 2)
- Kijumba hiki kilijengwa karibu na kijiji.
- o) Tunga sentensi ukitumia yambwa tendwa na yambwa tendewa. (alama 2)
- p) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale (alama 4)
- Yusuf alikuwa mhubiri hodari sana.
- q) Yakinisha : (alama 2)
- Nisipopita mtihani mwalimu hatafurahi.
- r) Sahihisha : (alama 2)

Mwanafunzi alipogonjeka alienda katika hospitalini.

4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

–Wananchi hoyee! Round hii kura ni zetu wapende wasipende...”

- a) i) Tambua sajili hii (alama 1)
 ii) Fafanua sifa tano za sajili husika. (alama 5)
- b) Eleza maana ya istilahi zifuatazo: (alama 4)
 (i) Pijini
 (ii) Lingua franka

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA NTIMA– 2016

KISWAHILI

102/3

KARATASI YA TATU

FASIH

SEHEMU A: USHAIRI

1. LAZIMA

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Naingia ukumbini, nyote kuwakariria,
 Ushairi niwapeni, hoja nitawaachia,
 Mnipe masikioni, shike nachoelezea,
 Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Naanza kwa uzalendo, nchi yetu tuipe,
 Yadhahirishe matendo, nchi yetu tuilinde,
 Wa kila mtu mwendo, usije kawa mpinde,
 Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili

Wote tuwe na umoja, tuache ukabila
 Kabila lisiwe hoja, mwenza kumnyima hela,
 Taifa letu ni moja, Mkenya ndilo kabila,
 Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Linda demokrasia, uongozi tushiriki,
 Haki kujielezea, wachotaka na hutaki.
 Changu naweza tetea, demokrasia haki,
 Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tena adili usawa, mgao raslimali,
 Bajeti inapogawa, isawazishe ratili.
 Idara zilizoundwa, faidi kila mahali,
 Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tuwe na uadilifu, twache tamaa ya hongo,
 Tusiwe na udhaifu, wa kuwa watu waongo,
 Tukomeshe uhalifu, kisha tuache maringo,
 Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.
 Ubinafsi si adili, ila ni kusaidia,
 Ukiwa nayo mali, asiyenacho patia,
 Kama mtu mswahili, ubinafsi achia,
 Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Na inavyoelezea, katiba ni kielezi,
 Tutii kwa mazoea, hadi kijacho kizazi,
 Kwa hayo nitamwachia. hiyo ya ziada kazi,
 Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili

- a) Eleza mambo yoyote **manne** ambayo mshairi anashauri taifa lifanye ili kuwa na aadili. (alama 4)
- b) Taja tamathali yoyote **moja** inayojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
- c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia kigezo kifuatacho : (alama 1)
 Mpangilio wa vina

MAKUENI COUNTY CLUSTER PREPARATORY EXAMINATIONS 2016**102/1****KISWAHILI****KARATASI YA 1****INSHA****JULAI / AGOSTI - 2016****MUDA: SAA 1 ¾****1. Lazima**

Wewe ni mkaazi wa eneo ya Tuzindukane na unataka kuwania Ugavana katika Kaunti ya Malishoni. Andika tawasifu utakayowasilisha kwa raia ili waweze kukuchagua.

2. Sinema za ughaibuni zina hasara nyingi. Jadili.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo; Mti mkuu ukigwa wana wa nyuni huyumba.

4. Andika insha inayomalizia kwa;

.....Kijasho chembamba kilianza kumtoka usoni huku akionyesha wasiwasi. Nilitambua wazi kuwa yeye ndiye aliyefanya kitendo hicho hasi!

MAKUENI COUNTY CLUSTER PREPARATORY EXAMINATIONS 2016**102/2****KISWAHILI****KARATASI YA PILI****(LUGHA)****JULAI/AGOSTI 2016****MUDA :SAA 2 ½****UFAHAMU (Alama 15)****Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya siasa baada ya uhuru, bali ni matokeo ya hali iliyokuwepo tangu enzi za mababu zetu, kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kisiasa kunaona na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa siku nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi ilimwandaa mwanamke kuwa chombo kitiifu cha mwanaume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima wa malezi kuwa chombo cha kumtumikia mwanamume, kumstarehesha, kumfariji, kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angeweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi nai husudu sana, ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya jiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwanamke aliyeshirikishwa hata kama alikuwa ajuza. Sifa waliyokuwa nayo wanawake ni ile ya ushiri na uganga. Mwanamke yeyote aliyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa wa uchawi, ulozi na ushirikina. Kwa hivyo, wanawake ndio waliokuwa washirikina wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara, alipuuzwa napengine kutukanwa hadharani.

Kwa bahati zuri kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya. Vita vya wanawake vya kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia

Wanawake wengi wemakiuka misingi na mizizi ya utamaduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kumyanyasa na kumuumbua utu mwanamke tangu jadi. Watetezi wa haki za wanawake zamani walilaumu suala la serikali za mataifa kutochukua hatua za utekelezaji wa maazimio yaliyoendelea kupitishwa na umoja wa mataifa mwaka hadi mwaka. Huku masuala ya wanawake ya kijamii, utu na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa, watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nchi moja. Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengi yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa, majukumu yao katika jamii, mfuko wa umoja wa mataifa wa wanawake (unifem) na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya umoja wa mataifa miongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu. Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na ya watu wengine. Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kuukubali ukweli huu, wapende wasipende.

KAUNTI NDOGO YA GATUNDU MTHANI WA MAKADIRIO
KISWAHILI
INSHA
102/1
KARATASI LA KWANZA

1. Inshaya Lazima.

- Kiranja mkuu wa shule amemdokezea mwalimu mkuu kuhusu matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa wanafunzi shuleni. Andika dayolojia katiyao.
2. Mizozo na maandamano ya kisiasa huathiri raia wakawaida kuliko wanasiasa wenyewe. Jadili.
 3. Dudu liumalo silipe kidole.
 4. Tunga kisa kinachomalizia kwa maneno yafuatayo:
kwakweli, penye nia hapakosi njia.

KAUNTI NDOGO YA GATUNDU MTHANI WA MAKADIRIO
KISWAHILI
102/2
LUGHA
KARATASI LA PILI

1. UFAHAMU (alama 15)

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuata.

Katika kongamano la wataalamu wa lugha lililofanyika jijini Nairobi mnamo Septemba mwaka wa 2013, **mwandishi mahashumu**, Prof. Euphrase Kezilahabi wa Tanzania alishangaa kwamba, ingawa Kiswahili ni lugha iliyochangia sana katika kuenea kwa dini, elimu na kufanikisha biashara, Afrika ya Mashariki na kati kwa muda mrefu, haijasaidia kuleta umoja na muumano maridhawa katika eneo hili. Kadhalika, kwenye kongamano hili, wataalamu wawili wa watunzi wapevu wa fasihi ya Kiswahili – Prof. John Hamu Habwe na Prof. Kithaka wa Mberia, wa Chuo Kikuu cha Nairobi walilalamika kwamba, wahakiki wa fasihi kwa muda mrefu wamekuwa wakiipuuza fasihi ya Kiswahili na **kuiweka pembezoni** katika taaluma nzima ya wasomi, wanasiasa, wanahistoria na hata wanahabari.

Si swala la mjadala tena kwamba lugha inayofumbata hisia za wenyeji wengi wa Afrika ya Mashariki ni Kiswahili. Ingawa watu wa mataifa haya waligawanywa kwa kuwekewa mipaka na wakoloni kwa minajili ya wakoloni hao kukidhi mahitaji yao ya kisiasa na kiuchumi, kimsingi watu wa eneo hili wana historia na tamaduni zilizokurubiana.

Sina hakika iwapo Prof. Kezilahabi amekwisha kusoma vitabu vitatu ambayo nafikiri vinaweza kujibu swali lake. Vitabu hivyo ni *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language* (Alamin Mazrui na Ali Mazrui), *The Power of Babel* (Mazrui na Mazrui), *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons* (Rocha Chimerah), na *Language Policy in East Africa* (Ileri Mbaabu). Katika *Swahili State and Society*, Prof. Ali Mazrui na Prof. Alamin Mazrui wanahoji kwamba ufuasi wa watu katika makabila yao bado ni mkubwa sana Afrika kwa jumla na hasa Afrika ya Mashariki.

Hali hii ilidhihirika katika Uchaguzi Mkuu wa Kenya uliofanyika Machi mwaka wa 2013 – ambapo tuliona watu wakiamini sana vyama vya kisiasa kwa misingi ya ukabila bila kutilia maanani sera za vyama hivyo. Aliyekuwa Waziri Mkuu, Bw. Raila Odinga alikuwa na wafuasi wengi kutoka watu wa kabila lake, huku Rais Uhuru Kenyatta akiwa na wafuasi wengi kutoka jamii yake ya Agikuyu, naye naibu wake William Ruto akiwa na wafuasi kutoka kwa jamii yake ya Wakalenjin.

Huku Prof. Kezilahabi akiwa ana wasiwasi kwamba Kiswahili bado hakijafanikiwa kuunganisha watu wa Afrika ya Mashariki, Prof. Chimerah ana mtazamo tofauti. Ameipanulia mawanda lugha hii na kuipigia upatu iwe **lingua franca** ya bara la Afrika. Mtazamo wa Prof. Ileri Mbaabu wa Chuo Kikuu cha Kenyatta kuhusu suala hili ni kwamba, mikakati ya kisera kuhusiana na lugha katika mataifa ya Afrika Mashariki ni tofauti. Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Tanzania.

Hivi majuzi, serikali ya Kenya ilikikweza hadhi Kiswahili kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza – licha kwamba bado Kiswahili ni lugha ya taifa. Nchini Uganda, Kiswahili bado hakijapokelewa vizuri kwa sababu kinaendelea kupata ushindani mkubwa kutokana na lugha ya Luganda. Isitoshe, kwa muda mrefu, Kiswahili nchini humo kimekuwa kikipigwa vita kwa sababu kilihusishwa na ukatili wa wanajeshi. Hatua ya Kenya kurasimisha Kiswahili sambamba na Kiingereza ni tamko la kisera.

Hadi sasa, hatujaona hatua za kimakusudi za kulifanyia kazi tamko hili. Kenya, haina chombo rasmi cha kiserikali kinachoweza kutekeleza majukumu ya kuendeleza Kiswahili kimakusudi.

Jukumu hili limeachiwa watu binafsi na vyombo vya habari kama vile gazeti la Taifa Leo. Kuhusu suala la kuwekwa pembezoni kwa fasihi ya Kiswahili na wahakiki wa fasihi wanaozingatia mno fasihi ya Kiingereza, ni hali ya kusikitisha mno. Wasichokifahamu wahakiki hawa ni kwamba, fasihi ya Kiswahili imepiga hatua mno hasa kuhusiana na utunzi wa kimajaribio.

Kwa hiyo, ni upumbavu wahakiki kuifumbia macho fasihi ya Kiswahili ambayo inazidi kupanuka kila uchao. Kimsingi, kinachozuia Afrika Mashariki kuungana na kuwa na mshikamano anaoutaka Prof. Kezilahabi ni tofauti za kisiasa, kiuchumi na kisera ambazo hazijawianishwa. Muungano wa Afrika ya Mashariki utakapoimarika, labda ndipo mataifa ya eneo hili yatakapofikia mshikamano wa kuridhisha utakaofanikishwa kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili.

MASWALI:

- (a) Upe ufahamu huu anwani mwafaka. (Alama 1)
 (b) Eleza matatizo yanayokumba Kiswahili kwa mujibu wa ufahamu. (Alama 5)
 (c) Linganua mitazamo ya Kezilahabi na Chimera kuhusu Kiswahili. (Alama 2)
 (d) Kwa nini mwandishi anadai kuwa hatua ya Kenya kurasimisha Kiswahili sambamba na Kiingereza ni tamko la kisera. (Alama 2)
 (e) Eleza sababu za kuonyesha kuwa haifai wahakiki wa fasihi kupuuza fasihi ya Kiswahili. (Alama 2)
 (f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa ufahamu. (Alama 3)
 i) Mwandishi mahashumu
 ii) Lingua franka
 iii) Kuweka pembezi.

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Kuna sababu kadha za kuwako na kushamiri kwa ajira ya watoto. Moja ya sababu hizo ni umaskini unaozikumba jamaa nyingi pamoja na *welwa* mdogo wa thamani ya elimu wa baadhi ya watu katika jamii. Wapo watoto ambao hushurutika kubeba jukumu la *kujizumbulia* riziki wenyewe kutokana na hali duni ya familia zao.

Hali hii huweza kutokana na baadhi ya wazazi *kutelekeza majukumu* yao ya kimsingi ya kuikimu jamaa yao. Aidha kuna sehemu nyingine ambapo hali hii imetokana na janga sugu la ukimwi. Yapo maeneo ambako kuenea kwa ugonjwa huu kumewafanya viongozi wa jamaa *kupukutika kama majani* ya mti na kuwalazimisha watoto kuyakatiza masomo yao ili wawakidhie haja wadogo zao. Kuhusiana na kutelekeza majukumu, kuna wazazi ambao wanakosea kwa kutowaelekeza watoto wao kujua maadili mema ni yepi. Kwa njia hii watoto hao wanaishia kutumbukia kwenye matatizo makubwa.

Baadhi ya ajira zina athari kubwa sana kwa watoto. Ukahaba, kwa mfano, ni mojawapo ya ajira ambazo watoto wa kike hulazimika kujiingiza. Hii ni ajira ambayo inaweza kuwatumbukiza watoto hao katika hatari kubwa kutokana na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa maradhi ya ukimwi. Asillimia kubwa ya watoto wanaotumbukia katika ajira hii, inapatikana katika maeneo ya mijini na sehemu ambako utalii umeshamiri sana. Umaskini pamoja na dhiki za mijini huwalazimisha watoto hao wa kike kuishia kwenye biashara za aina hiyo. Wengine hufanyiwa hila na wafanyabiashara ambao *wametovukwa na utu* kutokana na tamaa yao kubwa ya kujitajirisha. Katika maeneo ambako utalii umeshamiri, ukahaba wa watoto unatokana na umaskini pamoja na kusambaa na kuenea kwa *maadili ajinabi*, ya ulimwengu usio wetu.

Ikiwa umaskini ni chocheo kubwa la kuwapo kwa ajira ya watoto, basi inahalisi serikali zetu zifanye kila juhudi kuhakikisha kuwa umaskini umepigwa vita. Pana umuhimu wa kuhakikisha kuwa wanajamii wote wamepewa nafasi sawa za *kujikwamua kutoka lindi la umaskini*. Isitoshe, pana umuhimu wa juhudi nyingi kufanywa kuhakikisha kuwa nafasi za shule zimepanuliwa ili kuikidhi idadi kubwa ya watoto ambao wana kiu ya elimu. Serikali haina budi pia kuhakikisha kuwa zimepitishwa sheria zinazomlinda motto dhidi ya ukatili unaotokana na watu waliokosa hisia za utu na ubinadamu. Upo pia umuhimu wa kuvisaikia vikundi vinavyojitahidi kuwasaidia watoto ili kuzifanikisha juhudi zao kwa kuwa chanda kimoja hakivunji chawa kama tujuavyo.

Hatua nyingine ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kupunguza ajira ya watoto ni *kuwahamasisha wanajamii* kuhusu haki za mtoto. Mtoto yeyote yule ana haki ya kupata elimu ya msingi. Mtoto pia ana haki ya kuishi na kupata mahitaji ya kimsingi na ya lazima kama chakula, malazi au makazi na matunzo ya kiafya. Aidha mtoto ana haki ya ukuaji, yaani kukua kikamilifu pasi na kizuizi na katika mazingira yasiyombana kwa njia yoyote ile. Isitoshe, mtoto ana haki ya kupata ulinzi dhidi ya unyanyaswaji au udhalilishwaji wa aina yoyote ile au hata maonevu kwenye misingi yoyote iwayo. Mtoto pia ana haki ya kuwa huru kushiriki katika jumuiya yake, kutoa maoni na kujieleza, kushirikiana na kujiunga na vikundi. Mwisho, na muhimu zaidi, mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya ajira au aina yoyote ya kazi ambayo inaiharisha afya na siha yake au inamzuia asipate elimu.

- (a) Fupisha aya mbili za mwanzo bila kubadilisha maana. (maneno 60-70) (alama 7) alama 1 mtiririko.
 (b) Eleza hoja muhimu zinazojitokeza katika aya mbili za mwisho. (Maneno 50-60) (alama 6)(Alama 1 utiririko.)

3. MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)

- (a) Taja vitamkwa vyenye sifa zifuatazo. (Alama 2)
 (i) Vokali ya nyuma, kati.
 (ii) Nazali ghuna ya midomo.
 (b) Kiambishi ni nini? (Alama 2)

- (c) Unda kitenzi chenye mofimu hizi. (Alama 3)
- Nafsi ya tatu umoja.
 - Kiambishi cha wakati uliopita.
 - Kirejeshi.
 - Kiambishi cha mtendewa.
 - Mzizi wa kitenzi.
 - Kiishio.
- (d) Tumia kitenzi ~~amerudi~~ kuonyesha dhana ya tatu za kiimbo. (Alama 3)
- (e) Tambua hali katika sentensi ifuatayo. (Alama 2)
- Vyungu vya aina hii vyafinyangwa na huyu.
- (f) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano. (Alama 2)
- Lia (kutendeshwa) _____
 - Pa (kutendea) _____
- (g) (i) Eleza maana ya mzizi. (Alama 1)
- (ii) Toa mfano wa:- (Alama 2)
- Mzizi huru _____
- Mzizi funge _____
- (h) Andika katika hali ya ukubwa. (Alama 2)
- Kigombe kile kiliumia kwato.
- (i) Eleza matumizi mawili ya ~~k~~. (Alama 2)
- (j) Onyesha aina za virai katika sentensi hii. (Alama 3)
- Wazazi wetu watawasili kesho saa tatu.
- (k) Onyesha kiima na kiarifa katika sentensi ifuatayo. (Alama 2)
- Wanafunzi watakaolala darasani wataadhibiwa vikali.
- (l) Onyesha shamirisho katika sentensi ifuatayo. (Alama 3)
- Wanafunzi walikatiwa keki na mwalimu kwa kisu.
- (m) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali. (Alama 3)
- Sisi tulipokuwa shuleni tulisoma kwa bidii.
- (n) Onyesha matumizi mawili ya kibainishi katika sentensi. (Alama 2)
- (o) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa. (Alama 2)
- “Tutakuja kwenu leo”. Mama alisema.
- (p) Unda nomino mbili kutokana na neno ~~kdhulumu~~. (Alama 1)
- (q) Tambua miundo yoyote mitatu ya nomino za ngeli ya A-WA kwa kutoa mifano. (Alama 3)
- 4. ISIMU JAMII. (alama 10)**
- Fafanua sababu zozote nne zinazosababisha makosa katika matumizi ya lugha. (Alama 4)
 - Eleza nadharia zozote mbili zinazoelezea chimbuko la Kiswahili. (Alama 4)
 - Eleza mambo mawili yanayosababisha kufa kwa lugha. (Alama 2.)

KAUNTI NDOGO YA GATUNDU MTHANI WA MAKADIRIO
KISWAHILI
102/3
KARATASI YA TATU
FASIHI

SWALI LA LAZIMA.

SEHEMU A: TAMTHILIA: MstahikiMeya.

Timothy Arege.

1. –Dhikimbalimbalizimekuwapolakiniherinususharikulikosharikamili”.
- (a) Elezamuktadhawadondoohili. (Alama 4)
 (b) Tajatamathaliyausemiiiyotumikakatikadondoohili. (Alama 2)
 (c) Elezasifazozotetatzungumzaji. (Alama 6)
 (d) FafanuaainazozotenezamigogoroinayojitokezakatikatamthiliayaMstahikiMeya. (Alama 8)

2. SEHEMU YA B: RIWAYA

KIDAGAA KIMEMWOZEA: Ken Walibora.

–Wemawakoumeniuakabisa.....Nina jishtakimwenyewekilasikukwamiakanamiaka”.

- (a) Elezamuktadhawamanenohaya. (Alama 4)
 (b) Onyeshakwakutoamifanokuwaanayeambiwamanenohayaalikuwanawema. (Alama 8)
 (c) Eleza umuhimu wa mhusika mashaka katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (Alama 8)

3. SEHEMU YA C: USHAIRI

Jibuswali la tatu au nne.

Na iwekupawamali, yakuhadaamtima
 Niandameufidhuli, nitengananaowema
 Hilositokubali, japowajawangesema
 Siatikwendawema, uwapokuwanihali.

Sitomehekabaila, nganitenzanachewema,
 Mungunitianajela, kisamefanzakuruma,
 Haragwelenutalila, pamojanayenusima,
 Siatikutendawema, japotagonitalala.

Haufimungaufisha, auhamiapokarima,
 Molaatauhusisha, welekeapokuzama
 Mimi nihuomaisha, hadisikuyakiamia
 Siatikutendawema, nganitamshawasha.

Wema ungawa mchungu, tajaribukutotema,
 Tautenda nende zangu, niache wanaosema,
 Malipo yangu kwa mungu, hayoyenusilazima
 Siati kutenda wema, kiagharimu roho yangu.

Maswali:

- (a) Andikakichwakinachofaashairihili. (Alama 2)
 (b) Ni mambo yapikatikaubetiwa 1 and 4 ambayohatamshairiakifanyiwahaweziachakutendamema? (Alama 6)
 (c) Elezajinsimtuwashairihilialivyoutumiauhuruwake. (Alama 6)
 (d) Andikaubetiwamwishokatikalughanathari. (Alama 4)
 (e) Mshairialipatawapiariyakuzingatiawema? (Alama 2)

4. SHAIRI A

Umekatamtima
 Umeangukianyumbayako
 Umezimamtohasira
 Nyumbayakosasamafurikoni
 Na utahama
 Watotokuwakimbia.

Mbuzikumkaribiachui
 Alijigeuzapanya

Akaliakuliwanapakakichwani
Mchawikutakasanakutisha
Alijigeuza samba
Akalianarisisikichwani.

Jongookutakasanakukimbia
Aliombamiguelfu
Akaachwananyoka

Hadijawapisasautakwenda
Bwanakokumpasumu?
Hadijaumeshikanyokakwamkia,
Hadijaumepitianyamayapunda.

SHAIRI B

Pitenijamani, piteniharaka
Nendeni, nendenihukomwendako
Mimi haraka, harakasina,
Mzigowangu, mzigomzitomno
Na chinisitakikuweka.

Vijanakwaninihampiti?
Kwaninimwanichekakisogo?
Mzigonilioubebahaupokichwani
Lakiniumenipindamgongonamiguu
Na lazimanijiegemeze, kichwani
Chininendeko
Hayapiteni! Piteni! Haraka! Heei!
Mwafikirimwaniachanyuma!
Njiyamaishanimojatu
Hukomwendakondikonilikotoka
Na nilipofikiawenginewenu
Hawatafika.

Kula nimekulanasasamwasema
Nikonyumayawakati
Lakinikamamngepitambele
Na usowangukuutazama
Ningewambiasiriyamiakamingi.

Maswali:

- | | |
|--|-----------|
| (a) Hayanimashairiyaaainagani? | Alama 1 |
| (b) Washairihawawawiliwanalalamika. Yafafanuemalalamishiyao. | Alama 4 |
| (c) Onyesha vile kinaya kinavyojitokeza katika shairi A na shairi B. | (Alama 4) |
| (d) Taja tamathali mbili zilizo tumika katika ubeti wa pili wa shairi B na utoe mfano. | (Alama 4) |
| (e) Andika ujumbe unao jitokeza katika ubeti wa nne washairi A. | (Alama 2) |
| (f) Uhuru wa mshairi umetumiwa vipi katika shairi 'B': | (Alama 2) |
| (g) Linganisha shairi 'A' na shairi 'B' kwakuangalia dhamira ya mshairi. | (Alama 4) |

SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI (JibuSwali 5 au 6).

- | | |
|--|----------|
| 5. (a) Ulumbininini? | |
| (b) Elezasifazozotennezaulumbi. | Alama 8 |
| (c) Elezamaanayalakabu. | Alama 2 |
| (d) Elezasifazozotennezalakabu. | Alama 8 |
| 6. (a) Elezavipengelevitanovyafasihisimuliziambavyohujitokezkatikafasihiandishi. | Alama 10 |
| (b) Fafanuasifatanozaushairisimulizi. | Alama 10 |

SEHEMU YA E: HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE: Ken Waliborana S. A. Mohammed.

- | | |
|---|----------|
| 7. ElezawatafsirimaudhuiyafuatayoyalivyoendelezwakatikahadithizaSamakiwaNchizaJoto naMwanawaDarubini. | Alama 20 |
| (a) Utabaka | |
| (b) Ukatili. | |

MTIHANI WA PAMOJA WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI - 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**1. **Lazima.**

Mmetamatisha masomo yenu ya kidato cha nne, kuna sherehe ya mahafali. Umechaguliwa na wenzako kama kiranja mkuu kuyazungumzia matatizo yaliyowakumba katika kipindi cha masomo yenu, mbele ya mgeni mwalikwa, waziri wa elimu. Andika risala yako.

2. Eleza chanzo cha unywaji wa pombe haramu hapa nchini.

3. Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti.

4. Andika insha itakayoanza kwa:-

Nilikaa pale kwa mseto wa hisia, nisijue kama nilifurahishwa ama nilihuzunishwa na kisa hicho.....

MTIHANI WA PAMOJA WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI - 2016**KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI**1. **UFAHAMU*****Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Bila shaka, umewahi kusikia kuwa afya ni taji. Hakuna ajuaye haya vyema kama anayeugua. Wanaoelewa usemi huu huthamini na kudumisha siha yao kwa kila njia. Licha ya lishe bora, michezo ni muhimu katika kudumisha afya njema. Mtu asiposhiriki katika michezo au unyoshaji wa viungo, mwili hunyong'onyea na kunenepa. Mwili mnyonge ni windo rahisi la maradhi. Kushiriki katika michezo hukuepusha na kutingwa na shughuli za maisha ya kileo. Shughuli hizi zisipodhibitiwa huweza kumdhuru mtu kiafya.

Maradhi hatari ya moyo, akili na shinikizo la damu husababishwa na shughuli katika maisha yetu. Hapa ndipo michezo inaingilia. Michezo huyeyusha mafuta mwilini na kutukinga dhidi ya maradhi yanayosababishwa na unene wa kupindukia. Kushiriki katika michezo vilevile hujenga ushirikiano na umoja. Michezo hutufundisha uwajibikaji. Mathalani, mlindalango atalenga kulilinda lango na kuhakikisha kuwa hamna bao linaloingia langoni. Washambulizi nao watalenga kushambulia lango la wapinzani huku waking'ang'ania kwa udi na uvumba kufunga bao.

Wachezaji ni sharti watii kanuni na sheria zinazotawala mchezo. Aidha, lazima wakubali amri za refa, kocha na waamuzi wengine ili kuimarisha nidhamu michezoni.

Watu hujipatia riziki kwa kushiriki michezo. Sasa hivi, kuna wanamichezo ambao wamesifika sana duniani. Baadhi yao wamevuka bonde la uchochole na kuwa wakwasi kutokana na talanta zao michezoni. Bila shaka, majina kama vile David Rudisha, Vivian Cheruiyot, Jason Dunford, Colins Injera na Dennis Oliech yakitajwa, kila awajuao huwavulia kofia.

Tangu jadi, michezo imekuwa kitegauchumi kote duniani. Wagiriki, kwa mfano walianzisha michezo ya Olimpiki karne nyingi zilizopita, takribani miaka 776 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Michezo hii ilipoanza ilishirikisha Wagiriki kutoka himaya zote za Ugiriki. Baadaye, watu wengine waliposhuhudia faida zilizotokana na michezo hii, walikubali kushirikishwa. Michezo ya Olimpiki ikawa si ya Wagiriki tu, bali dunia nzima.

Baada ya hapo pamekuwa na michezo mingine ambayo inashirikisha watu kutoka kila pembe ya dunia. Mchezo wa kandanda wa kuwania Kombe la Dunia, michezo ya raga na riadha ni baadhi tu ya michezo ya kimataifa.

Watu kutoka maeneo mbalimbali ulimwenguni wanapokutana kwa michezo, nchi na watu wake hufaidika sana kiuchumi. Wenyeji hupata soko la kuuza bidhaa zao. Wakulima hufaidi kuuza vyakula wanavyokuza. Mikahawa nayo hujaa wageni tele huleta fedha za kigeni. Wafanyabiashara katika sekta ya usafiri na wenye hoteli nao huchuma kutoka kwa washiriki na mashabiki. Nchi inayoandaa mashindano hayo, aidha hupata sifa kimataifa.

1. Taja aina mbili za *mbinu-ishi* ambazo hupatikana kwa kushiriki katika michezo. (alama 2)
2. Michezo ina nafasi gani kiuchumi? (alama 4)
3. "Faida za michezo ni nyingi." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano minne kutoka kwenye taarifa. (alama 4)
4. Eleza maana za msamiati ufuatao kulingana na taarifa uliyoisoma. (alama 3)
 - (a) kwa udi na uvumba.
 - (b) limbukeni.
 - (c) huwavulia kofia.
5. Eleza faida nyingine mbili za michezo ambazo hazikutajwa katika taarifa. (alama 2)

2. UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Kadiri jamii mbalimbali zinavyotagusana, ndivyo lugha zinazozungumzwa na jamii hizi nazo zinavyoingiliana na kuathiriana. Mojawapo ya athari hizi ni ukopaji wa msamiati. Jamii zinazopakana au kutagusana kukopa msamiati kutoka kwa lugha jirani na kuutumia kuelezea dhana mpya zinazolingia katika utamaduni wao kupitia kwa mitagusano ya kijamii.

Lugha ya Kiingereza, kwa mfano, imekopa kutoka lugha nyingine kama vile Kifaransa na Kilatini. Mathalani, istilahi nyingi za kisheria zimekopwa kutoka lugha ya Kifaransa. Aidha, Kiingereza kimekopa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili kama vile mwalimu, jiko, mandazi, panga, buibui, ngoma na hata wananchi, sasa yameingia katika kamusi za Kiingereza, kumaanisha kuwa yamekubaliwa kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiingereza.

Kiswahili nacho kimeathiriwa na lugha nyingine. Kimekopa msamiati wa Kiingereza na hata Kiarabu. Katika tungo nyingi za kishairi, kwa mfano, Utenzi wa Mwanakupona utapata msamiati wa Kiarabu uliotoholewa. Lugha nyingine ambazo zimeathiri Kiswahili ni pamoja na Kijerumani ambako msamiati kama vile *shule* ulikopwa na kutoholewa na neno *schule*. Msamiati kama vile *Jeso*, *karata* na *mvinyo* yamekopwa kutoka lugha ya Kireno, huku majina *balazi* na *bahasha* yakikopwa kutoka Kituruki.

Pamoja na ukopaji wa vipengele vya lugha, mtagusano wa lugha una athari nyingine. Lugha zinapokuja pamoja, mazingira ya wingi-lugha husuka. Baadhi ya watu hujifunza zaidi ya lugha moja. Mtu anayeweza kuzungumza zaidi ya lugha moja anaweza kujieleza kwa urahisi kwa kuchanganya msamiati wa lugha tofauti. Aidha, anaweza kubadilisha msimbo kulingana na matilaha yake. Ikiwa anataka kukubalika na jamii-lugha anayotagusana nayo, atatumia lugha ya jamii hiyo ili kujinasihisha na kujitambulisha nayo. Wazungumzaji hupata visawe vya maneno kuelezea dhana zile zile, hivyo kuboresha mitindo yao ya mawasiliano.

Kadhalika, kutagusana kwa lugha kunaweza kusababisha kubuniwa kwa lugha ngeni ambayo inarahisisha mawasiliano. Wakati mwingine, watu wanaozungumza lugha tofauti wanapokutana, hubuni mfumo *sahili wa lugha* ili kufanikisha mawasiliano. *Pijini* ni mfano wa lugha iliyobuniwa kwa njia hii. *Pijini* huchota msamiati kutoka lugha zilizotagusana. *Sheng* ni mfano mwingine wa lugha ambayo ilibuniwa kutokana na kutagusana kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kiasili na Kiingereza.

Japokuwa kuna faida nyingi za wingi-lugha, hasara pia zipo. Mazingira ya wingi-lugha huwapa wazungumzaji fursa ya kuchagua lugha wanayotaka kuwasiliana kwayo. Katika hali hii, lugha yenye ushawishi mkubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa ndiyo inayopendelewa zaidi. Wingi-lugha unaweza kusababisha kukwezwa kwa lugha moja na kudunishwa kwa lugha nyingine. Mathalani, kuwepo kwa lugha nyingi nchini kulizua haja ya kukwezwa kwa lugha ya Kiswahili huku nyingine za kiasili zikipuuzwa.

Lugha hukua kwa kutumiwa. Lugha isipozungumzwa kwa muda mrefu, watu hupoteza umilisi ambao huifanya kuwa vigumu kuirithisha kwa vizazi. Lugha inaweza pia kukosa wazungumzaji ikiwa wale wanaoizungumza ni wachache, au ikaathiriwa na mtagusano na lugha nyingine iliyo na wazungumzaji wengi. Katika hali kama hii, lugha hiyo hukabiliwa na tisho la kudidimia au hata kufa. Ikiwa jamii lugha itakosa kudhibiti sera za matumizi ya lugha yake, baadhi ya lugha ama zitafifia u zitakufa na kusahaulika kabisa.

1. Bila kupoteza maana, fupisha aya za kwanza tatu.

(Maneno 50)

(Alama 10, 3 za mtiririko)

2. Kwa mujibu wa taarifa hii, mtagusano wa lugha una athari gani?

(Maneno 30)

3. SARUFI (MATUMIZI YA LUGHA): (ALAMA 40)

(a) Andika sifa zozote **mbili** za kila **mojawapo** ya sauti hizi. (alama 4)

/j/

/p/

/t/

/w/

(b) Eleza dhana ya **„mofimu“**. (alama 1)

(c) Badilisha kielezi **„bidii“** kiwe kitenzi kwa kukitungia sentensi. (alama 2)

(d) Yakinisha sentensi hii.

Asiposoma hatapita mtihani vizuri

(alama 1)

(e) Andika katika **wingi**.

Rukwama ya jirani iliharibiwa na mama huyo.

(alama 2)

(f) Tunga sentensi **ukitumia**.

(i) Kihusishi cha ulinganisho

(ii) Kihisishi cha hasira

(alama 2)

(g) Bainisha **virai** vyovyote **viwili** katika sentensi hii. (alama 2)

(alama 2)

- Kikombe cheupe pe kilicho juu ya meza ni cha mwalimu mgeni
- (h) Andika sentensi hii katika hali ya **udogo/wingi**. (alama 2)
Mbwa wetu alifukuzwa na mbweha karibu na mwitu.
- (i) Tunga sentensi yenye **muundo** ufuatao. (alama 2)
Kitenzi halisi + kirai kielezi + kitenzi + kitenzi kikuu + kiunganishi + nomino ya jamii.
- (j) Eleza **tofauti** kati ya (alama 2)
Dawa yote itanywewa
Dawa yoyote itanywewa.....
- (k) Nyambua kitenzi kilicho **mabanoni** katika kauli iliyotajwa. (alama 1)
Mhubiri katika maandalizi ya karamu hii,
(shiriki, tendeshwa)
- (l) Akifisha. (alama 2)
basi shemeji akasema otieno hivyo ndivyo tunavyoweza kufaulu katika maisha wewe waonaje
- (m) Tumia kiwakilishi cha „**a**“ unganifu pamoja na kiashiria cha mbali sana kutunga sentensi. (alama 2)
- (n) Kwa kutolea mifano ya sentensi eleza matumizi mawili ya kiambishi „**ku**“. (alama 2)
- (o) Kwa kutumia **jedwali**, changanua sentensi hii. (alama 4)
Mama alipata kunieleza ingawa hakutaka nimwamini.
- (p) Tunga sentensi katika kauli ya kutendata ukitumia kitenzi **fumba**. (alama 2)
- (q) Andika sentensi ifuatayo katika wakati **ujao** hali **timilifu**. (alama 2)
Gikonyo alitia embe kabatini na akafunga.
- (r) Andika sentensi hii katika hali ya kuamrisha **wingi**. (alama 1)
Ondoka hapa.
- (s) Taja aina za **yambwa**. (alama 2)
Watoto walimjengea mama yao nyumba kwa matofali
- (t) Kwa kutolea mifano **miwili** mwafaka, eleza dhana ya „**shadda**“. (alama 2)
- 4. ISIMU JAMII: (ALAMA 10):**
1. (a) Eleza nadharia **tatu** kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili. (alama 6)
(b) Taja matatizo yanayokumba kukua kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 4)

MTIHANI WA PAMOJA WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI - 2016**KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIH****SEHEMU A: HADITHI FUPI: Damu Nyeusi Na Hadithi Zingine****1. Lazima.**

—..... Naomba msaada wako ”

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Mhusika anayezungumziwa katika dondoo hili alikuwa na sifa gani? (alama 4)
 (c) Onyesha jinsi mhusika uliyemtotea sifa katika (b) na wahusika wengine kwengineko katika hadithi hii wanavyoonyesha kuwajibika. (alama 12)

SEHEMU YA B: TAMTHILIA: T. Arege Mstahiki Meya

Jibu swali la 2 au 3

2. —Njaa ina nguvu. Imeangusha miamba wenye mengi maguvu”.

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Fafanua sifa **nne** za mzungumzaji. (alama 4)
 (c) Onyesha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 10)
 (d) Bainisha mbinu **mbili** za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

3. Huku ukirejelea tamthilia ya Mstahiki Meya jadili changamoto zinazokumba ukuaji wa uchumi wa mataifa machanga. (alama 20)**SEHEMU YA C: K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea**

Jibu swali la 4 au 5

4. —Kini one day muwapo wadosi msinisahau mwenzenu”.

- (a) Weka dondoo hili kwenye muktadha wake. (alama 4)
 (b) Bainisha mbinu ya utunzi katika dondoo hili. (alama 2)
 (c) Kwa kurejelea riwaya nzima onyesha matumizi ya mbinu hii iliyotumika na maudhui yaliyoendelezwa kupitia kwayo. (alama 14)

5. —Kwa kila mtawala katili kuna umma unaomruhusu ama kumpa uwezo wa kutekeleza ukatili”.

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 (b) Fafanua ukweli wa dondoo kwa kutoa mifano ya kina. (alama 4)
 (c) Fafanua kuhusu maudhui ya ukatili riwayani. (alama 12)

6. USHAIRI:

Jicho, tavumiliaje, kwa haya ujaonayo?
 Jicho, utasubirije, maonevu yapitayo?
 Kiwacho, lijalo na lije, nimechoka vumiliya
 Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhui tusikiayo
 Nayo, visa mauko, wanyonge yawakutayo
 Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
 Naandika!

Hawa, wanatulimiya, Dhiki wavumiliayo
 Hawa, mamiya, na mali wazalishayo
 Hawa, ndo mamiya, na maafa waikutayo
 Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo
 Hawa, huwapa unene, kwao liko angamiyo
 Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo
 Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
 Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo
 Bado, tuling'owe shina, kwa shida waikutayo
 Naandika!

Maswali

- (a) Pendekeza anwani kwa shairi hili. (alama 2)
 (b) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
 (c) Fafanua ujumbe wa ubeti wa kwanza kwa lugha tutumbi. (alama 4)
 (d) Tambua nafsi-nenewa na sababu ya kunenewa? (alama 2)
 (e) Kwa kutoa mifano eleza jinsi idhini ya utunzi ilivyotumika katika shairi hili. (alama 2)
 (f) Ainisha bahari mbili zinazoafiki utungo huu na sababu za uamuzi wako. (alama 4)
 (g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
 (i) Timbuko
 (ii) Ndo mamiya

7. **USHAIRI:**

Maendeleo ya Umma

1. Maendeleo ya umma
 Sio vitu maghalani
 Kama tele vimesaki
 Lakini havishikiki
 Ama havikamatiki
 Ni kama jinga la moto
 Bei juu
2. Maendeleo ya umma
 Sio vitu gulioni
 Kuviona madukani
 Kuvishika mikononi
 Na huku wavitamani
 Kama tama ya fisi
 Kuvipata ng'o
3. Maendeleo ya umma
 Sio vitu shubakani
 Dhiki ni kwa mafakiri
 Nafuu kwa matajiri
 Ni wao tu washitiri
 Huo ni ustiimari
 Lo! Warudia
4. Maendeleo ya umma
 Ni vitu kumilikiwa
 Na wanyonge kupatiwa
 Kwa bei kuzingatiwa
 Bila ya kudhulumiwa
 Na hata kuhadaiwa
 Hiyo ni haki
5. Maendeleo ya umma
 Dola kudhibiti vitu
 Vijapo nchini mwetu
 Na kuwauzia watu
 Toka nguo na sapatu
 Pasibakishiwe na kitu
 Huo usawa
6. Maendeleo ya umma
 Watu kuwa na kauli
 Katika zao shughuli
 Vikaoni kujadili
 Na mwisho kuyakubali
 Maamuzi halali
 Udikteta la
7. Maendeleo ya umma
 Watu kuwa waungwana
 Vijakazi na watwana
 Nchini kuwa hakuna
 Wote kuheshimiana
 Wazee hata vijana
Kutoka Fungate ya uhuru

Maswali

TATHMINI YA PAMOJA YA KIMA 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA****1. LAZIMA**

Wewe ni katibu wa tume maalum ya kitaifa iliyoteuliwa na Rais wa nchi ya Kenya kuchunguza hatua zinazofaa kuchukuliwa hili kukabiliana na tatizo sugu la ufasadi nchini. Andika kumbukumbu za mkutano mliofanya.

2. Ukosefu wa usalama ni kikwazo kwa maendeleo ya taifa. Jadili.

3. Andika kisa kitakachoonyesha maana ya methali:

Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

..... Usiku huo alipoingia kitandani kulala, aliamua kurudi nyumbani kwao kesho yake na kumwomba babake msamaha.

TATHMINI YA PAMOJA YA KIMA 2016**KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU****Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.**

Wanawake, wanaoishi katika maeneo ya mashambani katika nchi ambazo zinazoendelea ni baadhi ya watu waliotopea na kuboea katika uchochole mkubwa. Jumla ya idadi kubwa ya wanawake hawa wanaoishi chini ya kiwango cha chini, cha umaskini inakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 600. Hii ni idadi kubwa hasa ikikumbukwa kuwa ni asilimia kubwa ya wanawake inayoishi kwa maeneo haya.

Ulimwengu umeshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu pamoja na kuwako kwa matatizo ya kiuchumi duniani. Kadhalika matatizo mengine ni mitarafuku na vita vya kikabila, majanga ya kiasili mathalani mafuriko, ukame na milipuko ya volkano. Usisahau kuwa pia kina uharibifu wa kimazingira, mabadiliko ya desturi na kusambaratika kwa familia na misingi yake. Tatizo lingine ni kuwa kuna kuongezeka kwa hali ya wanawake kuwa wazazi pekee na hivyo kuongeza familia zinazosimamiwa na wanawake (ambao tumewataja kuwa wanakumbwa na umaskini mkubwa).

Wanawake wanaoishi mashambani wanakumbwa na makubwa. Kwanza, kama maskini wanaishi katika mazingira magumu. Vile vile kama wanawake wanakabiliana na mapendeleo ya kisera na kitamaduni yanayowadharau na kuwapuuza wanawake na mchango wao katika maendeleo. Tatu, kama viongozi wa familia hasa wanaolea na kutunza jamaa na mzazi mmoja, wanapambana na ugonzi wa familia pamoja na uzalishaji. Aghalabu hawapati usaidizi wowote katika majukumu kama haya bali wanalazimika kupambana nayo pekee yao. Kutokana na hayo yote wanawake hawapati nafasi nzuri kushiriki katika maamuzi ya maswala yanayowahusu. Maswala mengi yanaamuliwa na wanaume pasipokuwahusisha wanawake.

Licha ya dhiki yao kubwa, wanawake hawa wanachangia katika maendeleo ya jamii na kiuchumi kwa njia mbalimbali. Mchango huu unaonekana katika kiwango cha jamii, taifa na familia. Katika kiwango cha kijamii na kitaifa wanawake ndio chazo cha nguvukazi kwani ni wao na watoto wao wanatekeleza kazi nyingi hasa za nyumbani na mashambani. Mara nyingi huwa na uwezo bora wa kutunza chochote walichonacho kuliko wenzao wanaume.

Kifamilia wanawake wa shambani wanashughulika mchana kutwa katika hali ngumu ya hewa aidha jua kali au mvua huku wameeleka wanao migongoni wakilima mashamba ili kupata chakula kwa familia zao. Jukumu la kuandaa chakula nyumbani bado linaachiwa wale wale wanawake wanaokizalisha mashambani.

Jambo lisilopingika ni kwamba wanawake wanatekeleza majuku makubwa na muhimu katika kizazi cha binadamu na ndio hasa miimili ya jamii yoyote staaarabu. Kwa hivyo, ni kinaya kitupu kudhalilisha wanawake. Mataifa mengi yaliyoendelea ni yale yaliyoondoa vikwazo vyote mbele ya wanawake na kuwaacha watekeleze wajibu wao. Kadhalika wanaume wa huko wanawaona wanawake kama wenzao katika kujenga jamii wala sio watumwa au watumishi wao wanaoumia na kutumikishwa kama vifaa na bidhaa. Inafaa jamii zinazodinisha wanawake zitambue kuwa ubaya wa tendo hili sio tu kudumaza maendeleo yake bali pia kutoa mfano mbaya kwa vijana ambao wataendeleza Ukandamizaji huu kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo, jamii inawajibika kutenda lililo sawa kwa kuwapa hadhi wanawake wote.

Maswali

- a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka (alama 1)
- b) Nakili maafa matatu ya kimaumbile yaliyotajwa katika kifungu hiki. (alama 3)
- c) Eleza sababu tatu zinazowazuia wanawake kushiriki katika maamuzi ya maswala yanayowahusu kulingana na makala haya. (alama 3)
- d) Wanawake hutekeleza majukumu gani katika jamii na taifa kutokana na makala haya? (alama 3)
- e) Kuna tofauti gani baina ya wanawake wa mataifa yaliyoendelea na yale ambayo hayajastawi. (alama 2)
- f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye taarifa: (alama 3)
- i) uchochole

- ii) kudhalilisha
- iii) mitafuruku

2. MUHTASARI

Kuna fikra inayotawala siku hizi kuwa jela si mahali pa adhabu bali matibabu. Yaani lengo la kumfunga mhalifu si kumuadhibu bali kumtibu kwa njia ya kurekebisha tabia ili aweze kuchangia katika maendeleo ya jamii yake anapoachiliwa.

Wataalamu wa masuala ya urekebishaji tabia wanasema kuwa mhalifu akiadhibiwa sana na kufanyishwa kazi ngumu anapokuwa kifungoni, huisha kuwa sugu zaidi kuliko alipofungwa. Kwa hivyo, wataalamu wanasisitiza umuhimu wa kutilia mkazo lengo la kumtia mtu jela kuwa ni kumjenga kitabia. Mijizi, minyang'anyi na wauaji wanapotoka gereza kama hawakubadilishwa hurejelea tabia zao za kuhatarisha zaidi maisha ya watu wengi.

Ajabu na kinaya ni kwamba baadhi ya wahalifu nchini na kwingineko wametokea kupata faida kuu kutokana na vifungo vyao. Kuna wagungwa ambao wamewahi kuandika hadithi za kuisimua kuhusu maisha yao na kutokea kuwa mabilionea. Magazeti na vyombo vya habari pia huvutiwa na habari kuhusu maisha yao. Mara kwa mara, magazeti hujaa habari kuhusu mambo kama haya. Pia kuna sinema nyingi ambazo zimetungwa kufuata maisha ya wahalifu Fulani.

Watetezi wa haki za kibinadamu wanadai kuwa yale wafungwa walikuwa wakitendewa, nab ado wanatendewa katika nchi nyingine ni kinyume nah akin za kimsingi za binadamu. Hali hii imepelekea magereza mengi kukarabatiwa ili kuweza kukidhi mahitaji ya kibinadamu.

Nchini kenya, wafungwa sasa wameanza kushughulikiwa kwa kila hali. Sikwambii wanapata chakula kizuri chenye viini lishe bora, malazi bora, maji safi na mazingira nadhifu kwa jumla. Kumeanzishwa pia mpango wa elimu ambao ni maalum kwa wafungwa magerezani. Sasa wafungwa wanapata elimu na kuhudhuria madarasa na hata kuufanya mtihani wa kitaifa. Vile vile magereza nchini wameanzisha pia mpango wa kuwa na mashindano ya kila aina, ya kati ya magereza mbalimbali. Kuna mashindano ya michezo mathalan kandanda, voliboli, na michezo mingine na juu ya yote majuzi magereza yalianzisha mashindano ya urembo baina ya wafungwa wa kike.

Kilele cha kuboresha kwa hali ya magereza nchini Kenya ni kuanzishwa kwa huduma za kuwastarehesha wafungwa hao. Sasa wafungwa wa humu nchini wanaweza kusoma magazeti na hata kutazama runinga ili kupata habari kuhusu yanayotendeka nchini wanapoendelea kutumikia vifungo vyao.

Hata ingawa serikali imeanzisha mipango hii ya kuboresha hali katika magereza ya kenya, kuna matatizo mbalimbali ambayo yanaendelea kukumba taasisi hii. Kwanza, ni msongamano wa wafungwa uliopo. Magereza mengi yana wafungwa maradufu ikilinganishwa na idadi yanayofaa kuwa nayo. Hali hii imepelekea kuzuka kwa magonjwa na madhara mengine. Hii imewafanya watetezi wa haki za kibinadamu kuitaka serikali ianzishe mpango wa kutoa vifungo vya nje kwa wahalifu wenye makosa madogo madogo kuondoka msongamano huo.

Maswali

- a) Eleza ujumbe muhimu unaojitokeza katika aya nne za kwanza. (maneno 50-60) (alama 7,1 ya mtiririko)
- b) Eleza mabadiliko ambayo yamefanywa katika idara ya magereza nchini Kenya (maneno 70 – 80) (alama 8, 1 ya mtiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)

- a) Toa mifano miwili miwili kwa kila sauti zifuatazo:
 - i) sauti ghuna ambazo ni vipasuo (alama 1)
 - ii) sauti sikhuna ambazo ni vikwamizo (alama 1)
- b) Onyesha mofimu katika:
 - kilichopewa (alama 3)
- c) Yakinisha sentensi hii:
 - Hajanivunjia mlango wala kuniibia (alama 2)
- d) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari.
 - Naam! Amekaa kabla ya mkurungezi mkuu yule. (alama 3)
- e) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa
 - Nitampokea mjoba iwapo nitampata,” Rehema alimwambia shangazi yake.
- f) Sahihisha sentensi ifuatayo:
 - Mwalimu mwenye ako nabidii amepeana mazoezi katika darasa yetu. (alama 2)
- g) i) Eleza maana ya shamirisho (alama 1)
- ii) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo:
 - Maimuna alimtumia babake barua ndefu. (alama 2)
- h) Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi mawili ya kinyota (*) (alama 2)
- i) Kwa kutumika njia ya jedwali, changanua sentensi ifuatayo:
 - Gofu hushabikiwa na watu wchache sana (alama 4)
- j) Geuza katika wingi ukizingatia nafasi ya pili.
 - Nitasafiri kuelekea kwake kesho kutwa (alama 2)
- k) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Uchochole wa kinjinsia umepigwa marufuku na kiongozi mwenye msimamo thabiti mno.

- l) Andika udogo wa: (alama 2)
Ndege huyu ana miguu midogo
- m) Eleza matumizi ya ki katika sentensi hii. (alama 3)
Ukikata kipira kitapotea.
- n) Tunga sentensi ukitumia kauli iliyobanwa ya kitenzi ulichopewa. (alama 2)
i) soma (kutendeshwa)
ii) -ja (kutendewa)
- o) Unda nomino kutokana na kila kitenzi ulichopewa: (alama 2)
i) abudu
ii) nena
- p) Tambulisha ngeli za nomino hizi: (alama 2)
i) Dagaa
ii) Roshani
- q) Tunga sentensi moja kubainisha tofauti kati ya: (alama 2)
i) Samani
ii) Zamani
- 4. ISIMU JAMII: (ALAMA 10)**
- a) i) Eleza maana ya usanifishaji. (alama 1)
ii) Tambua mambo yoyote manne yaliyosababisha usanifishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 4)
- b) Eleza manufaa mawili ya lahaja za Kiswahili kwa lugha hii ya Kiswahili. (alama 2)
- c) Taja nadharia tatu zinazohusiana na chimbuko la lugha ya Kiswahili. (alama 3)

**TATHMINI YA PAMOJA YA KIMA
KISWAHILI
102/3
KARATASI YA TATU
FASIHI**

SEHEMU YA A: USHAIRI

1. LAZIMA

Soma shairi ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata.

Kimya changu kimezidi, navunja yangu subira,
Marejeya ya miradi, kuhitimisha dhamira,
Kukejeli sina budi, niwafunze utu bora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?"

Serikali bila hadi, ndo kiini cha madhara,
Yanopiga kama radi, isokuwa na ishara,
Yamini kuwa gaidi, wakitupora mishahara,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Wamejifanya hasidi, wasopatana kifikira,
Wana yao maksuudi, kijisombea ujira,
Wakilenga kufaidi, tumbo zao za kichura,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Nchi yetu kufisidi, ni jambo linonikera,
Tangia siku za jadi, ufukara ndo king'ora,
Kutujazeni ahadi, nyie mkitia for a,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Maskini watozwa kodi, wapwani na walo bara,
Kwa uvumba na uudi, mwawalipa kwa hasara,
Hamudhamini miradi, mejihisi masongora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Mesema kazi ni chudi, basi sirikali gura,
Nafsi zenu mzirudi, mkubali kuchakura,
Makondeni mkirudi, muondoe ufukara,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Ujanjenu umezidi, demokrasia bakora,
Debeni takaporudi, michirizi kwenye sura,
Kuwachuja a! muradi, kwa za mkizi hasira
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Maswali

- a) Toa anwani mwafaka kwa shairi hili. (Alama 1)
b) Ainisha shairi hili kwa jinsi tatu huku ukitoa sababu. (alama 3)
c) Onyesha Mbinu mbili za lugha katika shairi hili. (alama 2)
d) Bainisha matumizi matatu ya uhuru wa mshairi katika shairi hii. (alama 3)
e) Andika ubeti wa nne katika mtindo tutumbi. (alama 4)
f) Fafanua maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)
g) Taja mpango mmoja unaotajwa kama njia ya kutatua matatizo ya nchi. (alama 1)
h) Eleza muhudo wa shairi hili. (alama 3)

SEHEMU B: RIWAYA

Kidagaa Kimemwozea: Ken Walibora

Jibu swali la 2 au la 3

2. –Hewalla!” ...”Umenena ndipo ndungu yangu.Hiyo ndiyo tanzia ya Afrika huru.”
a) Weka dondo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Kwa kurejelea Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea bainisha tanzia ya Afrika huru inayozungumziwa. (alama 16)
3. Onyesha jinsi mwandishi wa Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea alivyoshughulikia:
i) Nafasi ya vijana. (alama 10)
ii) Nafasi ya mwanamke. (alama 10)

SEHEMU C: TAMTHILIA

Mshtahiki Meya: T. Arege

Jibu swali la 4 au 5

4. Ndiyo yale ya ngome in‘tuumiza naswi tu mumo ngomeni.’
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Tambua tamathali mbili za usemi zilizo tumika katika dondoo hili. (alama 2)
c) Kwa kurejelea tamthilia onyesha jinsi ngome inavyowaumiza wanacheneo. (alama 10)
d) Wanacheneo wanatumia mikakati gani kukabiliana na hali ya (c) hapo juu. (alama 4)
5. Uongozi mbaya una athari kadha. Thibitisha madai haya kwa kurejelea Tamthili ya Mstahiki Meya. (alama 20)

SEHEMU D: HADITHI FUPI

Damu Nyeusi na Hadithi nyingine

6. Ndoa ya samani (Omar Babu)
Sikufahamu ikiwa hisia zenyeuwe zilikuwa kwa sababu ya —furaha au huzuni.”
Potelea pote! Liwalo naliwe!! Nilisikia sauti Fulani ikinadi ndani katika nafsi yangu.
I. a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Bainisha tamathali mbiliza usemi katika dondoo hili. (alama 4)
c) Ni yapi yaliyodhihirisha furaha au huzuni‘ katika hisia za anayeelezwa? (alama 6)
II. Jadili changamoto za elimu katika hadithi ya Kanda la Usufi. (alama 6)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

7. a) Eleza maana ya miviga. (alama 2)
b) Fafanua umuhimu wa miviga kwa wanajamii. (alama 4)
c) Eleza maana ya ulumbi. (alama 2)
d) Fafanua umuhimu wa ulumbi katika jamii. (alama 3)
e) Eleza sifa za mlumbi mahiri. (alama 4)
f) Eleza maana ya ngomezi. (alama 2)
g) Toa mifano mitatu ya ngomezi za kisasa. (alama 3)

MTIHANI WA MWIGO WA CEKENAS – 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**

1. Mwandikie mhariri wa gazeti la 'Tujuze' ukilalamikia swala la uharibu wa mazingira katika eneo unakoishi na jinsi ya kukabiliana na changamoto hii.
2. Mitandao ya kijamii imesababisha madhara mengi katika sekta ya elimu. Fafanua.
3. Mcha mwana kulia, hulia mwenyewe.
4. –Buum!’ Mlipuko huo ulitapakaza vifusi kote. Nilijua lazima ningejinusuru
Tendeleze insha hii.

MTIHANI WA MWIGO WA CEKENAS – 2016**KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU (alama 15)****Soma makala ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Utandaridhi (au globalization kwa lugha ya Kingereza) ni jinsi ya maisha inayoendelea kuutawala ulimwenguni wote katika karne hii ya 21. Neno utandaridhi ni neno mseto ambalo maana yake ni utamaduni uliotanda au kuenea ardhi nzima. Mtu mtandaridhi hivyo basi ni mtu aliyebobea kikamilifu katika utamaduni huu mpya kwa jinsi moja au nyingine. Mtandaridhi hujihusisha sana katika kutandaridhisha aina moja au nyingine ya amana muhimu za mavazi zilizotokea kupendwa ulimwenguni kote, muziki wa kisiku hizi, hasa vile op, raggae, ragga, rap, ambao asili yake ya hivi majuzi ni Marekani. Muziki huo waimbaji wake hutumia, sana sana, lugha ya Kingereza hususan kile cha Marekani na kadhalika.

Watandaridhi wana nyenzo zingine kadha wa kadha za kuendeshea maisha yao au kujitambulisha. Wao huwasiliana kutoka pembe moja ya dunia hadi nyingine wakitumi vitumeme, yaani vyombo vitumiavyo umeme kufanya kazi vya hali ya juu, kama vile tarakilishi na simu, haa za mkono. Watu hawa hawakosi runinga sebuleni mwao, usiseme redio. Hawa husikiliza na kutazama habari za kimataifa hupitia mashirika matandaridhi ya habari kama vile BBC la Uingereza na CNN la Marekani. Aidha watu hawa husafiri mara kwa mara kwa ndege na vyombo vingine vya kasi. Hawa hawana mipaka, wote wanaohusudu utandaridhi wanaamini kindakindakika kwamba utamaduni huu ni kilimwengu umeleta miahaka mwema baina ya watu binafsi, makampuni makubwa makubwa ya kimataifa na uwiano bora baina ya mataifa. Watu hawa husikika wakidai ya kuwa aina hii ya utamaduni imecupigisha mbele ustaarabu wa wanadamu ulimwenguni kote. Kwa upande mwingine, wakereketwa wa tamaduni za kimsingi za mataifa na makabila mbalimbali ulimwenguni wanadai ya kwamba utandaridhi umeleta maangamizi makubwa ya tamaduni hizo. Vile vile unaelekea kuangamiza lugha nyingi zinazofungamana na tamaduni hizo.

Kwa ajili hiyo basi, utandaridhi umesemekana kwamba unasababisha kutovuka kwa utu miongoni mwa wanadamu wote ambao wamo mbioni kusaka pesa na kuncemesha ubinafsi. Inadaiwa pia kwamba utandaridhi umesababisha kutovuka kwa adabu kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu. Huko kutovuka kwa adau kwa vijana, hasa wale wa mataifa yanayojaribu kuendelea, kumeleta zahama chungu mbovu, ikiwa ni pamoja na kuenea kwa UKIMWI kwa kasi ya kutisha.

Maswali

- (a) (i) Bainisha kwa kutoa maelezo kamili kwamba utandaridhi ni neno mseto. (alama 2)
- (ii) Toho maneno mawili kutokan ana neno kutandaridhisha kisha ueleze maana ya maneno haya. (alama 4)
- (b) Ni nini maana ya —hawa hawana mipaka”? (alama 1)
- (c) Kwa nini watandaridhi wanapenda kusikiliza na kutazama habari kupitia BBC na CNN? (alama 2)
- (d) Eleza kikamilifu maoni ya watandaridhi kuhusu utamaduni wao. (alama 2)
- (e) Je, utandaridhi unalaumika kwa nini katika kifungu hiki? (alama 2)
- (f) Msemu: —Chungu mbovu” ni msemu wa kimtaani tu. Msemu swa ni upi? (alama 1)

2. MUHTASARI (alama 15)**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Kiswahili lugha yenye asili yake katika ukanda wa Afrika Mashariki imeenea duniani ambako inafundishwa katika uyuo vikuu saba vya umma na vyuo vikuu viwili visivyo vya umma. Hivi ni Barotoni na Chuo kikuu cha Kikatoliki. Katika kiwango hiki, watu wanafunzwa isimu na fasihi mafunzo haya yanatolewa kuanzia shahada ya kwanza, shahada ya uzamili na shahada ya uzamifu.

Elimu ya juu ya Kiswahili inatiliwa mkazo katika vyuo vikuu nchini Tanzania na hasa Dar-es-Salaam. Chuo hiki ndicho mlezi wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Kwa muda mrefu, TUKI imechapisha mararida, kuzua istilahi na kuandaa kamusi. Vyuo vikuu nchini Uganda vikiongozwa na Makerere vimeanzisha mikakati kabambe ya kufunza Kiswahili. Kwingineko barani Afrika, Kiswahili kinafunzwa nchini Msumbiji, Sudan, Misri, Lesotho, Ghana, Nigeria n.k

lugha hii imepewa msimko mkubwa katika mitaala kuambatana na sera ya Afrika Kusini kutokuza lugha za Kiafrika. Ikumbukwe kuwa lugha hii ilichangia pakubwa ukombozi wa Afrika Kusini.

Ukitembelea baadhi ya vyuo vikuu katika nchi za mashariki ya mbali kama Japani, Kora Kusini na Uchina, utapata Kiswahili kwenye orodha ya masomo. Maandishi mengi yanatafsiriwa kwa Kiswahili katika vyuo hivi. Takribani nchi zote ulaya zina vyuo vikuu vinavyofunza Kiswahili. Lakini Uingereza, Ujeremani na nchi za Skandinevia zimetia fora, pamoja na kufunza lugha hii, vyuo vinafadhi utafiti na uchapishaji wa mambo kuhusu Kiswahili. Aidha nchi hizo huwadhamini wengi kusomea huko. Muhimu zaidi ni kuwa vyuo vikuu katika nchi hizo zimehifadh maandishi mengi ya Kiswahili. Hivi sasa masomo mengi wanayatumia kufanya utafiti hasa hukusu ushairi. Moja ya asasi hizi ni School of Oriental and African studies. Jijini London. Wataalamu waliosomea vyuo hivi wamerudi nyumbani na sasa wanajihusisha na uchapishaji wa vitabu vya nadharia, isimu, surufi, fasihi andishi na fasihi simulizi.

Hata hivyo, ni Marekani ambapo matumizi na mafunzo ya Kiswahili katika vyuo vikuu yamepanuka sana. Lugha hii inafunzwa katika majimbo kama Washington, New York, Chicago, Texas, California, New Jersey n.k. vyuo maarufu sana vile Cornell, Yale na Harvard vinafunza Kiswahili. Hali hii imesaidia kuingizwa kwa lugha hii katika mtandao.

Lugha hii inafunzwa kama ishara ya hisia za Uafrika. Wamerekani weusi wanaona fahari kuzungumza Kiswahili. Hii huwakumbusha kuwa wao wana asili ya barani Afrika. Kupitia mafunzo haya, Wamerekani wengi wanaiga utamaduni wa Kiafrika. Wengi wao wamejipa majina ya Kiswahili kama vile Baruti Katembo Maulana, Simba n.k. kwa hakika Kiswahili kinapata hadhi.

Maswali.

- (a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi, fupisha aya ya kwanza na ya pili. (alama 6 utiririko 1)
(maneno 50 - 60)
- (b) Kwa kuzingatia aya zilizobaki, eleza mambo muhimu anayoeleza mwandishi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu. (maneno 60 - 70) (alama 9, utititiko 1)

3. SARUFI. (alama 40)

- (a) (i) Kimadende hutumkwa vipi. (alama 1)
(ii) Eleza sifa mbilimbili za sauti zifuatazo. (alama 2)
/d/
/m/
- (b) Andika neno lenye silabi funge yenye muundo wa konsonanti moja. (alama 1)
- (c) Onyesha matumizi ya *-kwa* katika sentensi hii. (alama 3)
Kwa kuwa alikuwa mechelewa kwenda kwa nyanyake alisafiri kwa baiskeli.
- (d) Tunga sentensi kwa kutumia. (alama 2)
(i) Kivumishi cha *ki* ya mfanano.
(ii) Kielezi cha kiasi cha jumla.
- (e) Baihisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 4)
Kimathi alimwandikia babake bawa kwa kalamu jana jioni.
- (f) Tunga sentensi ukitumia kitenzi cha katika hali ya kutendwa. (alama 1)
- (g) Changanua sentensi hii kwa kutumia jedwali. (alama 4)
Mama alilima kwa bidii ingawa hakupta faida.
- (h) Tunga sentensi moja yenye kishazi huru na kishazi kitegemezi ukitumia *_O* rejeshi tamati. (alama 3)
- (i) Taja matumizi mawili mawili ya alama ifuatayo ya uakifishaji; (alama 2)
Mstari
- (j) Andika sentensi ifuatayo kwa udogo wingi. (alama 2)
Mtu yule haachi kuandamana na mbwa wake aliyedhoofika kiafya.
- (k) Andika katika msemu halisi. (alama 2)
Mwalimu alishangaa ni kwa nini Juma hakuwa amebaba mkoba wake siku hiyo.
- (l) Kanusha sentensi hii katika hali ya *_a* (alama 2)
Kibofu hupa angani.
- (m) Jibu kulingan ana maagizo. (alama 2)
(i) Ufisadi (unda kitenzi)
(ii) -pya (unda nomino)
- (n) Andika maana mbili za neno *-dango*. (alama 2)
- (o) Tambua kinai kilichopigwa mstari katika senensi hii; (alama 1)
Watu wenye woga mwingi hukimbia ovyo.
- (p) Mwanafunzi aliadhibiwa kwa uongo wake. (alama 2)
(Anza kwaUongo)
- (q) Andika kinyume. (alama 1)
Ukipitia kwao utalaaniwa.
- (r) Andika upya sentensi hii kwa kutumia visuwe vya maneno yaliyopigwa mstri. (alama 2)
Lupita ndiye alitakadamu upelelezi wa shamba hili.
- (s) Andika maana ya msemu. (alama 1)
Kawa na mihayara.

4. **Isimu Jamii. (alama 10)**

- (a) Kwa nini kulikuwa na haya ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. (alama 5)
Toa sababu **tano**.
- (b) Eleza sifa **tano** za sajili ya magazeti. (alama 5)

MTIHANI WA MWIGO WA CEKENAS – 2016**KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIHI****SEHEMU YA A****SWALI LA LAZIMA**

1. —Eo ndioyo mtanitambua. Mama gani anayemtazama mwana akigeuka afriti?”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Tambua mwana aliyegeuka afriti na ueleze hulka zake nne. (alama 6)
(c) Jadili maudhui yoyote matano yanayojitokeza katika hadithi husika. (alama 10)

SEHEMU YA B**Mtahiki Meva; Timothy Arege****Jibu swali la 2 au 3.**

2. —Siku moja kabla ya kufika kwa wageni. Meva ana mkutano na wawakilishi wa wafanyikazi ambao wameketi mkabala naye”.
- (a) Fafanua madai yaliyotolewa na wafanyakazi katiak mkutano huu. (alama 12)
(b) Eleza jinsi Meva alivyojibu madai ya wawakilishi wa wafanyakazi. (alama 8)
3. Tamthilia ya mstahiki Meva ni kioo cha jamii ya nchi za Afrika zinazoendelea. Thibitisha. (alama 20)

SEHEMU YA C**Kidagaa kimemwozea.****Jibu swali la 4 au 5.**

4. Elimu ya kajielewa sisi nani, na twatoka wapi, twaelekea wapi na utu tutaurejeshaje pahali pake....
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Taja mfano mmoja wa tamathali ya usemi kwenye dondoo. (alama 2)
(c) Dhahirisha jinsi utu ulivyotoka pahali pake, ukirejelea riwaya nzima. (alama 14)
5. Thibitisha kauli kuwa, —~~M~~ naye huliwa zamu yake ifukapo’. Ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

SEHEMU YA D.**USHAIRI****Jibu swali la 6 au 7.**6. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Angaza, mtazame mlimwengu
Bidii, nayo matokeo chungu
Wezesha, kuishi bila uchungu
Teknolojia maendeleo.

Angaza, zitazame barabara
Aenda, kwa kasi pia salama
Bidhaa, sokoni upesi fika
Teknolojia maendeleo.

Angaza, majokofu majumbani
Vyakula, na vinywaji hifadhika
Nafuu, zizima maji ridisha
Teknolojia maendeleo.

Angaza, leo pote madukani
Mikebe, vyakula vinywaji tiwa

Mimea, huwawirishwa haraka
Teknolojia maendeleo.

Angaza, nguo kwa mashine stimu
Upesi, runinga na simu juza
Angani, burudika eropleni
Teknolojia maendeleo.

Angaza, tarakilishi nguzoye
Mauzo, mawasiliano kwayo
tibani, ni mwenzi kwake tabibu
Teknolojia maendeleo.

Angaza, mja hajakoma katu
Shughuli, kila uchao shajara
Apate, tulia kwa ufanisi
Teknolojia maendeleo.

- (a) Eleza dhamira ya msanii katika shairi hili. (alama 2)
 (b) Onyesha mifano **mitano** ya maendeleo katika maisha ya binadamu. (alama 5)
 (c) Eleza umbo la shairi hii. (alama 4)
 (d) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. (alama 4)
 (e) Eleza kwa kifupi mtazamo wa mshairi kuhusu teknolojia. (alama 3)
 (f) (i) Majokofu
 (ii) Hunawirisha
 (iii) Shajara

7. **Soma shairi ifuatalo kish aujibu maswali.**

Jana ilikuwepo, ikapita
Kwenye giza la sahai
Jana ilipiga kuathiri
Athari ijayo leo
Leo tunajua kesho tunaibashiria

Kesho ipapo na hatuijui
Kesho, itapiga au itapuliza?
Au itapita pasi na chochote
Kama moshi usio mashiko?

Kesho hatuioni
Lakini yaja ...
Twaihisi
Twaihisi
Twaimaizi
Ipo,

Yajongea
Hiyo na taathira zake
Inakuja
Yasogea
Yaja mbio
Yafikia upeo unaoitwa leo
Basi kumbuka
Maisha ni ubishi, yakabili!
Maisha ni jasiri, jusurisha!
Maisha ni huzuni, yashinde!
Maisha ni msiba, uweze!

Maisha ni wajibu, tekeleza!
Maisha ni ni fumbo, liague!
Maisha ni tatizo, litatue!
Maisha ni ahadi, itemize!
Maisha mapambano, wana nayo!

Maisha ni zawadi, ipokee!
 Maisha ni mchezo, uxhezee!
 Maisha ni nyimbo, iimbe!
 Maisha ni fursa, itumie?
 Maisha ni ureda, furahia!
 Maisha maumbile, changamkie!
 Maisha ni lengo, lifike!
 Maisha ni mwendo, yaendee!
 Maisha ni uzuri, ustarehee!
 Maisha liwazo, yapumzikie!

- (a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili. (alama 2)
 (b) Fafanua maudhui ya shairi hili. (alama 6)
 (c) Onyesha muundo wa shairi hili. (alama 4)
 (d) Taja na ueleze tamathali tatu za semi alizotumia mwandishi wa shairi hili. (alama 6)
 (e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumia katika shairi. (alama 2)
 Twaimaizi
 Yajongea

SEHEMU YA E
FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 8.

8. (a) Misimu ni nini? (alama 2)
 (b) Onyesha kwa kutoleo mifano minne, jinsi misimu huzuka. (alama 4)
 (c) Eleza vikwazo vitano vya ukuaji wa Fasihi Simulizi. (alama 10)
 (d) Tafautisha kati ya;
 (i) Ngonjera za ushairi na za maigizo. (alama 2)
 (ii) Ngoma na ngomezi. (alama 2)

JARIBIO LA TATHMINI YA GITHUGURI**INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**

1. Umealikwakushirikimahojianokatika studio zaruningamaarufunchini. Andikamazungumzokatiyakonamwanahabarikuhusukiini cha udanganyifukatikamihaniwakitafananamnyakuboreshamatokeoyamitihaninchini.
2. Ukupigaondiukufunzao. Thibitishaukweliwamsemohuu
3. Elezajinsiyakukabiliananaswalasugu la mihandaratinchini.
4. –Umeletwahapanawasamariawema.” Sautiya kike ikanieleza. Nikavutakumbukizi.....

JARIBIO LA TATHMINI YA GITHUGURI**102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU (AL 15)****Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Takwimu za hivi punde zinaonyesha kuwa maradhi ya saratani imejifaragua na kuwa miongoni mwa **senene kuduku** duniani maadam inatishia kuupiku ukimwi. Wagonjwa wanoendelea kuyasalimia amri wanaelekea kufikia kiwango cha kutisha. Licha ya tawala nyingi duniani kuwekezea tafiti anuai za kuyapindua, miale ya welewa wa kiini chake bado ni hafifu ajabu. Wataalam wa utabibu wanaeleza chanzo cha saratani kama mgawanyiko usio wa kawaida wa chembechembe za damu katika viungo vya mwili vinavyohusika. Viungo huanza kukua kwa kasi isiyo ya kawaida.

Japo uvumbuzi unaonyesha kwamba kuna uwezekano mkubwa kwa watu wa umri wa makamo kuambukizwa ugonjwa huu. Wazee wamo hatarini zaidi. Hata hivyo vimeshuhudiwa visa vingi ambavyo hata watoto wachanga huathiriwa pakubwa. Saratani ya tezi-kibofu. Ya koromeo nay a mapafu ni baadhi ya aina zinazowaathiri wanaume. Saratani ya tezi-kibofu huwasogelea zaidi mabuda wa umri wa miaka zaidi ya sitini. Kwenda haja ndogo kila mara. Ugumu wa kupitisha mkojo, ugume wa kuanza au kumaliza kukojoa, damu kwenye mkojo na maumivu ya mgongo ni baadhi ya dalili zake. Mwishowe, tezi-kibofu huzidi kuwa kubwa na kufungia mkojo kutoka.

Kansa zinazowalenga sana wanawake ni pamoja nay a nyumba ya uzazi, mlango wa uzazi na **maziwa**. Kansa ya maziwa huwachachawiza zaidi wanawake wenye umri wa miaka thelathini na mitano au zaidi. Dalili ya awali ni uvimbe unaohisika kwa ndani na maziwa kutoa usaha. Inaenea haraka na kuviambukiza viungo vya ujirani mathalani mapafu na ini. Saratani ya mlango wa uzazi inaambukizwa na virusi vinavyoita **papolloma**. Virusi hivi hupata mwanya iwapo mwanamke aliaza mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo, akiwa na wapenzi wengi, akiwa matumizi wa dawa fulani za kupanga uzazi na apulizapo moshi wa sigara.

Inapendekezwa kuwa **ukaguzi wa ada** ufanywe ili kuugundua kabla haujasambaa kutokana na kauli kwamba mwanzoni hausababishi uchungu wowote. Ukaguzi wa kibinafsi kwenye viungo vilivy na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa kisha jambo lolote lisilo la kawaida kama vile uvimbe na ugumu wa kumeza liwasilishwe mara moja kwa daktari. Ushauri zaidi unahusu aina ya vyakula na mitindo ya kisasa ya maisha. Vyakula vilivyosheheniwa na protini zipitikanazo katika nyama na mayai ni miongoni mwa vyakula hatari. Vyakula vya kiasili kama mboga, miwa, matunda, mafuta yanayotokana na mimea na nyama nyeupe hupendekezwa. Uvutaji wa sigara, unywaji pombe, na baadhi ya vipodozi vyenye zebaki huweza kurutubisha uwezekano wa kuambukizwa saratani.

Ijapokuwa saratani ni kama sikio la kufa lisilosikia dawa, ni muhimu wawele wazibe ufa kabla ya kuangukiwa na ukuta usioweza kujengeka tena. Ikgunduliwa mapema. Maradhi haya huweza kudenguliwa kutumia tibakemikali, tabamiale, chanjo dhidi ya baadhi ya virusi vya saratani, upasuaji wa viungo vilivyoathiriwa na dawa za kupunguza makali yake.

Utafiti wa kina uliofanywa na kukamilishwa mwezi wa Machi, mwaka wa 2014 na madktari wa Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta kwa ushirikiano wa wengine kutoka Uingereza umegundua kuwa dawa aina ya **Lopinavir** inyotumiwa kupunguza makali ya ukimwi ina uwezo wa kukabiliana na maradhi haya. Uchunguzi uliofanyiwa wawele baada ya muda Fulani wa uwekaji wa dawa hii kwenye mlango wa uzazi ulibainisha kuwa chembechembe za saratani huangamizwa na dawa hii. Ni jambo la kutia moyo kuwa harakati za kukabiliana na janga la ukimwi zinaelekea kutoa sulhu kawa maradhi haya ya kansa. Inakuwa shani inaposadifu kuwa nuhusi iliyowahi kutokea katika mapisi ya siha ya insi imekuwa kitivo kinachopaswa kuenziwa. Hakika hizi ni harakati zinazostahili kupongezwa na kuzidishwa iwapo zimwi hili litafukiwa katika lindi la usahaulivu.

- a) Kwa nini maradhi ya saratani yanaelekea kuwa hatari zaidi kuliko ukimwi? (al 1)
- b) Ni kwa nini ni vigumu kuitambua saratani mwanzoni? (al 2)
- c) Taja mambo yanayoweza kuchangia maambukizi ya saratani ya mlango wa uzazi. (al 3)
- d) Eleza njia ambazo mtu anaweza kutumia kugundua kama ana saratani. (al 2)
- e) Eleza baadhi ya mambo yanayoweza kuchochea maambukizi ya saratani. (al 2)

- f) Eleza maana ya methali ifuatayo kwa mujibu wa makala haya. (al 2)
Dalili za mvua ni mawingu.
- g) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kwenye makala. (al 3)
i) senene kuduku.....
ii) maziwa
iii) ukaguzi wa ada

2. UFUPISHO (AL 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Kiwango cha ufanisi wa taifa lolote lile hugezwa kutokana na hali ya miundomsingi. Mataifa sampuli hii hutenga fulusi si akali ya makadirio ya bajeti yake kwa miradi ya maendeleo. Nchi nyingi zinazoendelea hujikuta katika njia panda kwa mujibu wa utekelezaji wa sera amilifu za kukwamua chumi zao. Utawala wa Kenya umekuwa ukijikuna kichwa katika harakati za ujenzi wa nguzo hii ya ufanisi. Mbali na asasi za utabibu kuwa chache. Zile zilizopo ziko katika hali mahututi. Udufu huu umesambaratishwa zaidi na idadi kubwa ya madaktari na wauguzi wanaoendelea kugura tangu usimamizi wa huduma zao kuhamishiwa serikali za gatuji, sikwambii changamoto zinazonyemelea sekta za elimu, utumishi wa umma na zaraa.

Katika harakati za kupata suluhu, serikali imetoa rai ya kupunguza tija kwa watumishi wake. Rais, naibu wake na makatibu wa wizara wamekuwa vielelezo kwa kujitolea kunyoa 20% ya mishahara yao. Katika mdahalo wa kitaifa kuhusu matumizi ya mfuko wa umma ulioandaliwa na tume ya Mishahara nchini, rais alizirai bunge, mahakama, seneti, mashirika ya umma na magatuzi kudurusu mishahara kwa watumishi wake. Hii ni kwa sababu serikali inatumia 55% ya mapato ya ushuru ambayo inafasirika kama 13% ya mfuko wa umma kulipia mishahara. Kiasi hiki kimekuwa kikiongezeka kutoka shilingi bilioni 240 hadi bilioni 500 kwa muda wa miaka minne iliyopita. Wabobezi wa maswala ya iktisadi wamefichua kuwa hiki ni zaidi ya kiwango cha kimataifa cha 35% kinachotekelezwa na nchi zilizoendelea. Mbona tussige nchi za Malasya na Uswizi ambazo zimepunguza janguo kwa viongozi wao kwa 50%?

Wataalam hawa wanashauri kuwa harakati hizi ni kama tone la suluhu kwenye bahari ya sintofahamu ikizingatiwa kuwa kupunguza mishahara ya wafanyakazi hasa wa ngazi za chini. Kutawanyonga katika uchumi ambao mfumuko wa bei umefikia kiwango cha kuvunda. Uhunifu unahitajika kupanua mfuko wa umma. Makadirio yanayotengewa wizara na shughuli nyingine za serikali zisizo za kimsingi yapunguzwe. Serikali pia inahitajika kuziba mianya ambayo kwayo darahimu lukuki hunywelea kutokana na ubadhirifu. Inatarnausha kutanabahi kuwa wizara ya usalama wa ndani haiwezi kuwajibikia matumizi ya shilingi milioni 548.7!

Wakenya walitoteza mamilioni kutokana na Benk Kuu ya Kenya kukaidi ushauri wa kisheria na kanuni za zabuni za kandarasi zinazohusu mitambo ya usalam na utengenezaji wa pesa. Si ajabu gavana wake Profesa Njuguna Ndung'u alifunguliwa mashtaka ya utepetevu na matumizi mabaya ya mamlaka.

Wanaotolea nchi hii futuko wataweza tu kutua mori iwapo makabiliano haya na vyombo vya sheria yatawasukuma wahitifaki hawa wa chauchau nyuma ya kizimba. Waaidha, ziara za ughaibuni ambazo zilimpokonya mlipa ushuru milioni 348 mwaka wa 2013 pekee hazina budi kupunguzwa maradufu. Maafisa wa serikali lazima waghairi kutumia magari mazito yanayogubia mafuta. Inabainika kuwa gharama ya warsha na makongamano yanayonuiwa kuboresha ujuzi wa watumishi wa umma imeghushiwa licha ya utupu unaoambatana na mada zake.

Serikali itaelezaje kauli kwamba imekuwa ikitumia shilingi bilioni 2 kuwakimu wafanyikazi hewa? Isitoshe, kuna wafanyikazi wengi wanaofanya kazi ombwe. Kwa mfano, makamishina wa magatuzi waliotumwa huko na serikali kuu wanatoa huduma zipi zisizoweza kutolewa na magavana? Ni ruya au halisi kuwa makdmishna wa Tume ya Mishahara nchini hulipwa marupurupu ya shilingi 400,000 kila mwezi kando na mishahara yao yenye minofu? Hii ni haramu ambayo lazima ilaaniwe. Ninashuku kuwa wakenya wangepigwa na mshtuko wa moyo iwapo marupurupu yanayohusishwa na taasisi nyingine za umma kama vile urais, mahakama na bunge yangeanikwa.

- a) Dondoa hoja muhimu katika aya mbili za mwanzo. (Maneno 75-80) (al 6)
b) Kwa kutumia maneno yasiyopungua 90 wala kuzidi 95, eleza mikakati inayoweza kutumiwa kudhibiti mfuko wa umma. (al 9)

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

- 1) Toa mfano mmoja wa aina sauti zifuatazo. (al 3)
i) Kitambaza irabu za mbele
ii) Konsonanti zinazotamkiwa kwenye koromeo.
- 2) Eleza maana mbili tofauti za sentensi hii. (al 2)
Nitakuja kukagua kazi hiyo baada ya saa mbili.
- 3) Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi. (al 2)
i) Lau
ii) Almuradi

- 4) Tumia neno vile kama. (al 3)
 i) Kivumishi ...
 ii) Kiwakilishi
 iii) Kielezi
- 5) Andika wingi wa sentensi zifuatazo; (al 2)
 i) Sokwe aliukwea mti huo wa kasi.
 ii) Mshale mkali ulitumiwa kumwua samba.
- 6) Badilisha sentensi ifuatayo iwe mazoea kwa kutumia O rejeshi. (al 1)
 Malipo ambayo anapewa ni yale ambayo yanaridhisha.
- 7) Eleza maana ya nahau zifuatazo: (al 2)
 i) Furaha ghaya
 ii) Maneco yalimkata maini.
- 8) Akifisha sentensi ifuatayo. (al 3)
 Karibu mgeni akaitika mwenyeji mbona huingii na mlango u wazi stareheni kwenye viti ahsante wakajibu..
- 9) Andika sentensi ifuatayo katika msembo halisi. (al 3)
 Mama alimwuliza mwanawe alikochelewa na kisha akamtahadharisha kuwa haikuwa tabia njema kwa mtoto wa kike kama yeye kuzoea kutembea usiku.
- 10) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (al 4)
 Atanishughulikia vizuri.
- 11) Tumia kaimbishi –ku- kutunga sentensi tatu zitakazoonyesha matumizi matatu mbalimbali. (al 3)
- 12) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi hii. (al 2)
 Mbuga za wanyama zitapata wageni wengi mwaka ujao.
- 13) Tumia neno vibaya kama. (al 2)
 i) Kivumishi
 ii) Kielezi
- 14) Toa maneno yenye maana sawa na haya. (al 2)
 a. Izara
 b. Anisi
- 15) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al 2)
 Nitaenda maktabani ingawa ninaumwa na kichwa.
- 16) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika hali ulizopewa. (al 2)

KITENZI	TENDEWA	TENDATA
Paka		
Kama		

- 17) Tunga sentensi moja tu kutofautisha maneno haya. (al 2)
 Mkembe, mkebe.

4. ISIMU JAMII

- Jadili sababu tano zinazofanya sheng isiwe lugha ya taifa. (al 10)

JARIBIO LA TATHMINI YA GITHUGURI**102/3****KARATASI YA TATU****FASIHI****SEHEMU A: USHAIRI****1. LAZIMA***Soma shairilifuatalokishaujibumaswaliyote.*

Nina hiarikwaari, kukariri, vizurihilishairi,
Niwatambuliesiri, nibashiri, hayadhahirishahiri,
Subirayavutaheri, msubiri, niambiekwaumahiri,
Shairi la mashauri, nikariri, busaraniutajiri.

Tendawemakwahiri, nakwaari, yoteyatakuwashwari,
Utakuwamashuhuri, nahodari, tabasamu tashamiri,
Yalotendwakwahiri, hunawiri, hadimwishowadahari,
Shairi la mashauri, nikariri, busaraniutajiri.

Imaninadesturi, nihiari, iwepo tazihitri,
Iwekutoamahari, kutahiri, lakiniujihadhari,
Usitemeyasukari, namazuri, urambeyaloshubiri,
Shairi la mashauri, nikariri, busaraniutajiri.

Ninakupamashauri, sighairi, siwemwenyetaksiri,
Matajirimashuhuri, askari, nahatamadakitari,
Majivunohuaziri, tahayuri, ndomalipoyakiburi,
Shairi la mashauri, nikariri, busaraniutajiri.

Kutokaalfajiri, adhuhuri, alasinanadhari,
Japotawekanadhiri, tafakari, tafadhalitahadhari,
Lazimauwetayari, naniheri, utimizekwahiri,
Shairi la mashauri, nikariri, busaraniutajiri.

Maishakamabahari, nihitari, yabidiuwejasiri,
Katuhakunayaheri, yasoshari, kwayoteuwetayari,
Hadhariyasikwathiri, tahadhari, kablayakeathari,
Shairi la mashauri, nikariri, busaraniutajiri.

Nyenyekewajabari, sighairi, hekimafurikefuri,
Siwekamamsafiri, nikafiri, msimamohadhiri,
Leo hebustakiri, tabasuri, sidharaumashauri,
Shairi la mashauri, nikariri, busaraniutajiri.

- | | |
|--|--------|
| a) Elezadhamirayamtumziwashairihili. | (al 2) |
| b) Thibitishakwambashairihilini la arudhi. | (al 4) |
| c) Fafanuamashaurimanneyanayoangaziwanamtunziwashairihili. | (al 4) |
| d) Tambuambinumbilizalughazinazotumikakatikashairi. toamifano. | (al 2) |
| e) Elezamatumiziyaidhinyamshairikatikashairihili. | (al 2) |
| f) Andikaubetiwasitakwalughanathari. | (al 4) |
| g) Elezamaanayamanenoyafuatayokamayalivyotumiwaktikashairi. | (al 2) |
| i) Ari | |
| ii) Umahiri | |

SEHEMU B: RIWAYA**K. Walibora: KidagaaKimemwozea.***Jibuswali la 2 au la 3*

2. —. Hebulitazame umbo langu, naumriwanguhanaibayangu. Je, kwelinalinganikana Yule ajuzawakomwenyemanyamatembweretebwerekamayanguwe?”

- a) Wekadondoohilikatikamuktadha wake kamili. (al 4)
 b) Tajanauthibitishembinuzauandishikatikadondoohili. (al 4)
 c) Fafanuakwahojasitajinsimrejelewaalivyorithiukolonimkongwe. (al 12)
3. a) MwandishiwaKidagaaKimemwozeaamemulikaukiukajiwahakizakibinadamu. Jadili. (al 10)
 b) ElezajinsimbinurejeshiilivyotumikakatikariwayayaKidagaaKimemwozea. (al 10)

SEHEMU YA C: TAMTHILIA**Timothy Arege: MstahikiMeya****Jibuswali la 4 au la 5**

4. –Watuwenyematumboyasiyotuliahuwaakilizaonazohazitulii.
 Haweshikukunamatumboyaovitandanimwaonabaadayamudahunzakunavichwavyao.
 jambohilinihatarikwakiongoziyeyote. Walahamnahajakuwachezeawatunyimbozakizalendomiakahamsinibaadayauhuru.
 Babuzetuhawakupiganiauhurutujekusalitijuhudinandotozao.”
- a) Wekadondoohilikatikamuktadha wake. (al 4)
 b) Elezamaudhuimawiliyanayojitokezkatikadondoo. (al 4)
 c) Onyeshakwahojasitajinsikaulihiiinahalisismataifayanayoendelea. (al 12)
5. Ukitumiamifanomwafaka, onyeshadhimayakuwatumiawahusikawafuataokatikatamthiliayaMstahikiMeya. (al 20)
- a. Diwani III.
 b. DaktariSiki.
 c. Tatu.
 d. Mhubiri.
 e. Askari.

SEHEMU D: HADITHI FUPI**K.Waliborana S.A Mohammed: Damunyeusinahadithinyingine.****Jibuswali la 6 au 7.**

6. “**DamuNyeusi.**” (K. Walibora)
- a) –Fanguhapoameendeleakuwamwanafunzimzuri... Amejifunzakuwahakunamahalikamanyumbani.”
- i) Elezamuktadhawadondoohili. (al 4)
 ii) Bainishamifanomitatuyambinurejeshinakiini cha mifanohiyokatikahadithihii. (al 6)
- b) –Wenzanguwotemwafahamuhadithiyakobe? Mzeebabualiuliza. Wotewalijibu, –Ndio!”
 Elezamuhimuwahadithiyakobeukirejeleahadithiyakikaza. (al 10)
7. Jadilijinsimasualayafuatayoyameshughulikiwanamwandishikatikahadithiya –**MkeWangu**”
- a) Ukengeushi
 b) Thamaniyautendakazimaishani.

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI.**8. Soma kifungukifuatachokishaujubumaswali.**

Ndimikisoi, dume la ukoomtukufu.

Ulojipambanuakwamabigwa

Wachezajihodariwangoma

Ndimidumeliloingianyanjani

Makooyakatetemeka

Yakang‘ang‘aniangozekusakatanami.

- a) Tambulishakiperakinachojitokezkatikakifunguhiki. (al 2)
 b) Elezasifatanobainifuzakiperahikikatikafasihisimulizi. (al 10)
 c) Fafanuaumuhimuwakiperahiki. (al 8)

MTIHANI WA PAMOJA WA RAISMARADE**INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**

1. Weweni Rais wanchimo jawapoya Jumuiyaya Afrika Mashariki, mwandike Rais wanchiya ujumbewarisalaku tokananamsuru ruwa visa vyaugaidivilivyoshuhudiwanchini humo.
2. Kumesuhudiwa ongezeko la vijana wengikushirikimihadarati. Eleza sababu nasuluhuzatizohilinchini.
3. Uzuri wamkakasindanikipande cha mti.
4. Chifu alimwulizamzee Matatasababuyakumwozabintiyemapema. Mzee Matata alimkodolea macho
..... Endeleva.

MTIHANI WA PAMOJA WA RAISMARADE**102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

Mafuta yanayopatikana kwenye fukwe za bahari, moshi wa magari, takataka na bidhaa nyinginezo zinazotupwa hapa na hapa ni vichafuzi vya mazingira. Vichafuzi huadhiri afya zetu na kuathiri wanyama na mimea. Wanadamu wanayachafua mazingira yao kwa kila aina ya bidhaa mbaya za kikemikali zinazotoka viwandani mwa kawi / nguvu. Bidhaa hizo ni matokeo ya maisha ya siku hizi anayoishi binadamu.

Licha ya ukweli huu, ni muhimu kujua kuwa uchafuzi wa mazingira haukuanza leo. Miaka na miaka iliyopita, viwanda vimekuwa vikitoa mawingu makubwa ya moshi yenye sumu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira umeongeza mara dufu kutokana na kuongezeka kwa viwanda. Uchafuzi umesambaa ardhini, kwenye anga na majini. Msambao huu unapatikana katika pembe zote za ulimwengu wetu. Je, kuna aina zipi za uchafu?

Kwanza, kuna uchafu wa hali ya anga. Huko juu angani kuna tabaka linalojulikana kama ozoni. Tabaka hili ni aina ya gesi ya oksijeni na linaunda kinga fulani dhidi ya miale ya jua. Miale hiyo ya jua huweza kusababisha saratani ya ngozi inapomfikia binadamu. Hata hivyo, uchafu wa mazingira unaelekea kuliathiri tabaka hili vilevile baadhi ya kemikali zinazotumiwa katika jokofu au kwenye mikebe ya marashi ya kupulizia na upakiaji bidhaa, huuharibifu ukanda huo.

Uchafu mwingine ni uchafuzi wa kiajali. Uchafuzi huu hutokea bila binadamu kukusudia. Mfano mzuri ni meli inayovuja mafuta baharini. Mafuta haya huwaathiri na kuwaua wanyama wanaoishi baharini kama samaki na ndege na hata kuyaharibu mazingira yenyewe.

Miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi mwingine unaohusiana na kuwako kwa idadi kubwa ya magari. Magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazoletwa na viwanda vikubwa. Mchanganyiko huu unapoungana na maji, husababisha mvua ya asidi. Mvua hii huweza kuiua mimea, kuathiri majengo na hata kuwaua wanyama wa pori ambao huenda wakayatumia maji hayo. Magari hayo hutoa moshi uliochanganyika na madini aina ya risasi ambayo huweza kuathiri siyo tu mazingira bali pia mfumo wa akili wa binadamu.

Uchafuzi mkubwa ni utupwaji ovyo wa takataka. Fauka ya hayo, watu hufukia ardhini takataka ambazo huweza kuwa na matokeo mabaya kwa sababu ya kupenyeza kwenye udongo na maji yanayotumiwa na watu na mimea. Kila siku tunatupa takataka bila kujali wala kukubali. Takataka hizi ni kama makopo, mifuko ya plastiki, mabaki ya sigara au maganda ya matunda. Baadhi ya takataka ni hatari kwa wanyama na nyingine huweza pia kusababisha majanga kama moto. Aidha, hufanya mazingira yaonekane machafu.

Sote tunajukumu kubwa la kuchangia kupunguza uchafu wamazingira. Kwanza, kuelimisha na kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira yetu. Tunapaswa kutia takataka zetu kwenye vijalala maalum au mahali tunapoweza kuzichoma na kuzitekeza. Tuhakikishe tunatunza vitu kama mifuko, chupa na kadhalika ambavyo huweza kuundwa upya na kutumika tena. Hali kadhalika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na juhudi za kuwahimiza wenye magari kutumia mafuta ya gari ambayo hayana madini ya risasi. Kwa njia hii, tutasaidia kuyaboresha mazingira yetu. Vilevile pana umuhimu wa kutilia mkazo utumiaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuoza na kuvunjikavunjika au kusagika na kuwa sehemu ya udongo. Hatua ya kwanza ya kupambana na uchafuzi wa mazingira ni kujielimisha na kuwajibika. Kila mmoja akitoa mchango wake, tutafanikiwa. Kumbuka: kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

- a) Ongezeko la viwanda limechangiaje uchafuzi wa mazingira? (alama 3)
- b) Tabaka la ozoni huathiriwaje na uchafuzi? (alama 2)
- c) Eleza athari zozote tatu za kutotunza mazingira. (alama 3)
- d) Kwa nini miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi kuliko sehemu nyingine? (alama 2)
- e) Eleza nui mbili za uchafuzi wa mazingira zilizotajwa katika kufungu hiki. (alama 2)

- f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)
- Msambao -
 - Makopo -
 - Kinga -

2. UFUPISHO: ALAMA 15

SOMA TAARIFA IFUATAYO KISHA UJIBU MASWALI:

Biashara ya kimataifa ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile. Nchi mbalimbali zimekuwa zikitegemeana kwa namna moja na nyingine. Kwa mfano, nchi ya Kenya imekuwa ikiuza maua na mboga katika nchi za ng'ambo na kupata fedha za kigeni ambazo hutumiwa humu nchini kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo

Biashara ya kimataifa huziwezesha nchi ambazo hazizalishi bidhaa na hata huduma mbalimbali kupata bidhaa hizo kutoka nchi nyingine zinazohusiana nayo kibiashara. Mathalan, Kenya ni nchi ambayo imekuwa ikitegemea kilimo lakini haijaendelea katika sekta ya viwanda. Kenya huagiza bidhaa kama vile vipuri vya magari na hata magari yenyewe kutoka nchi kama vile Japan. Nayo Kenya huza mazao ya shambani kama vile pareto, chai na kahawa ng'ambo.

Kupitia kwa biashara ya kimataifa, nchi hupata masoko kwa bidhaa zake. Kwa vile biashara ya kimataifa huziwezesha nchi husika kuzalisha bidhaa mahususi ambazo hazitahigharimu pesa nyingi kuzalisha, nchi hizo aghalabu huzalisha kiwango kikubwa cha bidhaa kuliko mahitaji yake ya nyumbani. Nchi basi hulazimika kutafuta masoko nje ya mipaka yake. Kwa njia hii, uchumi wa nchi huendelea kuimarika.

Aidha, biashara ya kimataifa huwezesha nchi kupata huduma za kitaaluma ambazo hazipatikani katika nchi husika. Kuna nyanja za kiuchumi ambazo huhitaji wataalamu mahususi. Kwa mfano, katika sekta ya matibabu nchini humu tumepata kwamba kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanahitaji matibabu maalumu. Wanaouguua magonjwa haya huagiziwa madaktari kutoka ng'ambo au hata kupelekwa ng'ambo kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

Biashara ya kimataifa hukuza ushirikiano wa kimataifa. Nyakati za majanga ya kimaumbile na hata mengine yanayosababishwa na kutowajibika kwa binadamu, nchi hupata husaidiza kutoka nchi za ng'ambo. Kwa mfano, wakati wa mkasa wa bomu wa 1998, Kenya ilipata msaada wa kukabiliana na janga hili kutoka Israeli, Marekani, na hata Ujerumani ambako baadhi ya waathiriwa wa mkasa huo walipelekwa kwa matibabu zaidi. Ushirikiano huo wa kimataifa huwezesha wananchi kutoka nchi fulani kuenda kusomea na hata kufanya kazi katika nchi nyingine. Katika miaka ya hivi karibuni, Wakenya wengi wamekuwa wakienda kusomea vyo vyo vikuu vya ng'ambo. Wengine wamediriki kupata kazi katika mashirika ya kimataifa katika nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Rwanda, Msumbiji na kadhalika.

Biashara ya kimataifa husaidia kukuza ushindani kati ya nchi husika. Ushindani huu ni hakikisho la uzalishaji wa bidhaa za thamani bora. Kila nchi itafanya juu chini kuzalisha bidhaa ambazo zinaweza kukubalika katika soko la kimataifa. Pia, wananchi wa nchi husika hupata aina tofauti za bidhaa badala ya kutegemea ainamoja tu ya bidhaa zinazozalishwa nchini mwao.

Biashara ya kimataifa huleta ushirikiano wa kisiasa na uelewano zaidi kati ya madola mbalimbali. Mathalan muungano wa nchi za Afrika Mashariki – Kenya, Uganda na Tanzania, hauchangii tu kuleta manufaa ya kiuchumi bali huleta ushirikiano zaidi wa kisiasa.

Ingawa biashara ya kimataifa inahitajika, biashara hii huandamana na hasara mbalimbali. Biashara hii imesababisha kuwapo kwa masoko huru ambayo yameleta ushindani mkubwa kwa wafanyibiashara wadogo wa humu nchini. Baadhi ya wafanyibiashara wamelazimika kufunga biashara baada ya kufilisika. Ushuru mkubwa unaotowza baadhi ya bidhaa zinazolingia huwafanya wananchi wengi kutofaidika kwa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, kuna ucheleweshaji wa bidhaa zilizoagizwa. Bidhaa hizi mara nyingi huchukua muda kabla ya kutoka nchini. Kwa hivyo, wafanyibiashara wengi hulazimikakungojea kupata bidhaa hizi na kuwauzia wateja wao.

Vilevile, kutokana na biashara ya kimataifa, bidhaa duni huweza kupenyezwa katika mataifa yanayoendelea. Pia, baadhi ya wafanyibiashara wa kimataifa huchukua fursa hii kulangua dawa mbalimbali za kulevywa ambazo huwaathiri vijana wa nchi husika. Wengine huhusika katika vitendo vya kigaidi kama vile ulipuaji wa majengo mbalimbali kwa bomu na mauaji ya wananchi wasio na hatia.

Ni kweli kuwa biashara ya kimataifa ina hasara zake. Hata hivyo, ni mhimili mkubwa wa uchumi wa mataifa machanga.

- a) Kwa maneno yasiyozidi themanini, eleza umuhimu wa biashara ya kimataifa. (alama 7)
Matayarisho (1 mtiririko)
- b) Kwa maneno maneno yasiyozidi 40, eleza ujumbe wa aya tatu za mwisho. (alama 6)
Matayarisho. (1 mtiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- a) Eleza sifa zozote mbili za sauti /j/. (alama 2)
- b) Vitaje vipashio vya lugha kwa kuvipanga vinavyofuatana kuanzia cha chini hadi cha juu. (alama 2)
- c) Andika sentensi hii katika hali ya umoja. (alama 2)
Vilifi vivi hivi ndivyo vimekuwa vikitumiwa na meli zizi kutia nanga bandarini.
- d) Toa maana ya semi zifuatazo: (Alama 2)
i) Shupaa mwili –
ii) Kunja jamvi -
- e) Eleza maana mbili za sentensi hii (alama 2)
Wamekuja kutuliza.

- f) Geuza sentensi hizi katika kauli ulizopewa kwenye mabano; (alama2)
- i) Mwalimu aliyakataa maoni ya wanafunzi. (kutendwa)
- ii) Msamaria mwena alimuokoa mtoto aliyekuwa ametupwa pipani. (kutendata)
- g) Tunga sentensi kutofautisha maana ya vitate hivi; (alama 2)
- tuza
- tunza
- h) Eleza matumizi ya ku katika sentensi hii. (alama 1)
- Kucheza kwakekulifurahisha wengi
- i) Changanua sentensi hii kwa kutumia kielelezo cha visanduku. (alama 4)
- Mzee aliyemdhulumu msichana yule ametiwa mbaroni tena.
- j) Andika katika ukubwa wingi. (alama 2)
- Ukitaka kumla nguruwe chagua aliyenona.
- k) Tumia neno kitoto kama; (alama 1)
- i) kivumishi (alama 1)
- ii) kielezi (alama 2)
- l) Taja ngeli za nomino zifuatazo; (alama 2)
- i) Muundo
- ii) Senti.
- m) Bainisha mofimu katika neno hili; (alama 3)
- Alinizindusha
- n) Tumia amba – rejeshi na nomino ulizopewa katika sentensi kuonyesha upatanisho wa kisarufi. (alama4)
- i) ukwenzi
- ii) sandukuni.
- o) Ainisha nomino zilizopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo; (alama 2)
- Kikosi cha askari kiliwanasa wezi waliohusika katika wizi wa ng'ombe katika tarafa ya kindondoni.
- p) Jaza viashiria vya uradidi vya mbali kidogo. (alama 2)
- i) Mbuzi –
- ii) Gazeti –
- q) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumiziz mawili ya po – ya wakati. (alama 2)
- r) Kanusha. (alama 2)
- Wanafunzi wale wala wakiongea.

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

- a) Eleza dhana ya isimujamii (alama 2)
- b) Eleza dhana ya sajili. (alama 2)
- c) **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Wanafunzi : Shikamoo mwalimu ?

Mwalimu : Marahaba . Karibuni katika funzo la leo. Mnamo jana , juzi na mwisho wa juma tumejifunza kuhusu vitenzi , vivumishi, vielezi na vihishishi. Today..... samahani! But kabla hatujaendelea , do you remember all that ?

Wanafunzi : Samahani mwalimu , hatukushughulikia vihishishi.

Mwalimu : Really ? Nilidhani tulipiga hatua na kupitia..... anyway , msijali.

Taja kanuni inayothibiti matumizi ya lugha katika kifungu hiki na kupelekea kuwepo kwa sifa zifuatazo katika mazungumzo haya;-

- i) Lugha ya adabu – (alama 2)
- ii) Kuchanganya Ndimi – (alama 2)
- iii) Msamiati maalum – (alama 2)

MTIHANI WA PAMOJA WA RAISMARADE**102/3****KARATASI YA TATU****FASIHI****SEHEMU YA A: TAMTHILIA****Timothy Arege :MstahikiMeya****1. Lazima**

Ubadhirifunaukosefuwamipangomadhubutindiochanzo cha matatizoyawafanyikazikulecheneo. Eleza (alama20)

SEHEMU YA B: RIWAYA**Ken Walibora:KidagaaKimemwozea****Jibuswali la 2 au 3**

2. –Hakinakwambiawe,afadhalimkolonimzungukulikomkolonimweusi”.

a) Andikamuktadhawadondoochili (alama4)

b) Elezasifazamkolonimweusi (alama10)

c) Msemajianaonajekuwamkolonimzungualikuwaafadhali ? (alama6)

3. a) Ni mbinuzipiMtemiNasaba Bora alizozitumiakatikauongozi wake? Eleza (alama10)

b) Orodheshamasai buwanasokomokowaliyokumbananayochiniyauongoziwamtemiNasaba Bora (alama10)

SEHEMU YA C: USHAIRI

4. **Soma shairilifuatalokishauyajibumaswaliyanayofuata. (alama 20)**

Ulimwenguunalia, ukimwi _mekuwajanga,
Hakunalilosalia, angamizilenyepanga,
Nanilitakubalia, _ishijapokwakutanga,
Ni dhikimtawalia, uchunguunaidunga.

Kilasiku; kiwadia, nivilionamatanga,
Wala hakunafidia, nikamasisiwajinga,
Haliwezihurumia, gonjwalisokinga.
Sisisotetwaumia, aliwapiwakupinga.

Hekimayatuambia, tuwacheniwakupanga,
Wanetuhebukimbia, epukahuuupanga,
Ni wengiwaliojuta, hulkayakutojichunga,
Hasha _siukumbatia, ukimwiutakuchanga.

Nyienanyimlao, sheriamliitunga,
Hakunavyakudondoa, kwajiranimkipunga,
Si sharimkibomoa, ndoayenubilakinga,
Wako pekeechumia, bilahilohutaunga

Maradhiyalodunia, ni baa lisilo change,
Wajibunikuamua, tukwepelehilijanga,
Ukimwi _sakaribia, gurakatafutekinga,
Ukimwi we tokomea, sionetenamatanga.

Maswali:

(a) Tajanauelezebaharimbilizashairihili. (alama 4)

(b) Eleza umbo la shairihili. (alama 5)

(c) Kwa kutoleamifano, elezaainambilizauhuruwakishairikatikashairihili. (alama 4)

(d) Tajakwakutoleamifanombinumbilizaughakatikashairihili. (alama 2)

(e) Elezaujumbewashairihili. (alama 3)

(f) Elezamaanayamanenohayakamayalivyotumiwakatikashairi. (alama 2)

(i) Janga

(ii) Shani

SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**Jibuswali la 5 au 6**

5. a) Ulumbininini? (alama6)

b) Elezaumuhimuwaulumbi (alama8)

c) Elezamaanayamaapizo (alama2)

d) Tajanauelezesifannezamaapizo (alama8)

6. a) Taja inazama lumbanoyautani (alama 6)
 b) Eleza si fanne zamalumbanoyautani (alama 8)
 c) Malumbanoyautani yana umuhimu gani katika jamii (alama 6)

SEHEMU YA E : HADITHI FUPI

K. Waliborana S.A Mohamed: Damu Nyeusi na hadithi nyingine

Jibuswali la 7 au 8

7. Umaskini ndichokikwazokikuu cha maendeleo.
 Ukirejelea hadithi zote **tano** katika diwani ya **Damu Nyeusi na hadithi nyingine**, thibitisha ukweli wakaulihii. (alama 20)
8. Hichondichokilichokuwakiitikio na lilionakuwajibu pekee mwa fakakwa alioimba.....”
 (a) Eleza muktadha wa dondoohili. (alama 4)
 (b) –Wimbogani alioimba” ulikuwanajumbegani? (alama 6)
 (c) Aliyekuwana –jibu pekee” kwawimbo lioimba alikuwanahulkazipi? (alama 10)

5. a) niuhodariwakutumialughakwaufundiwakipekeeniufundiwalughakwamvutonaufasaha
 b) umuhimuwaulumbi
- hukuzauwezowakujielezahadharani
 - ninyenzoyakukuzaujuzinaufasahawalugha
 - huhifadhiutamaduniwajamii
 - huburudishanakuelimishawanajamii
 - hukuzauzalendo
 - huwezakutumiwakuwasilishaujumbemuhimu au ulionaatharikubwa au ambaounamakalinausiorahisikueleza
 - nikitambulisho cha utabaka
 - nimsingiwakuteuaviongozi
 - nimsingiwakuheshimiwakatikajamii (8 x1) (zozote 8)
- c) nimaombimalumyakumtakamungukumwadhibumhusikahasidi au mwovu (2 x1)
- d) maapizozaliyotolewakablayaulajiviapo
- yalitolewakwawatuambawaliendakinyumenamatarajioyajamiiza.
 - Hutolewamojakwamojana Yule aliyeathirika
 - YanawezakutolewakamalaanabaadayamhusikakukaidiamrizaMungu
 - Huletamaangamizikwajamii, hivyowanajamiihushauriwakuyaepukakwakutendamema.
 - Hutumialughafasaha
 - Hutumialugha kali ianyomuuwakujazawogailikuonyadhidiyamaovu. (4x2) (zozote 4)
- 6.
- a) utaniwamababu/mabibinawajukuu
- utaniwamarafiki
 - utaniwakoo,makabila au mban
 - utaniwamawifunamashemeji
 - utaniwamarika
 - utaniwamaumbu
- b) hufanywanawatuwawili au makundiwawiliyawatuwanapokutana
- watuwenyeuhusianomzurindiohutaniona
 - watuhufanyianamizahaambayoinadhibitiwanamashartianayotawalauhusianowao
 - huwezakuwakatiyamakabila ,marafikiwajukuunamababu,wajukuunamabibi,maumbu,bwananabibiarusinahatamataifa
 - mbinuyachukuhutumiwakwaufanifumkubwa
 - huchukuanjiayaushindani,kilammojaakijaribukumpikumwenzake
 - watuhutaniawasiokuwepo
 - huhusishauigizaji (zozote 4) (4 x 2)
- c) umuhimumalumbanoyautani
- hupunguzaurasmimiongonimwawanajamii
 - humarishaurafiki
 - hukuzautangamanomiongonimwawatumamakabilambbalimbaliyanapokujapamojakutaniana
 - hutambulishajamiikwaktajabaadhiyasifazakekatikautani.
 - Hukosoanakukashifutabiahasi
 - Huburudisha
 - Huelimisha (zozote 6) (6 x1)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016**INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**1. **Insha ya lazima.**

1. Andika dayalojia baina yako na kiongozi wa nyumba kumi kuhusu jinsi ya kuimarisha usalama katika eneo lenu.
2. Simu tamba, kiungambali, rununu au simu sogezi zina faida na hasara yake. Jadili.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali; Hisani haozi.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno; ... niliaibika. Nilipopiga darubini nyuma na kutafakari kuhusu kitendo nilichotenda, nilitamani ardhi ipasuke nitumbukie huko nisionekane tena.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016**INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**1. **UFAHAMU.**(alama 15)**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.**

Watahiniwa na wanafunzi wengine wanapoendelea kujiandaa kwa mitihani yao hasa wakisubiri ule wa mwisho, wanatumia mbinu mbalimbali katika kujiandaa huko. Mojawapo ya mbinu bora ya kutumia ni ile ya makundi. Mbinu hii huhusu kuwaweka wanafunzi katika makundi mbalimbali ili wayatumie katika udurusu wao.

Aghalabu, mwalimu huongoza shughuli hii ambapo hutumia uwezo wa wanafunzi katika kupanga makundi hayo. Hili huwa muhimu kwa kuwa huwafanya wanafunzi wanaoonekana kuwa na uwezo wa chini kujumuika na wale wanaoonekana kuwa wenye uwezo wa juu. Hata hivyo, huwa ni muhimu kujaribu kusawazisha makundi hayo ili wanafunzi wa kiwango cha juu wasione kuwa wanapoteza wakati wao na kwamba wanawafaidi wengine bila wao kufaidi. Hivyo basi, hulazimu kuwa na wanafunzi wawili wa viwango mbalimbali ili wote wanufaike. Idadi ya wanafunzi katika makundi hutegemea idadi yao, uwezo na mtazamo wa mwalimu wao. Yafuatayo ni baadhi ya manufaa.

Wanafunzi wanapokuwa katika makundi, huwa na uhuru zaidi wa kuchangizana na kuelezana wanayoyajua. Hufanya hili bila uoga ambao wanaweza kuwa nao hasa mwalimu anapokuwa darasani. Imebainika mara nyingi kuwa, mwanafunzi anaweza kuelewa au kulijua jambo fulani, lakini akakosa kulisema au kutoa mchango wa jambo hilo darasani anapoulizwa na mwalimu. Sababu huwa tofauti tofauti kama vile uoga, kutokuwa na uhakika, kutotaka kusikika, n.k. Wanafunzi wanapokuwa katika makundi, haya hayajitokezi na huonekana wakizungumza kwa wazi na ukakamavu. Hivyo basi, husema wayajuayo, na kuwapa wanafunzi wenzao uwezo wa kuyasikia na kuyakosoa mawazo yao. Aidha, ikiwa watataka kunyamaza makundini, wenzao watasisitiza kuwa watoe maoni yao, na kuchangia kuhakikisha kuwa wananoleka ifaavyo. Wanafunzi wanapokuwa katika vikundi, huwa na uhuru wa kusema kuwa hawalijui jambo fulani, na kutoa fursa kwa wenzao kuwauani. Wanapojadili suala fulani, kila mmoja hutoa mtazamo wake, wakajumuisha pamoja na kuishia kuyajua mengi zaidi kuliko walivyojua mwanzoni. Huwa si ajabu kuona wanafunzi wanaoonekana kuwa dhaifu wakiwa makini kusikiliza na kusaidiwa, wakaanza kuelewa mambo kwa njia bora zaidi kuliko walivyoielezwa na mwalimu. Kwa kufanya hivyo, huwa na uhuru wa kuwomba wenzao warudie maelezo fulani na kufafanuliwa polepole, wakaelewa kuliko walivyoielezwa na mwalimu.

Wanafunzi wanapokuwa katika makundi, wanaweza kupewa suala fulani kujadili. Wanapopewa vitabu wanaweza kutathmini yaliyojadiliwa na kubaini makosa. Wanaweza kujiuliza mbona masuala fulani hujitokeza jinsi yalivyo katika vitabu hivyo. Mfano mzuri katika shule za upili ni baadhi ya maelezo yanayokanganya katika baadhi ya vitabu kuhusu masuala kama vile vitenzi na virai, ambapo wanafunzi wanaweza kuyaangazia katika makundi na kubaini utata unaojitokeza. Hii ni mbinu bora ya kujihakikishia uelewa bora. Vilevile, wanafunzi wanaweza kubaini mengi wakichambua vitabu vya fasihi kwa pamoja, ambapo wanaweza kubaini masuala mengi ambayo huenda mwalimu hakuyadavua. Wengi hujitokeza kubaini makubwa na madogo katika vitabu hivi. Pia, wanaweza kuwa na vitabu mbalimbali vinavyoeleza masuala yanayojadiliwa, na kusaidia kupata mambo mengi zaidi.

Wanafunzi wanapokuwa katika makundi, huhimizana kuzungumza na hivyo basi wale ambao kwa kawaida huwa waoga wakaanza kupata ujasiri. Wanaweza kuanza kuchangia mara moja moja, na kadri wanavyozoeana makundini ndivyo wanavyozidi kuzungumza zaidi, wakajitokeza kuwa jasiri zaidi. Hili hasa huzidi huonekana kwa kuwa, wao kupata himizo kutoka kwa wenzao. Ili kuhakikisha kuwa ujasiri huo umekuzwa kabisa, mwalimu anafaa awaelekeze wanafunzi mbalimbali wa vikundi hivyo kuwasilisha hoja zao mbele ya wenzao. Ni muhimu wanafunzi waelewe kuwa kila mmoja wao atapata fursa ya kuwasilisha mbele ya wenzao, ili waimarike kabisa.

Wanafunzi, wanavyozidi kuwa pamoja ndivyo wanavyozidi kuzoeana na kuishia kuwa marafiki wa toka nitoke. Wao huendelea kukurubiana katika masuala mbalimbali. Aidha, mwalimu anaweza kuzua mashindano baina ya makundi, yatakayowalazimu wanafunzi kuhusika kwa karibu zaidi na kushirikiana kuhakikisha wanaibuka kuwa bora.

Maswali.

1. Toa anwani mwafaka ya kifungu ulichosoma. (alama 2)
2. Kuna umuhimu gani kwa mwalimu kuutumia uwezo wa wanafunzi anapopanga makundi? (alama 2)
3. Idadi ya wanafunzi katika kila kikundi hutegemea mambo yapi? (alama 3)
4. Eleza manufaa ya kujifunza kwa mbinu inayozungumziwa katika makala haya. (alama 4)
5. Ujasiri wa mwanafunzi unaweza kukuzwa vipi? (alama 2)
6. Eleza maana ya maneno haya jinsi yalivyotumiwa; (alama 2)
 - (i) Marafiki wa toka nitoke.
 - (ii) udururu

2. **UFUPISHO (alama 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Watu wengi, wanaamini kwamba kufundisha watoto nyimbo shuleni ni kupoteza wakati unaofaa kwa masomo ya maana. Lakini muziki nyumbani na shuleni una manufaa mengi.

Muziki ni kitulizo kikubwa sana cha moyo wa binadamu. Muziki una njia ya kipekee ya kuwasiliana. Baadhi ya ujumbe hauwezi kupitishwa kwa njia nyingine ila kwa muziki.

Muziki umetajwa kumsaidia mtoto kwa mambo yafuatayo:

Kuendeza hisia nzuri, za kuburudisha na kuzuzua. Muziki humsaidia mtoto kuweza kukabiliana na tajriba mbaya. Unampa fursa ya kutoa moyoni simanzi na dhiki yake na hivyo kumrejeshea raha tana. Liwazo la muziki ni dhahiri wakati mtoto anapolala pindi anapoiambiwa bembezezi.

Inaaminika pia kwamba muziki unakomaza akili ya mtoto na ni nyenzo muhimu sana katika hafla yake ya kujifanyia mambo, hasa kwenye miaka yake ya mapema. Muziki huhitaji umakinifu ili kutambua miondoko na maneno halisi ya wimbo huo na mambo haya humfanya mtoto kuhamisha umakini huu kwenye masomo mengi darasani. Inaaminika pia kwamba kupitia kwa muziki mtoto anaweza kujifunza mbinu ya kukumbuka mambo anayofunzwa masomoni.

Watoto ambao hujifunza muziki mara kwa mara hujipatia mbinu za werevu shuleni haswa kwenye somo la hesabu na werevu wa mambo mengine kwa jumla. Utafiti umeonyesha kwamba watu wazima ambao walijifunza muziki kabla wafikishe umri wa miaka kumi na mbili huwa na utumizi mzuri wa maneno magumu na msamiati kuliko wale ambao hawakujifunza kuimba.

Muziki pia husaidia watoto walio na kasoro za kuzungumza au walio na ulimi mzito wa kuzungumza. Watoto au watu wazima walio na shida ya kigugumizi huweza kujieleza kwa ufasaha kwa kupitia muziki na jambo hili huboresha kujiamini kwao kwa kibinafsi. Watoto kama hao huweza kujifunza na kuelewa mila na tamaduni zao.

Maswali.

- (a) Dokeza mambo muhimu yaliyomo katika aya ya kwanza hadi ya tatu..(maneno 50 - 55)
- (b) Fupisha aya mbili za mwisho kwa kuzingatia manufaa ya kujifunza muziki. (maneno 65 - 70) (alama 6, utiririko 1)

3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)

1. Tofautisha sauti /th/ na /dh/ (alama 2)
2. Ainisha viambishi tamati katika tungo lifuatalo; (alama 2)

Waliombewa
3. Tunga sentensi ya neno moja yenye visehemu vifuatavyo; (alama 4)
 - (i) Kiambishi kikanushi
 - (ii) Kiambishi cha hali timilifu.
 - (iii) Kiambishi cha mtendewa.
 - (iv) Mzizi wa kitenzi
 - (v) Kauli ya kutendea
 - (vi) Kitamatishi
4. Onyesha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mhudumu mmoja awalettee gilasi ya maji.
5. Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo; (alama 2)

Kasisi alipoingia kanisani, waumini walianza kushangilia.
6. Bainisha matumizi ya ni katika sentensi; (alama 2)

Rudini uwanjani mkanitafutie vikombe ambavyo ni vya kunywea chai.
7. Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi hii; (alama 2)

Kitabu chochote kitafaa kwa kazi ii hii.
8. Tumia kiambishi ji katika fungutenzi ili kuleta dhana na kurejelea kiima. (alama 2)

Vilevile kitumie kama kiwakilishi cha nafsi ya pili.
9. Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali; (alama 4)

Alienda usiku ingawa nilimtahadharisha.
10. Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa; (alama 3)

-Mtaweza kumsaidia mtoto wangu kesho?" mzazi akamuuliza mhisani.

11. Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)
 (i) - la (kauli tendeshea)
 (ii) Toa (tendeka)
12. Eleza matumizi ya alama zifuatazo za uakifishi. (alama 2)
 (i) Alama ya hisi
 (ii) Paradesi
13. Andika katika ukubwa wingi; (alama 2)
 Ngoma hii itachezwa uwanjani
14. Andika katika wingi karibu; (alama 2)
 Kijakazi yuyo huyo aliupoteza ufunguo uo huo licha ya kukanywa.
15. Geuza sentensi ifuatayo iwe katika hali ya -a- (alama 2)
 Chui hula swara.
16. Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari. (alama 2)
 Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na viongozi wenye misimamo thabiti mno.
17. Tumia 'O' rejeshi tamati; (alama 1)
 Kiatu kinachonunuliwa si kile unachotaka.
18. Yakinisha sentensi hii katika nafsi ya tatu umoja (alama 2)
 Tusipoonana na wazazi hatutapata pesa

4. **ISIMUJAMII.(alama 10)**

Soma kifungu kinachofuata kisha ujibu maswali yanayofuata.

Aliyenaswa na pembe 50 za ndovu ashtakiwa.

Mwanamume aliyekamatwa akiwa na pembe 50 za ndovu katika nyumba yake mtaani Githurai alishtakiwa kwa makosa mawili ya kupatikana na bidhaa za wanyama pori.

Maswali

- (i) Bainisha sajili ya makala haya. (alama 2)
 (ii) Eleza sifa za sajili uliyoitaja kwa ujumla. (alama 8)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016

102/3

KARATASI YA TATU**FASIHI****SEHEMA YA A: USHAIRI**1. **Lazima.****Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.(alama 20)**

Natwaa hino nafasi, lilo tanza kukariri,
Nayafichua upesi, ambayo kamwe si siri,
Msikize nyinyi mbasi niwapashe i habari,
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Kuntu ndaningu nafsi, likanipa tafakari
Mechunguza si kiasi, katanabahi dosari,
Ndipo miye nikahisi, kuliamba kwa hiari,
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Kila siku Jumamosi, Dominika desturi,
Magazeti binafusi, nashufu kila nahari,
Watunzi wote sisisi, ndisi wavuli mahiri,
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Nikatwaa karatasi, na peni yangu saghiri,
Niongozwe na Kudusi, kasarifu mistari,
Na pasipo wasiwasi, nudhumu hino sawiri,
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Swala ninaloakisi, muda mwingi limejiri,
Nalonga sifanyi kesi, ingawa ni taksiri,
Haya yaso ufanisi, wadhiha yamekithiri,
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Mlo kike mwatughasi, kutoshiriki dhahiri,
Talanta mnazo basi, ila hamwonyeshi ari,
Umalenga u kuasi, ni wazi ja meno ngiri,
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Beti nane za utesi, zanisemesha kwaheri,
Kuwashutumu sikosi, yamo murwa yakijiri,
Nitiye habta kasi, miye shaha machachari,
Ugani wa mashairi, wapi watunzi wa kike?

Maswali.

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 2)
- (b) Taja bahari mbili zinazojitokeza katika shairi hili kwa kuzingatia; (alama 2)
- (i) Vina
- (ii) Mishororo
- (c) Thibitisha kuwa shairi hili ni la kiarudhi. (alama 4)
- (d) Eleza maudhui yanayojitokeza katika ubeti sita. (alama 2)
- (e) Bainisha toni ya mshairi. (alama 2)
- (f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (g) Toa mifano miwili inayoonyesha idhini ya mshairi. (alama 2)
- (h) Eleza maana ya maneno haya;
- (i) mwatughasi
- (ii) utesi

SEHEMU B: RIWAYA.**Ken Walibora: Kidagaa Kimwemwozea.****Jibu swali la 2 au la 3**

2. –Basi leo ni leo asemaye kesho ni mwongo ...”

–Akiona cha mtema kuni.”

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

(alama 4)

- (b) Eleza mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
- (c) Kwa kutoa mfano eleza jinsi suala la uozo wa viongozi linavyojitokeza katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 14)
3. Kwa kutolea mifano mwafaka eleza jinis mbinu zifuatazo zimetumika kufanikisha riwaya ya Kidagaa kimemwozea. (alama 20)
- (i) Sadfa
- (ii) Jazanda

SEHEMU C: TAMTHILIA**Timothy Arege: Mstahiki Meva****Jibu swali la 4 au la 5**

4. –Tumechoka kuumbuliwa. Miaka yote tuliyoifanya kazi sisi hatuoni matunda yake. Karibu tunastaafu lakini hakuna hazina maana hakuna cha kuweka. Ni kazi ya kijungu jiko!”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Bainisha tamathali ya usemi uliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
- (c) Tamthilia ya Mstahiki Meva imeangazia harakati za kuleta ukombozi. Fafanua mbinu zilizotumiwa na wanacheneo kujikomboa. (alama 14)
5. –Kama huku si kuwatusi wananchi basi ndio kutembea nyuma ya punda aliyedhika.”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Eleza mbinu zozote nane ambazo Meva Sosi alitumia ili kuendeleza utawala wake. (alama 16)

SEHEMU D: HADITHI FUPI**Ken Walibora na S.A Mohamed (wah): Damu Nyeusi.**

6. –Mwanzoni sikuridhia kwa kuwa nilikuwa kama mtu aliyeona unyasi baada ya kuumwa na nyoka.”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Taja tamathali ya usemi inayobainika wazi katika dondoo hili. (alama 2)
- (c) Eleza nafasi ya mwanamke katika hadithi hii. (alama 10)
- (d) Mbinu ya kinaya imetumika katika hadithi hii. Thibitisha. (alama 4)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.

7. (a) Eleza maana ya maigizo. (alama 2)
- (b) Tofautisha aina mbili kuu za maigizo. (alama 4)
- (c) Kwa kutoa hoja **nne** eleza umuhimu wa maigizo. (alama 4)
- (d) Eleza dhima ya nyiso. (alama 10)

MTIHANI WA MWIGO WA GATUZI NDOGO LA KIGUMO 2016**KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**1. **LAZIMA**

Mwandikike mhariri wa gazeti la Tukuza kuhusu ufanisi na changamoto za elimu bila malipo nchini Kenya.

2. Mpango wa kuwapa wanafunzi tarakilishi utaimarisha viwango vya elimu nchini.

Jadili.

3. Samaki mkunje angali mbichi.

4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo;

..... nilipojitazama nilijidharau kwa aibu niliyojipa. Niliapa kutorudia kitendo hicho maishani mwangu.

MTIHANI WA MWIGO WA GATUZI NDOGO LA KIGUMO 2016**102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI**1. **UFAHAMU (alama 15)****Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Macho ya Abdul yalipigwa na mwali mkali wa jua la asubuhi. Ilikuwa ndiyo mara yake ya kwanza kuuona mwanga halisi wa ombwe lijiitalo dunia tangu alipohukumiwa kifungo gerezeni. Punde tu komeo la mlango wa seli lilipofunguliwa, ilimlazimu Abdul ayafumbe macho kabla ya kuyafumbua tena taratibu ili yazoe mabadiliko yake.

Ilikuwa ndiyo siku ya Abdul ya kuachiliwa huru kutoka kwenye kifungo kirefu kilichoyapa macho yake mazoea ya giza la kaburi mle gerezeni. Macho yake yalipokwisha zoea ile hali na kumhakikishia kuwa kila alichokuwa akikiona si kizuka ila uhalisia, alipiga hatua. Akatoka nje ya mlango wa seli, kisha kwa kutoamini, akageuka nyuma kulitazama tena lile pango alimokuwa ametikwa katika muda huo wote. Akayafikicha macho kwa kutoamini huku machozi yakimdongoka asijue kama yalikuwa ya furaha au ya huzuni. Alipogeuka kuanza safari ya uhuru wake, macho yake yalikumbana na lango la gereza. Hapo, akasita kidogo, labda kuhakikisha kama kweli alikuwa huru. Bila shaka, hakuna askari wa gereza aliyemshikia bunduki au kumuamuru asimame. Walimtaazama tu na kumpa tabasamu.

Taratibu, Abdul aliendelea kupiga hatua. Mhemko alikuwa nao kutokana na hewa safi iliyompenya mapafuni uliufanya moyo wake upige kwa kasi. Ghafila, tabasamu ikapasua mashavuni pake. Akasita. Akainua pua yake iliyompa hakikisho kuwa uvundo na uozo wa seli haukuwa naye tena. Ingawa mwili wake ulijaa mabaka ya uchafu na matambara yaliyouficha uchi wake kuvunda, hilo halikumkera tena. Kwa hivyo, akatia tena tabasamu. Lake kuu lilikuwa shukrani kwa kuepuka yale madhila ya joto na rundo la wafungwa. Na kama hilo halikutosha, aligeuka tena ili sasa kuliangalia lile gereza. Bila kutarajia, alipiga magoti, akainua mikono kupiga dua, "Ewe Mungu, niepushe na balaa nyingine."

Safari ya Abdul kutoka katika majengo ya gereza ilikumbwa na mseto wa mawazo. Alipokuwa katika ujia uliomwelekeza katika barabara kuu, mambo mengi yalimpitikia mawazoni asipate jawabu. Hakujuu kama wazazi wake walikuwa wangi hai, na kama walikuwa bado wanaishi katika nyumba ile ya kukodi kwa miaka hiyo kumi aliyokuwa jela. "Je, nikiwakosa, nitaenda wapi? Nitaanzia wapi kuwatafuta?" Mawazo hayo yaliifungua mifereji ya machozi, kisha ile ya makamasi. Balagha hiyo ilimfikisha katika kituo cha magari ya uchukuzi kwa ule aliouona kuwa muda wa kufumba na kufumbua. Aliyafuta machozi yake haraka kwa kiganja kisha akaziba tundu la pua, tayari kupenga kamasi. Hata hivyo, kabla hajafanya hivyo, nafsi yake ilimtahadharisha kuwa hatua hiyo ingekatiza uhuru aliopeva kwa kuchafua mazingira. Kwa hivyo akaghairi. Akavuta ncha ya shati lake na kuitumia kama hankachifu kutimiza azma yake.

Hapo kituoni, matatu iliyokuwa mbele ilikuwa na watu wachache. Abdi akaingia na kukaa upande wa kioo ambapo tafakuri nyingi zilimjia. Akakumbuka jinsi kesi yake ilivyoendeshwa kinyume kabisa na ukweli na hukumu kutolewa kinyume cha haki. Mimi Abdul, mtoto twaa tangu kuzaliwa kwangu hata mdudu sijawahi kumponda kwa udole wangu, ndiyo sasa nije kusingiziwa kuu mtu? Mungu wangu! Kwa nini dunia hii haina wema? Kwa nini wanaodaiwa kuwa wasomi hata wakapewa jukumu la kuwakilisha maslahi ya raia ndio wanaowadhulumu hao raia? Hivi, hata hukumu na tajiriba yake aliamua kufuatilia zile porojo za wanaojiita majasusi? Angeahirisha hukumu yake ili kufanya uchunguzi zaidi, bila shaka nisingepata mapigo na dhuluma hizo zote. Kwa kweli, hii ni dunia ya mwenye nguvu mpishe! Abdul alijisemea.

Maswali

- | | |
|--|-----------|
| (a) Kwa nini Abdul alifungwa? | (alama 2) |
| (b) Kwa kurejelea kifungo eleza mashaka katika asasi za kurekebish atabia. | (alama 4) |
| (c) Ni kinyume kipi kinachoonekana katika kifungo hiki? | (alama 2) |
| (d) Ni mambo yapi yaliyomtia Abdul machugamachuga alipoachiliwa huru. | (alama 2) |
| (e) Abdul anaelekea kuwa na hulka gani? Fafanua kwa kurejelea kifungo. | (alama 2) |
| (f) Msamiati ufuatao una maana gani kwa mujibu wa kifungo hiki. | (alama 2) |

- (i) Ombwe
(ii) Mhemko

2. **MUHTASARI (alama 15)**

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivini vitendo vya kinyama vinavovyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inakera sana kwa vitendo vya kigaidi inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawakinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wameelaaniwa na siku zao zimehesbiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watalipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yoa. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hili ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanaponaswa hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wemeteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii yanaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

Maswali.

- (a) Ni nini maoni wa mwandishi kuhusu suala la ugaidi. (alama 7 utiririko 1)
(b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fipisha aya mbili za mwisho. (alama 6, 1 utititiko 1)

Matayarisho.

3. **Matumizi ya lugha. (alama 40)**

- (a) Sauti zifuatazo hutamkiwa wapi. (alama 2)
/f/
/dh/
- (b) Huku ukitia mifano onyesha matumizi mawili ya paradesi (alama 2)
- (c) Kanusha fungu linalofuata; (alama 2)
Nitamsalimia mtoto ambaye ni nadhifu.
- (d) Andika kinyume cha: (alama 2)
Tajiri aliyekashifiwa amelaaniwa.
- (e) Andika katika usemi halisi. (alama 3)
Mwalimu wetu alitwambia kuwa watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa maskini.
- (f) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)
fa (Tendesha)
ja (Tendeana)
- (g) Andika sentensi hii katika hali ya udogo - wingi. (alama 2)
Tulipomwona alikuwa akichezea kisu kikali.
- (h) Yakinisha sentensi ifuatayo; (alama 2)
Usimwazime, hatakurudishia.
- (i) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali. (alama 4)
Soka ni mchezo maarufu.
- (j) Tunga sentensi moja yenye sehemu sifuatazo. (alama 3)
(i) Kitondo
(ii) Kipozi
(iii) Ala
- (k) Ainisha virai katika sentensi inayofuata; (alama 2)
Anapenda kula mara nyingi.
- (l) Tambua aina ya vishazi katika sentensi hii; (alama 2)
Ingawa tulifika mapema hatukumkuta.
- (m) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)
(i) Karatasi

- (ii) Kipepeo
- (n) Tunga sentensi yenye kielezi cha namna mfanano. (alama 1)
- (o) Eleza uamilifu wa maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
Kijana anamchezea mkulima kijana.
- (p) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya kuendelea. (alama 2)
 Mkulima anapalilia mihogo.
- (q) Tumia tanakali ya sauti yenye maana sawa na maneno yaliyopigwa mstari chini yake. (alama 2)
 (i) Tumbo lilipomwuma, alilala tumbo chini.
 (ii) Daudi alitunukiwa zawadi nyingi.
- (r) Eleza matumizi ya na katika sentensi hii; (alama 1)
 Majisifu na Nasaba Bora wataenda Wangwani nasi.
- (s) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo. (alama 2)
 Kama wanafunzi hawawezi kuwathamini walimu wao hawawezi kupita mtihani.
 Anza: Ni vigumu
4. Isimu Jamii. (alama 10)
 Jadili mikakati iliyowekwa kusaidia kukua kwa Kiswahili nchini baada ya uhuru. (alama 10)

MTIHANI WA MWIGO WA GATUZI NDOGO LA KIGUMO 2016**102/3****KARATASI YA TATU****FASIHU****SEHEMU YA A****SWALI LA LAZIMA**1. **USHAIRI** (alama 20)

Sinisumbuwe akili, nakusih e mwandani,
Afya yangu dhalili, mno nataka amani,
Nawe umenikabili, nenende sipitalini,
Sisi tokea azali, twende zetu mizumuni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani,
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini,
Kwa nguvu za irijali, Mkuyati uamini,
Kaafuri pia kali, dawaya ndwele fulani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa hali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni subili, au zongo huanoni,
Zabadili pia sahali, kwa maradhi yako ndani,
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani,
Nifwateni sipitali, na dawa zike nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini,
Daktari k'ona mwili, tanenea kensa tumboni,
Visu sitiwe makali, tayari kwa pirisheni,
Ukatwe kama fagili, tumbo nyangwe na maini,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Japo maradhi dhalili, kutenguliwa tegoni,
yakifika sipitali, huwa hayana kifani,
Waambiwa damu katili, ndugu msaidieni,
Watu wakitaamali, kumbe ndiyo bunani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mizimu wakupa kweli, wakueleze undani,
Maradhiyo ni ajali, yakata vitu thamani,
Utete huku wawili, wa manjano na kijani,
Matunda pia asali, vitu vya shimoni
Nifwateni sipitali, na dawa zi langoni?

Maswali.

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 2)
 (b) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
 (c) Kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika shairi hili? (alama 2)
 (d) Onyesha jinsi uhuru wa utunzi ulivyodhihirishwa katika shairi hili. (alama 3)
 (e) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya tutumbi. (alama 4)
 (f) Tambua mbinu ya utunzi inayobainika katika mshororo wa mwisho wa kila ubeti. (alama 2)
 (g) Onyesha maana ya maneno yanayofuata kama yalivyotumiwa na mshairi. (alama 3)
 (i) Dhalili
 (ii) Kensa
 (iii) Ndwele

SEHEMU YA B**RIWAYA: K. WALIBORA. KIDAGAA KIMEMWOZEA.****Jibu swali la 2 au 3.**

2. –Wanaume wangepastahi wanawake kidogo, wawaone kama abiria wenzao katika mashua ya maisha, dunia ingekuwa pahali pema pa kuishi ...”
 (a) Fafanua usemi huu. (alama 4)
 (b) Eleza sifa na umuhimu wa msemaji. (alam 16)

3. Kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea onyesha jiinsi sheria zilivyokiukwa katika nchi ya Tomoko. (alama 20)

SEHEMU YA C

TAMTHILIA: MSTAHIKI MEYA T. AREGE

Jibu swali la 4 au 5.

4. –Sina pingamizi maana hii ni grand idea”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Grand idea inayozungumziwa ni gani? (alama 2)
- (c) Ni maudhui gani yanayojitokeza katika muktadha wa dondoo hili. (alama 2)
- (d) Taja mbinu ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
- (e) Fafanua sifa zozote tano za msemaji. (alama 10)
5. Jadili maudhui yoyote kumi yanayodhihirika katika tamthilia ya mstahiki Meya. (alama 20)

SEHEMU YA D

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE: MHARIRI KEN WABORA

Jibu swali la 6 au 7.

6. –Mwalimu nina swali ambalo ningetaka unijibu. Je, ni kwa nini sisi huwaleta watoto shuleni.”
- (a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
- (b) Eleza hulka za wazungumzaji. (alama 8)
- (c) Fafanua maudhui yanayohusishwa na dondoo hili. (alama 8)
7. Damu nyeusi (Ken Walibora)
- Fafanua mabadiliko ambayo mwandishi angeyataka yafanywe ili ubaguzi ukomeshwe kabisa katika hadithi Damu Nyeusi (Ken Walibora) (alama 20)

SEHEMU YA E

FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 8.

8. (a) Eleza maana ya maigizo katika Fasihi Simulizi. (alama 2)
- (b) Eleza sifa **tano** za maigizo. (alama 10)
- (c) Eleza umuhimu wa maigizo katika Fasihi Simulizi. (alama 8)

MTIHANI WA MWIGO WA GATUZI NDOGO LA GATANGA 2016**INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA**

1. Lazima.
Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Tomoko Leo ukiangazia madhara na jinsi ya kukabiliana na uwindaji haramu nchini.
2. Ugatuzi una faida nyingi kuliko hasara. Jadili.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
Kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma.
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:
... niliketi nikishika tama, iliyokuwa nyumba yangu ikawa jivu tu! Sikuyazuia machozi yaliyonibubujika.

MTIHANI WA MWIGO WA GATUZI NDOGO LA GATANGA 2016**102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI**

1. UFAHAMU.(alama 15)
Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.
Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma. Nchini Kenya ufiisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano kuna maafisa wa serikali wajipatia pesa kwa kuuza stakabadi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho n.k. Kwa raia, kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya. Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini.
Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari, nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyi kazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujezi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu. Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umaa kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umaa wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, wahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambao hukwepa **majukumu** yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi. Wengine wasio wataalam huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara. Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwingine hulazimika kusalimu amri na kutoa hongo ili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika kuwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale **wasiojimudu** kifedha hubaki **wakilia ngoa**. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na **undugu** kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza hudumia jamii.
Ufisadi **umekita mizizi** na **kushamiri** katika sekta za umma na za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyikazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyikazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.
Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufiisadi. Kwa hivyo, wafanyikazi wenye bidii hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.
Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufiisadi. Tayari tume kadhaa zimeteuliwa kuchunguza visa vya ufiisadi ulitotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza **Kashfa** ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni ya shilingi) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia sizizo halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufiisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.
Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi waliohasiriwa na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa wawalipa, au wakilipwa kuwatetea mahakamani wanakwepa jukumu hilo ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

*Jg Academic Consultancy Nairobi 2011 Mocks Topical Analysis.***Maswali.**

- (a) Eleza aina **nne** za ufiisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma. (alama 4)
- (b) Kulingana na kifungu ulichosoma ufiisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani? (alama 3)
- (c) Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufiisadi? (alama 2)
- (d) Kwa maoni yako unafikiri ufiisadi husababishwa na nini? (alama 2)
- (e) Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa. (alama 1)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)
 - (i) Kashfa
 - (ii) shamiri

(iii) wakilia ngoa

2. **UFUPISHO (alama 15)****Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kutoka kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza ubongo hunasa jambo kisha hulihifadhi. Baadaye huanzisha mfumo wa kutoa kilicho hifadhiwa. Ubongo ukiathirika kwa namna yoyote katika mojawapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminike kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine, wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitaji mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini), bidhaa za soya, matunda, maziwa, bidhaa za ngano, samaki, pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madini haya ni mboga za kijani, mawe, ndengu, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja na nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendesha glukosi mwilini. Kwa hivyo, vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari kisicho hatarisha maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikitini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mthani au mahojiano. Lakini unapaswa kuwa makini.

Woga huo usikiuke mpaka na kumvuruga kiakili. Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na pia namna ya kukitoka. Halikadhalika, mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa na mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha ubongo na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na taratibu ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya hayo, mazoezi ya kiakili, kama vile kusoma makala yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo, vitanza ndimi ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo wa kuyakumbuka mambo ni jamii iliyopiga hatua kimaendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

Maswali.

- (a) Fupisha ujumbe wa aya sita za mwanzo kwa maneno..(maneno 90 - 100) (alama 9, 1 ya mtiririko)
Matayarisho
- (b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 40 - 50) (alama 6, 1 ya mtiririko)
Matayarisho

3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)

- (a) Tofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)
(i) /m/ na /n/
(ii) /e/ na /a/
- (b) Andika maneno mawili yenye muundo ufuatao wa silabi: Kiyeyusho na irabu. (alama 1)
- (c) Pambanua viungo vya kisaruifi katika kitenzi. (alama 3)
Tuliwalimia
- (d) Tunga sentensi ukitumia yile kama; (alama 3)
(i) Kiwakilishi
(ii) Kivumishi
(iii) Kielezi.
- (e) Kwa kutolea mfano, tofautisha kati ya mzizi huru na mzizi fungu. (alama 2)
- (f) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo; (alama 2)
Wavulana watatu wanaingia darasani kwa haraka.
- (g) (i) Eleza maana ya kirai. (alama 2)
(ii) Bainisha aina za virai katika sentensi ifuatayo; (alama 2)
Gari lilianguka kando ya barabara.
- (h) Yakinisha sentensi ifuatayo; (alama 2)
Asingefika mapema asingempata mwalimu wake.
- (i) Andika katika hali ya udogo wingi. (alama 2)
Nyundo iliyokuwa kwenye kikapu imeibwa.
- (j) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya parandesi. (alama 2)

- (k) Tunga sentensi kuonyesha wakati ujao hali timilifu. (alama 2)
- (l) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali. (alama 4)
Ali alimlaumu Juma ilhali kosa lilikuwa la Hassan
- (m) Tunga sentensi ukitumia kivumishi kimilikishi cha nafsi ya tatu umoja pamoja na nomino ya ngeli ya I - I. (alama 2)
- (n) Andika upya sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. (alama 2)
Dawa ilimfanya mtoto afe. (tendesha)
- (o) Sahihisha (alama 2)
Hapa mna siafu wengi.
- (p) Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Osundwa amenitupia tiara.
- (r) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi ya -ndi-. (alama 1)
- (s) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi mawili ya neno —~~ka~~?. (alama 2)
4. **ISIMUJAMII**,(alama 10)
Eleza jinsi shughuli zifuatazo zimechangia kukua kwa Kiswahili nchini;
- (a) Vyombo vya habari. (alama 3)
- (b) Uchapishaji (alama 2)
- (c) Elimu. (alama 3)
- (d) Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha rasmi nchini. (alama 2)

MTIHANI WA MWIGO WA GATUZI NDOGO LA GATANGA 2016

102/3

KARATASI YA TATU

FASIHU

SEHEMA YA A: USHAIRI

1. **Lazima.**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.(alama 20)

Barabara.

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili pupanda tena
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
–Kuwa tayari kupanda na kushuka.”

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka.

Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendeleo kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.

(Timothy Arege)

Maswali.

- (a) Taja na ueleze aina ya shairi hili. (alama 2)
- (b) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
- (c) Fafanua dhamira ya shairi hili. (alama 2)
- (d) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)
- (i) Tanakali za sauti.
- (ii) Mbinu rejeshi
- (iii) Taswira
- (e) Eleza umhimu wa maswali balagha katika shairi. (alama 2)
- (f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 4)
- (g) Eleza matumizi ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 2)
- (h) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3)
- (i) Kuruba
- (ii) Siha
- (iii) Machweo

SEHEMU B: RIWAYA.**Ken Walibora: Kidagaa Kimwemwozea.****Jibu swali la 2 au la 3**

2. –Nilikuwa nimekwenda ibada kaka.”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Ni ibada gani anayozungumizia msemaji. (alama 1)
- (c) Hii ibada imemfanya akose kuwajibika. Thibitisha. (alama 6)
- (d) Eleza **sifa** zozote tano za msemewa. (alama 5)
- (e) Eleza umuhimu wa msemaji wa kauli hii. (alama 4)
3. Jadili jinsi mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea anashughulikia maudhui yafuatayo;
- (a) Kisasi (alama 10)
- (b) Usaliti (alama 10)

SEHEMU C: TAMTHILIA**Timothy Arege: Mstahiki Meya****Jibu swali la 4 au la 5**

4. Haki yetu!
Jasho letu!
Haki yetu!
Jasho letu!
Damu yetu!
- (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Eleza kwa tafsili haki, jasho na damu inayorejelewa. (alama 10)
- (c) Fafanua sifa zozote **sita** za anayeelekezewa kilio hiki. (alama 6)
5. Onyesha matumizi ya mbinu zifuatazo katika tamthilia;
- (i) Uzungumzi nafsiya. (alama 5)
- (ii) Majazi (alama 8)
- (iii) Taswira (alama 7)

SEHEMU D: HADITHI FUPI**Ken Walibora na S.A Mohamed (wah): Damu Nyeusi na Hadithi nyingine.****Damu Nyeusi (K. Walibora)**

6. –Msifikiri kwamba mzungu anatupenda sisi watu weusi.” ;
- (a) Eleza ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya Damu Nyeusi. (alama 10)
(Tazama na Mauti - S.A. Mohamed)
- (b) ---. Lakini yeye hataki riziki, anataka muluki.”
- (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (ii) Fafanua sifa **sita** za mrejelewa. (alama 6)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.

7. (a) (i) Eleza tofauti ya ngoma na ngomezi. (alama 2)
- (ii) Taja aina **nne** za ngomezi za kisasa. (alama 4)
- (b) (i) Mivigha ni nini? (alama 2)
- (ii) Eleza sifa zozote **nne** za miviga. (alama 4)
- (c) Fafanua majukumu ya michezo ya watoto (chekechea) (alama 8)

KAUNTI NDOGO YA KEIYO KUSINI (KESO)
KISWAHILI
KARATASI YA KWANZA
PRE - MOCK
INSHA

1. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la mwangaza ukijadili sababu za ongezeko la ukosefu wa usalama nchini na kwenye mipaka ya nchi yetu.
2. Ufisadi umekuwa saratani katika nchi nyingi zinazoendelea barani Afrika. Jadili janga hili na upendekeze jinsi ya kukabiliana nalo.
3. Onyesha hatua ambazo serikali ya Kenya inachukua katika kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana.
4. Amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Thibitisha kauli hii huku ukizingatia hali ilivyo nchini Kenya.

KEIYO KUSINI (KESO) 2016
KISWAHILI
LUGHA
PRE - MOCK
KARATASI YA PILI

1. **UFAHAMU**

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali

Katika karne hii, juhudi zetu za kushughulikia changamoto za usalama zimeimarishwa zaidi kwa matumizi ya teknolojia. Kuimarika kwa ufugaji miolango, matumizi ya vifaa vya kamsa, njia za kisasa za utambuzi, utafiti na uchuguzi wa kiuhalifu ni baadhi tu ya maendeleo yaliyoafikiwa na jamii ili kujihami. Sasa hivi huduma zinazotolewa na polisi kwa umma zimewafikia watu kwa njia rahisi. Hata hivyo, maendeleo haya ya teknolojia yamehusishwana hatari fulani. Baadhi ya mifumo inaweza kutumiwa vibaya au ikawa na athari zinazotarajiwa kama vile kumdhuru mtu asiyekusudiwa.

Matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuukabili uhalifu wa jinasi si suala geni. Tangu kuvumbuliwa kwa kikosi cha askari polisi katika karne ya kumi na tisa, utendakazi na maendeleo yake yamepimwa kwa kigezo cha kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika harkati za utoaji huduma kwa raia. Tumeshuhudia maafisa wetu wakitumia vifaa vya utambuzi kwa alama za vidole na matumizi 7ya vifaa visivyotumia nyaya katika mawasiliano. Lakini kutokana na kuimarika kwa ubunifu wa wahalifu, pana haja ya vikosi vyetu kijipiga msasa zaidi ili kuzuia au kuzima kabisa njama za kihalifu. Matumizi ya teknolojia katika kuzuia visa vya uahalifu yameanza kukubalika na wanajamii kama sehemu ya maisha yao. Leo hii kuna vifaa vya kuchunguza iwapo mtu ana kifaa chochote cha chuma hususan silaha ndogondogo wakati aingiapo kwenye kumbi za umma au anapoabiri magari ya uchukuzi ya umma. Kifaa hiki kimezuia pakubwa uhalifu wa utekaji nyara uliokuwepo awali hasa miongoni mwa magari ya umma mijini. Aidha vifaa vya kudhibiti kasi ya magari vimeimarisha usalama barabarani. Uwekaji wa taa za umeme kwenye **viunga** vya miji huuhakikisha umma usalama wao na vilevile kuchangia kuwafichau wavamizi.

Kamera za ofisi katika za kibinafsi, majengo ya umma na kwenye baadhi ya barabara za miji makuu huwa hifadhi ya matukio anuwai na hivyo kuwa muhimu wakati wa kesi zinazohusisha uvamizi au uhalifu mwigine wowote. Vifaa vidogo vinavyotumia mawimbi ya kielektroniki na ambavyo hutumiwa mifukoni ni muhimu wakati wa mawasiliano ya dharura. Huwasaidia sana watu wenye umri mpevu ambao huwa ni windo jepesi la wahalifu. Aidha huwapa hakikisho la kuwa huru kyaendesha maisha yao kinyume na wali ambapo maisha yao yalitawaliwa na unyanyapaa baada ya kusikia au kuhusika visa vya uhalifu. Kwa sasa teknolojia inayotumia miale kufichua silaha haramu zilizofichwa au kumtambua mtu anayenuia kupenyeza mihandarati kwa kumeza vindoge **inagonga ndipo**. Njia hii hufanya hivi bila kumkaribia mshukiwa na kuepuka hali ya kuahatarisha maisha ya afisa wa ukaguzi. Aidha huwezesha mshukiwa kutambulika mara moja na hatari husika kutandarukiwa bila ajizi.

Licha ya ufaafu wa teknolojia ya kisasa katika kuzuia au kuzima kabisa visa vya uhalifu, atahari zake **hasi** zimeweza kushuhudiwa. Kwa mfano matumizi ya vifaa vya kwenda kwa kasi kuwafuata wahalifu yanaweza kuwa hatari kwa mtumiaji, mshukiwa au hata raia asiyehusika.

Kifaa cha kuzima kasi ya magari kwa mbali kinaweza kulisimamisha gari ghafla na kusababisha maafa makubwa. Matumizi ya mwangaza mkali au gesi kama njia ya kumdhhibiti mhalifu yanaweza kuwa kusababisha ulemavu wa kuona anu hata kupumua. Baadhi ya vifaa ambavyo hutumia miale vinaweza kuwa na athari ya kudumu na hata kusababisha maradhi ya kansa. Inapendekenzwa kuwa matumizi ya teknolojia ya kuangamiza uhalifu yazingatie haki za binadamu. Aidha njia husika iwe nafuu, pawe na uazi na uwajibikaji katiika mmatumizi yake na vilevile matumizi yake yazingatie maadili.

Maswali

- (a) Kwa mujibu wa kifugu wahalifu bado wanazididi nguvu asasi za kiusalama katika jamii. (alama 1)
- (b) i) Onyesha jinsi teknolojia imeimarisha usalama katika sekta ya usafiri. (alama 2)
ii) Ni kwa njia gani teknolojia imesiadia kupatikana kwa haki? (alama 1)
- (c) Eleza manufaa ya kutumia miale Kama njia ya kuzuia uhalifu. (alama 2)
- (d) Taja mambo mawili ambayo yanafaa kuiongoza jamii wakati wa kuteua mbinu ya kuukabili uhalifu. (alama 2)
- (e) Eleza changamoto zinazotokana nateknolojia ya kisasa katika uhalifu. (alama 3)
- (f) Eleza maana ya msamiati huu ulivyotumiwa kwenye kifungu. (alama 3)
i) Viunga

- ii) Gongwa ndipo
- iii) Hasi

2. UFUPISHO(Alama 15)

Soma makala yafuatayo na ujibu maswali.

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo ulimwenguni ni viwand. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malighafi yanayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji, viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwand ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu hasa kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaulengwa na bidhaa za viwanda. Katika msingi huu, viwanda vikubwa vitawiwa vugumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwand pia vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasnia, mataifa yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watbu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzoya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Samabamba na suala hii ni kuwa ni rahisi kujaribisha bidhaa mpya kwa mapana, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hizo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa zenyewe.

Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo. Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa ni chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimesambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huu wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwand vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

Licha ya faida zake, ueneaji au kutanda kwa viwanda hukabiliwa na matatizo mbalimbali. Tatizo la kwanza linahusiana na mtaji. Lazima pawepo na mbinu nzuri za kuweka akiba ili kuwa na mtaji wa kuanzisha biashara. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kwa kutegemea masoko ya mitaji amabyao katika mataifa mengi hayaendelezwa vyema. Inakuwa vigumu katika hali hii basi kupata pesa kwa uzaji wa hisia kwenye masoko hayo.

Tatizo jingine linalotokana na ukosefu wa mikopo ya muda mrefu ya kibiashara kwa wenye viwanda vidogo vidogo. Mikopo ya aina hii huwa muhimu hasa pale ambapo anayehusika ana mradi wa kununua vifaa kama mashine. Mikopo ya muda mfupi inayopatikana kwenye mabanki huweza kuwashinda wengi kutokana na viwango vya riba kuwa juu. Haimkiniki kwa viwanda kama hivi kukopa kutoka nje ya nchi zao. Juhudi za kuendeleza viwanda hivi huweza pia kukwamizwa na tatizo la kawi kama vile umeme. Gharama za umeme huenda ziwe juu sana. Isitoshie, si maeneo yote ambayo yana umeme. Matatizo mengine huhusiana na ukosefu wa maarifa ya kibiashara, ukosefu wa stadi za ujasiriamali au kuwa na ujasiri wa kujiingiza kwenye shughuli Fulani na miundo duni.

Ili kuhakikisha kuwa viwanda vimekuzwa na kuendelezwa pana haja ya kuchukua hatua kadha. Kwanza, kuwepo na vihamasisho kwa wanaoanzisha viwanda vidogo vidogo kama vile punguzo la kodi, kuhimiza kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo na kusaka kuyapanua masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo. Aidha kuanzishwa na kupanuliwa kwa taasisi za kuendeleza upanuzi huo. Pana haja ya kuwekeza kwenye rasilimali za kibinadamu; kuelimishwa na kupanua uwezo wao wa kuyaelewa mabo mbalimbali. Miundo msingi haina budi nayo kupanuliwa na kuimarishwa. Upo umuhimu pia wa kuongeza kasima inayotengewa maendeleo na ukuzaji wa viwanda ili kuharakisha maendeleo yake pana umuhimu wa kupambana na ufisadi unaoweza kuwa kikwazo kikubwa. Inahalisi kutambua ikiwa viwanda vitatand nchini, uchumi wan chi nao utawanda.

- a) Kwa **maneno 65-75**, eleza ujumbe muhimu unaopatikana katika aya ya pili hadi ya nne. **(alama 8,1 utiririko)**
- b) Kwa **maneno(50-55)** fafania mabo yanayotinga ukuaji wa viwanda. **(alama 5,1 utiririko)**

3. MATUMIZI YA LUGHA

- a) Tofautisha kati ya sauti (i) /e/(ii)/u/ (alama.2)
- b) Taja vigezo **vitatu** vya kuainisha sauti za irabu. (alam.3)
- c) Tunga sentensi kwa kutumia **kibadala cha kiasi** jumla. (alama.2)
- d) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. (alama.2)
 - i) (-la)(kauli ya kutendesha)
 - ii) Toa (tendeka)
- e) Tambulisha aina za nomino katika sentensi ifutayo. (alama.2)
Umma katika Jamhuri yetu unataka haki ya kila mja itekelezwe.
- f) Badilisha katika usemi wa taarifa
"Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi." afisa wa usalama akasema..
- g) Tunga sentensi moja udhahirishe maana mbili za neon hili. **Rudi**. (alama.2)
- h) Bainisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama.2)
Mzalendo amemwandikia mhariri barua.
- i) (a) fafania dhana ya chagizo. (alama.1)
(b) tolea mfano kwa kutunga sentensi. (alama.3)
- j) Akifisha. (alama.2)
mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akaema afisa wa kilimo.

- k) Andika katika wingi. (alama.2)
Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.
- l) Tofautisha kati ya
(i) Mwenye macho haambiwi ona.
(ii) Mwenyewe haambiwi ona.
- m) Rekebisha sentensi hii kwa kuiandika upya (alamal.2)
Mbuji aliyenunulia alikuna nazi vizuri
- n) Andika upya kwa **udogo-wingi**. (alama.2)
Bahari zote huhifadhi samaki anuai.
- o) Tunga sentensi iliyo na vishazio viwili huru. (alama.2)
- p) Andika upya sentensi zifuatazo kwa kutumia jina lingine lililo na maana sawa na lililopigiwa mstari. (alama.3)
(i) Ni nadra kumpata msichana asiyetoboa masikio siku hizi.
(ii) zahama ilizuka wafanyikazi walipogoma.
(iii) Azma ya kila mwanafunzi ni kupasi mtihani.
- q) Andika kinyume cha neno lilopigiwa mstari. (alama.1)
Mhalifu huyu **alitunga** mimba.
- r) Bainisha matumizi yak i katika sentensi ifuatayo. (alama.1)
Jua limekuwa likiwaka.
- s) Tumia kivumishi cha **-a unganifu** pamoja na nomino ya ngeli ya I-I kutunga sentensi. (alama.1)
- t) Tumia kistari kifupi katika sentensi sanifu za Kiswahili ili zilete maana mbili tofauti za kimatumizi. (alama.2)
- 4. Isimu jamii**
- a) Eleza sababu zozote sita zinazochangia katika kufa kwa lugha. (alama.6)
- b) Taja mitazamo mine kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili. (alama.4)

MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KEIYO KUSINI (KESO) – 2016**102/3****KISWAHILI****KARATASI YA 3****FASIHI****PRE - MOCK****SEHEMU YA A: MSTAHIKI MEYA****1. Lazima**

–Matosha kumkunja kila aliye chini yake kama ua la wakati wa alasiri”

- a. Eleza muhtadha wa dondoo hili ? (alama 4)
- b. Onyesha tamthali ya usemi iliyotumiwa. (alama 2)
- c. Kwa kurejelea tamthalia nzima eleza mbinu za kiutaawala alizotumia Meya kudumisha utawala wake (alama 10)
- d. Eleza sifa nne za mzungumaji (alama 4)

SEHEMU YA B: RIWAYA**“Kidagaa Kimemwozea” – Ken Walibora*****Jibu swali la 2 au 3*****2. –Tembo itakuu ndugu yangu. Punguza ulevi bwana. Siku hizi naona aibu kukuita ndugu yangu”**

- a. Fafanua muhtadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b. Wahusika hawa wawili ni kama shilingi kwa ya pili. Thibitisha. (alama 16)

3. Dhihirisha umuhimu wa mbinu zifuatazo katika Kidagaa Kimemwozea.

- i. sadfa (alama 10)
- ii. mbinu rejeshi (alama 10)

SEHEMU YA C: USHAIRI***Jibu swali la 4 au 5*****4. Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo.**

Walimwengu nambieni,
Mie nipate fahamu,
Hawamo vijana wetu,
Meingilia yapi mambo,
Hulkazo hawa wana, tewengu zatia waja,
Sampuli ya hivi viumbe,
Lipi jama uelimisha.

Watembea kwa vishindo,
Mirindimo ardhi tia,
Ole wako kikutana, nao hawa Masultani,
Takupita ja risasi, vikumbo nusura upigwe,
Wanadi maisha ni shoti,
Wapapie kwa haraka.

Viatu vya chuchumia, ati mbingu wafikila,
Magotini vyabisha hodi, waungwana waole,
Vishati vya kuninginia,
Matumboni ja kima,
Waso haya wana haa,
Wana mji wao ati.

Kikutana nao njiani,
Manywele taambani, maashiki wa rasta,
Bobmale waabudu, ndio jagina wao wana,
Ziki lao la kisasa, lashangaza wengi waja,
Sautiyo maskio,
Kusikiza ole wako, tajipata umepokewa,

Na hapa jahazi, langu ufukoni lafikile,
Enyi vijana pilika,
Ya kisasa kufuata,
Bila hadhari si haki,
Tuchuje yenye tijara,

Ya izara tupuzile,
Heshima tudumisha, tamaduni tuienzi.

Maswali

- a) Kwa kutoa mifano, eleza mambo anayolalamikia mshairi. (alama 3)
 b) Eleza ukitoa mifano namna utungo huu umezingatia kaida za ushairi kimuundo. (alama 3)
 c) Andika mfano mmoja wa;
 i) Mistari mishata. (alama 2)
 ii) Msitari kifu. (alama 2)
 d) Eleza namna uhuru wa mshairi ulivyodhihirika katika utungo huu. (alama 4)
 e) Andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi. (alama 4)
 f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
 i) Libasi
 ii) Tijara

5. **Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo.**

Kama wanipenda sana, wangu wamtakiani?
Sitaki la kupishana, kama hilo samahani,
Penzi watu kupendana, twaingiliana nini?
Naepuka kupitana, nakusihi kwa hisani,
Wanipendani kidada, mke wangu wakuganya.

Mke wangu nakuganya, hakuwepo barazani,
Vipi mambo wachanganya, si mwizini wewe kwani,
Sije mambo hutafanya, siri tia mvunguni
Na bwanako wamfanya, huadhaninuhaini?
Kupenda kwa hilo choyo, yoyo halikosekani.

Halikosekani yoyo, fikiria mara thani,
Waama nakupa onyo, heri tuache utani,
Kuzidi ni mtawanyo, nitajiweka pembeni,
Lau hutaposa moyo, hubanduka ukumbini,
Sidhani unanipenda, mke wangu sitamwacha.

Ukimpenda nipende, simkere mhisani,
Ukija mweke upande, simfanye kasirani,
Kitaka chake kipande, acha inda hadharani,
Sema naye umpende, upitie ardhini,
Panya huvuvia dada, nyama au punje kila.

Maswali

- a) Toa kichwa mwafaka cha shairi ulilosoma. (Alama 1)
 b) Shairi hili ni la aina gani? Fafanua. (Alama 2)
 c) Eleza ujumbe wa mshairi katika ubeti wa pili. (Alama 3)
 d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (Alama 4)
 e) Taja mbinu zozote tatu za lugha katika shairi hili na uzitolee mifano. (Alama 3)
 f) Eleza muundo wa shairi hili. (Alama 5)
 g) Nakili mloto wa ubeti wa pili kisha ueleze maana yake. (Alama 2)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

“Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine” – Ken Walibora

Jibu swali la 6 au 7

6. Jadili vile mwandishi amefanikisha anwani yake katika hadithi ya —~~Saka~~ ya Mambo”. (Alama 20)
 7. (i) —Nani basi atamwambia vingine na yeye ameiona kwa macho yake ingawa ndotoni?”
 a) Eleza muktadha wa dondo hili. (Alama 4)
 b) Onyesha mbinu iliyotumika katika dondoo. (Alama 2)
 c) Kwa kurejelea hadithi hii, fafanua athari za tamaa. (Alama 6)
 (ii) Kwa kurejelea hadithi ya —~~Mwana~~ wa Darubini” eleza dhuluma zinazomkumba mtoto wakike. (Alama 8)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza sifa tano zinazotumika katika uainishaji wa nyimbo. (Alama 10)
 b) Jadili njia ambazo jamii ya kisasa hutumia ili kudumisha fasihi simulizi. (Alama 10)

**MTIHANI WA MUUNGANO WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI ZA NANDI MASHARIKI NA TINDERET
2016
KISWAHILI
INSHA
102/1
PRE - MOCK
KARATASI LA KWANZA**

1. Wewe unaomba kazi ya muda katika tume ya kupambana na ufisadi. Andika tawasifu yako utakayoambatanisha kwenye barua ya kuomba kazi.
2. Teknologia imetumika kufanikisha uhalifu. Jadili
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali "mgema akisifiwa, tembo hulitia maji."
4. Andika insha itakayoishia kwa:
... Licha ya kufanikiwa nilifahamu kuwa hiyo ilikuwa hatua moja kati ya nyingine.

**MTIHANI WA MUUNGANO WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI ZA NANDI MASHARIKI NA TINDERET
2016
KISWAHILI
102/2
LUGHA
PRE - MOCK
KARATASI LA PILI**

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma makala haya kasha ujibu maswali

Wahenga walisema majembe yakikaa pamoja hayaachi kugongana. Methali hii imekaririwa kuonyesha migingano na migogoro baina ya viumbe vyenye uhai hasa adinasi. Hii ndio sababu kuna sheria ama amri ambazo hutuzunguka. Aghalabu mtu azikiukapo, anawaliwa na hisi ya ndani sana inayoweza kupima thakili ifaayo. Mtu anaposhindwa, hisi hiyo humtawala siku nyingi na kumpa kujuta makosa yake kwa adabu kali inayomkabili. Kila jamii hutawalia kwa sheria au huwekewa mipaka ambayo unapoivuka unahesabika kuwa wafanyi inadi, ambapo ni sharti uadhibiwe.

Mambo haya hata hivyo yamekuwa hadithi siku hizi. Sheria zetu za leo zilibuka wakati wa ukoloni lakini zimefanyiwa marekebisho kadhaa, baada ya muda Fulani. Jamii zetu za kijadi hazikuwa zinaishi hobelahobela, zilitawaliwa na mwongozo Fulani. Miongozo ilitofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine. Miongozo hiyo ilitokea kwa wanajamii tangu wakiwa wadogo sana na hatua hiyo iliendelezwa hadi walipokomaa. Badala ya kuweka misahafu ya amri na sheria zenye kuandamishwa na adhabu za vifungo gerezani faini na nyingine nyingi, miongozo iyo ya kijamii ilitolewa kwa njia mwanana ya kuvutia na hamasa. Hapakuwa na haja kuumwa vichwa ili kuwenga vifungu hivyo akilini wala kuhifadhi majipande ya maneno ambayo yalikusudiwa kubeba uzito Fulani uliolingana na kosa lake. Uhifadhi wake ulitumia taswira mbalimbali za wadudu, wanyama, ndege, mazimwi au madude mengine, ambayo waliyapa uhuishi na kuchukua tabia za binadamu.

Ingawa sheria katika jamii za jadi zilitolewa kwa njia mwanana, isije ikaeleweka kuwa watu walikuwa huru kufanya watakalo. La hasha. Kulikuweko na chombo mwafaka cha kuadhibu wakosefu. Baraza la wazee kilikuwa chombo mahususi cha kulinda jamii hizo, hata hivyo kiongozi anayehusika hakulazimika kukesha akikariri misahafu ya sharia hakuhitajika kwenda na vidokezo vyovyote kwa madhumuni ya kuvirejelea kila inapobidi. Kwa upande wa mstakiwa, moyo wake haukupaa kwa ajili ya kiwewe cha yale yatakatofuata. Baada ya kuvutana, alihitajika kuwaomba rahi wazee kwa dhati na kutoa ahadi kutorudia kosa hilo. Hivyo kuwaacha wazee na rajua njema.

Ingawaje mashauri yalikuwa yakifanyika kwa njia isiyodhuru, hapakuwa na lelemama yoyote. Mambo hayakuchukuliwa kijuujuu. Ilibidi kutunza wakati barabara. Uropokaji haukuruhusiwa aswilani. Mkosaji wa aina hiyo alilipuliwa kwa adhabu. Mara mingi alitowza faini ya mifugo, nafaka na hata kufanya kazi maalumu kama vile kurekebisha boma la mkutano, kusafisha joshu na mengine.

Mahakama ya kijadi yalifikiria uwezo wa mtu binafsi. Aidha, adabu ilitolewa kulingana na uzito wa kosa lenyewe. Kwa kuwa ilibidi nidhamu itunzwe wakati mwingine, wazee wa baraza waliweza kubadilisha wale waliokusudiwa kubarizi. Kwa mfano, katika mashauri yaliyohusu ugoni-mtu na mkewe hawawezi kuwekwa pamoja katika baraza moja isipokuwa kwa nadra sana, baada ya kila suluhisho kukosekana

Katika kuendesha mashtaka, tanzu za fasihi simulizi, kama methali, zilitumika ili kumwangazia mhusika aelewe ubaya wa kosa lake, ili afikie majuto ya dhati na ajifunze kuwa raia mwema kama wengine.

Sheria hizo ziliweza kubadilishwa na kufanyiwa mabadiliko ya aina Fulani pindi inapobidi. Kwa mfano, mgeni anapojiunga na jamii, ilibidi baraza la wazee kumjulisha desturi, mila na sheria za jamii ile.

MASWALI

- a) Je mwandishi anaonyesha tofauti zozote kati ya mahakama ya kisasa na ya jadi? Fafanua (alama 4)
- b) Fasihi simulizi na sheria za jamii za jadi zimeoanishwa vipi? (alama 2)
- c) Chanzo cha umuhimu wa sharia katika jamii ni nini? (alama 2)
- d) Unafikiri kulikuwa na upinzani ama utetezi katika uendeshaji wa mashtaka wa kijadi? (alama 3)
- e) Kwa ufupu, eleza vile mkosaji alivyoadhibiwa kulingana na sheria za jadi (alama 2)
- f) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumiwa katika taarifa (alama 2)
- i. Misahafu
- ii. Lelemama

2. MUHTASARI (ALAMA 15)

Kila jamii ina vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi ambavyo vina tambulisha utamaduni wake. Jamii ya waswahili ina ngoma za aina mbalimbali kama chakacha, vugo, ngoma, marimba, chapuo, zumari n.k kuupa uai wimbo. Nyimbo ni tungo zenye mahati ya sauti inayopanda na kushuka ambazo huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na jazanda na mapigo ya silabi. Nyimbo hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimsingi.

Shughuli nyingi za binadamu huandamana na nyimbo. Nyimbo huwa na mawazo mazito na hubuniwa kuonyesha uhusiano wa kijamii, migogoro, kukekeli, kubembeleza, kuliwaza, kutumbuiza na kuburudisha.

Kuna aina mbalimbali za nyimbo katika jamii za kiafrika. Kwanza, kuna nyimbo za kazi. Hizi zinaimbwa wakati wa kazi kuimiza watu kufanya na kuendelea na kazi. Kwa kawaida, nyimbo hizi zinaweza kuwa fupi ama ndefu, kutegemea kazi inayofanywa ama mtunzi wa wimbo wenyewe. Mdundo pia hutegemea kazi inayofanywa kwa kuwa baadhi ya nyimbo zina midundo ya haraka ambayo haiwezi kuandamana na utenda kazi Fulani.

Pia, kuna nyimbo za watoto au bembelizi ambazo huimbiwa watoto wadogo kwa sauti nyororo ili kuwabembeleza kulala ama kuwanyamazisha wanapolia. Wakati mwingi, pembelezi huimbwa na walezi ama akina mama. Mtundo wa aina hizi za nyimbo huwa ni wa taratibu na maneno yenye kumvutia mtoto anyamaze ama kulala.

Vilevile, kuna nyimbo za kuomboleza ama mbolezi ambazo huimbwa wakati wa matanga. Lugha na toni inayotumika ni ya kuhuzunisha na kusikitisha na maneno yake hutegemea Yule aliyeaga dunia na hadhi yake katika jamii. Mara nyingi, imani ya jamii kuhusu kifo hutahirishwa katika nyimbo hizi. Wakati mwingine, baadhi ya nyimbo hutaja sifa za aliyeaga na vitendo vyake vitakavyokosekana kutokana na kufa kwake.

Aidha kuna nyimbo za kisiasa ambazo hutumika kuendeleza sifa ama sera Fulani na wale walio uongozini, pia, hutumika na wale wanaodhulumiwa katika kupinga wale walio uongozini na sera zao. Kwanza hutumika na viongozi kueneza propaganda ama msimamo Fulani kuhusu uongozi wao na kuhamisisha wananchi. Pia, nyimbo hizi hutumika kuwasifu ama kuwakashifu viongozi. Pia, kuna nyiso, ambazo ni nyimbo zinazoimbwa wakati vijana wanapotiwa jandoni. Kwa muda mrefu, tohara imekuwa shughuli muhimu katika jamii nyingi za kiafrika kwa sababu ya kuchukuliwa kuwa hatua muhimu ya kutoka utoto na kuingia utu uzima. Nyingi zilitoa sifa kwa waliopitia hatua hiyo, wazazi pamoja na wasimazi wao. Ziliimbwa kwa dhamira ya kuwafanya wavulana kukikabili kisu cha ngariba; kutoa mafunzo kwa wavulana kuhusu majukumu yao mapya katika jamii baada ya kupitia hatua ile na kuwaonya dhidi ya kuogopa na matokeo ya woga wao kwa kisu cha ngariba.

Nyimbo katika jamii zina umuhimu mwingi ambao ni pamoja na kushauri, kuonya, kusifu, kuburudisha katika hafla mbalimbali na kudumisha utamaduni wa jamii husika kwa kuwa maswala yanayoshughulikiwa yanahusu jinsi mambo yanavyofanywa katika jamii wakati wimbo unaohusika ukitungwa. Nyimbo vilevile ni njia mojawapo ya kutoa ama kupitisha mafundisho ya jamii, malezi, na hekima kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Isitoshe, baadhi ya nyimbo hutumika kama njia ya kuhifadhi matukio muhimu ya kihistoria. Kuna nyimbo ambazo hushughulikia matukio kama ukombozi wa jamii nan chi kwa jumla.

MASWALI

- a) Eleza aina mbalimbali za nyimbo katika jamii za kiafrika (manemo 20-30) (alama 7)
- b) Eleza dhima ya nyimbo katika jamii (maneno 30-40) (alama 8)

2. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- a) Tofautisha sauti zifuatazo (alama 2)
- /dh/ /sh/
- b) Eleza matumizi ya ki iliyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo (alama 1½)
- Ukirusha kipira hiki kitapotea
- c) Ziandike sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno badala yay ale yaliyopigwa mstari (alama 2)
- i. Si desturi yangu kuwatusi watu
- ii. Mwalimu alifunga ndoa mwaka jana
- d) Andika katika kauli ya kutendesha. (alama 1)
- Toa
- Lewa
- e) Tofautisha sentensi hizi (alama 2)
- Anataka vyakula vyote
- Anataka chakula vyovyote
- f) Andika sentensi hii kwa ukubwa (alama 1)
- Mwizi aliiba kikapu na kisu
- g) Changanua sentensi ifuatayo kwa matawi (alama 4)

- Alipoiba jana alipigwa kitutu
- h) Eleza maana ya methali hii (alama 2)
Mnyonge msonge
- i) Bainisha virai katika sentensi hii (alama 3)
Wakulima wengi wenye mashamba makubwa wamevuna mwaka huu mazao tele
- j) Eleza maana tatu ya sentensi hii. (alama 1½)
Alimlilia mwanawe
- k) Tofautisha vitate hizi (alama 2)
Susu
Zuzu
- l) Ainisha viambishi katika neon lifuatalo. (alama 3)
Kitakachowaumiza
- m) Tambua na ueleze aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Kipsang alimnunulia simu mpenzi wake.
- n) Tambua na ueleze dhana ya viunganishi vilivyomo kwenye sentensi zifuatazo. (alama 1)
i. Yeye ni askari tena msalihina
ii. Aliwahi mapema maadamu alipata basi
iii. Alikila japo hakukipenda
- o) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo (alama 2)
Fuata
Sheheni
Tahiri
Feta
- p) Tumia tanakali ifuatayo kutunga sentensi sahihi. (alama 1)
Bwakia bwaku
- q) Bainisha ngeli za maneno haya (alama 1)
Kalafati
Parare
- r) Eleza dhana ya silabi funge na wazi kwa kutumia mifano mwafaka. (alama 3)
- s) Kanusha sentensi ifuatayo (alama 1)
Watakapofika hospitalini watatibiwa
- t) Akifisha sentensi hii (alama 2)
Lo ghafla nilijikuta pekee yangu dunia ilikuwa imenigeuka
- u) Eleza maana ya msembo ufuatao (alama 2)
Pembe za chaki
- v) Eleza maana mbili za neno Tete (alama 2)

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

TOM: Vipi Tracy? Naona leo unalinga sana.

Umenivaria miwani, mbona hivi? Is it because you are very smart today?

TRACY: Niko poa! Hata hivyo naona una yako mengine wewe! Siringi! Niko busy tu sana.

Plus company yako inatisha, hujui siku hizi nimechil. Tena umenibore.

TOM: Kumbe wewe ni.....

- a) Taja sajili inayojitokeza katika dondoo hii (alama 1)
- b) Taja mifano inayojitokeza katika dondoo ya
- i) Kubadili msimbo (alama 1)
- ii) Kuchanganya msimbo (alama 1)
- c) Ni kwa nini wazungumzaji hubadili na kuchanganya msimbo (alama 2)
- d) Ni mzungumzaji yupi ana lafudhi? Ni nini maana ya lafudhi (alama 3)
- e) Taja sababu mbili za kuwa na lafudhi. (alama 2)

MTIHANI WA MUUNGANO WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI ZA NANDI MASHARIKI NA TINDERET**2016****KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIHI****PRE- MOCK****1. SWALI LA LAZIMA****ULIYATAKA MWENYEWE:** *D.P.B Massamba*

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,
 Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo! Hutaki,
 Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
 Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
 Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindikiki,
 Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
 Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
 Mishikeli mia mia, kwako ona haitoki,
 Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
 Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
 Ulimwengu ni shujaa, hilo kama hukumbuki,
 Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
 Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
 Ulijidhania simba, hutishiki na fataki,
 Machungu yamekukumba, hata neno hutamki,
 Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
 Na tena ukajiona, kwambawe mstahiki,
 Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki.
 Uliyataka mwenyewe!

Majuto ni mjukuu, huja kinyume rafiki,
 Ungejua mwisho huu, ungetenda yalo haki,
 Uko roho juu juu, popote hapakuweki
 Uliyataka mwenyewe!

Maswali

- | | |
|---|-----------|
| a) Eleza dhamira ya shairi hili. | (alama 2) |
| b) Tambua jinsi <u>mbili</u> anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake. | (alama 2) |
| c) Taja na utoe mifano ya aina zozote <u>mbili</u> za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi | (alama 4) |
| d) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari. | (alama 4) |
| e) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili. | (alama 4) |
| f) Bainisha toni ya shairi hili. | (alama 2) |
| g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. | (alama 2) |
| i. Mstahiki | |
| ii. Hupuliki | |

SEHEMU YA B: TAMTHILIA: MSTAHIKI MEYA – TIMOTHY AREGE

- | | |
|--|------------|
| 2. Jadili jinsi maudhui ya usaliti yanayofafanuliwa katika tamthilia hii | (alama 20) |
| AU | |
| 3. –Hilo ndilo nililokuitia mtumishi.” | |
| a) Eleza muktadha wa dondoo hili. | |
| b) Ni mambo yepi ambayo mtumishi alikuwa ameitiwa? | |
| c) Uongozi wa baraza la mji wa cheneo umejaa ubadhirifu mkubwa. Thibitisha | (alama 12) |

SEHEMU YA C: KEN WALIBORA: KIDAGAA KIMEMWOZEA

Jibu swali la 4 au la 5

- | | |
|--|-----------|
| 4.Huyo mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi? | |
| a) Eleza muktadha wa dondoo hili. | (alama 4) |

- b) Jadili uhusiano uliopo baina ya mzungumzaji na maudhui (alama 6)
- c) Taja mbinu ya lugha zilizotumika katika dondoo (alama 2)
- AU
5. a) Mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea amemulika ukiukaji wa haki za kibinadamu. Jadili. (alama 10)
- b) Eleza jinsi mbinu rejeshi imetumika katika riwaya ya kidagaa. (alama 10)

SEHEMU YA C: FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 6 au la 7

6. a) Eleza maana ya Miviga (alama 2)
- b) Toa mifano ya sherehe za kiafrika zinazoambatanishwa na miviga. (alama 5)
- c) Eleza sifa tano za Miviga (alama 5)
- d) Bainisha umuhimu wa Miviga (alama 5)
- e) Miviga ina udhaifu gani? (alama 3)
7. a) Misimu ni nini? (alama 2)
- b) Onyesha jinsi misimu huundwa (huzuka). (alama 5)
- c) Eleza sifa tano za misimu (alama 5)
- d) Eleza umuhimu wa misimu (alama 5)
- e) Toa mifano mitatu ya misimu ya Kiswahili na maana zao. (alama 3)

SEHEMU D: HADITHI FUPI; Ken Walibora na Said A. Mohamed (Wahariri)

Jibu swali la 8 au la 9

8. Onyesha jinsi hali ya kutojielewa inavyojitokeza katika hadithi ya *Damu Nyeusi* ya Ken Walibora. (Alama 20)
9. Jadili sifa na umuhimu wa wahusika wafuatao ukirejelea hadithi ya *Mke Wangu* ya Muhamed Said Abdulla.
- a) Msimulizi (alama 10)
- b) Aziza (alama 10)

MAZOEZI

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BURETI

KISWAHILI

INSHA

102/1

KARATASI LA KWANZA

1. LAZIMA

Wewe ni mkenya. Umefuzu shahada ya ukapera na uzamili, na kuajiriwa kazi katika idara ya forodha. Andika TAWASIFU yako.

2. Eleza juhudi ambazo serikali imefanya kushirikisha vijana katika ujenzi wa taifa.
3. Andika insha kuthibitisha methali. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.
4. tunga kisa kinachomalizikia kwa maneno yafuatayo:
.... Mhadhiri mkuu wa kitivo alipoita jina langu, nilishusha pumzi, kweli safari imekuwa ndefu.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BURETI

KISWAHILI

102/2

LUGHA

KARATASI LA PILI

1. UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwa msururu wa migomo na maandamano ya raia. Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiashara wakipiga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama, kuku na ndege. La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipwa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti!

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo. Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu. Wegine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunahitajika muda mrefu ili kufaulu.

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya. Matatizo yanakumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu. Swali ni je, hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni Suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya. Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na Ukandamizaji. Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebishwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipya ya kiutawala si yoyote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wa kuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimamia maisha ya watu. Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

Maswali

- a) Yape makala haya anwani mwafaka. (alama 1)
- b) Eleza mtazamo wa Wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu. (alama 3)
- c) –Ugatuzi nchini Kenya ni mfumo wa kibepari” thibitisha kauli hili kwa kurejelea makala. (alama 4)
- d) Kulingana na taarifa uliyosoma, nini chanzo cha misururu ya migomo na maandamano ya raia? (alama 3)
- e) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuzi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu. (alama 2)
- f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa hii. (alama 2)
 - i) Ugatuzi
 - ii) Kibepari

2. UFUPISHO

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhabisha kuona wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu yam wananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na Imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila Mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, Mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea wakenya mateso. hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya Mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanapaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, Mbinu hii yaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

- i) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu Suala la ugaidi. (maneno 60-70) (alama 7, 1 utiririko)
 ii) Kwa kutumika maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. (alama 6, 1 utiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA

- a) Onyesha tofauti zilizopo kati ya
 i) /e/
 ii) /u/ (alama 2)
- b) Ainisha viambishi katika neno waliibiana (alama 2)
- c) Tambua matumizi ya kiambishi ji katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
 Jino la jitu lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji yule
- d) Taja vigezo vitatu vya kuainisha sauti za irabu. (alama 3)
- e) Andika kinyume cha sentensi hii
 Baba amejenga nyumba nzuri iliyosifiwa na mgeni
- f) Eleza tofauti ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari (alama 2)
 i) Hiki ni kitabu cha mwalimu
 ii) Hikini cha mwalimu
- g) Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya kistari kifupi (-) (alama 4)
- h) Andika katika usemi wa taarifa
Mbona unamfanyia karaha mwenzako?Je, utaenda kumwomba radhi?Phanice aliuliza.
 i) Tumia maneno yafuatayo katika sentensi moja ili kubainisha tofauti zao kimaana: (alama 2)
 i) Chuuza
 ii) Chuza
- j) Eleza maana mbili katika sentensi hii. (alama 2)
 Majambazi walimwibia Letangule gari jipya
- k) Andika kwa ukubwa
 Kiti kilichokuwa kimekaliwa na mwanamke yule kilivunjika. (alama 2)
- l) Bainisha vielezi na ueleze ni vya aina gani katika sentensi hii. (alama 2)
 Sipendi wanaohama kwao ili kuenda kuishi kizungu.
- m) Akifisha:
 rais alimwamuru usiwashughulikie mabalozi wajeuri (alama 3)
- n) Tambua shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama 2)
 Mwalimu mkuu alituandalia karamu ya kufana
- o) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi ndi- (alama 2)
- p) i) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu lake (alama 1)
 ii) Tunga sentensi moja ya kuonyesha rai (alama 1)
- q) Weka kirejeshi O' tamati kwenye kitenzi **chungu** kisha ukitungie sentensi. (alama 1)
- r) Nomino hizi ziko katika ngeli gani? (alama 2)

4. ISIMU JAMII

Maenezi ya Kiswahili Afrika Mashariki punde baada ya uhuru yalikuwa na mchango tele. (alama 10)
 Fafanua zozote tano.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BURETI**KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIH****SEHEMU YA A****1. Lazima**

Onyesha namna mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea amefaulu kutumika Mbinu zifuatazo.

- a) Kiangaza mbele (alama 10)
b) Stihizai (alama 10)

SEHEMU YA B**Tamthlia ya Mstahiki Meya: Timothy Arege****Jibu swali la 2 au 3****2. –Hwapo umefanya yapo mengi ambayo hayakunyooka.”**

- a) Andika muktadha wa dondoo. (alama 4)
b) Eleza jinsi baadhi ya wahusika walivyojaribu kuyanyoosha mambo. (alama 6)
c) Dhahirisha unadhirifu katika tamthlia ya Mstahiki Meya. (alama 10)

AU**3. Hatua tuchukuazo maishani mwetu zaweza kutuathiri na kuathiri nchi pakubwa. Fafanua kauli hii ukimrejelea Meya Sosi. (Hoja kumi)****SEHEMU C: USHAIRI****Jibu swali la 4 au la 5****4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.****Amiri A.S Andanenga: Sauti ya Kiza**

1. Ngakua na mato, ya kuonea
Ngalisana kito, cha kuchezea
Kilicho kizito, cha kuelea
Kikamuenea, akivae
2. makusudi yangu, ngaliandaa
Ngafinyanga chungu, cha mduwaa
Ngatia vitangu, vinavong'aa
Ili ziwe taa, kwa apikae
3. Mkungu wa tano, wa mduwara
Ulo bora mno, kisha imara
Ulo na maono, kuwa ni dira
Kwenye barabra, itindiae
4. Ngaomba baraka, kwake Rabana
Punje za nafaka, kila aina
Chunguni kuweka, kwa kulingana
Hajaangu suna, yule alae
5. Ngafanya bidii, kwenda mwituni
Sio kutalii kukata kuni
Ya miti mitii, huko jikoni
Isio na kani, ni iwakae
6. Kwa yangu mabega, nikathubutu
Ngabeba mafiga, yalo matatu
Bila hata woga, kwenye misitu
Samba tembo chatu, sinitishie
7. Miti yenye pindi, na jema umbo
Ngajenga ulindi, mwemw wimbombo
Fundi aso fundi, penye kiwambo
Moyo wake tambo, apekechae
8. Singaajiri, ngachimba mimi
Kisima kizuri, cha chemchemi
Maji ya fahari, ya uzizini
Jua la ukami, siyaishae
9. Tamati nafunga, kwa kuishia
Mato ndo malenga, kanikimbia
Nahofu kutungwa, mabeti mia
Asije chukia, ayasomae

- a) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 2)
- b) Kwa kurejelea ubeti wa pili, eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi alioutumia mshairi. (alama 4)
- c) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
- e) Fafanua aina tatu za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 6)
- f) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

5. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

1. Sema semea wajibu, mwenye kutetema,
Sema na walo karibu, mbali ukisema,
Sema kufunza wajibu, noleji, hekima,
Sema ajue Fulani, usihulu sema
2. Sema yanayokukaa, yanakusakama,
Sema yaliyozagaa, kwa mwako mtima,
Sema unajihadaa, kwani tawafuma?
Sema wajue ni nani, usiache sema
3. Sema yote si uasi, si tenge si noma,
Sema toa wasiwasi, upate salama,
Sema japo ni risasi, longi litauma,
Sema yote hadharani, radidia sema
4. Sema pasi na ukali, mwiza taloloma,
Sema neno la asali 'taramba' kitema,
Sema kwa mzo akili, watakushituma,
Sema kwa yako maghani, usikome sema
5. Sema zitaje ghururi, duniya ni dema,
Sema ana maghubari, duniya ni rima,
Sema duniya hatari, mwina wa nakama,
Sema sema kwa yakini, masa ghaya sema
6. Sema 'kwani hamuoni, waloachwa nyuma?'
Sema pasi taraghani, uliyoyasema,
Sema wachuma tumboni, ja minyoo sema,
Sema sema mwafulani, u salama sem

Maswali

- a) Toa mifano miwili ya idhini ya kishairi katika shairi hili. (alama 2)
- b) Tambua bahari zozote nne zinazopatikana katika shairi hili na utoe sababu. (alama 4)
- c) Onyesha vile shaha alivyofua dafu katika kutumia Mbinu zifuatazo: (alama 2)
- i) Anafora
 - ii) Usambamba wa kiusawe
- d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
- e) Ujumbe wa nafsineni unamlenga nani? (alama 2)
- f) Eleza sifa za kiarudhi katika ubeti wa pili. (alama 4)
- g) Andika ubeti wa tano katika lugha tutumbi/nathari. (alama 4)

SEHEMU YA D

Hadithi fupi: Damu nyeusi na hadithi nyingine

6. Huku ukirejelea hadithi zifuatazo, jadili maudhui ya ukengeushi
- i) Mke wangu
 - ii) Samaki wa nchi za joto
 - iii) Damu nyeusi
 - iv) Tazamana na mauti

SEHEMU YA E

Fasihi simulizi

7. a) Taja tanzu zozote tano za Fasihi simulizi kisha utoe mifano miwili ya vipera vyake. (alama 10)
- b) Eleza sifa zozote tano ambazo hupote Fasihi simulizi inapoandikwa. (alama 5)
- c) Miviga ni nini? (alama 1)
- d) Fafanua sifa nne za miviga. (alama 4)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI NDOGO YA GEM

102/1

KISWAHILI

Karatasi ya 1

(Insha)

Julai/Agosti 2016

Muda: Saa 1³/₄**1. LAZIMA**

Wewe ni katibu wa Baraza la Mitihani nchini Kenya. Umeudhishwa na visa vya wizi wa mitihani ya kitaifa. Andika tahadhari kwa wahusika.

Au

Umezata habari kwamba binamu wako anayeishi Uholanzi ameanza kutumia mihadarati. Mwandikie barua pepe ukimweleza kuhusu athari hasi za tabia hiyo.

2. Jadili namna ambavyo binadamu anaweza kukabiliana na majanga yoyote matano ya kimaumbile.

3. Mwenye shoka hakosi kuni. Thibitisha.

4. Andika insha itakayoishia maneno yafuatayo :

... nilijitazama jinsi nilivyohasirika kupindukia, nikajikuta machozi yakinitiririka njia mbilimbili ndipo nikakumbuka ushauri niliopewa na wazazi wangu wapendwa.

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI NDOGO YA GEM

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

Julai/Agosti 2016

Muda: Saa 2½**1. UFAHAMU (alama 15)****Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali yaliyoulizwa.**

Miaka na dahari iliyopita katika nchi ya Uyunani aliishi mtaalamu anayefahamika kama Aristotle. Mtaalamu huyu anachukuliwa na watu wengi lama kitovu cha taaluma nyingi. Msingi wa msimamo huu ni kuwa kauli, matamko na maandishi yake mengi yameishia kuwa kama msingi ambako majengo mbalimbali ya kitaaluma yamejengwa. Aristotle alisema kuwa binadamu au mja kimaumbile kuvutwa na hisia za kuishi katika jamii. Hisia hii ya kuishi katika jamii ndiyo msingi mkuu wa kushirikiana kwa njia anuwai, mathalani, maisha ya jamaa, ya mjini, vijijini, shuleni, serikali na hata tawala mbalimbali.

Maisha yoyote ya jamii humjuzu binadamu ashirikiane na wenzake pamoja na kuvishirikisha vipawa vyake ili kuimarisha na kuyakomaza maisha au jamii yenyewe. Yaani kuimarika na kukomaa kwa maisha ya jamii hutegemea kwa kiasi kikubwa mchango, japo ukufi, wa kila mwanajamii hiyo. Mchango huo hutokana na nia ya kutaka kuyaona maendeleo makubwa yamefikiwa siyo kwa nia ya kujinufaisha kama mtu binafsi bali kwa faida ya umma. Katika ushirikiano huo, ni lazima pasiwe na ubaguzi wala kutengana kwa misingi yoyote ile; ya rangi, maumbile, dini au hata hali ya maisha. Inahalisi kuikumbuka maana ya msembo kuwa rangi na ngozi ni utambuzi si ubaguzi.

Waja hushirikiana katika hatua mbalimbali. Binadamu anazaliwa katika jamaa na pale pale hujiunganisha na majirani. Ujirani huu wa binadamu wenzake pamoja na mazingira yao huiunda tabia yake. Kadiri anavyokua ndivyo anavyoanza kujihisi mmoja wa watu wanaomzunguka, jamii ile, kabila lile au hata taifa lile. Ili kukabiliana na mazingira yake, binadamu huhitaji msaada na hata ulinzi wa watu wengine. Huu hasa ndio msingi wa methali ya kuwa mtu ni watu. Tangu akiwa mwana mkembe, mja huhitaji msaada wa watu wengine kupewa chakula, kusimama na kutembea, kufundishwa jinsi ya kujielezea, kupata matunzo wakati wa magonjwa, kuelekezwa jinsi ya kupambana na mazingira yake, kusoma na kuelewa jamii yake na hata kufuata imani fulani. Binadamu hutamani kufanya mambo ya kila nui ambayo havezi kuyatimiza peke yake. Kwa mfano, mja hutegemea haki zake zilindwe na wengine, mathalani, serikali.

Popote binadamu alipo, ana haki ya kushirikiana na wenzake katika jamii yake. Haki ya kuishi maisha ya kijamii ni mojawapo katika haki za kimsingi katika maisha ya binadamu. Haki hii inaenda sambamba na uhuru wa binadamu wa kuchagua kikundi au tapo la wanajamii analotaka kujihusisha nalo. Haki hii ni ya lazima na inapaswa kulindwa isipokuwa pale tu inapokwenda kinyume na sheria za jamii fulani. Kwa mfano, ikiwa kujihusisha na kikundi fulani kunaelekea kuwa tishio kwa usalama wa jamii, basi haki hii huwa imetumiwa vibaya. Pili, binadamu anayeishi katika jamii anaweza kujipatia mali kutokana na kazi au juhudi zake. Hii ni haki yake. Hata hivyo, huruhusiwi kuiba ili aweze kuipata mali hiyo.

Ushirikiano kati ya binadamu au ushirikiano katika jamii ni msingi imara wa kuwepo kwa maendeleo katika jamii fulani. Kila tutumiapo neno 'maendeleo', humanisha kujielekeza lengo maalum tulilochagua na ambalo litayakuza maisha yetu. Maendeleo huhusisha kupiga hatua mbele. Mtu anayesonga mbele hana budi kuwa na kitu au lengo analoliendea huko mbele.

Ikiwa hana lengo, basi takuwa anawayawaya kama kuku aliyedenguliwa kichwa na anapaswa kujitathmini. Maendeleo yanahusisha kutoka hatua fulani duni hadi hatua nyingine afueni.

Kaitika zama kongwe za mawe, binadamu alitegemea mawe kama silaha za kufanya shughuli zake nyingi. Hivi leo maendeleo ya kisayansi yamefikia ngazi za juu sana katika *awamu hii ya utandawazi* ambapo kuwepo kwa tarakilishi na vifaa vingine kumesahilisha mambo mengi sana. Kuna mambo mengi chanya ambayo yametokana na maendeleo ya kisayansi kama vile: kurahisisha mawasiliano, kuharakisha na kuboresha uzalishaji mali, kufanya usafiri bora na mwepesi miongoni mwa wengine. Hata hivyo, kuna *maendeleo hasi* kwa kuwepo kwa *silaha za haki* zinazoweza kuuangamiza ulimwengu mzima. Nchi ambazo zina satua kubwa huweza kutumia uwezo wao wa kiuchumi na kimaendeleo kuzidhalilisha jamii nyingine. Hata hivyo, ni vizuri maishani binadamu, mkubwa kwa mdogo, mwenye uwezo kwa asiyekuwa nao atambue kuwa mja anahitaji jamii.

- a) Je, ina maana gani kusema *Aristotle* anachukuliwa kama kitovu cha taaluma nyingine ? (alama 2)
 b) Taja haki mbili kuu za binadamu. (alama 2)
 c) Je, kwa mujibu wa kifungu hiki, maana ya maendeleo ni nini ? (alama 3)
 d) Kulingana na taarifa hii, ni kwa nini mja huhitaji jamii. (alama 3)
 e) Kifungu hiki kinatoa ushauri gani kwa binadamu ? (alama 2)
 f) Eleza maana ya maneno na kifungu kifuatacho kama kilivyotumiwa katika taarifa hii. (alama 3)
 i) Satua
 ii) Anawayawaya

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata.

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana. Akiwa na nidhamu hiyo, atakuwa mtu mwadilifu anayeweza kustahiwa na kusadikika katika mambo, shughuli na hali tofauti.

Kwanza, mtoto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani mwao, shuleni na pia katika jamii. Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa vijulanga wale wanamtegemea kama msimamizi wa mambo nyeti ya maisha yao. Kwa hivyo, ni dhahiri shahiri kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume cha mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili, huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, mathalani jukumu ama dhima fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Bila shaka, watu watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambao tayari wamekwishatiwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadilifu daima atajiepusha na shutuma na manjanga yote yanayoweza kuchipuka.

Kuna msemu maarufu kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu kwamba, "aliye kando haangukiwi na mti. Pia waliambiwa kwamba, *–pilipili usiyoilu yakuwashiani?*"

Ni bayana kutokana na misemo hiyo miwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuwakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya 'watoro ambao ni watovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozo na mielekeo ya watu wazima ambao wako mazingirani mwake. Ndipo wa kale wale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbani hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kutikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu wote katika maisha yake. Ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayana kwamba mabaya yote wayatendayo duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani, watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu. Ni heri mja kujihidi mwenyewe, kwani uhalifu haulipi chochote.

- a) Kwa kurejelea aya tano za kwanza, eleza madhara yanayoweza kumpata mtu kwa kutokuwa na nidhamu. (maneno kati ya 50 - 60) (alama 6, 1 ya mtiririko)
 b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (Tumia maneno 55-60) (alama 7, mtiririko 1)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- a) i) Sauti ni nini katika lugha ? (alama 1)
 ii) Taja sifa mbili za sauti /k/ (alama 2)
 b) Tunga sentensi moja ukitumia : (alama 2)
 i) Kiunganishi tegemezi / cha masharti
 ii) Kihusishi cha kinyume cha matarajio

- c) Kanusha sentensi ifuatayo kwa wingi, wakati uliopita hali ya kuendelea. (alama 2)
Mwalimu alikuwa alimwadhibu mwanafunzi mwenye hatia.
- d) i) Elezamaanaya kiambishi. (alama 1)
ii) Tunga sentensi iliyo na vipashio vifuatavyo vya sarufi : (alama 3)
nafsi
wakati ujao
hali ya matarajio
kirejeshi
yambwa
mzizi
kiishio
- e) Eleza sifa mbili za vishazi tegemezi. (alama 1)
- f) Yakinisha katika udogo umoja. (alama 3)
Watu wale hawaachi kuandamana na mbwa wao waliodhoofika kiafya.
- g) Changanua sentensi ifuatayo kwa mtindo wa mshale / vishale. (alama 4)
Omondi ni mhasibu lakini hatii bidii kazini.
- h) Andika sentensi hii katika usemi halisi. (alama 2)
Mwalimu alimuamuru mwanafunzi amalize kazi hiyo haraka.
- i) Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendeka. (alama 2)
i) cha
ii) pa
- j) Andika kisawe cha : (alama 2)
i) Hawala .
ii) Katani ..
- k) Eleza maana ya shamirisho kitondo kisha utunge sentensi ili kukibainisha. (alama 2)
- l) Kwa kutumia mifano miwili, eleza uamilifu wa shadda. (alama 2)
- m) Eleza matumizi mawili ya kinyota. (alama 2)
- n) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Tulimkuta akiwa katika uchungu mwingi.
- o) Bainisha matumizi ya 'ku' katika sentensi hii. (alama 1)
Naomi atakupikia chai halafu aende kule uwanjani.
- p) Fafanua maana zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo : (alama 2)
Mabaharia walisema hawatawasili
- q) Mtu aneyejiingiza katika matatizo yanayomshinda kutoka huambiwa methali gani. (alama 1)
- r) Andika nahau inayojumuisha ujumbe ufuatao. (alama 1)
Mtu anayekuwa na wanawake wengi.
- s) Kikosi ni kwa askari, ni la maji na la nywele. (alama 2)

4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

- a) Taja sababu mbili zinazochangia kufa kwa lugha. (alama 2)
- b) Eleza vyanzo viwili vya makosa katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. (alama 2)
- c) Taja mambo mawili yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili. (alama 2)
- d) ... ah ... naomba kumwongelesha chucho ... Naam, naam chucho
Hujambo? ... si ... si ... sina neno .. naam. Mjomba amezidiwa si wa maji si wa chakula ...
kweli ? ... Muungu ? Mkuu amedhihirisha ... yes ... ok ... yeah ... ala! Ameishiwa na pesa.
- i) Tambua sajili husika katika dondoo hili. (alama 1)
- ii) Kwa hoja zozote tatu, eleza sifa za sajili hii. (alama 3)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI NDOGO YA GEM

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

Julai/Agosti 2016

Muda: Saa 2½**SEHEMU YA A : USHAIRI****1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

- | | | |
|----|--|--|
| 1. | Haki ya mtu thawabu
Hata 'nipatishe tabu
Kulitenda la wajibu
Nitafanya majaribu
Haki yangu 'taidai | kuidai sitasita
muhali mimi kukita
liwe hai au mata
na inapobidi matata
hata iwe ni kwa vita |
| 2. | Haki ya mtu u'ngwana
Sitaukiri ubwana
Na ikiwa ni kuwana
Sikiri kuoneana
Haki yangu 'taidai | siseme mimi nateta
na jeuri unoleta
sitajali sitajuta
na kupakana mafuta
hata iwe ni kwa vita |
| 3. | Haki ifukie chini
'Tumbukize baharini
Ukaifiche jangwani
Itundike milimani
Haki yangu 'taidai | ipige na kuibuta
'tazamia kuifwata
nitakwenda kuileta
nitawana kuileta
hata iwe ni kwa vita |
| 4. | Haki ijengee ngome
Na fususi isimame
Tainuka nishikame
Sifa kubwa mwanamume
Haki yangu 'taidai | izungushe na kata
iwe inapitapita
haki yangu kukamata
kuenda huku wasota
hata iwe ni kwa vita |
| 5. | Uungwana siuuzi
Ahadi za upuuzi
Kwa kila alo maizi
Tope yake makaazi
Haki yangu 'taidai | kwa njugu au kashata
na rai kuitaita
hawi mithili ya bata
na chakula cha kunata
hata iwe ni kwa vita |

Maswali

- | | | |
|----|---|-----------|
| a) | Bainisha dhamira ya mshairi. | (alama 2) |
| b) | Eleza umuhimu wa mbinu zozote mbili ambazo mwandishi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. | (alama 4) |
| c) | Andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi. | (alama 5) |
| d) | Fafanua aina tatu za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. | (alama 3) |
| e) | Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. | (alama 2) |
| | i) Idadi ya mishororo | |
| | ii) Mpangilio wa vina | |
| f) | Fafanua toni ya shairi hili | (alama 1) |
| g) | Taja nafsini katika shairi hili. | (alama 1) |
| h) | Tambua na ueleze maana ya mshororo ufuatao
Mleo wa ubeti wa mwisho. | (alama 2) |

SEHEMU B : TAMTHILIA**Mstahiki Meya : T. Arege****Jibu swali la 2 au la 3**

- | | | |
|----|--|------------|
| 2. | –Duniani kuna watu na viatu na Cheneo ina watu na viatu.” | |
| a) | Eleza muktadha wa dondoo hili. | (alama 4) |
| b) | Kwa kutoa mifano mwafaka, fafanua undani wa kauli ya msemaji. | (alama 6) |
| c) | Onyesha sifa za msemaji wa kauli hii pamoja wa umuhimu wake katika tamthilia. | (alama 10) |
| 3. | a) Jadili mambo ambayo yanachanjia kuanguka kwa utawala wa Meya. | (alama 10) |
| | b) Eleza njia ambazo Wanacheneo walitumia katika kuleta mabadiliko katika Mji wa Cheneo. | (alama 10) |

SEHEMU C : RIWAYA**Kidagaa Kimemwozea : K. Walibora****Jibu swali la 4 au la 5**

4. –Nina furaha kukujulisheni kwamba ... mnamo mwisho wa mwezi. Naomba mradi ... usitishwe ...”
- a) Weka mambo haya katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Kuna dhana anayoikataa katakata msemaji wa maneno haya. Itaje na ueleze japo kifupi. (alama 2)
- c) Dhana hii inaonekana kukita mizizi katika jumuiya ya Wanatomoko. Dhihirisha. (alama 14)
5. Ndoa ni asasi ambayo kwayo mwanamke amedhulumika pakubwa katika jamii. Jadili kwa mujibu wa riwaya hii. (alama 20)

SEHEMU D : HADITHI FUPI**Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine****Walibora K. na Mohamed S.A - Wahariri****Jibu swali la 6 au la 7**

6. Katika hadithi ‘_Ndoa ya Samani’ —Sitaka kueleza jambo la ziada. Nilitamauka kabisa kiasi cha kwamba tulipokuwa ...”
- a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
- b) Kuna sababu iliyotolewa baadaye kama chanzo cha kutibuka kwa jambo hili. Itaje. (alama 2)
- c) Taja na ueleze sifa zozote tatu za mnenaji wa maneno haya (hapo juu) (alama 6)
- d) Eleza kinaganaga maudhui yanayojitokeza katika hadithi hii. (alama 8)
7. a) Ubaguzi ni kati ya masuala mazito yanayojadiliwa katika —_Damu Nyeusi”. Thibitisha. (alama 10)
- b) Ushirikina umedhihirika wazi katika hadithi ‘_Glasi ya Mwisho Makaburini’. Tetea dai hili kwa maelezo na mifano mwafaka. (alama 10)

SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI

8. a) Ngano ni nini ? (alama 2)
- b) Eleza sifa zozote sita za ngano. (alama 6)
- c) Vyanzo vya ngano vina umuhimu gani ? (alama 5)
- d) Tofautisha kati ya mighani na ngano za mashujaa. (alama 4)
- e) Ngano za kiayari zina umuhimu gani katika jamii zetu ? Taja tatu. (alama 3)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA WESTLANDS

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

102/1

KISWAHILI

Karatasi ya Kwanza

(INSHA)

Julai /Agosti 2016

Muda: Saa 1¼

1. Swali la lazima.

Andika barua kwa rafiki yako aliye nchi nyingine kuhusu hofu iliyozushwa na suala la ugaidi nchini na jinsi ambavyo lingeweza kukabiliwa.

2. Jadili jinsi unywaji wa pombe kupindukia umechangia majonzi mengi nchini.**3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali:**

Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwegu.

4. Tunga kisa kinachomalizika kwa maneno yafuatayo:

... tulishangazwa na jinsi watu tofauti wanavyoweza kuletwa pamoja kwa jambo kama hili.

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA WESTLANDS

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI

Karatasi ya Pili

(Ufahamu, ufupisho, Sarufi na Matumizi ya lugha na Isimujamii)

Julai / Agosti 2016

Muda: Saa 2½

1. UFAHAMU (alama 15)Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kama kuna jambo ambalo limeiparaganya akili ya mahuluki ni kuelewa dhana ya demokrasia. Kiumbe huyu heshi kuuliza mkururo wa maswali. Demokrasia ni nini hasa? Tunaweza kula demokrasia? Ni dude gani hili? Lina kichwa au mkia pekee yake? Je, demokrasia inazuia njaa? Demokrasia ni himaya ya wasomi tu au vilevile ni haki ya mafalahi? Kwa muda mrefu kumekuwa na kinyang'anyiro kikubwa katika jamii ambacho azma na matokeo yake yamekuwa ya kutatanisha. Baadhi ya watu wamejitokeza kama mchuzi wa ugali na kuzusha zahama ambayo si ya kuyumkinika. Vichwa vya adinasi vikafyekwa kwa mindu na maparange na matumbo yakapasuliwa na kupakaza utumbo na vijusi kila mahali. Shingo zikapigiwa vigingi na kukomewa ardhini. Demokrasia si mchezo wa lelemama. Ni sharti tujifunge vibwebwe tumwage damu na tufe ili tupate demokrasia ya kweli. Mmoja wa mibabe wa demokrasia aliguruma kadamnasi ya umati huku ngoma za vita zikirindima. "Hata Marekani na Ulaya. Walimwaga damu. Mamilioni ya watu walipukutishwa na kimbunga cha demokrasia. Chini walilaliana kama vimatu na tunutu. Hawa manafiki wanafikiri hatuwajui. Katu hatutakubali porojo zao. Wanatupikia majungu kisha wakatoweka na demokrasia ya Afrika na ile ya Ulaya." **Mkereketwa** wa Uafrika akachangamanua.

Demokrasia ya Afrika basi imefuata mkondo huu wa umwagaji damu. Kila kukijiri uchaguzi zahama hutawala. Walio madarakani hawataki kubanduka. Hutafuta visababu vya kukwepa wimbi la ushinde. Demokrasia ni mchezo wa mizengwe tu ati. Hali hii imesababisha maafa makubwa. Uharibifu mkubwa wa mali, majeraha, ukimbizi wa raia ndani na nje ya mataifa husika, dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake, kuzagaa kwa magonjwa ainati na uhasama wa kikabila. Jambo la kusikitisha ni kwamba raia na viongozi hawaelekei kujifundisha lolote kutokana na hali hii. Huku mataifa mengi ulayani na Asia yakikwea daraja moja baada ya nyingine kimaendeleo, Afrika imedumaa tu. Imesalia kuimba ule wimbo wake kutokea azali: 'Tutaendelea vipi na tunadhulumiwa na kaka wakubwa.' Siasa na demokrasia katika bara la Afrika ina taji kubwa hususan kwa wachache waliofanikiwa kudhibiti nyenzo za kutia tonge kinywani. **Ulitima** wa umma husalia miradi hewa ya tabaka la viongozi ambayo hutumiwa kuvinadi zamu nyingine ifikapo tena. Demokrasia ya kweli imo mikononi mwa umma pale utakapojikomboa kiawazo na kwa ujasiri kudai huduma bora uwajibikaji na kuheshimiwa kwa mkataba wa kijamii ulioasisiwa na Jean Jaiques Rousseau.

Maswali

- Kwa maoni ya mwandishi, binadamu amaechanganyikiwa kwa njia gani? (alama 2)
- Eleza ni vipi demokrasia ya kweli inaweza kufikiwa. (alama 2)
- Kwa nini inasemekana kuwa 'Demokrasia ni mchezo wa mizengwe'? (alama 2)
- Kuna athari nyingi zinazotokana na kinyang'anyiro cha Demokrasia. Eleza zozote nne. (alama 4)
- Fafanua ni vipi dhiki za raia zimesalia kuwa miradi-hewa ya wanasiasa. (alama 2)
- Andika maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye kifungu. (alama 2)
 - Mkereketwa
 - ulitima

2. UFUPISHO (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mirundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji wake ni tisho kubwa kwa siha ya umma pamoja na mazingira. Hii ni kwa kuwa taka huwa ni makazi ya wadudu na wanyama waharibifu kama nzi, mbu, kombamwiko na panya ambao hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye thamani. Maji taka nayo, pamoja na mifuko ya plastiki, huwa mastakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa mbalimbali. Mifuko ya plastiki ina madhara zaidi kwa kuwa huziba mitaro ya maji na kuzuia upitaji wa maji. Madhara hutokeza wakati mvua za gharika zinaponyesha. Maji hukosa njia yake ya kawaida ambayo huwa imezibwa na mifuko hii. Maji haya husababisha mafuriko ambayo huleta hasara ya mali na wakati mwingine ya uhai. Fauka ya haya, mifuko hii huwasakama tumboni wanyama sio wa nyumbani tu, bali wa porini na majini.

Kwa sababu ya hatari zitokanazo na taka, pana haja kutafuta njia na teknolojia ya kuweza kukabiliana na taka ili kuyatunza mazingira na siha ya umma. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na rasilmali ili kupunguza uzalishaji wa taka. Matumizi ya bidhaa kwa njia ya ubadhirifu huwa chanzo cha uzalishaji wa taka kwa wingi. Kwa mfano maji ni rasilmali ambayo imeendelea kutumiwa kwa ubadhirifu na hiyo huzalisha maji taka kwa wingi. Rasilmali hii inaweza kutumiwa kwa uangalifu. Kwa mfano badala ya kutumia bafu ya mnyunyu kuogea, mtu anaweza kutumia maji ya karai.

Watu wengi huchukulia taka kuwa kitu kisicho na manufaa yoyote. Hawajui kuwa kwa kutumia teknolojia endelevi, taka nyingi zinaweza zikageuzwa na kuwa na manufaa mengi. Vijana wadogo sehemu za mashambani wanahitaji pongezi kwa kuwa na utambuzi huu wengi kwa kukosa hela za kununua mipira ya viwandani hutumia makaratasi na mifuko ya plastiki kutengeneza mipira wanayoitumia. Hii ni teknolojia endelevi ambapo taka hugeuzwa na kuwa na manufaa.

Baadhi ya wananchi wenye ubunifu nao wameanzisha miradi ya kuzoa takataka kutoka majumbani mwa watu. Hutoza ada fulani ya uzoaji, kisha huzipeleka taka hizi kule zitakakobadilishwa ili ziwe na manufaa. Mifuko na mabaki ya plastiki kama vile matangi, mitungi, sapatu na champali. Huwa malighafi ya kutengenezea bidhaa nyingine. Taka za chupa na chuma nazo huuzwa katika viwanda vinavyozigeuza kuwa na manufaa tena. Taka za karatasi hutumiwa kutengenezea bidhaa kama vitabu, katoni, shashi za chooni, magazeti na kadhalika.

Taka zinaweza pia kugeuzwa kuwa zenye faida kwa kuzitumia kufanyia mboji. Ni muhimu kutambua kuwa si kila aina ya taka inaweza kutumiwa hapa. Taka zinazoweza kufanyiwa mboji ni zile ambazo huoza kwa haraka nazo ni kama vile mabaki ya vyakula, mboga na matunda. Hizi ndizo taka zinazozalishwa zaidi siku hizi na hasa sehemu za mjini na katika maeneo ya biashara kama mikahawa, hospitali n.k. Mtu akiwa na nafasi anaweza kuchimba shimo ambalo atafukia taka hizi ili kutengeneza mbolea. Hii ni njia isiyodhuru mazingira nayo ina manufaa kemkem. Kwanza, hugeuza taka ambayo inaweza kuwa hatari na kuifanya iwe yenye manufaa. Kwa hivyo, hutatua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokana na mirundiko ya taka. Mchanga nao hufaidika kupata virutubishi. Mbolea kama hii inaweza ikatumika kukuzia mboga au maua katika bustani.

Maji taka, hasa yanayotumiwa kuoshea vyombo, nayo yanaweza kutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani za maua. Maji taka haya yanahitaji kutayarishiwa njia mahususi ya kuyaelekeza katika mashamba haya baada ya kutumiwa.

Aghalabu watu wengi wana mazoea ya kuchoma taka, Ni kawaida kupata matanuri ya kuchomea taka katika baadhi ya mitaa, shule, hospitali n.k badala ya kupoteza moto bure inawezekana pakawekwa birika kubwa au tangi la chuma ambalo litatumia moto huo kuchemshia maji ambayo yanaweza kutumiwa katika shughuli za nyumbani.

Hata hivyo ni muhimu kukumbuka kuwa kuna baadhi ya taka ambazo ni hatari na huenda zisigeuzwe ili kutumika kwa njia yenye faida. Taka hizi ni kama mikebe au vifaa vingine vyenye kubeba sumu au dawa hatari. Ni bora kuzitupa dawa hizi katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo

Kwa vyovyote vile, si jambo muhali kuwa watu popote wanapoishi kulinda siha yao pamoja na kutunza mazingira. Ulinzi na utunzaji huu huhitaji uangalifu mkubwa katika utupaji taka.

Maswali

- a) Fupisha ujumbe wa aya **mbili** za kwanza kwa **maneno 70**. (alama 6, 1 ya mtiririko)
- b) Kwa kurejelea aya **tano** za mwisho, eleza umuhimu wa taka kwa **maneno 100**. (alama 9, 1 ya mtiririko)
- 3. MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)**
- a) Tofautisha sauti zifuatazo: (alama 2)
- i) / e /
/ i /
- ii) / p /
/ b /
- b) i) Shadda ni nini? (alama 1)
- ii) Andika maana ya maneno yafuatayo. (alama 2)
- 'mbuni
m'buni

- c) Kiambishi na mofimu hutofautianaje? (alama 2)
- d) Tunga sentensi yenye kiulizi *-ngapi* katika ngeli ya mahali (ndani). (alama 2)
- e) Kanusha katika hali ya udogo.
Ng'ombe na mbuzi wote walionunuliwa wamepelekwa kichinjioni. (alama 2)
- f) Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia kisawe cha neno lililopigiwa mstari.
Siha ya mtoto yule imeimarika. (alama 1)
- g) Ainisha vielezi katika sentensi ifuatayo : (alama 2)
Mwalimu alitoka shuleni na akatembea haraka haraka.
- h) Tumia neno **mzazi** kutungia sentensi kama: (alam 4)
i) nomino
ii) kivumishi
- i) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale. (alama 4)
Alimwona mamba majini alipopiga mbizi jana.
- j) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari katika kinyume. (alama 2)
Baba **alimbariki** mwanawe **mtiifu**.
- k) Tunga sentensi mbili kubaini matumizi mawili tofauti ya mshazari. (alama 2)
- l) Andika katika kauli yakinishi. (alama 2)
Hatakuja tusipomwarifu mapema.
- m) Geuza katika usemi halisi. (alama 3)
Mwanafunzi alishangaa na kusema kuwa hakuamini alipata alama nyingi vile katika insha.
- n) Ainisha shamirisho. (alama 3)
Mtoto alipikiwa chai na mamake kwa sufuria chafu.
- o) Tunga sentensi ukitumia kitenzi 'ota' katika kauli ya kutendea. (alama 2)
- p) Bainisha kirai kivumishi na kielezi. (alama 3)
Raa wenye bidii husifiwa kote ulimwenguni.
- q) Tunga sentensi ili kutofautisha maana ya : (alama 2)
i) fuja
ii) vuja

4. ISIMUJAMII (alama 10)

Una fursa ya kuwazungumzia wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa sarakasi. Eleza sifa **tano** za lugha utakayotumia.

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA WESTLANDS

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

FASIHI YA KISWAHILI

KARATASI YA TATU

Julai / Agosti 2016

Muda: Saa 2½

1. (LAZIMA)**SEHEMU A: HADITHI FUPI****Damu Nyeusi na Hadithi nyingine : K. Walibora na S.A. Mohamed**"Jitihada haiondoi kudura." Huku ukirejelea hadithi zozote **tano** katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*, eleza ukweli wa methali hii. (alama 20)**SEHEMU B : RIWAYA:****Kidagaa Kimemwozea ; K. Walibora****Jibu swali la 2 au la 3**

2. –Unautukanisha ukoo wetu mtukufu. Siku hizi hata naona aibu kukuita ndugu yangu”.

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Wahusika hawa ni riale kwa ya pili? Fafanua. (alama 16)

AU

3. Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* imeangazia kwa kina ujenzi wa jamii mpya. Thibitisha kwa kurejelea mifano **kumi**.

(alama 20)

SEHEMU C : TAMTHILIA**Mstahiki Meya : Timothy M. Arege****Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Nina hakika umeona mji ulivyo mehafu. Harufu kila mahali . . ."

a) Eleza muktadha wa usemi huu. (alama 4)

b) Fafanua sifa **nne** za msemewa. (alama 4)

c) Kwa kutoa mfano taja mbinu moja ya sanaa inayojitokeza katika dondoo. (alama 2)

d) Mbali na harufu inayorejelewa katika dondoo hili, jadili 'harufu' nyingine inayojitokeza katika baraza la mji wa Cheneo. (alama 10)

AU

5. a) Kwa kurejelea Tamthilia ya *Mstahiki Meya* eleza matumizi ya :

(alama 10)

i) majazi

ii) uzungumzi nafsia

iii) nyimbo / ushairi

iv) tashbihi

v) kuchanganya ndimi

b) –Siuoni mpango wa kuwanufaisha watu wetu.”

i) Msemaji analalamikia manufaa gani katika muktadha huu? (alama 4)

ii) Eleza umuhimu wa msemaji. (alama 6)

SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

6. a) i) Kwa kutoa mfano mmoja eleza dhana ya maigizo. (alama 2)

ii) Fafanua dhima ya maigizo. (alama 8)

b) Nafasi ya miviga katika jamii ni muhimu. Jadili aina **tano** zozote za miviga. (alama 10)**SEHEMU E: USHAIRI**7. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Sebuleni niliketi

Mapema moja jioni

Nikaanza kumbo kuupiga

Mlima wa ugali

Mboga na nyama nikautowelea

Kabla ya maziwa mafunda kupiga

Na maji kuteremsha, koo kusafisha

Pembeni niliketi

Nikipumua kwa shida

Na kushindwa kujinyanyua

Taratibu askari wakaninyemelea

Na bakunja kunipiga

Nilipozinduka nilikuta changu kisanduku

Macho kikiwa, habari kinamwaya

Ndipo nikaona wenzangu wananchi

Mizizi wakila na matunda mwitu
Vyote wakivisaka kwa taabu

Katika mazingira hayo ya sarabi
Miili yao ilikuwa taabu kuibeba
Kwa unyonge wa njaa.

Nikashangaa tulivyoishi
Chini ya bendera moja
Lakini tukiwa mbalimbali
Katika limwengu tofauti
Kama ardhi na mbingu

- | | |
|---|-----------|
| a) Eleza aina ya shairi hili? | (alama 2) |
| b) Tambua nafsineni katika shairi? | (alama 2) |
| c) Fafanua sifa za utunzi alizotumia mshairi. | (alama 4) |
| d) Eleza toni ya mshairi inayojitokeza katika ubeti wa kwanza na wa pili. | (alama 2) |
| e) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. | (alama 5) |
| f) Kwa kurejelea shairi dondoa mifano miwili ya mbinu za lugha. | (alama 2) |
| g) Fafanua maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika shairi. | (alama 3) |
| i) kumbo | |
| ii) bakunja | |
| iii) sarabi. | |

TATHMINI YA GATUZI DOGO LA KISII YA KATI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI

Karatasi ya Kwanza

(INSHA)

Julai / Agosti 2016

Muda: Saa 1¼

1. Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la visa vya wizi wa mitihani ya kitaifa humu nchini. Mwandikie barua rafiki yako aliye ughaibuni upendekeze jinsi ya kukabiliana na tatizo hili sugu.
2. Usalama wa nchi yetu unazidi kuzorota kila kukicha. Jadili.
3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali:
Zinduko la mwoga ni kemi.
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya:
. . . tulijifunga vibwebwe kuwavua wahasiriwa waliokuwa wamefunikwa na vifusi lakini jitihada zetu ziliambulia patupu.

TATHMINI YA GATUZI DOGO LA KISII YA KATI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI

Karatasi ya Pili

(Ufahamu, ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimujamii)

Julai / Agosti 2016

Muda: Saa 2½

1. UFAHAMU (alama 15)Soma taarifa inayofuata kisha uyajibu maswali

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti kabisa na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyaake na mamaake kuu.

Yeye hatarajii kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana kumzalia mumewe watoto, na daima dawamu kuwa 'mwendani wa vijungu jikoni' akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume Akanyagapo mume, naye papo huutia wayo wake.

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika msomo ya lugha, historia, jiografia, hesabu, sayansi na mengineyo sawa sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega akazifanya. Akataka kuwa mwalimu akawa. Akataka kuwa daktari akafanikiwa. Almuradi siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili, mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi. Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa hateswi akafyata ulimi. Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali 'mahali pake' katika jamii alipotengewa na wanaume wenye mawazo ya kihafidhina yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake, iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha ukatani

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo lolote bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine mwanaume wa kisasa ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama mshirika sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende shingo upande analazimika kumkubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho bali ni ya aushi

Maswali

- a) Fafanua msembo: 'Mwendani wa vijungu jiko' unavyodokeza hali ya mwanamke katika jamii. (alama 2)
- b) Ni vipi jamii imemfanya mwanamke hayawani wa mizigo. (alama 2)
- c) Mwanamume wa kisasa anamwonaje mwanamke wa kisasa? (alam 2)
- d) Taja mifano sita ya 'mawazo ya kihafidhina' (alama 6)
- e) Eleza maana ya (alama 3)
 - i) akafyata ulimi .
 - ii) ukatani.
 - iii) Taasubi za kiume .

2. MUHTASARI (alama 15)Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Siku hiyo nilipitia mahali hapo kama yalivyokuwa mazoea yangu. Nilimuona yule mtu amelala pale pale, hatingishiki, kama nilivyokuwa nikimuona siku hizi zote, mwaka nenda mwaka rudi. Nilisimama huku nikishangaa kwa mara nyingine tena.

Nilikuwa najitayarisha kujiendea na hamsini zangu mtu huyo alipojipinda kwa mbali sana, kwa hakika nilidhani macho yangu yananihadaa. Nikayakodoa zaidi ili nione vizuri zaidi ibura yote iliyomoe mwilini mwangu ili niyatoe matongo ambayo

nilituhumu kwamba yaliitia zingezinge nadhari yangu kiasi cha kunifanya kutoona barabara. Nilipohakikisha ya kwamba ni akili yangu tu iliyokuwa imenihadaa, nikaamua kuendelea na safari yangu kwenda kujitafutia riziki.

Hatua ya kwanza na ya pili, moyo haukunipa sauti katika kilindi cha moyo wangu ikanisihi na kunitafadhalisha nitazame nyuma. Kutupa jicho nyuma, nikamnasa mtu huyo akigeuka! Nikashtuka sana! Jambo la kwanza nilidhani macho yangu yameingiwa na kitu kilichoyafanya kuona mambo yasiyokuwepo. Pili, nilidhani iwapo niliyoyaona yana msingi wowote, basi huenda ama nina wazimu, au yule mtu ni mzuka, hasa kwa vile ilionekana ni mimi tu nimuonaye. Nilikuwa niko katika hali ya kufanya uamuzi kuhusu dhana zangu hizi aina aina mtu huyo alipojigeuzageuza, kisha akafunua macho! Moyo ulinienda mbio. Nilitaka kutifua vumbi ili wazimu usinizidie, lakini sikupata nafasi. Mtu yule alijizoaoza, na kuketi kitako. Kisha akatokwa na maneno katika lugha iliyofanana sana na Kiswahili. Niliyaelewa aliyokuwa akisema.

Ajabu ya maajabu, mtu huyo alidai ya kwamba tangu alipolala kivulini hapo tangu jana baada ya chakula cha mchana, hakuota ndoto hata moja bali usingizi wake ulikuwa mithili ya gogo! sasa nilikuwa na hakika kwamba ikiwa mimi sina wazimu, basi kiumbe yule aliyevaa ngozi iliyochakaa sana katika mpito wa miaka hakika ana wazimu. Nilitaka kuhakikisha, hivyo nilimkumbusha kwamba amelala mahali hapo kwa muda wa miaka mingi sana.

Kusikia hayo alianza kunikagua. Akasema nimevaa kizungu. Akanitajia tofauti nyingi baina ya vijana aliowazoea na mimi. Mwisho wa yote akaniuliza kama siku hiyo si tarehe kumi na nane mwezi wa pili mwaka wa 1897. Nikadhani anafanya mzaha kwa hivyo nikacheka. Nilipoona kicheko changu kinamuudhi, nikamwambia siku hiyo ni tarehe kumi na nane mwezi wa pili mwaka wa 1997. Nilipoona amaeshangaa kwa dhati, nikagundua ukweli. Alikuwa amelala kwa karne nzima!

Maswali

- a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno 80 (alama 9, 2 utiririko)
- b) Bila kupoteza maana fupisha aya mbili za mwisho. (Maneno 45) (alama 6, 1 utiririko)
- 3. MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)**
- a) Taja vigezo vitatu vitatu vinavyotumiwa kuainisha sauti za irabu na konsonanti (alama 3)
- b) Ainisha viambishi vya neno: 'mmtumaye' ukizingatia majukumu (alama 2)
- c) Tambua chagizo katika sentensi hii.
Mandela alisafiri kwa mangera. (alama 2)
- d) Tunasema : Yeye ndiye aliyenituma. Sasa kamilisha. (alama 2)
- i) Mimi .
- ii) Sisi .
- e) Weka nomino hizi katika ngeli zao (alama 2)
- i) Mjusi.
- ii) Uasi .
- f) Changanua kwa kielelezo cha mistari. (alama 4)
- Aliyenituma ni mtoto mchanga sana.
- g) Andika kwa kinyume (alama 1)
- Mtoto mweusi ametababsamu sana.
- h) Andika kwa umoja. (alama 2)
- Mishale yao ilifungwa kwa manyoya mengi meusi
- i) Tunga sentensi moja kutofautisha kati ya fua na vua. (alama 2)
- j) Nyambua vitenzi hivi kwa kauli ya kutendeshea. (alama 2)
- i) Lia .
- ii) Nya .
- k) Neno KINA hutumiwa kuelezea watu wenye jinsia, ukoo, ujamaa, tabia au hali fulani. Kwa mfano, kina mama. (alama 2)
- Toa matumizi mengine mawili.
- l) Andika neno moja lenye visehemu vifuatavyo vya kisarufi. (alama 2)
- nafsi ya pili umoja, hali isiyowezekana, yambwa tendwa, mzizi, kauli tendea.
- m) Onyesha kiima katika hii sentensi na ueleze muundo wake. (alama 2)
- Mimi na juma tutaenda kwao leo.
- n) Ainisha virai vilivyopigiwa mistari chini yao. (alama 2)
- Mtoro aliruka juu ya ua na kutorokea mbali kabisa.
- o) Andika kwa udogo wingi: (alama 2)
- Yule nyoka alikatwa mkia.
- p) Andika upya ukitoa visawe vya maneno yaliyopigwa mstari. Ndovu alimfukuza hadi juu ya kiduta na kumwangusha nacho. (alama 2)
- q) Toa maana tatu za hii sentensi: Alinunuliwa kuku na mtoto wake. (alama 3)
- r) Andika sentensi sahili zilizoko katika sentensi hii. (alama 3)
- Kizito ni mgonjwa na amesema ataenda hospitali kesho.
- 4. ISIMUJAMII (alama 10)**
- a) Eleza sifa tatu kuu za lugha ya taifa. (alama 3)
- b) Kwa mifano saba onyesha majukumu ya lugha za taifa. (alama 7)

102/3

TATHMINI YA GATUZI DOGO LA KISII YA KATI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI

FASIHI YA KISWAHILI

Julai / Agosti 2016

Muda: Masaa 2½

1. LAZIMA : SEHEMU YA 'A'**USHAIRI**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Na wahenga wakalunga, daraja tulivuke
Kwa karibu tukisonga, tusije fanya uhuni
Daraja kuhongahonga, tunekane hayawani
Uwazi wako na mimi, maisha bora ya kesho.

Ni daraja lenye miba, kesho kiwa mikononi
Utatamani kuiba, kesho yako kuauni
Madhara yake ni tiba, kesho yako i motoni
Uwazi wako na mimi, maisha bora ya kesho.

Daraja ukishavuka, kozi gani taandama?
Tabibu handisi toka, ni ndoto ilotuama.
Uhuni ulokutoka, kozini ukaungama.
Uwazi wako na mimi, maisha bora ya kesho.

Ya nini kuparamia, daraja kuvuka bila
Kujali ya jalia? Kama si kuacha mila
Ya mkato kutandia, mwisho kupata madhila
Uwazi wako na mimi, maisha bora ya kesho.

Wanafuu takateni, wakufuu takateni
Ya kesho tayatakeni, ulivyoota ndotoni
Ya nini kuharibuni, miaka yote shuleni
Uwazi wako na mimi, maisha bora ya kesho.

Wazazi walimu acha, na wanagenzi acheni!
Wa mtihani wizi acha, maisha yetu tuguni
Maisha bora kukicha, sote hapa twatakeni
Uwazi wako na mimi, maisha bora ya kesho.

Daraja ni mtihani, tulofanya kulangua,
Viongozi takateni, mtihani sisumbua
Achini purukushani, kesho ya wanetu kua
Uwazi wako na mimi, maisha bora ya kesho.

MASWALI

- a) Eleza dhamira ya mshariri katika utunzi huu. (alama 2)
- b) Kwa kuzingatia vina na mishororo, bainisha bahari mbili zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
- c) Taja madhara ya kuibia mtihani kwa mujibu wa shairi. (alama 2)
- d) Kwa mfano mwafaka, onyesha matumizi ya mishata. (alama 2)
- e) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
- f) Tambua na ueleze umuhimu wa idhini ya mshairi kama inayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)
- g) Fafanua muundo wa ubei wa pili. (alama 3)
- h) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)

SEHEMU YA B**TAMTHILIA:****Mstahiki Meya : Timothy M. Arege****Jibu swali la 2 au la 3**

2. 'Wanafaa kusukumwa kabisa mpaka wajue kuwa wao ni wananchi na kuna wenye nchi.'
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Kwa kurejelea dondoo hili, taja na ueleze sifa mbili za msemaji. (alama 4)
- c) Huku ukirejelea tamthilia hii ya mstahiki meya, thibitisha kuwa kuna wananchi na wenye nchi. (alama 12)
3. Tamthilia ya Mstahiki Meya imepewa anwani ya kitashtiti. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia nzima ya *Mstahiki Meya*. (alama 20)

SEHEMU YA C**RIWAYA:****Kidagaa kimemwozea ; Ken Walibora****Jibu swali la 4 au la 5**

4. "We cherish the freedom enjoyed by all citizens of this country. We cherish every opportunity to freely partake of the national cake. We cherish the freedom to eat the fruits of independence without fear or favour . . ."
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
- b) Bainisha tamthalia moja ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
- c) Kwa kurejelea riwaya nzima ya *Kidagaa kimemwozea*, onyesha kinyume cha maneno haya. (alama 14)
5. Kwa kurejelea riwaya *Kidagaa kimemwozea* onyesha haki za watoto zinavyokiukwa. (alama 20)

SEHEMU YA D:**HADITHI FUPI****Damu Nyeusi na Hadithi nyingine : Ken Walibora na Said A. Mohamed****Jibu swali la 6**

6. a) *Mwana wa Darubini* : K.M Mbai (alama 10)
- "Nimebaini nimekosa mwisho wa kukosa. Dhambi zangu ni nyingi na sitaki ziniandame kaburini"
- i) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- ii) Kwa kurejelea hadithi "*Mwana wa Darubini*," fafania matatizo sita yanayomkumba mwanamke. (alama 6)
- b) *Damu Nyeusi* : K. Walibora. (alama 10)
- "Msifikiri kwamba mzungu anatupenda sisi watu weusi."
- Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi "*Damu Nyeusi*". (alama 10)

SEHEMU YA E:**FASIHI SIMULIZI****Jibu swali la 7**

7. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu Maswali yanayofuata:
- Ikiwa kweli wewe ni mwanangu,
Niliyefungua kiburebure kuelimisha.
Mpaka chuo kikuu cha Uingereza,
Inakufanya sasa ujione bora kuniliko,
Upite ukinitemea mate,
Unidharau kiasi cha kunikana,
Miungu na waone chozi langu, wasikie kilio changu,
Radhi zao wasiwahi kukupa,
Laana wakumiminie,
Uje, kulizwa mara mia na wanao
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watakalokupa likuletee simanzi badala ya furaha!
- a) Tambua kipera cha fasihi simulizi kinachohusishwa na kifungu hiki. (alama 2)
- b) Fafania sifa zozote tano za kipera hii. (alama 10)
- c) Misimu hundwa kwa njia mbalimbali. Thibitisha. (alama 8)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WA WILAYA YA GUCHA KUSINI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI

Karatasi ya Kwanza

(INSHA)

Julai /Agosti 2016

Muda: Saa 1¼

1. Andika barua kwa Mkurugenzi wa Elimu nchini ukimwelezea kuhusu mikakati inayostahili kuwekwa ili kupambana na tatizo la udanganyifu katika mitihani ya kitaifa.
2. Ukosefu wa ajira ni tatizo sugu humu nchini. Pendekeza njia zinazoweza kutumiwa katika kubuni nafasi tosha za kazi humu nchini.
3. Mjinga mpe kilemba utamwona mwendowe.
4. Anza kwa, "Walipofungua mlango huo, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Walilia kwi! kwi! kwi! kwa maafa waliyoshuhudia . . ."

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA KUSINI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI 102/2

Karatasi ya Pili

(Ufahamu, ufupisho, Sarufi na matumizi ya lugha na Isimujamii)

Julai / Agosti 2016

Muda: Saa 2½

1. UFAHAMU (alama 15)Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Utandaridhi (au globalization kwa lugha ya Kiingereza) ni jinsi ya maisha inayoendelea kutawala ulimwengu wote katika karne hii ya 21. Neno utandaridhi ni neno mseto ambalo maana yake ni utamaduni uliotanda au kuenea ardhi nzima. Mtu mtandaridhi hivyo basi ni mtu aliyebobea kikamilifu katika utamaduni huu mpya kwa jinsi moja au nyingine. Mtandaridhi husisha sana katika kutandaridhi aina moja au nyingine ya **amara** muhimu za kitandaridhi. Hizo ni kama vile biashara za kimataifa, lugha za kimataifa, aina za mavazi zilizotokea kupendwa ulimwenguni kote, muziki wa kisiku hizi, hasa vile *pop, reggae, raga, rap*, ambao asili yake ya hivi majuzi ni Marekani. Muziki huo waimbaji wake hutumia, sana sana, lugha ya Kiingereza hususan kile cha Marekani na kadhalika. Watandaridhi wana nyenzo zingine kadha wa kadha za kuendesha maisha yao au kujitambulisha. Wao huwasiliana kutoka pembe moja ya dunia hadi nyingine wakitumia vitumeme, yaani vyombo vitumiavyo umeme kufanya kazi ya hali ya juu, kama vile tarakilishi na simu, hata za mkono. Watu hawa hawakosi runinga sebuleni mwao, usiseme redio. Hawa husikiliza na kutazama habari za kimataifa kupitia mashirika matandaridhi ya habari kama vile BBC la Uingereza na CNN la Marekani. Aidha watu hawa husafiri mara kwa mara kwa ndege na vyombo vingine vya kasi. **Hawa hawana mipaka**. Wale wanaohusudu utandaridhi wanaamini kindakindaki kwamba utamaduni huu wa kilimwengu umeleta **mlahaka** mwema baina ya watu binafsi, makampuni makubwa makubwa ya kimataifa na uwiano bora baina ya mataifa. Watu hawa husikika wakidai ya kuwa aina hii ya utamaduni imeupigisha mbele ustaarabu wa wanadamu ulimwenguni kote. Kwa upande mwingine, **wakereketwa** wa tamaduni za kimsingi za mataifa na makabila mbalimbali ulimwenguni wanadai ya kwamba utandaridhi umeleta maangamizi makubwa ya tamaduni hizo. Vile vile unaelekea kuangamiza lugha nyingi zilizofungamana na tamaduni hizo. Kwa ajili hiyo basi, utandaridhi umesemekena kwamba unasababisha kutovuka kwa utu miongoni mwa wanadamu wote, ambao wamo mbioni kusaka pesa na kuneemesha ubinafsi. Inadaiwa pia kwamba utandaridhi umesababisha kutovuka kwa adabu kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu. Huku kutovuka kwa adabu kwa vijana, hasa wale wa mataifa yanayojaribu kuendelea, kumeleta zahama **chungu mbovu**, ikiwa ni pamoja na kuenea kwa UKIMWI kwa kasi ya kutisha.

Maswali

- a) i) Bainisha kwa kutoa maelezo kamili kwamba utandaridhi ni neno mseto. (alama 1)
- ii) Tohoa maneno mawili kutokana na neno kutandaridhisha kisha ueleze maana za maneno hayo. (alama 1)
- b) i) Nini maana ya "hawa hawana mipaka"? (alama 1)
- ii) Kwa nini watandaridhi wanapenda kusikiliza na kutazama habari kupitia BBC na CNN? (alama2)
- c) i) Eleza kikamilifu maoni ya watandaridhi kuhusu utamaduni wao. (alama 3)
- ii) Je, utandaridhi unalaumiwa kwa nini katika kifungu hiki? (alama 3)
- d) Msemo : "chungu mbovu" ni msemo wa kimtaani tu. Msemo sawa ni upi? (alama 1)
- e) Eleza maana ya maneno yafuatayo: (alama 3)
 - i) amara .
 - ii) mlahaka
 - iii) wakereketwa .

2. UFUPISHO (alama 15)**Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata**

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana. Akiwa na nidhamu hiyo, atakuwa mtu mwadilifu, anayeweza kustahiwa na kusadikikika katika mambo, shughuli na hali tofauti tofauti.

Kwanza, mtoto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani mwao, shuleni na pia katika jamii. Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa vijulanga wote wanamtegemea kama msimamizi wa mambo nyeti ya maisha yao.

Kwa hivyo, ni dhahiri shahiri kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume na mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili, huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, mathalani jukumu ama dhima fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Watu hapana shaka watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambao tayari wamekwisha tiwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadilifu daima atajiepusha na shutuma na majanga yote yanayoweza kuchipuka. Kuna msemu maarufu, kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu, kwamba "aliye kando haangukiwi na mti." Pia waliambiwa kwamba, pilipili usiyoilala yakuwashiani?

Ni bayana kutokana na misemo hiyo mwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuwakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya 'watoro' ambao ni watovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozo na mielekeo ya watu wazima ambao wako mazingirani mwake. Ndipo wa kale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbani hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kufikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu wote katika maisha yake. Ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayana kwamba mabaya yote ayatendayo duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani, watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu. Ni kheri mja kujihidi mwenyewe, kwani uhalifu haulipi chochote.

Maswali

- a) Nini umuhimu wa nidhamu? (Maneno kati ya 50 - 55) (alama 1 ya mtiririko) (alama 6)
- b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (Tumia maneno 55 - 60) (alama 1 mtiririko) (alama 7)
- 3. MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)
- a) Eleza dhana ya shadda. (alama 2)
- b) Ainisha viambishi na silabi kwa kutumia kitenzi: (alama 2)
- Walipigishwa.
- c) Nini wingi wa sentensi hii katika ukubwa? (alama 2)
- Ulimi wa mtundu huwa mrefu.
- d) Eleza matumizi matatu ya kiimbo. (alama 3)
- e) Changanua kwa kutumia mstari / mshale. (alama 4)
- Wazazi wengi sana waliofika shuleni mapema walileta vyakula vingi.
- f) Yakinisha kwa wakati ujao hali timilifu. (alama 2)
- Hakuwa na kalamu nyeupe.
- g) Andika upya sentensi hii ukifuata maagizo. (alama 2)
- Wembe ulipopotea mwanafunzi alikasirika. (Anza: Kupotea . . .)
- h) Toa maana mbili za sentensi hii: (alama 2)
- Nionyeshe vile nitakavyokubeba.
- i) Kwa kutoa mifano katika sentensi, bainisha matumizi ya kibainishi. (alama 2)
- j) Andika katika usemi wa taarifa: (alama 3)
- "Mbona unamfanyia karaha mwenzako? Je, utaenda kumwomba radhi?" Natasha aliuliza.
- k) Nomino za ngeli ya A - WA zina sifa gani kimuundo? (alama 2)
- l) Bainisha vishazi vilivyotumika katika sentensi hii. (alama 2)
- Ingawa alimshtaki hatapata haki.
- m) Eleza kazi ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
- i) Jumapili ijayo nitakuwa sherehe
- ii) Wageni watakuja Jumapili
- n) Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya 'ndi'. (alama 2)
- o) Onyesha shamirisho katika sentensi. (alama 3)
- Kipkemboi alimbebea mwalimu mzungu kwa gari.
- p) Bainisha nomino katika sentensi hii: (alama 3)
- Uhubiri wa Nabii Dkt. David Edwin Owuor una mvuto mkubwa.
- q) Tumia 'o' rejeshi mazoea kuandika upya sentensi hii: (alama 2)
- Mwanafunzi ambaye anasoma kwa bidii ndiye ambaye anafaulu mtihani
- 4. ISIMUJAMII (alama 10)**
- a) Eleza sababu sita zinazosabahisha watu kubadili na kuchanganya msimbo (alama 5)
- b) Toa ithibati kwamba lugha ya Kiswahili ina asili ya kibantu. (alama 4)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA KUSINI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

102/3

KISWAHILI

FASIHI YA KISWAHILI

Julai / Agosti 2016

Muda: Masaa 2½

1. LAZIMA : SEHEMU YA 'A'**HADITHI FUPI****Damu Nyeusi na Hadithi nyingine : Ken Walibora na Said A. Mohamed**

1. Matatizo yanayolikumba bara la Afrika yanaweza kusuluhishwa kwa njia zipi?

Jadili kwa kurejelea Diwani ya *Damu Nyeusi*.**SEHEMU YA B****TAMTHILIA:****Mstahiki Meya : Timothy M. Arege****Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Jina si Kitu. Tumbo ndilo muhimu. Tumbo lako na jamaa yako."

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Fafanua jinsi tumbo limewekwa mbele ya jina katika tamthilia hii. (alama 16)
3. Thibitisha ukweli wa msembo kuwa: Sikio la kufa halisikii dawa kwa mujibu wa Tamthilia ya *Mstahiki Meya*. (alama 20)

SEHEMU YA C**RIWAYA:****Kidagaa kimemwozea ; Ken Walibora****Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Wachache hawa hawaogopi, ashakum si matusi, hata kutema mate au kumwaga mkojo usoni mwa haki, usawa na uhuru ulipiganiwa na kumwagiwa damu . . ."
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Kwa kutoa ithibati onyesha mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
- c) Thibitisha kwa kutoa mifano saba namna haki za kibinadamu zimekiukwa katika riwaya ya *Kidagaa kimemwozea*. (alama 14)
5. Wananchi wa Tomoko wamesalia katika ndoto ya uhuru. Dhihirisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

SEHEMU YA D:**USHAIRI**

6. Tohara kwa mwanamke, ni hatari,
-
- Madhara, kwa wake uke, hushamiri,
-
- Hasara, yake peke yake, hudhihiri,
-
- Zinduka!

Epuka, hao ngariba, wajuaji
Hufika, navyo viroba, wachinjaji
Kumbuka hawana tiba wauaji
Amka!

Kiwembe, kilichochofua, na kibusu,
Viumbe, huathirika, ni kwa kutu,
Siombe, yakakufika, mwana kwetu,
Zinduka!

Maradhi, hujitokeza, ya vidonda,
Yaridhi kujichomoza pepopunda,
Na hedhi, hukuchagiza, ikavunda.
Amka!

Isiwe, wembe mmoja, wengi wari,
Ujuwe, Ukimwi huja, ni hatari,
Na iwe, katu si hoja, kuwa mwari,
Zinduka!

Wacheni, mila dhaifu, zinotesa

Kwepeni, amali chafu, nawasa.
Shikeni, uadilifu, tangu sasa,
Zinduka!

(Kutoka: Diwani ya wasakatonge, Muhammed Seif Khatibu, OUP Dares Salaam) Uk 2.

1. Shairi hili ni la bahari gani? Tetea jibu lako. (alama 4)
2. Mshairi antoa mwito gani katika ubeti wa pili? (alama 4)
3. Fafanua msimamo wa mshairi kuhusu tohara. (alama 4)
4. Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari. (alama 3)
5. Taja na utolee mifano mbinu zozote mbili zilizotumika katika shairi. (alama 4)
6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
 - i)Hushamiri
 - ii)Kibutu
 - iii)Idhilali
 - iv)amali.

SEHEMU YA E:

FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 7 au la 8

7.
 - a) Eleza mafunzo matano yanayotolewa na methali za Kiswahili. Kwa kila funzo andika methali moja. (alama 10)
 - b) Fafanua dhima ya utanzu wa nyimbo katika jamii. (alama 10)
8.
 - a) Maigizo ni nini? (alama 2)
 - b) Fafanua sifa zozote tatu za maigizo. (alama 6)
 - c) Eleza tofauti kati ya ngoma na ngomezi. (alama 4)
 - d) Fafanua hasara tatu za miviga na namna ya kusuluhisha hasara hizo. (alama 6)
 - e) Tofautisha kati ya mighani na maghani. (alama 2)

THARAKA KASKAZINI/KUSINI
KISWAHILI
INSHA
102/1
KARATASI LA KWANZA

1. Umekutana na rafiki yako miaka miwili baada ya kumaliza kidato cha nne. Mna mengi ya kuzungumza kuhusu vile mnavyoendelea maishani. Andika mazungumzo yenu.
2. Akina mama hawafai kufanya kazi mbali na wao. Jadili.
3. Samaki huanza kuoza kichwani.
4. Andika insha itakayomalizika kwa:
 Nilishusha pumzi, nikashukuru. Kwa kweli hiyo safari haikuwa rahisi kwangu.

THARAKA KASKAZINI/KUSINI
KISWAHILI
102/2
LUGHA
KARATASI LA PILI

1. UFAHAMU (alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ulimwengu unapaswa kuzuka na Mbinu za kulitadarukia tatizo ambalo linakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini uno yakabili mataifa yanayoendelea, unayatosha kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea kama vile Marekani nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umaskini huu ni anuwai mathalan, ufisadi, uongozi mbaya, turathi za kikoloni, Uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa Uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini, unaothiri nchi Fulani una athari pana sana. Uvunjivu unaotokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambapo matendo mabaya huchipuka. Raia maskini Huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburia madeni ya mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa la pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umaskini. Njia nyingine ni kustashafu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeokuula mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa haushi kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sela za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

Maswali

- a) Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea? (alama 4)
- b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)
- c) Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la umaskini? (alama 4)
- d) Mfumo wa soko huru una madhara gani kwa mataifa machanga? (alama 2)
- e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: (alama 3)
 - i) kulitandarukia
 - ii) kuatika
 - iii) kuyaburia madeni

2. UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata.

Watoto wa mitaani niwatoto wanaorandaranda kwenye barabara za mji au mitaa wakitaifuta vyakula au usaidizi wa aina yoyote kutoka kwa wakazi wa maeneo hayo. Watoto hawa wamepachikwa lakabu maarufu 'chokora'. Watoto hawa hutoka wapi? Je, wanazaliwa mitaani?

Kuna vyanzo mbalimbali vya watoto hawa: mosi ilikuwa ni ukahaba, baadhi ya wazazi wa watoto hawa ni makahaba ambao kwa bahati mbaya wanapotungwa mimba na wakashindwa kuavya huishi kuzaa wanaharamu ambao huwalea kwa muda wa miaka mitatu na kisha kuwarusha mitaani.

Asili nyingine ya watoto wa mitaani ni kuvunjika kwa ndoa: wazazi wanapotengana watoto hukosa mihimili na hivyo kushuka hamsini zao hadi mtaani kutafuta usaidizi. Sababu nyingine ni watoto wanaoachwa na wazazi wao (mayatima) baada ya wazazi hawa kuaga dunia. Hawa hukosa mtu wa kuwashughulikia na hatimaye hujipata mitaani.

Asili nyingine ni familia maskini ambazo hushindwa kutimiza mahitaji ya kimsingi ya watoto na hatimaye watoto hawa wakaishia mitaani. Vilevile kuna watoto wanaozaliwa mitaani kutokana na wanaume na wanawake ambao wameishi mitaani hadi wakawa wazazi.

Watoto wa mitaani hukumbwa na matatizo chungu nzima. Wao hukosa chakula, mavazi na malazi. Hawana mahali pa kulala hivyo basi wanajinyata kwenye mitaro ya maji taka na kwenye mijengo ambayo haijakamilika kujengwa au magofu ya nyumba huku wakibugunywa na baridi na hatimaye hupata maradhi ya kila aina. Usalama kwao ni msamiati usioweza kugongwa vichwa vyao.

Suala la watoto wa mitaani ni kero kwa kila anayetumia huduma za mjini. Watoto hawa hupamba miji kwa sura mbaya ambayo huchora taswira ya jamii katili isiyothamini ubinadamu. Baadhi ya 'chokora' hutumia lugha chafu na vitisho katika kuomba usaidizi kutoka kwa adinasi wapitanja. Swali linalopita kwenye akili ya watu wengi ni je, hali hii itakomeshwa vipi? Uwepo wa watoto mitaani ni tatizo la kijamii hivyo basi linahitaji kila mwanajamii kuhakikisha ametoa mchango madhubuti kukomesha tatizo hili. Wanajamii wanafaa kuwa waadilifu, wajepushe na ukahaba na ngono za kiholela. Aidha, kila mtu anafaa kutia bidii kutafuta riziki na pia kupata idadi ya watoto anaoweza kuwalea bila usumbufu. Watoto mayatima nao walelewe na jamaa wa wazazi wao. Wasio na jamaa wapelekwe kwenye mashirika ya kutunza watoto. Watoto ambao tayari wako mitaani wasaidiwe na serikali kupata makao na ajira. Tukifanya hivyo mitaa yetu itakuwa nadhifu, salama na mahali pazuri pa kuishi.

a) Ukiangazia mambo muhimu pekee, fupisha aya tatu za kwanza. Tumia maneno 70. (alama 7)

b) Eleza matatizo ya watoto mitaani na uonyeshe jinsi ya klukabiliana na kero hili. Tumia maneno 70-80. (alama 8)

3. MATUMIZI YA LUGHA

- a) Tofautisha sauti zifuatazo
- i) /t/ (alama 1)
- ii) /d/ (alama 1)
- b) Ainisha sentensi ifuatayo katika viungo vya kisarufi; Alijipelekea (alama 3)
- c) Onyesha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo; Seremala alimtengenezea baba kiti kizuri kwa mbao. (alama 3)
- d) Tumia neno kimya katika sentensi kama;
- i) kielezi (alama 1)
- ii) kihisishi (alama 1)
- e) Eleza matumizi ya na katika sentensi ifuatayo; Kwa nini wewe na Johana mnadanganyana eti mu wapenzi? (alama 3)
- f) Tunga sentesi yenye muundo ufuatao. (alama 3)
- S- N+T+N+U+W+T
- g) Bainisha kirai na utaje ni cha aina gani katika sentensi; Walimtunza kwa uhodari (alama 2)
- h) Andika sentensi upya ukitumia urejeshi ufao. (alama 1)
- Daktari alifika na akaondoka.
- i) Changanua sentensi uliyopewa kwa mtindo wa jedwali. (alama 4)
- Madhara ya ukimwi yamekwisha kupunguzwa sana.
- j) Eleza maana mbili za kitawe kifuatacho; (alama 2)
- Kucha
- k) Kanusha sentensi hii; (alama 1)
- Tumechukua sandarusi chache kuchoma. (alama 1)
- l) Tofautisha vitate hivi; (alama 1)
- i) saili
- ii) sahili
- m) Andika kwa msembo wa taarifa. (alama 2)
- Mimi nitawakaribisha wageni leo jioni kisha nitaondoka kwenda kwangu kesho.” Maria alimwambia Njeru.
- n) Tambulisha nyakati au hali za sentensi; (alama 2)
- i) Naja
- ii) Nilikuwa nimeketi aliponitembelea
- o) Andika ukubwa wa sentensi hii; (alama 2)
- Mwizi aliiba mbuzi na ng’ombe.
- p) Tumia vitenzi vifuatavyo vya silabi moja kutungwa sentensi katika kauli ya kutendewa. (alama 2)
- Ja- (alama 2)
- La- (alama 2)
- q) Unda nomino moja kutokana na kitenzi tafakari. (alama 1)

4. ISIMU JAMII

Huku ukitoa mifano, fafanua sifa tano za sajili ya hospitalini. (alama 10)

THARAKA KASKAZINI/KUSINI
KISWAHILI
102/3
KARATASI YA TATU
FASIH

SEHEMU A: TAMTHILIA.

T. Arege: Mstahiki Meya

1. Swali la lazima

Anwani 'Mstahiki Meya' ni pande mbili za sarafu moja. Thibitisha. (alama 20)

SEHEMU B: RIWAYA

Ken Walibora; Kidagaa Kimemwozea

2. –Sakafu ilipaswa kupakwa rangi ya kijani kiwiti badala ya nyekundu. Wekundu ni rangi ya damu na.....”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 b) Wekundu ulitumika kuwakilisha damu. Tambua Mbinu ya kifasihi iliyotumika hap ana ufafanue. (alama 2)
 c) Kwa kurejelea riwaya, fafania matumizi mengine saba ya Mbinu uliyoitambua katika (b). (alama 14)

AU

3. Fafania masuala ibuka kumi katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

SEHEMU C; HADITHI FUPI

K. Walibora na S.A Mohammed; Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine

4. 'Damu Nyeusi' Ken Walibora

–... Amejifunza kuwa hakuna mahali kama nyumbani.”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 b) Eleza sababu nane zinazomfanya anayerejelewa atamani na kuthani kwao Afrika. (alama 16)

AU

5. Jadili swala la ukiukaji wa haki za kibinadamu kwa kurejelea hadithi zifuatazo;

- i) Maeko
 ii) Maskini Babu yangu
 iii) Mwana wa Darubini
 iv) Mizizi na Matawi

SEHEMU D: USHAIRI

6. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata

PANDA

Panda, panda la mnazi, l'anzalo kupatuwa,
 Panda juu ya mnazi, moyo wako wishe ngowa,
 Panda mti wa mapenzi, uwepushe na juwa,
 Panda ni wako uluwa, panda darajani panda!

Panda juu ya farasi, kwa haiba na sitawa,
 Panda kiwango mkwasi, uukimbie ukiwa,
 Panda, situpe viasi, wendako ukikujuwa,
 Panda ni kwako uluwa, panda darajani panda!

Panda ngano na mpunga, afudhuli ya viliwa,
 Panda Wimbi na kimanga, vipawa vya wakupewa,
 Panda, usitunde ch'anga, tauwa mbivu tauwa,
 Panda ni wako uluwa, panda darajani panda!

Panda mwema mshajari, wite t'anzu wa mauwa,
 Panda utunde johari, mwivi asjezanguwa,
 Panda juu ya mimbari ulingane sawasawa,
 Panda ni wako uluwa, panda darajani panda!

Abdulaziz H.M

MASWALI

- a) Shairi hili ni la aina gani? (alama 2)
 b) Eleza lengo (dhamira) la mshairi. (alama 2)
 c) Thibitisha ufaafu wa mada ya shairi hili. (alama 4)

- d) Ni Mbinu gani za lugha zilizotumiwa katika ubeti wan ne? (alama 4)
 e) Eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumika katika shairi. (alama 4)
 f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 4)
 i) mimbari
 ii) uluwa
 iii) wendako
 iv) haiba

7. **Soma shairi ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Maovu yamezidi mithili ya uvundo jalalani
 Watu watenda feeli bila kuajabia
 Ulimwengu umengeuka kitwa ntwariki
 Binadamu kuharibika mia fil mia

Kanisani na sinagogi uzinifu umetanda
 Si mteka maji, si waumini hata wahubiri
 Mapasta hawabagui mapadri hawachuji
 Wadonoa kuku sawia na vifaranga

Shuleni si salama, shuileni kwawaka moto
 Mihadarati imekithiri, kwao ndio uraibu
 Teknolojia yawazuzua, picha chafu zinafurahiwa
 Awali ni mengine, masomo ni halafu

Vijijini hakukaliki, ulevi umezagaa
 Asubuhi watoa loki, mchana wajichangamsha
 Jiono mwavuta jasho hadi Usiku manane
 Jamii yaelekea wapi?

Afisini kwanuka sombo, uozo wa ufisadi
 Ukipata pata huduma, chauchau ni sharti
 Maafisa watononoka, kwa kazi wa kalamu
 Wananchi tuende wapi?

Manzilini balaa, watoto wakosa amani
 Purukushani moto mmoja, mke na mume vituko
 Wayumbayumba, afadhali makuti
 Taifa laelekea wapi?

Maswali

- a) Shairi hili ni la aina gani? Thibitisha. (alama 2)
 b) Mtunzi analalamika mambo gani? Taja manne. (alama 4)
 c) Eleza maana ya mshororo ufuatao:
 Wadonoa kuku sawia na vifaranga. (alama 2)
 d) Eleza nafsiheni (msemaji) katika shairi hili. (alama 2)
 e) Eleza umbo la ubeti wa nne. (alama 4)
 f) Taja na ufafanue Mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika shairi. (alama 4)
 g) Eleza maneno yafuatayo kwa mujibu wa matumizi yake katika shairi. (alama 2)
 i) Sombo
 ii) Watononoka

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. a) Fafanua maana ya ushairi simulizi. (alama 2)
 b) Taja njia tatu za utendaji waushairi simulizi. (alama 3)
 c) Taja tamathali za semi zitumiwazo katika ushairi simulizi. (alama 5)
 d) Eleza umuhimu wa ushairi simulizi katika jamii. (alama 5)
 e) Taja sifa za ushairi simulizi.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA NYERI*Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya*

102/1

KISWAHILI**Karatasi 1**Saa 1 $\frac{3}{4}$ 1. **Swali la lazima**

Umekerwa na wizi wa mitihani ya kitaifa uliofanyika nchini mwako hivi karibuni. Mwandikie waziri wa elimu nchini ukimwelezea sababu ya wizi huo na jinsi ya kukabiliana na changamoto hiyo.

2. Mafuta yaliyovumbuliwa kaskazini mwa Kenya yataleta faida nyingi kuliko hasara. Jadili.

3. Pang'okapo jino pana pengo.

4. Kelele zilitanda Usiku katika kijiji kizima. Ghafla zikafifia. Nilihihi mpigo wa moyo ukinienda mbio, punzi tele kifuani na harara ikinitiririka Endeleza

JARIBIO LA TAMTHILIA YA PAMOJA YA KAUNTI YA NYERI**KISWAHILI***Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya.*

102/2

KISWAHILI**Karatasi 2**Saa 2 $\frac{1}{2}$ **UFAHAMU (ALAMA 15)****Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali.**

Mchezo wa kandanda umenifunza jambo moja, mashabiki ndio wachezaji bora sana. Wao hawakosei kufunga bao wala kuhata peneti wanavyosema magwiji wa mchezo huu wenyewe. Mchezaji akiukosea mpira, mashabiki hunung'unikia kupiga yowe. Katika hilo yowe, huwa kumebewa makombora mengi. Yapo ya mwondo nje ya uwanja, yapom ya kocha lazima aende' na yapo ya asipwe nambari tena. ' wajua tena kandanda.!

Tunaweza kutumika kandanda tukajifunza na mengine maishani. Kwa mfano, juu ya sheria na haki za watu. hebu fikiria, mashabiki kufanya yowe hata timu ikashinda kombe! Au hata kufanya yowe hadi mchezaji akabadilishwa na wengine bora kuletwa uwanjani. Isitoshe, shabiki ambaye ni mfalme wa uwanja, yowe lake linaweza kumfanya hata kocha wa kilabu maarufu duniani kama Manchester United au Arsenal au Real Madrid kuondoka! Mbona hatufanyi hivyo dhidi ya sheria zinazovuruga maisha ya ndugu zetu?

Mbona hatupigi yowe dhidi ya ubakaji? Wapi yowe mwanamke anapopigwa na mumewe hadi kufa? Wapi yowe mtoto wa kike anaponyimwa urithi kwa sababu ya sheria potofu za kitamaduni? Wapi yowe dhidi ya wizi wa kimabavu?

Watoto wetu leo hawawezi kutembea peke yao, haswa magharibi yanapoingia. Je, hatuwajui watu wanao wahatarisha wana wetu? Tunafanya kitu gani? mbona hatupigi kelele polisi au utawala ukasikia hatua ichukuliwe?

Si kitambo tuliposikia kuhusu biashara ya ngozi za binadamu huuzwa ghali sana, hasa katika nchi za ujirani ili waganga watengenezee dawa za kuwapumbazia waja. Huu ni uchawi wa kilele cha ushetani. Katika nchi jirani juzi juzi, walishikwa watu wawili ambao walikuwa wamechinja mtoto wa kiume na kumchuna ngozi. Walijulikana baada ya kuzuka ugomvi baina yao, pale mmoja alipomhutumumu mwenzake kufanya njama ya kukata kumchinja amchune ngozi kwa ushirikiano wa waganga waua watu. Kioja hiki kiliwaacha wengi na mshangao mkubwa. Yaani tumeuza za wanyama zikatushinda sasa tunauza za watu?

Tatizo kubwa ni kwamba watu wanaofanya biashara haramu, tunawajua. Je, tunachukua hatua gani? haijali wanavaa nguo gani? za fisi au za mwana kondoo! Tunahitaji kuwaweka wazi ili biashara zao zijulikane. Wawe weusi au manjano, weupe ama kijani, sharti weupe uwepo ili kuondoka hofu na taharuki kwa ajili ya kila mwanajamii.

Hatua ya kwanza itakuwa ya kugeuza sera na mtazamo wa vikosi vyetu vya usalama kuhusu upokeaji wa rushwa kutoka kwa umma. Endapo hawatasita kufichua wanaowapa habari watajikuta katika hatari ya kuonwa na raia kama wapinga amani na lazima wachukue lawama kwa uongezekaji wa uhalifu nchini. Kwa wazalendo hata hivyo, yowe ni silaha yetu.

Maswali

- | | |
|--|-----------|
| a. Yape makala haya anwani mwafaka. | (alama 2) |
| b. Mchezo wa kandanda una mchano gani katika taarifa hii? | (alama 1) |
| c. Ni sehemu gani zingine ambazo zinaweza kunufaika na mchezo huu? | (alama 3) |
| d. Ni matatizo gani ambayo mwandishi anailaumu jamii kwayo? | (alama 3) |
| e. Ni nini maana ya mistari ifuatayo: | |
| i) Haijalishi wanavaa nguo gani, za fisi au kondoo. | (alama 2) |
| ii) Sharti weupe uwepo ili kuondoa hofu na taharuki | (alama 2) |
| f. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa | (alama 2) |
| i) Kuwapumbazia | |
| ii) Alipomhutumumu | |

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Maendeleo ya taifa hutegemea jinsi wananchi wanavyojitolea katika kulibingirisha gurudumu la uchumi wao. Kila mwanajamii anahitajika kujibidiisha katika kazi au taaluma yake. Mzalendo yeyote Yule hupata motisha ya kufanya kazi iwapo anaweza kupata ile kazi aliyokuwa akiitamani.

Kumakinika katika taaluma Fulani si jambo jepesi na huchukua muda kutengeneza. Kwa mfano, ili mhazili apate staha ya uhazili sharti apatie ngazi mbali mbali. Mwanzo kabisa lazima ahitimu vyema katika masomo rasmi darasani. Masomo hayo pamoja na cheti huweza kumpa fursa ya kujiunga na vyuo mbali mbali vya uhazili. Anapojiunga na vyuo hivyo mdipo safari inapoandaliwa. Kukamilisha safari hii kunahitaji muda wa miaka mine. Anapohitimu huwa tayari ameimudu shughuli hiyo. Hata hivyo, anatakiwa afanye mazoezi kila mara ili asisahau yanayohitajika katika taaluma hiyo.

Wengi waliokwisha pata ujuzi huo wa uhazili huona kuwa hawatapata kazi nzuri yenye mshahara mkubwa. Baadhi yao hujilinganisha na wale wenzao ambao katika masomo ewana utaaluma kama wao. Ijapokuwa wote ni wahazili, viwango vyao ni tofauti na mishahara pia hutofautiana. Tofauti hapa ni daraja zao za vyeo. Baada ya kuhitimu na kupata vyeti vya uhazili ni rahisi kupata au kutopata kazi zenye ujira wa kuvutia. Anayefanikiwa an safari ya kujikakamua hasa kwa upande wa uzingativu wa kazi kikamilifu na kutunza hadhi ya ofisi yake.

Kuna mashirika makubwa yanayojiweza kiuchumi, ambayo raslimali yake ni imara. Mashirika madogo huwa yana raslimali yanayoyumbayumba. Mashirika haya yana wahazili na wafanyikazi ambao hupata mishahara duni. Waanyakazi hawa hufanya kazi kwa kutokuwa na uhakika wa kulipwa mshahara mwisho wa mwezi. Watu kama hao hawawezi kutilia maanani kazi zao. Mashirika mengimne hayana utaratibu maalum wa kulipa mishahara kwa vile utengemea utu wa mkurugenzi. Baadhi ya wakuu hawa huwa na wabanizi na huwapuja wafanyikazi wao. Hili ni swala nyeti ambalo linahitaji litatuliwe kwa kuwa na chama cha kupigania haki za wafanyikazi. Wakati wanapotafuta kazi, wahazili wengi huwa ni wahitaji na hukubali chochote wanachopewa.

Wale waliobahatika kupata nafasi ya kujira katika kampuni kubwa za kimataifa, mishahara huwa ni ya kutia moyo. Katika dunia hii wahazili wana vibarua vigumu kwa sababu lazima wapate tajriba na uzoefu wa taaluma inayoendelea na shirika Fulani. Wakurugenzi mara nyingi huwa hawana subira. Mhazili anapotumia msamiati usioenda sambamba na shughuli za kiofisi hawasiti kufoka. Wavumilivu miongoni mwao hula mbivu. Hawa hawafi moyo bali hujitahidi zaidi ili wasikumbwe na kimbunga cha kufokewa. Kuna wengine ambao humwaga unga.

- a) Fupisha aya ya tatu za kwanza. (maneno 60-70) (alama 6)
 b) Huku ukizingatia aya mbili za mwisho, eleza masuala muhimu ambayo mwandishi anaibu. (maneno 65-70) (alama 7)

3. MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)

- a. Eleza tofauti kuu iliyopo kati ya Konsonanti na Irabu. (alama 3)
 b. Tambulisha kielezi, kivumishi na kitenzi katika sentensi ifuatayo: (alama 3)
 Msichana mrembo alikuja upesi akimkimbilia dadake.
 c. Bainisha mofimu zinazounda neon: (alama 3)
 Halijafunguka
 d. Yaweke maneno yafuatayo katika ngeli. (alama 2)
 i) Ukope
 ii) Lumbwi
 e. Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli uliyopewa. (alama 2)
 Chwa (Tendewa)
 Funga (Tendama)
 f. Tumia **ki** ya masharti kuandika upya sentensi hii: (alama 1)
 Atakuja kasha twende kwao.
 g. Akifisha sentensi hii ili kuleta maana mbili tofauti. (alama 2)
 Baba alimpiga motto akalia.
 h. Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo: (alama 2)
 Mama alimpiga motto akalia.
 i. Changanua sentensi ifuatayo kwa mchoro wa mishale. (alama 3)
 Mwembe uliokatwa jana utakauka.
 j. Andika katika hali ya udogo wingi. (alama 2)
 Mvulana Yule alipewa kipande cha mkate na msichana mrembo.
 k. Andika katika usemi taarifa. (alama 2)
 — Wewe ni nani na unataka nini?
 l. Yakinisha sentensi ifuatayo: (alama 2)
 Nguo za motto Yule hazijajaa uchafu.
 m. Andika majina yanayotokana na vitenzi vifuatavyo: (alama 2)
 Jaribu

Tokea

- n. Tunga sentensi yenye mpangilio huu.
Kitenzi + kitenzi + kitenzi + kielezi (alama 2)
- o. Viambishi na maneno yaliyopigiwa msitari katika sentensi hii yanaleta dhana gani?
Mjakazi alijikata kwa shoka kali na akapelekwa hospitalini. (alama 2)
- p. Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia ~~amba~~”
Kuchelewa kwa wahubiri hawa kufanyikako kila ijumaa kunarudisha injili nyuma. (alama 1)
- q. Andika kinyume cha sentensi hii: (alama 2)
Mtii sheria ni anayeishi ndani ya taifa husika.
- r. Andika sentensi ifuatayo upya ukianza kwa yambwa tendewa. (alama 2)
Mzalendo amemwandikia mhariri barua.
- s. Tunga sentensi moja kuu ukionyesha maana mbili za neno panda’ (alama 1)
- t. Tunga sentensi moja moja ukitumia neno ila’ kama: (alama 2)
Nomina
Kiunganishi

4. ISIMU JAMII: (ALAMA 10)

Konda: Ingia bebi, ingia hii mat ukitaka ukae poa na ufike salama.

Bebi : Ni high time m’warespect wateja wenu. Mara kugeuza fare, kubaki na change au kubonga vibaya after kuulizwa maswali.

- a. Ni kina nani wanaozungumza? Thibitisha: (alama 2)
- b. Bebi anadokeza kuwa konda ana tabia gani? (alama 2)
- c. Toa sifa za sajili iliyohusika. (alama 6)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA NYERI**KISWAHILI**

102/3

KARATASI 3

SEHEMU A: TAMTHILIA**T. Arege: mstahiki meya****1. LAZIMA**

Onyesha jinsi maudhui ya usaliti yanavyojitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 20)

SEHEMU B: RIWAYA**K. WALIBORA: Kidagaa Kimemwozea****Jibu swali la 2 au 3**

2.kutenda kitendo kile na Bi. Mkubwa niliyemwona kama mamangu mzazi? Haidhuru yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 b) Taja tamathali mbili zilizotumika katika dondoo hili. (alama 2)
 c) Eleza sifa nne za anayeambiwa maneno haya. (alama 4)
 d) Dondoo hili linawasiwirije maudhui ya mabadiliko? (alama 10)

3. Umdhaniaye ndiye siye. Dhibitisha ukweli wa methali hii kwa kurejelea riwaya ya kidagaa kimemwozea. (alama 20)

SEHEMU C: HADITHI FUPI**K. Walibora na S.A Mohammed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine****Jibu swali la 2 au 3**

4. Maisha ni fumbo: 'Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili ukweli wa usemi huu. (alama 20)

- a) Mke wangu
 b) Shaka ya mambo
 c) Tazamana na mauti
 d) Mwana wa darubini

5. –Shangazi wakumbuke watoto. Waonee huruma.”

- a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake (alama 4)
 b) Fafanua mbinu ya kisanaa inavyojitokeza katika nukuu hili. (alama 2)
 c) Jadili jinsi aina ya uovu unaondokezwa katika dondoo hili ulivyoendelezwa na wahusika wengine katika hadithi husika. (alama 8)
 d) Fafanua sifa zozote sita za shangazi. (alama 6)

SEHEMU D: USHAIRI**Jibu swali 6 au la 7****6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Ya mgambo inalia, kusema nayotendewa
 Taifa ninawajia, kuamba nayofanyiwa
 Wenzangu nawalilia, mimi ninavyodakiwa
 Nipe ushauri wako, ewe mkuu tabibu

Tulifata Bibilia, Pete yangu kamgawa
 Tukawekewa zulia, na Baraka tukapewa
 Jap oleo natilia, heri n'baki mtawa
 Naja kwenu matabibu, nipe wenu ushauri

Mtu amejitakasa, dini nayo kabobewa
 Sura nzuri niliposa, urembo kakirimiwa
 Sikujua ninakosa, maradhi nimeletewa
 Tokezeni matabibu, ninaomba ushauri

Mapenzi yake muhimu, yamefanya napagawa
 Chakula chake kitamu, anajua kupakuwa
 Ila anao wazimu, uraibu wakulewa
 Naja kwenu matabibu, nawaomba ushauri

Mwenzangu huyu msiri, kiwewe nimeingiwa

Mwenyewe ninavyokiri, ndugu zangu naimbiwa
Mara nyingi nasafiri, hupeana naambiwa
Mko wapi matabibu, si mnipe ushauri

Ni mtani kweli kweli, anajifanya kujuwa
Humtoi kwa kejeli, wazi ninapekuliwa
Niambieni ukweli, vipi nitajiokowa
Enyi wangu matabibu, nahitaji ushauri

Mja huyu shindani, s'oni nikimtobowa
Amejawa kisirani, kasoro ni kumtowa
Mwenzenu sina amani, lini nitakuwa sawa
Nasubiri ushauri, Kazi kwenu matabibu

- a. Lipe shairi hili anwani yake? (alama 1)
b. Liweke shairi hili katika bahari mbili. (alama 2)
c. Nafsi neni inaelekea kulalamika. Fafanua mambo manne yanayolalamikiwa. (alama 4)
d. Onyesha jinsi mtunzi ametumia mbinu zifuatazo: (alama 2)
i) Jazanda
ii) Kinaya
e. Fafanua dhamira ya mshairi. (alama 2)
f. Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari. (alama 4)
g. Fafanua mbinu tatu alizotumia mtunzi kutosheleza arudhi za ushairi. (alama 3)
h. Kwa mujibu wa muktadha wa shairi, maneno yafuatayo yanarejelea nani? (alama 2)
i) Mkuu tabibu
ii) Matabibu
iii)

7. Soma shairi lifuatalo na kisha ujibu maswali yafuatayo.

Dunia yetu dunia, watu wanakufitini
Dunia huna udhia, watu wanakulaani
Dunia huna hatia, wabebeshwa kila zani
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia umenyamaza, umetua kwa makini
Dunia vitu mejaza, watu wanataka nini?
Dunia wanakucheza, binadamu maliuni
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia mtu akose, hukutia mdomoni
Dunia hebu waase, Hao watu mafatanio
Dunia chuki mpuse, muipate afueni
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia una lawama, za uongo si yakini
Dunia wanakusema, ni manjunju si razini
Dunia huna hasama, waja ndio kisirani
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia kuharibika, hayo amezusha nani?
Dunia watu humaka, hao wanaokuhini
Dunia umejazika, kila tunu ya thamani
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia unatukisha, bwerere bila undani
Dunia unatukosha, maji tele baharini
Dunia unaotesha, mimea tosha mashambani
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia hujageuka, tangu umbwe na Manani
Dunia watu ndo nyoka, mahaini na wahuni
Dunia una baraka, mwenye pupa hazioni
Dunia huna ubaya, wabaya ni insani

(Wallah, J. Malenga wa Ziwa Kuu, UK. 110)

- Hawatai majibu kwa usahihi wanapoulizwa maswali.

(hoja zozote $2 \times 1 = 2$)

c) **Sifa za lugha ya usafiri**

- i) Ina uradidi ili kusisitiza abiria watarajiwa wamsikie
- ii) Hutuimbia ushawishi ili apate abiria haraka
- iii) Lugha ya mitaani/sheng hutawala ili kujinasibisha
- iv) Lugha si sanifu wala haizingatii kanuni, lugha fasaha inasumbua.
- v) Lugha rasmi haitumiki
- vi) Kuna Kuchanganya msimbo iwe rahisi kujieleza
- vii) Msamiati mahsusi (nauli, matatu, abiria) unaosadifu na kazi yenyewe
- viii) Lugha ya ahadi – ukae poa na ufike salama kuwavutia abiria.
- ix) Hutumia kiimbo cha juu ili asikike.
- x) Pengine lugha ya kukashifu hutumika ili kudhibiti ushindani kwa mfano gari gani hilo lisilo na video n.k.

(hoja zozote $3 \times 2 = 6$)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA MERU KUSINI

102/1

KISWAHILI

Karatasi 1

Julai/ agosti 2016

1. Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la unywaji wa pombe haramu nchini uliosababisha vifo vya adinasi wengi. Andika tahariri kataika gazeti la mkombozi kuhusu juhudi zizozofanywa na serikali kukabiliana na hali hii.
2. Vijana wana mchango mkubwa kuliko wazee katika kuinua uhcumi wa nchi yetu. Jadili.
3. Tunga kisa kitakachodhihirishs maana ya methali ifuatayo : Subira ni ufunguo wa faraja.
4. Tunga kisa kinachomalizika kwa maneno yafuatayo :..... Niulipoona wakisherehekea matokeo ya kitaif, machozi yalinitiririka nilipokumbuka kilichosababisha kufutiliwa mbali kwa matokeo yangu.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA MERU KUSINI

102/3

KISWAHILI

Karatasi 3

Julai/ agosti 2016

SEHEMU YA A : USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Ajabu ajabu hii ajabu

Mwenye maneno hasemi

Asonayo atasema

Na nyuma hawatazami

Mbele wamekuandama

Ajabu ajabu hii ajabu

Wanaolima hawali

Wasolima Wamakula

Hula viso vya halali

Nguvu pia na fadhila

Ajabu ajabu hii ajabu

Wachokao hawalali

Walalao ni wazioma

Hulala pema pahali

Nahuku wakikoroma

Ajabu ajabu hii ajabu

Watendao si muhimu

Wasotenda watukufu

Wao ni watu adhimu

Kila siku twawasifu

Ajabu ajabu hii ajabu

Mwenye haki si wa haki

Asonacho hunguruma

Kwa uhuru na miliki

Mwenye haki humtuma

Maswali

- a) Lipe shairi hili anwani mwafaka alama 2
 b) Ni nani shabaha ya mshairi huyu. Alama2
 c) Shairi hili linaweza kuingia katika bahari gani? Alama2
 d) Mbinu ya kinaya injitokezaje klatika shairi hili? Alama6
 e) Tambua aina za idhini ya mshairi katiak shairi hili. Alama 2
 f) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. Alama5
 g) Eleza maana ya kifungu fifuatacho kama kilivyotumika katika shairi hili.
 –Wao ni watu adhimu” alama1

SEHEMU YA B: TAMTHILIA

Mstahiki Meya-Timothy Arege

2. –Nitawapa mapokezi ya kupigiwa mfano”
 a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. Alama4
 b) Tambua tamathali ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. Alama2
 c) Ni mambo yapi yanayofanya mapokezi yawe ya kupigiwa mfano kwa mujibu wa msemaji. alama4
 d) Fafanua mifano mingine inayodhihirisha ubadhirifu wa mali ya umma katika tamthilia hii. alama10
 3. Umdhaniaye ndiye kumbe siye. Jadili ukweli wa methali hii kwa kuwarejelea wahusika mbalimbali katika tanthilia ya Mstahiki Meya. Alama20

SEHEMU YA C: RIWAYA

Kidagaa kimemwozea-Ken walibora.

4. Kwa kurejelea wanaoifuata thibitisha kauli kwamba njia ya mwongo ni fupi.
 a) Mtemi Nasaba Bora alama12
 b) Mwalimu Majisifu. Alama8
 5. _..... alisimama jadidi na kuwatazama hawa watu wawili waliosimama wima kutetemeka kama waliokuwa wamepigwa na dhoruba ya theluji. _
 a) Eleza muktadha wa dondoo hili. Alama4
 b) Tambua mbinu yoyote ya lugha katika dondoo hili. Alama2
 c) Fafanua uhusiano katiya wanaotetemeka. Alama4
 d) Jasili namna mwanamke alivyosawiriwa katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. Alama10

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

6. Fafanua jinsi wanyonge wanadhulumiwa katika hadithi zifuatazo:
 a) Damu Nyeusi alama10
 b) Mwana wa Darubini alama10

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

7. a) Eleza maana ya maigizo. Alama2
 b) Andika sifa nne bainifu za maigizo. Alama4
 c) Eleza majukumu ya ngomezi katika jamii. Alama4
 d) Eleza changamoto za matumizi ya ngomezi katika jamii ya kisasa. Alama4
 e) Miviga ni nini? Alama2
 f) Eleza sifa nne za miviga. Alama4